Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Mei, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mkutano wa Kumi na Tano unaanza. Kikao cha Kumi, Katibu tuendelee.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 66

**Kuhusu Mpango wa Kutenga Ardhi ili Imilikishwe kwa Wanawake Kuanzisha Mashamba ya Miti kwa Matumizi ya Mkaa na Kuni**

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI** aliuliza:-

Serikali inatilia mkazo utunzaji wa misitu na maeneo mengi kutengwa kama Hifadhi za Taifa na kupelekea nishati ya kuni na mkaa kuwa ghali na pia wanawake hawana ardhi ya kuweza kupanda miti ya kuni:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga ardhi ili imilikishwe kwa wanawake kuanzisha mashamba ya miti kwa matumizi ya mkaa na kuni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba wanawake ni sehemu ya jamii, hivyo mipango ya Serikali iyopo inawajumuisha wanawake. Kwa sasa mpango uliyopo umeainishwa kwenye mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2009.

Katika mkakati huo imesisitizwa vijiji, miji, taasisi na watumiaji wengine wa miti kuni na mkaa. Mfano Taasisi za elimu, majeshi na viwanda kuwa na mashamba mahususi ya miti kwa ajili ya matumizi ya nishati, mkaa na matumizi mengine.

Aidha, mkakati umeelekezwa uanzishaji wa kilimo mseto kinachohusisha ukuzaji wa mimea ya mazao na miti kwa pamoja kwenye mashamba. Hivyo utaratibu huu umelenga kuwanufaisha wenye mashamba madogo kwa kuwa inayotokana na mashamba hayo itawasaidia kiuchumi kupata kuni na kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Serikali inahimiza juhudi za kusambaza matokeo yenye mafanikio ya nishati mbadala na teknolojia sahihi kama vile majiko sanifu na banifu, matanuru bora, matumizi ya vumbi la mbao, makapi ya mpunga, nishati ya jua na upepo, ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha na kuelimisha wanawake kupunguza matumizi ya mkaa na kuni kwa kutumia mbinu nilizozitaja hapo awali.

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na mipango ya Serikali ya kuhakikisha wanawake na wananchi wanatumia nishati mbadala, lakini ni ukweli usiopingika kwamba wanawake wengi hasa wa vijijini bado wanatembea umbali mrefu na wengi wanatumia kuni na hata kupelekea macho kuwa mekundu na baadhi yao hata kuuawa kwa imani za kishirikina.

Je, sasa Serikali ina mkakati gani wa haraka na endelevu utakaoleta matokeo ya haraka sasa ili wanawake waweze kutumia nishati mbadala kama vile ya gesi, majiko sanifu na banifu na nishati zingine?

Swali la pili. Kwa kuwa wanawake wamekuwa wakiachwa nyuma katika suala zima la kumiliki mazao yanayotoka katika mashamba yanayochanganyika wanayolima wanawake na wanaume.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvitambua vikundi vyote vya wanawake hapa nchini na kuviwezesha kuvipatia ardhi, mikopo na miche ili waweze kuotesha na kusambaza katika mashamba yao yatakayogawiwa na kusambaza kwa wananchi na katika Taasisi mbalimbali hapa nchini? Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Amina Makilagi kwa kufuatilia suala hili na kuhakikisha kwamba tunawapunguzia mzigo wanawake katika kutafuta kuni. Ni kweli hili ni changamoto kubwa sana inayowakabili wanawake hasa walioko vijijini. Nakushukuru sana Mheshimiwa Makilagi.

Sasa nikijibu swali lako la kwanza sisi kama Serikali tuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba tunawapatia wanawake hasa walio vijijini nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama Ofisi ya Makamu wa Rais tulichokifanya ni kuhakikisha kama nilivyosema kupitia mpango huu ni kuhakikisha kwamba jamii zetu zinapanda miti kadiri inavyowezekana ili pia kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na nishati ya kutosha. Lakini kubwa ambalo tunalisisitiza ni kuongeza matumizi ya majiko sanifu na banifu na hayo tumeyafanya kwa kupitia miradi mbalimbali tukishirikiana na mashirika yasiyo ya Serikali. Sasa hivi majiko yale yanapatikana kwa bei nzuri hasa katika vijiji.

Lakini kubwa Mheshimiwa Naibu Spika, ambalo ningependa kutumia Bunge lako Tukufu pia kulisema hapa ni kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, tukishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini tunahimiza matumizi ya gesi majumbani. Gesi ni rahisi sana Mheshimiwa Naibu Spika hasa kwa wanawake ambao wako mjini Ilala, Kinondoni, Tanga Jiji na hili kwa kweli tutaendelea kulisisitiza. Mimi binafsi natumia mtungi wa gesi wa kilo 15 ni shilinhi 54,000/= kwa mwezi karibu inapeleka siku 26 lakini ukimtazama mwanamke mkaa shilingi 2,000/= mpaka shilingi 4,000/= kwa siku.

Kwa hiyo, mwanamke anayetumia mkaa anatumia hela nyingi sana. Kwa hiyo, pale ambapo tupo mijini tutahimiza matumizi ya gesi na tunayo mpaka mitungi ya kilo 6 ambayo ni shilingi 22,000/=, kwa familia ndogo za watu wawili hadi watatu unaweza ukamudu. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Wabunge tunaposimama katika majimbo yetu tuhakikishe kwamba tunahimiza matumizi ya gesi za kutumia kwa sababu Serikali imeshusha kodi, imeshusha pia ushuru katika baadhi ya vifaa vya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ningependa kulijibu, tunavisaidia vipi vikundi vya wanawake ili kupata ardhi na kupata miche.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwanza kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 ndizo zinasimamia umiliki wa ardhi na Sheria hizi zimeweka wazi kwamba haki za wanawake kumiliki ardhi Kifungu cha 3(2) kimesema kwamba haki ya mwanamke kumiliki na kutumia ardhi itakuwa sawa kama ilivyo kwa wanaume.

Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo tuwahimize Mheshimiwa Amina kuhakikisha kwamba wanawake wanaomba kumiliki ardhi. Sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tutashirikiana na vikundi vingine kuhakikisha kwamba wanapata miche na mbinu mbadala za kupanda misitu. Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali dogo fupi la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Ninapenda kushukuru sana kwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini mara nyingi nishati mbadala pamoja na teknolojia muhimu, mara nyingi ziko mijini tu. Sasa ningependa kujua hasa vijijini ambako ndiko kwenye uhitaji mkubwa sana.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuleta wataalam watakaoweza kuwaelimisha wananchi ili waweze kutumia hizi teknolojia mpya?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa swali lako Mheshimiwa Lolesia. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika vijiji vyetu suala la matumizi ya nishati mbadala bado ni changamoto. Lakini kama nilivyosema tunazo juhudi mbalimbali ambazo tunafanya Ofisi ya Makamu wa Rais, tukishirikiana pia na Wizara ya Nishati na Madini, hasa *Rural Electical Authority (REA)* kuna juhudi mbalimbali zimefanywa katika kuhakikisha kwamba tunahakikisha upatikanaji wa nishati mbadala kwa wananchi hasa vijijini na siyo tu kwa ajili ya kupikia. Lakini katika hospitali za vijijini kuhakikisha kwamba tunapata nishati mbadala kwa ajili ya kufanyia operesheni na shughuli nyingine za hospitali.

Kwa hilo Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kwamba tutaendelea kuelimisha wanawake na wanaume walioko vijijini na hili tumelifanya kwa kiasi kikubwa sana kwa kutumia televisheni kwa kutumia redio na vijarida.

Lakini bado pia tunao washirika mbalimbali katika vijiji vyetu. Kubwa ambalo ningetaka kulisisitiza ili kuhakikisha tunaongeza matumizi ya nishati mbadala vijijini, tuwahamasishe wanawake waunde vikundi. Tunao Mfuko wa Mazingira, *I mean Global Environmental Facility* ambao inasaidia ku-*fund* miradi midogo midogo hasa ya wanawake katika kuhakikisha kwamba wanapata nishati mbadala.

Lakini pia tunayo miradi mingine chini ya *Tanzania Forest Fund*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wanawake kuhakikisha kwamba tunaandika *concept paper* tuwasaidie kuandika *concept paper* ili tupate miradi ya kuweza kupata nishati mbadala katika vijiji vyetu.

Lakini kubwa majiko sanifu na majiko banifu ndiyo yatasaidia sana kupunguza matumizi ya kuni na misitu katika vijiji vyetu. *(Makofi)*

Na. 67

**Ujenzi wa Ukuta wa Bahari**

**MHE. OMARI R. NUNDU (K.n.y. SALEH A. PAMBA)** aliuliza:-

Mfuko wa Mazingira Duniani *(Global Environmental Facility)* imeipata Tanzania dola za Marekani milioni tatu (3,000,000) ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi na sehemu ya fedha hizo, zitatumika kujenga ukuta wa bahari ili kuhifadhi maji Mji wa Pangani.

Je, ujenzi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imepata msaada takribani dola za Marekani milioni 3.3 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuhimili *(adaptation)* mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa Pwani.

Kati ya fedha hizi, dola za Marekani milioni 1 zimepangwa kutumika kukarabati ukuta wa bahari wa Pangani ili kukinga mji wa Pangani kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi za kuongezeka kwa ujazo wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilisha taratibu zote za kupata fedha kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia, serikali iko katika hatua za maandalizi ili ukarabati kamili wa ukuta uweze kuanza. Hatua hizi ni pamoja na tathmini ya athari kwa mazingira *environmental impact assessment* uboreshaji wa taarifa za awali *base line information* na taratibu za kumpata mtaalam elekezi wa ukarabati wa ukuta.

Mchakato wa kumpata mtaalam elekezi wa athari ya mazingira na yule wa kuboresha taarifa za awali uko katika hatua za mwisho za kuchambua maombi yaliyowasilishwa kwa kazi hiyo, wakati mchakato wa kumpata mtalaam elekezi wa ukarabati wa ukuta uko katika hatua za maandalizi ya hadidu za rejea. Baada ya maandalizi hayo ambayo yamepangwa kukamilika mwezi Juni mwaka huu 2014 inatarajiwa kuwa ukarabati wa ukuta utaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwa wananchi wa Pangani wawe na subira wakati hatua hizi za maandalizi zinakamilishwa. *(Makofi)*

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa majibu yanayotia moyo sana hasa kwa jitihada zinazofanyika kuhakikisha kuwa mji wa Pangani ambao una magofu ya kale ni vivutio na unalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwambao wa Bahari ya Hindi tuna sehemu ambazo zina magofu ya kale kama vile Tongoni na Chongoleani ambao sasa hivi yanaliwa na mali. Sasa swali langu, Serikali haioni umuhimu wa kujaribu pia kuhifadhi sehemu hizo ambazo zina vivutio kwa watalii?

Swali la pili, Serikali ilianzisha mfumo nzuri tu wa kuzuia watu wasijenge mita 60 kutoka baharini. Lakini kilichojitokeza hasa katika mwambao wa kutoka Tanga mpaka Pangani sehemu ambazo zilikatazwa kujengwa mwaka 1988 sasa viwanja vimetolewa na sehemu hizo bado hazikidhi mita 60.

Serikali haioni kuwa kuna wajibu sasa kutoa tamko la kufuta viwanja vyote ambavyo viko katika mfumo huo huo na ambavyo havijajengwa badala ya kungoja vijengwe halafu waje wapate hasara ya kuvunja majumba hapo baadaye? Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya sehemu za mwambao wa pwani Tongoni, kuna mmomonyoko *I mean* maeneo hayo hayako vizuri magofu ya kale, lakini ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge wa Tanga Mjini ni kwamba sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tutashirikiana na wenzetu wa Maliasili na Utalii tuone ni jinsi gani tunaweza tukaboresha au kufanya *rehabilitation* ya maeneo hayo.

Lakini ninavyofahamu tayari kuna kazi imeweza kufanyika katika magofu ya kale ya Tongoni. Lakini nitaenda kucheki ni hatua gani imefikiwa katika suala hilo kwa sababu na mimi

ni mdau wa Tanga Jiji. Nitahakikisha kwamba suala hilo tunalifanyia kazi na tunalipa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu ujenzi ndani ya mita 60 kutoka fukwe za bahari au maeneo ya kingo za mito. Ni kweli Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inakataza ujenzi katika ndani ya mita 60. Kwa hiyo, sisi kupitia *NEMC* Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira tulianza kazi ya kuyachambua maeneo hayo katika Jiji la Dar es salaam.

Kwa hiyo, naamini kabisa kamba tutaenda nalo na sasa katika Jiji la Tanga. Tuone pia ni viwanja vingapi vimetolewa ndani ya mita 60 kama Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inavyokataza na nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutachukua hatua za kisheria. Kwa sababu hili siyo sduala la mtu, ni suala la Sheria na Sheria lazima itekelezwe. Ni marufuku kufanya shughuli zozote kuendeleza binadamu ndani ya mita 60 kutoka eneo la kingo za mito au ufukwe wa bahari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tuendelee na Wizara ya Ujenzi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga Jecha.

Na. 68

**Barabara ya Mwanza *Airport Bypass***

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Katika Bajeti ya Mwaka 2012/2013 kulikuwa na barabara iliyotamkwa Mwanza *Airport By Pass:-*

Je, barabara hiyo ilikuwa ni ipi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara iliyotamkwa *Mwanza Airport By Pass* katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 ni ile ya kutoka Nyakato-Buswelu-Muhonze-*Airport*. Katika mwaka huu fedha barabara hii ilitengewa jumla ya shilingi milioni 70 kwa ajili ya matengenezo ya kilomita 3.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huo wa fedha 2012/2013 Wizara yangu kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii iliongeza fedha shilingi milioni 500 kutoka *Road Fund* kwa ajili ya kazi kuifungua barabara ya Nyakato-Buswelu-Muhonze. Sehemu ya hiyo ya barabara tayari imefunguka. Aidha, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 450 kwa ajili ya kukarabati sehemu ya barabara kutoka Buswelu hadi Nyakato.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Waziri wake kwa kukamilisha daraja la Mabatini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza. Kwa kuwa, barabara ya *Mwanza – Airport By Pass* tukiwa katika Kamati ya Miundombinu tulikwenda kuitengea na ndio tukakubali kupitisha Bajeti hiyo. Na Wizara ikaenda kuchukua barabara ya Mwanza – Nyanguge *By Pass.* Ni

nani aliyetoa mamlaka ya kubadilisha barabara ya Mwanza – *Aiport By Pass* na akaenda kuchukua barabara ya Mwanza – Nyanguge *By Pass?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Sidhani kabisa kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuniaminisha kwamba, nyeupe iwe nyekundu, sidhani. Pamoja na kwamba, tunasema kwamba, tunaanzisha Halmashauri mpya tunasogeza huduma kwa wananchi. Kwa kukimbia Barabara ya Mwanza – *Airport By Pass* unamlazimisha mwananchi wa Wilaya ya Ilemela aingie Wilaya ya Nyamagana kwanza na ndio aende Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela.

Ni lini sasa Wizara yako itachukua barabara hii kama ilivyoipandisha na kuifanyia kazi, ili wananchi wa Wilaya ya Ilemela waweze kufika kwenye kutatua matatizo yao kwa urahisi zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge majibu ya uhakika kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mwenye jukumu la ku-*classify* barabara hizi ni Waziri wa Wizara ya Ujenzi.

Kwa hiyo, anaposema ni nani, basi tunakwambia ni Waziri wa Ujenzi ndiye aliyepewa mamlaka ya kuamua barabara hii ipande daraja au ishuke daraja na ndio tunavyofanya maana tumegawana majukumu. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kitu cha kwanza tunataka barabara hizi ziwasaidie wananchi, ili wananchi waweze kufanya kazi wajiletee maendeleo, ndio nia ya Serikali na ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatufanyi tu barabara kuitengeneza kwa sababu, ya kuitengeneza. Tunakuwa na malengo ya kuwasaidia wananchi kwa ajili ya maendeleo yao kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, kama kuna suala ambalo mlikuwa mmelijadili kwenye Kamati za Mabaraza ya Mkoa na kama kuna jambo lolote ambalo ni lazima liletwe kwenye Wizara ya Ujenzi tunalifanyia kazi na kuweza kuona ni kitu gani ambacho tunataka tukifanye kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Na. 69

**Matengenezo Katika Barabara ya Nangurukuru – Liwale**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI (K.n.y. FAITH M. MITAMBO)** aliuliza:-

Barabara ya Nangurukuru hadi Liwale imekuwa ikitengenezwa kila mwaka kwa pesa nyingi huku maeneo korofi yakibaki vilevile na kusababisha barabara hiyo kupitika kwa shida wakati wa masika:-

Je, ni lini Serikali itaitengeneza barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 231 kwa lami, ili kupunguza matengenezo haya ya kila mwaka yasiyo na tija?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mbunge wa Liwale, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nangurukuru – Liwale ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 231 inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS*. Barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum kila mwaka kulingana na Bajeti inayotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti kwa sasa Serikali haina mpango wa kuijenga barabara ya Nangurukuru – Liwale kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, Serikali itaangalia uwezekano wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami katika mipango ya muda mrefu. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii, ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. *(Makofi)*

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nangurukuru – Liwale ni barabara ambayo ni ya uchumi. Kwa nini, nasema hivyo; ni ya uchumi kwa sababu, pori kubwa la *Selou* linapita katikati ya barabara hiyo. Ina uchumi wa utalii, ina uchumi wa korosho, ufuta, na kadhalika. *Game Reserve* iko pale. Kwa nini wasishirikiane na *Game Reserve,* kwa nini wasishirikiane na wahusika wa Utalii wa pale, ili waweze kushirikiana kuweza kuitengeneza barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia kwamba, Liwale haina barabara zingine, barabara zote mpaka ufike Liwale uende Mikunya, ufike Liwale uende Makata, ufike Liwale uende Mihumo, hazina pacha, Liwale – Mpiga Miti. Sasa hii ndio waliyoitegemea; ndiyo kuna barabara Liwale – Mpiga Miti, sasa barabara hii ya Liwale – Nangurukuru ndiyo wanayoitegemea sana wananchi. Tunaomba sana Mheshimiwa mtafute kila njia mshirikiane na Mashirika kuweza kutengeza barabara hii, naomba jibu? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majina aliyoyataja Mheshimiwa Fatuma Mikidadi ni ya kweli. Barabara hizo za Liwale, Mipata, Kimambi, mimi mwenyeji Liwale kule.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubalianenaye kwamba, barabara hii ni ya muhimu na ni ya uchumi kiutalii. Ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nimesema tutaiangalia katika mipango yetu ya baadaye kwa sababu, namna tunavyojenga hizi barabara za lami, tumeanza kwanza kujenga barabara kuu. Nifurahi kulitaarifu Bunge lako kwamba, katika Mkoa wa Lindi ambao una kilometa 348 ambazo ni za barabara kuu, 333 ni za lami. Kwa hiyo, ni bado kilometa 14 tu ndio hatujajenga kuwa za lami.

Kwa hiyo, tulishakubaliana kwamba, tuanze kwanza hizi barabara kuu zinazounganisha Mikoa na Mikoa na baadaye tutaanza kujenga barabara hizi zinazounganisha kati ya Wilaya na Wilaya kwa hiyo, barabara hiyo, tutaishughulikia katika mipango ya baadaye. *(Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, ujenzi wa barabara za lami huambatana na

ubomoaji wa nyumba za wananchi na ulipwaji wa fidia. Nataka kufahamu ni lini sasa Serikali ambayo imeweka X katika nyumba za Wapiga Kura wa Jimbo la Mchinga katika maeneo ya Milola, Rutamba, wananchi wale watafidiwa ili waweze kuwa na uhakika na maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Mtanda, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuweka X kwenye eneo la Jimbo lake maana ni kutoa taarifa kwamba, nyumba ile ipo ndani ya hifadhi ya barabara, sasa hiyo ni hatua ya kwanza. Tumeweka X za aina mbili, kuna X nyekundu na kuna X za kijani. Zile X nyekundu tunamtaarifu yule mtu kwamba, nyumba hiyo imeingia kwenye hifadhi ya barabara kinyume cha Sheria. Kwa hiyo, nyumba hiyo inabidi uibomoe mwenyewe kwa gharama zako mwenyewe. Vinginevyo Serikali itaibomoa na hulipwi fidia. Lakini zile nyumba ambazo tumeziwekea X ya kijani hii ina maana kwamba, Serikali itakufidia wakati ambapo tunaanza kuitengeneza barabara ile.

Kwa hiyo, katika mipango yetu ya kukarabati barabara zetu au kuzijenga, wale wenye alama za X ya kijani, wale watafidiwa na Serikali kwa mujibu wa Sheria iliyopo. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, swali la msingi linauliza barabara ya Nangurukuru hadi Liwale na tatizo wanazungumzia wakati wa masika. Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ni Injinia, unajua kwamba, maji ni adui mkubwa wa barabara. Sasa hii *routine maintainance* inayofanyika haoni kuwa kipaumbele kiwekwe kwenye *drainage system,* ili maeneo haya mwinuko na mteremko, barabara hii iweze kupitika kwa muda huu mfupi wakati mkiwa na muda mrefu wa kujenga barabara hii kwa lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Mbatia, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, adui mkubwa wa barabara ni maji. Siku zote maji lazima yasikae kwenye barabara, inabidi uyaondoe kwa maana uwe na mfumo mzuri wa mifereji. Lakini barabara unaweza ukaifanyia *routine maintainance* kama iko katika kiwango cha kuifanyia *maintainance.*

Kwa hiyo, kwanza lazima uikarabati iwe kwenye kiwango ndiyo utengeneze mifereji ambayo inaweza ikatoa maji katikati ya barabara yakaenda kwenye mifereji. Kwa hiyo, kazi hiyo ndio tunayoifanya. Kwa hiyo, tunazikarabati kwanza, tunaweka mfumo mzuri wa mifereji, ili kusudi wakati wa masika mvua zikizidi maji yasiwe yanakaa barabarani na barabara iweze kupitika majira yote ya mwaka. *(Makofi)*

Na. 70

**Zao la Zabibu za Mezani**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA)** aliuliza:-

Tafiti za kilimo zimeonyesha wazi kuwa, zao la zabibu za mezani hunawiri na kutoa zabibu nzuri, tamu na zilizo bora kama zile zinazozalishwa India, Italy, Afrika Kusini na hata nchi nyingi za Ulaya, na ushahidi umethibitika tulipotembelea na kuona Vitalu vya maonesho ya kilimo yaliyofanyika Dodoma miaka ya hivi karibuni:-

Je, kwa nini Serikali hailifufui shamba lake la zabibu huko Makutupora na kuotesha mbegu za zabibu za mezani badala ya zabibu kali tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimia Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe - Zanzibar, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mikakati ya kufufua shamba la zabibu la Makutupora kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone, ili kuweza kupata matawi ambayo yatatoa mbegu za zabibu za mezani kwa wingi. Aidha, Wizara imejenga Maabara ya Sayansi ya kuzalisha miche ya zabibu kwa njia ya *tissue culture,* pamoja na kujenga nyumba ya kinga, yaani *screen house,* kwa ajili ya kutunza miche itakayozalishwa kwa njia ya chupa, yaani *tissue culture.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hiyo, itasaidia kuongeza uwezo wa Kituo cha Utafiti cha Makutupora, kuzalisha miche mingi zaidi ya mizabibu ambayo itajumuisha miche ya zabibu za mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa miche ya aina zote za zabibu, za mvinyo, za mezani na za kukausha kwa njia ya vijiti, yaani *rooted cuttings,* unaendelea katika Kituo cha Makutupora ambapo mwaka jana Kituo cha Makutupora kilizalisha miche 26,000 na kuisambaza kwa wakulima katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Wilaya za Bunda na Iringa; kati ya hiyo miche 3,000 ni ya zabibu za mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Kituo kinatarajia kuzalisha miche ya zabibu za mezani takribani 50,000 na kuisambaza kwa wakulima. Aidha, kasi ya uzalishaji wa miche ya zabibu inatarajia kuongezeka baada ya maabara mpya ya sayansi kuwekewa vifaa na kuanza kufanya kazi kikamilifu. Ahsante sana.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kutia moyo. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza, la kwanza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa, watu wa Dodoma wanajishughulisha na kilimo cha zabibu, lakini kimsingi wenyewe hawafaidiki nacho sana hicho kilimo kwa sababu, mara nyingi zabibu wanazozilima ni zabibu kali zinazalishwa mvinyo, ambao wengi wao siwaoni kuwa wa uwezo wa kuunywa. Sasa je, ni lini Serikali itawahamasisha watu hawa wa Dodoma waongeze uzalishaji wa zabibu za mezani ambazo sio tu wataweza kuzila wenyewe endapo zitakosa soko, lakini pia zina soko kubwa hasa katika miji muhimu kama Dar-es-Salaam, Mwanza na miji mingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Ni wazi hapa mjini sasa hivi ukiangalia zabibu wengi wanatanga nazo ndani ya masanduku na mwisho zinaoza.

Je, Serikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka wa kutafuta soko la uhakika la zabibu, ili wale watakaozilima, sio Dodoma tu, lakini na sehemu nyingine za nchi yetu, wakawa na uhakika wa kuuza badala ya kutembea nazo ndani ya masanduku tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimia Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa anataka kujua kama tuna mikakati ya namna gani ya kuhamasisha wakulima, ili waweze kulima zabibu za mezani ambazo zinaweza zikawafaidisha pia wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba, na niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli wananchi wa Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine kwamba, Wizara tayari ina mkakati wa kuwahamasisha wakulima wengi katika Mkoa wa Dodoma. Sio Mkoa wa Dodoma tu, lakini na maeneo mengine ambayo wanalima zabibu na ndio sababu, tayari tumeshaanza kutumia Chuo cha Hombolo cha Utafiti, kutafiti miche mingi zaidi, lakini na kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tayari tumeshazalisha mbegu za aina mbili na tunatarajia baadaye mwakani au mwaka kesho, tuweze kuzalisha mbegu nyingine za aina nne na kuzisambaza kwa wananchi, kwa maana hiyo wakulima. Lakini pia tunawahamasisha wananchi hawa kujiunga kwenye vikundi vyao vya ushirika, ili waweze pia kupata fursa za mikopo. Kwa maana hiyo, waweze kuzalisha mashamba makubwa ambayo itakuwa na tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa anataka kujua kama tunayo mikakati gani ya kutafuta soko;. Ni kweli, liko tatizo kubwa la soko, naomba tukubaliane. Kwa sasa soko kubwa la zabibu ni kwa wafanyabiashara wachache au kwa wenye viwanda vidogovidogo hapa Dodoma, lakini pia na Dar-es-Salaam na tunategemea pia wanunuzi wachache wanaotoka nchini Kenya.

Kwa hiyo, ambacho tumeamua katika Wizara ni kuhakikisha kwamba, tunawahamasisha wananchi hawa wajiunge kwenye Vikundi vya ushirika na wakijiunga kwenye vikundi vya ushirika, tunaweza kwa maana hiyo kukawa na uhakika wa kuwatafutia soko zuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na uko tayari mpango kule Chinangali ambako kuna ushirika mkubwa wa hawa wakulima, ambao baada ya kuwa wameshajiunga vizuri, basi tuna uhakika nadhani na sisi kama Wizara tutaunganana0, ili kuweza kutafuta soko zuri na la uhakika zaidi kwa wakulima. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 71

**Kuanzishwa kwa Mfuko wa Akiba wa Taifa wa Gesi Asilia**

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Niwape pole tu wananchi wa Igalula kwa Diwani Kapalu kufariki, Mungu amweke mahali pema peponi.

Tanzania inajiandaa kufaidi utajiri wa mapato ya Gesi Asilia kwa kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Akiba *(Sovereign Wealth Fund)* kama nchi za Qatar, Norway, Abu Dhabi, Trinidad and Tobago, Algeria na Lipya:-

(a) Je, mfuko huu utakuwa na uwazi kiasi gani?

(b) Je, Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo na kiuchumi itapewaje kipaumbele na mfuko huu?

(c) Je, Sera ya Gesi Asilia 2013 itajifunza nini kwa Mfuko huu kwa matumizi mabaya ya mapato ya Gesi na Mafuta kwa nchi kama Nigeria na Mexico ambako wananchi wana maisha duni katikati ya utajiri mkubwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Gesi Asilia ya Mwaka 2013 imeainisha kwamba, Uanzishwaji na Utawala wa Mfuko wa Gesi Asilia utazingatia uwazi, uwajibikaji katika ukusanyaji, ugawaji, utumiaji na utawala bora wa mapato yatokanayo na gesi asilia. Katika kuhakikisha uwazi Kanuni za Uendeshaji zitapitishwa kwa kupitia Mjadala wa Kitaifa kuhusiana na matumizi na utawala wa fedha hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu utakuwa na Kanuni za Uendeshaji ambazo zitazingatia mahitaji na matumizi ya nchi. Vilevile matumizi ya Mfuko yatazingatia utawala bora, kama tulivyosema hapo awali, na kuhakikisha unahusisha mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo hapa nchini.

Mojawapo ya malengo ya Mfuko huu ni kuhakikisha kwamba, unanufaisha kizazi kilichopo na kinachokuja. Kwa namna hii Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo itaweza kunufaika na uwepo wa Mfuko huu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Gesi Asilia ni gesi inayokwisha, ili kuepukana na matumizi mabaya ya mapato ya gesi asilia na mafuta, kama tulivyoona katika nchi nyingine, Sera ya Gesi Asilia ya mwaka 2013 imehakikisha kwamba, Kanuni za Uendeshaji zinazingatia uwazi na kupitishwa kwa kupitia Mijadala ya Kitaifa kuhusiana na matumizi ya fedha hizo.

Vilevile Mfuko huu utasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, ili kuhakikisha kwamba, shughuli za Gesi Asilia hazina athari katika Sera za Fedha na kusababisha kuyumba kwa uchumi.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; Mfuko wa Gesi Asilia utasaidiaje kuongeza utulivu wa uchumi mpana *(Micro Economic Stability)* na uwekezaji katika miradi mikakati nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la pili. Nchi nyingine kama Bahrain, Australia, Abudhabi, Norway, Mifuko hii ya Gesi ina Wajumbe kutoka katika Bunge, Serikali na Taasisi za Elimu ya Juu *(Academia)* na uwanachama katika *Extractive Industries Transparency International.*

Je, Wizara ina mikakati gani katika kuangalia masuala haya mawili muhimu sana, ili Mfuko huu uwe endelevu na utusaidie watu tunaotoka katika Mikoa iliyo nyuma kiuchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, kama ifwatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mifuko hii ya aina hii ambayo kitaalamu inaitwa *Sovereign Wealth Fund,* kwanza ni kutunza akiba ya nchi kwa matumizi ya baadaye, hasa nchi inapotokea kuwa na mapato ya ziada hasa kwenye Bajeti ama kama sisi ambavyo tumegundua gesi, ambapo tutakuwa na mapato ya ziada.

Lakini malengo ya pili, ni ku-*stabilize* uchumi wa nchi kwa sababu, mnapopata mapato mengi, hasa mnapokuwa na *surplus Budget,* ili ku-*stabilise* uchumi ni lazima kuwa na Mfuko ambao mapato ya ziada yote yatatunzwa na kuweza kuufanya uchumi ukue kwa asili na siyo ukue kwa *artificial. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko hii kama alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, kwenye nchi mbalimbali hutumika na Serikali haswa kwenye kuwekeza kwenye miradi mingine mbadala kwa maana ya ku-*diversify* uchumi. Kama tunapata mapato mengi kupitia gesi asilia sasa Serikali inaweza kutumia mapato hayo kuwekeza kwenye miradi mingine ya kiuchumi ambayo itatumika baadaye ambapo gesi itakuwa imekwisha. Hiyo ndiyo faida kubwa ambayo Watanzania wataipata katika mfuko huu ambao tunakusudia kuuanzisha hivi karibuni. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Nimesikitishwa kidogo na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali inakusudia huu mfuko kutengenezewa kanuni badala ya sera ya gesi ya mwaka 2013 kutungiwa Sheria ili Bunge lishiriki katika kutunga Sheria na mfuko huu uongezwe na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali.

Je, Serikali iko tayari kwa kuwa sasa Sera ya gesi imetengenezwa pamoja na kuwa ina udhaifu lakini iko tayari sasa kusitisha hizi kazi zinazoendelea ama za kuandaa Kanuni au mambo mengine yoyote mpaka kwanza Tanzania itunge Sheria ya gesi ambayo tumeahidiwa mpaka leo haijaletwa humu Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, iko siku Mnyika ataridhika tu. Sera ya gesi imekamilika na nimeeleza hapa mchakato wa kuanzisha *sovereign fund* utafanywa kupitia mjadala mkubwa wa kitaifa ambao utahusisha Wabunge, utahusisha wadau mbalimbali.

Tumekamilisha kutunga sera ya gesi kinachofuatia sasa ni kutayarisha Sheria na Kanuni mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za gesi pamoja na kuanzisha Sheria itakayoanzisha mfuko wa gesi asilia. Sasa haya mambo yote yatafanyika kwa taratibu ambazo ziko Kisheria, itapitia *process* ambayo Wabunge watahusishwa.

Kwa hiyo kama ana mawazo, ana *inputs* anafikiri zitaboresha basi muda utakapofika tutakapokuwa tunaleta hapa tunaomba alete mawazo yake ili tuweze kuyashirikisha na kuwa na sera bora na Sheria bora pamoja na kuwa na mfuko bora. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika utajiri huu wa gesi yako mambo mengine mengi. Wananchi wakafaidika mbali tu na hiyo mfuko wa akiba na kwa kuwa hivi karibuni tumesikia malumbano baina ya Wizara yako na wafanyabiashara kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika mambo haya ya gesi. Kwa maana ya *local content* na kwa kuwa pia natambua Wizara yako imeanza kutengeneza sera ya ushirikishwaji wa wananchi.

Je, Mheshimiwa Waziri, utawasaidiaje wananchi kuhusu kuharakisha ili taratibu au sera ya *local content* ushirikishwaji wa wananchi ili wafaidike kwa mapana zaidi kama zilivyofaidika hizi nchi zilizotajwa alipouliza mwanzo swali?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sera yetu ya gesi ambayo imekamilika hivi karibuni ya mwaka 2013 *local content* tumeweka mkazo mkubwa. Watanzania kupitia sera ile haswa kwenye eneo la *local content* tumeweka msisitizo hasa kwenye *local procurement*, tumeweka msisitizo kwenye ushirikishwaji wa Watanzania kwenye shughuli za gesi. Tumeweka msisitizo pia katika kuhakikisha kwamba bidhaa za ndani kwa maana yaku-*promote* viwanda vya ndani na uzalishaji wa ndani kunakuwa na mkazo kwa watu wote wanaoshiriki katika shughuli za gesi kuhakikisha kwamba wanatoa kipaumbele kwenye bidhaa za ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malumbano haya yanayoendelea hayana tija kwa nchi kwa sababu Serikali inafanya kazi kwa kupitia *document*, sera, Sheria, pamoja na kanuni. Kwenye sera yetu ya gesi tumeweka wazi kabisa namna Watanzania watakavyoshirikishwa, tumeweka wazi kabisa namna ambavyo Watanzania wataweza kupata fursa mbalimbali za uwekezaji katika gesi na nina uhakika kwamba hiyo ndiyo njia sahihi ya Serikali kuwasiliana.

Kwa hiyo, kama unataka kujifunza zaidi na kujua namna gani Watanzania watashiriki katika gesi kwenye sera yetu tumechapisha kwenye magezeti wiki hi kuonyesha *local content* namna ambavyo tumeitayarisha na namna inavyotoa fursa mbali mbali kwa Watanzania. Kwa hiyo, kwenye mambo haya ya Kiserikali ningependa tu mambo mengine yale ya mitaani yasiwe sehemu ya mipango mikubwa ya Serikali. *(Makofi)*

Na. 72

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Nkunga, Ibililo, Lupepo na Mboyo - Rungwe**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Umeme umefikishwa katika kijiji cha Kiwira na chuo cha Magereza Kiwira, Wilayani Rungwe lakini vijiji vya Nkunga, Ibilibo, Lupepo na Mboyo ambavyo vinatenganisha sehemu hizi mbili havina umeme.

Je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa vijiji vilivyotajwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia wakala wa nishati vijijini *REA* inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika maeneo ya vijiji vya Wilaya vya Wilaya ya Rungwe chini ya mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili. Mradi huo ulianzwa kutekeleza na Mkandarasi *State Grid and Electrical Works Limited,* mwezi Aprili, 2014 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 na unahusisha vijiji naomba nivitaje vijiji vya Nkunga, Ibililo, Lupepo, Mboyo, Isange, Makwitwa, Kilonganongwa, Lufumbi, Bunyangomale, Bulugwe, Simike, Masebe, Lutete, Kasokela, Ngulu, Ipagika, Mpata, Lukasi, Lupaso, Mbingili, Mpombo, Lusanje, Manou, Kabura, Ndola, Kyambambembe, Ijigha, Masukulu, Isyukila, Iponjola, Lugombo, Katebe, Kaburu, Kyanguluka, Rufurio, Ilima, Lubanda, Lugombo, Ilima Sekondari, Zahanati ya Ikama, Ikama, Ijoko, Mpimbo, I na II, Bujeshi Lupando, Bunyang'ombe, Mbegele, Kisondele Igaramo, Lusungo Itila na Kang'eng'e.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya mradi huo zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 397.7. Njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 347.5. Kufunga *transfoma 133* na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 4443. Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 8.1.

**NAIBU SPIKA:** Natumaini Mheshimiwa Profesa umeridhika maana yake mradi mkubwa huu. Swali la nyongeza Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru Wizara kwa majibu mazuri sana na vile vile kwa kupitia kwa Waziri nawaomba niwapongeze na kuwashukuru *REA* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kwamba vijiji nilivyoviuliza katika swali langu la msingi viko kando kando ya mto mmoja mkubwa unaitwa Kiwira, mto huo una maporomoko makubwa nilitaka kujua kama Serikali inaweza ikaenda ikaangalia uwezekano wa kuweka mitambo tupate umeme wa ziada kwa eneo hilo?

Swali la pili kuna mradi mwingine unaotoka Mbambo mpaka Busisya mwendo wa kilomita kumi na moja lakini karibu kilomita nane ambapo vipo katika vijiji vya Landani na Mibula hakuna umeme, umeme haujashushwa pale. Mheshimiwa Naibu Waziri Malima alikuja na akaukagua na akatuahidi kutupa *transfoma* mbili lakini ni miaka miwili mpaka sasa hatujapata hizo *transfoma.* Nilitaka kujua ni lini hizo *transfoma* zitapelekwa sehemu hiyo, ili watu wapate umeme katika hivi vijiji nilivyovitaja, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN JULIUS MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini kuna maporomoko mengi sana ya mito na nilifanya ziara kule na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishuhudia baadhi ya wananchi wawekezaji wa ndani wakiwekeza kwenye shughuli za kuzalisha umeme.

Nitoe wito kwa Watanzania ambao wana uwezo wa kuwekeza kwenye miradi midogo midogo ya megawati moja ama chini ya hapo waweze kutumia fursa hiyo ya uwekezaji lakini pia *TANESCO* wamesikia suala hili nitawaagiza waweze kwenda kufanya utafiti wa kuona kama wanaweza wakawa na mradi mdogo wa kuzalisha umeme kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ahadi ya *transfoma* mbili niombe tu kuipokea kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge na nitafuatilia kwa *TANESCO* kuhakikisha kwamba *transfoma* hizo

zinapatikana na kwa kuwa Mkandarasi bado yuko *site* anafanyakazi itakuwa ni rahisi kwa mkandarasi yule kuongezewa kazi ya ziada kuhakikisha vijiji hivyo vinajumuishwa katika ukamilishaji wa mradi wa umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umebaki mdogo sana yamebaki maswali mawili tuyatendee haki. Swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, kuendelea na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Na. 73

**Ugawaji wa Ranchi ya Kitengule**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kupima upya ugawaji wa Ranchi ya Kitengule ili wananchi wa vijiji vya Kishojo, Kihanga, Katanda, Kibwera, Mushabaiguru, Mlamba na wengineo wapate maeneo ya malisho.

Je, ni lini zoezi hilo litakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gesbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ranchi ya Kitengule ina eneo la hekta 14,062.94 ambazo zinamilikiwa na *NARCO* na hekta 28,600 zinazomilikiwa na mwekezaji Kagera *Sugar Company Limited* kwa ajili ya kulima miwa na kunenepesha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kilio cha muda mrefu cha wafugaji wa vijiji vya Kishojo, Kihanga, Katanda, Kibwera, Mshabaiguru, Mramba na wengineo cha kupatiwa maeneo ya malisho upimaji ulifanyika mwaka 2010 ambapo *NARCO* ilibaki na hekta 14,062.94, *Kagera Sugar* hekta 28,600 na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe pamoja na vijiji vyake hekta 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi zoezi hili lilizingatia uwepo wa amani na utulivu, kuondoa migogoro inayotaka kujitokeza, kulinda wawekezaji, kusimamia ufugaji bora na wa kisasa wa kibiashara na kulinda ardhi isiharibike kwa mmomonyoko kutokana na mifugo kuchungwa kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kutokana na migogoro ambayo imeendelea kuwepo kati ya *NARCO,* wawekezaji wadogo na vijiji Serikali iliahidi hapa Bungeni wakati Wizara ikiwasilisha hotuba ya mwaka 2013/2014 kwamba Serikali imeamua kupima upya ranchi zote kuanzia mwaka 2013/2014 ili kuhakikisha migogoro hiyo inamalizika moja kwa moja. Zoezi hili kwa bahati mbaya halijafanyika lilifanywa na wenzetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kushirikiana na wadau wengine.

Kwa bahati mbaya zoezi hilo halikuweza kutekelezwa mwaka huo wa fedha 2013/2014 kutokana na kukosekana kwa fedha. Inatarajiwa kuwa zoezi hili litafanyika katika mwaka huu wa fedha 2014/2015. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nitoe masikitiko makubwa sana kwa majibu mepesi katika swali gumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama mara yangu ya ishirini nasimama hapa kuzungumzia suala hili na inashangaza kuambiwa kwamba vijiji karibu saba vinapewa hekta elfu mbili tu wakati mwekezaji mmoja anapewa hekta ishirini na nane elfu. Sasa swali langu la msingi nilikuwa nauliza.

Je, ni lini Serikali itakwenda pale kupima na kuwapatia wananchi eneo la kutosha ambalo halijajibiwa kwa sababu majibu haya ninayo karibu miaka yote. Sasa nilitaka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni kweli mko *serious* kweli kwenda kutenga maeneo hayo na kuwapatia wananchi wa Kihanga, Kishojo, Katanda, Mushabaiguru na Kibwera? Nataka nijue hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nimekuwa nikimwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi aende pale akazungumze na wananchi. Nilitaka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kama yuko tayari tuondoke wiki ijayo haya majibu akayatoe kwa wananchi hapo Kihanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Ndugu yangu Blandes.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimewahi kuwa Mkuu wa Wilaya katika Wilaya ya Karagwe na migogoro hii nilikuwa najaribu kushughulikia nikiwa mgeni sana katika Wilaya ile hata mimi nimeshangazwa kidogo kama huu mgogoro haujaishi tangu wakati huo mpaka leo.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi kifupi cha muda wetu tutakaokuwa madarakani kwanza nikuhakikishie kwamba tuko *serious* na mimi mwenyewe niko *serious* kwa sababu nilishafanya kazi katika Jimbo lako la Uchaguzi.

Lakini pia tuna maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tupitie upya kuangalia mashamba yote yaliyoko chini ya *NARCO* ili kuweza kuangalia ni namna gani maeneo ambayo yamekosa sifa au yanafanyakazi chini ya kiwango tuweze kurejesha kwa wafugaji wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Blandes kwamba tuna maelekezo hayo. Pia Waziri Mkuu ametoa maelekezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuangalia maeneo ya mashamba pori ambayo nayo hakuna hata ndege, hakuna digidigi, ili tuweze kufanya hiyo kazi ya kuwapa wafugaji maeneo hayo.

Lakini lingine nitamwomba tu Mheshimiwa niko tayari kwenda na wewe lakini ngoja kwanza tumalize. Tukishapitisha Bajeti yetu na tunaomba Waheshimiwa Wabunge wapitishe Bajeti ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ili tuweze kwenda kufanya kazi hizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 74

**Eneo kwa Ajili ya Wafugaji**

**MHE. MODESTUS D. KILUFI** aliuliza:-

Je, Serikali iko tayari kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wafugaji nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dockson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutekeleza Mipango ya Matumizi bora ya ardhi katika vijiji mbalimbali hapa nchini kadiri fedha inavyopatikana. Utengaji huo unafanywa kwa mujibu wa ibara ya 28(1)(a) ya Sheria ya Mipango ya matumizi ya ardhi Namba 6 ya Mwaka 2007 ambao inahitaji maeneo yanayofaa kutengwa hususan katika ardhi ya vijiji.

Katika kutekeleza Sheria hiyo hadi sasa jumla ya hekta 1,349,132.50 zimetengwa kwa ajili ya ufugaji katika vijiji 543, katika Wilaya 75 na katika Mikoa 21. Kati ya hekta hizo, hekta 41,027.81 ziko katika vijiji 18 vya Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya zoezi la uandaaji wa Mipango ya Matumizi bora ya ardhi Halmashauri zitaandaa Mipango ya kina na usimamizi wa maeneo itakayobainisha uwezo wa kila eneo kwa malisho, miundombinu iliyopo na inayohitajiwa na njia mbalimbali za kuyaboresha ili kuyaongezea tija kulingana na sura ya tatu ya Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Wanyama ya Mwaka 2010, Kifungu Namba 19.

Aidha ili uzalishaji wa maeneo haya uwe endelevu yatakamilishwa kwa wafugaji mmoja mmoja au kikundi ili kuboresha usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuandaa Mipango ya Matumizi bora ya ardhi katika vijiji vilivyobaki kama njia ya kuongezea tija kuifanya iwe endelevu na kupunguza migogoro. *(Makofi)*

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo nina maswali madogo ya nyongeza. Kwa vile kwa maeneo hayo yanayotajwa kuwa ya malisho katika vijiji sasa hivi hayapo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu.

Je, sasa Serikali iko tayari kuleta mipango kamili ya kutenga maeneo ya wafugaji kama vile inavyofanya kutenga maeneo ya wanyamapori.

Swali la pili, imetamkwa kwamba kuna vijiji 18 Wilayani Mbarali ambavyo vimetengewa maeneo ya malisho.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akataja vijiji hivyo ili niweze kufuatilia?

**NAIBU SPIKA:** Mbarali palivyobana vile Mheshimwia Kilufi, maeneo ya wafugaji yatatoka wapi pale. Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Kwa kuwa tuna maelekezo pia ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hizi *ranch* zina maeneo yote ambayo yanakaliwa na wafugaji tutafanya zoezi la kutosha kabisa na itakuwa ni mara moja baada ya kumaliza Bajeti hii tutaanza hiyo kazi.

Itakapofika mwezi wa saba, tutakuwa na kikao kikubwa cha wadau wa mifugo. Kikao hivcho kitakachofanyika huko Mwanza, ambapo tutakuwa tunawasilisha hizi taarifa. Kama alivyosema kwamba maeneo haya ya wafugaji nayo yatengwe yajulikane kama ambavyo mashamba ya wanyamapori yanavyojulikana na yanasimamiwa na sheria.

Lakini tatizo lingine ni kwamba haya maeneo tukishayabaini na kuyatenga kitakachofuata ni lazima kuyamilikisha kwa wafugaji ili yaweze kusimamiwa kisheria ili watu wasiendelee kuyavamia. Wafugaji nao wataacha kuhamahama kufuatilia mambo mengine hayo huko wanakokwenda.

Lakini jambo la mwisho, ni kwamba kuna orodha kabisa na nitampa hiyo orodha Mheshimiwa Mbunge ya maeneo katika jimbo lake yaliyotengwa na nitamwomba kwamba atakapomaliza Bunge hili aende kuhakikisha kama haya kwa jinsi ya taarifa tulizopata sisi kutoka kwa wataalam kama ni kweli yapo au hayapo ili tuweze kuingiza katika utaratibu mzima wa kuangalia maeneo ya wafugaji. *(Makofi)*

Na. 75

**Uratibu wa Masuala ya Diplomasia ya Uchumi**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Kitengo Mahsusi cha Uratibu wa Masuala ya Diplomasia ya Uchumi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Diplomasia ya Uchumi ni Sera Mtambuka na utekelezaji wake una lengo la kuvutia wawekezaji watalii, kutafuta masoko ya bidhaa yanayozailishwa nchini na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania.

Kwa ujumla ni sera inayohusisha kuchukua hatua madhubuti zinazohakikisha tunatetea, kulinda na kukuza maslahi ya kiuchumi ya nchi na wananchi wetu katika mahusiano yetu na nchi za nje na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara yangu, Uratibu wa Masuala ya Diplomosia ya Uchumi hufanywa na Idara ya Sera na Mipango chini ya mkurugenzi wa idara hiyo. Kwa upande wa balozi zetu utaratibu wa masuala ya diplomasia ya uchumi hufanywa na mabalozi kwenye maeneo yao ya uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu kubwa la Wizara ni uratibu wa sera hii inayosimamia maslahi yetu nje ya nchi, Wizara inadhani ni vyema ikaendelea na utaratibu

uliopo sasa chini ya idara ya sera na mipango. Hata hivyo, Wizara iko tayari kuongeza nguvu kazi kwenye idara hii ili kazi za uratibu ifanyike kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nina maswali mawili. Kwanza kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba ni jukumu la Wizara yake kuratibu na kusimamia sera hii.

Je, ni nini mafanikio katika kupunguza umaskini, kukuza ajira na kuongeza pato la Taifa?

La pili, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba balozi zetu na zenyewe zipo katika suala zima la kuratibu suala hili. Tunajua kabisa kwamba balozi zetu, mabalozi zetu ni vyeo vya kisiasa, ni vyeo vya heshima. Kwa hivyo basi, mabalozi wengi ambao wanateuliwa kuiwakilisha Tanzania wanakuwa hawana taaluma ya *economic diplomacy*.

Sasa kwa nini Wizara isianzishe kitengo hiki cha kuratibu masuala haya ya kiuchumi ili kuweza kuvutia wawekezaji mbalimbali katika sekta ya utalii na kukuza ajira na hivyo basi kufikia ule mkakati wa 2025 kwamba Tanzania iwe katika pato la kati.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu mafanikio ya kupunguza umaskini kukuza ajira na kuongeza pato la Taifa napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kadiri ambavyo Serikali inajitahidi kukuza mahusiano ya kiuchumi iwe na nchi kama Serikali au wawekezaji binafsi, basi hapo ajira zinapatikana na vijana wetu wa kike na wa kiume wanapata fursa hizo na mifano ipo.

Vijana wetu wengi wameingia kweye shughuli za ujasiriamali katika eneo la mawasiliano, uwakilishi wa kiuchumi na hiyo inatokana na utekelezaji mzuri wa sera hii ya demokrasia ya kiuchumi.

Kwa maana hiyo kipato kikiongezeka Mtanzania mmoja ni hivyo hivyo pato la Taifa linaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili katika uteuzi wa mabalozi ambayo ni ridhaa ya Mheshimiwa Rais anazingatia vigezo vingi wapo maafisa wa kibalozi ambao wamekuwa katika taaluma ya ubalozi wanapanda vyeo mpaka wanafikia ubalozi na hao ni wengi kuliko hao ambao wanatoka katika maeneo mengine.

Lakini hata wanaotoka katika maeneo mengine wanakuwa na utaalamu unaochangia suala la diplomisia ya kiuchumi ambayo sasa hivi siyo tu ni sera ya mambo ya nje. Tumeshuhudia hata hapa ndani ya Bunge wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wanafanya kazi hiyo kuunganisha majimbo yao na taasisi na nchi kwa ajili ya kukuza uhusiano wa kiuchumi.

Kuhusu kitengo hicho sasa kuwa kazi yake kuratibu, kama tulivyokwishajibu katika jibu letu la msingi ni kwamba idara ya mipango na sera inashughulikia suala hilo na tunao mpango wa kuongeza nguvu ili wale watakaokuweko pale waweze kuendelea kuratibu na kila mtu achukue nafasi yake katika kukuza sera hii ya diplomosia ya kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri nawashukuru wote waliouliza maswali na Waheshimiwa Mawaziri katika majibu yenu nawashukuru sana. Sasa wageni, tunaanza mgeni ambaye yuko kwenye gallery ya Spika, naye ni Mbunge wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Angelina Kiziga. Ahsante sana, karibu sana. Tunakupongeza sana wewe na wenzako kwa kazi nzuri mnayofanya kwenye Bunge la Afrika Mashariki, katika kutuwakilisha

huko, japo hatujui hii kanyanga inayoendelea huko, sijui mtaendeleaje kesho kutwa. Kuna shughuli ya kumwondoa Spika kule. *(Makofi/Kicheko)*

'

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanafunzi wa kutoka *UDOM* karibuni sana, tunawakaribisha sana hapa Bungeni, mjifunze mpate kuelewa namna mambo yanayofanyiwa kazi katika Bunge.

Tunaomba muwe na juhudi zaidi katika masomo najua ningewauliza swali mngesema bumu bado. Kwa hiyo, nimwambie tu Naibu Waziri wa Fedha namwona hapa, wanafunzi wanasema bumu hawajapata. Ahsante sana kaeni tu. *(Makofi)*

Wanafunzi 150, kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii, *TRACDI* nadhani Tengeru, wale wa Maendeleo ya Jamii ahsante sana na karibu sana Dodoma. Karibuni mjifunze namna Bunge linavyofanya shughuli zake. Wanafunzi wanane wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tawi la *Dodoma Computer Center,* karibuni sana ninyi mpo hapa hapa karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo la kazi, kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria na Utawala, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anaomba wajumbe wa Kamati yake Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala ikutane saa saba mchana katika ukumbi namba 229 ghorofa ya tisa jengo la Utawala.

Baada ya matangazo hayo sasa nadhani inabidi tuendelee. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2014/2015 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**NAIBU SPIKA:** Nilipata ombi maalum kabla ya Majadiliano kuendelea na Mheshimiwa Mbatia kwa muda mfupi sana tafadhali.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, nimesimama hapa kwa niaba ya Kambi Rasmi Bungeni kwa hali ya sitofahamu ambayo ilitokea humu ndani ya Bunge jana, kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wenzetu kutoka Zanzibar ikaunganisha kambi yote rasmi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kukuhakikishia wewe na Watanzania kwamba tunaamini katika mfumo wetu wa Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika na hatuna mgogoro wowote.

*Debate* iliyoko ni muundo wa Muungano na Wazanzibar walioko humu ndani, wana haki kwa mujibu wa katiba kuwemo humu ndani na wana haki ya kujibiwa maswali kama Wabunge kwa mujibu wa Katiba. Kwa kuwa ni jambo la kiuungwana na sisi humu ndani asubuhi ya leo tumeanza kwa dua na hasa pale tuliposema Mwenyezi Mungu atujalie hekima na busara kufanya maamuzi sahihi.

Jana Mheshimiwa Jaji Werema aliomba radhi kwa kuteleza kwa kauli yake aliyoitoa humu ndani tunataka kumhakikishia Jaji Werema na Bunge lako Tukufu kwamba sisi ni waungwana na tumeridhia ombi lake la kutekeleza kwa kauli aliyoita na iwe ni changamoto basi kwetu sisi wengine tuliomo humu ndani kutokuonyeshana siasa za kibabe za jino kwa jino. Siasa ambazo zinaleta maudhi ambayo zinaweza zikasababisha kuvunjika kwa amani ya Bungeni letu na umoja ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaaswa na leo ni siku ya Ijumaa Mtume Mohamed *Swalallah Alayh Wasalaam* anatuambia kwamba ukiona uovu unatendeka zuia, ukishindwa kuzuia kemea, ukishindwa kukemea onyesha basi hata chuki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kilichofanyika jana tulionyesha chuki zetu kutokana na yaliyotokea. Lakini kwa kuwa tumeaswa tuweze tukaridhiana tumefanya hivyo. Sisi tuwahakikishie kwa moyo wa dhati kuna kweli kila mtu akitoa kauli ana haki ya kujibiwa lakini kuna wengine viongozi wengine wenye uzoefu wengine wana miaka mitatu, minne katika Bunge lakini wengine wana uzoefu sasa wakianza basi watumie uzoefu wao kuonyesha *leadership* lakini Biblia Takatifu Wagalatia 5.26 inasema: Tusijisifu bure kwa kuchokozana na kuhusudiana. *(Makofi)*

Sasa ili Bunge lako Tukufu na hasa kiti chako tukiombe kiwe kinasimamia haki, kwa kuwa haki ndiyo msingi mkuu wa amani. Ukisimamia haki jitahidi hata kama una mapenzi na upande fulani lakini haki ikitendwa na kiti hicho tunakuhakikishia kwamba Bunge hili litafanya majukumu yake kwa amani na utulivu bila kuegemea upande wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe, nisichukue muda mrefu kusema kwamba Mathayo 5:10 inasema: Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki maana ufalme wa mbinguni ni wao. Ukweli utatuweka huru na sisi leo kwa kuwa ni Ijumaa tunaamini tutashiriki na kuna mjadala wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara hii ni nyeti sana tutashiriki bega kwa bega ili nafasi ya Bunge Tukufu kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63 tuweze tukafanya wajibu wetu ili Taifa letu liendelee kuwa la amani na utulivu. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru kwa kuongea kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Naamini yaliyopita yamepita tulishaomba radhi, tuendelee na kazi yetu ambayo imetuweka hapa Dodoma. Sasa moja kwa moja naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, iliyopitia Wizara ya Mambo ya Nchi, Makadirio yake. Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, karibu endelea. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI NA ULINZI NA USALAM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) pamoja na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Aprili, 2013 sasa kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato kwa Matumizi kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mathias Chikawe na wasaidizi wake tarehe 1 Mei, 2014 na tarehe 2 Mei, 2014 na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mipango wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa mafungu matano ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Fungu 14 - Kikosi cha Zima Moto na Uokoaji;

Fungu 28 - Jeshi la Polisi;

Fungu 29 - Jeshi la Magereza;

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mehsimiwa Naibu Spika, Kamati ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 katika ziara hiyo Kamati ilibaini kwamba kwa kiasi kikubwa fedha za miradi hazikutolewa kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa ushauri wa Kamati, wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2013/2014 Kamati yangu ilitoa ushauri na maoni mbalimbali kwa Wizara hii kwa lengo la kufanikisha malengo ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyotoa kwa Kamati inaonyesha kwamba kwa kiasi kikubwa Wizara imezingatia ushauri wa Kamati japo kwa viwango tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya huduma kwa jamii namba sita mwaka 2012 waharifu wa makosa madogo madogo wanaohukumiwa kifungo kisichozidi miaka mitatu wanatakia kutumikia adhabu hiyo nje ya magereza wakitumikia jamii. Lakini sheria hii inafanya kazi mikoa 18 naomba Hansard isahihishe ni 18 tu hivyo Kamati ilishauri Serikali itenge fedha za kutosha ili sheria hii ifanye kazi katika mikoa yote ya Tanzania Bara, kwa lengo kwa kupunguza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Serikali imeeleza kwamba ushauri huu umezingatiwa katika Bajeti ya 2014/2015 ambapo kasma hii imeongezwa kutoka shilingi bilioni 215 hadi shilingi bilioni 777 na kwamba kiwango hiki kitaongezwa kila mwaka ili kukidhi mahitaji.

Pili, Serikali ilishauriwa itekeleze kwa dhati Sheria ya Huduma kwa Jamii na Sheria ya *Parole* inayotoa nafasi kwa wahalifu kutumikia adhabu za vifungo nje ya Magereza ili kupunguza gharama za kuwatunza wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kwamba Sheria ya Huduma kwa Jamii Namba 6 ya Mwaka 2002 na ya *Parole* zimetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha, kwani katika kipindi hiki jumla ya wahalifu 1,118 walipata adhabu ya vifungo vya nje chini ya Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia Sura namba 247. Aidha, wafungwa 784 walimaliza adhabu zao kupitia Sheria hizi.

Tatu, Kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza kiwango cha posho ya chakula kwa Askari kufikia angalau Shilingi 7,500/= kwa siku kutoka shilingi 5,000/= za sasa.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Serikali ni kwamba, Wizara imekamilisha taratibu za kuomba nyongeza hii ya posho na kuwasilisha mapendekezo hayo Tume ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi kabla ya kuwasilishwa Hazina.

Nne, kwamba, kasma iliyotengwa kwa ajili ya chakula cha wafungwa Magerezani ni wastani wa shilingi 500/= tu kwa siku kwa mtu mmoja, Kamati iliona kiasi hiki ni kidogo mno hivyo kiongezwe kifikie walau shilingi 3,000/= kwa siku.

Mheshimwa Spika, maelezo ya Serikali ni kwamba katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 kiwango kilibaki kile kile cha shilingi 500/= kwa siku kutokana na ufinyu wa Bajeti na kwamba hali hii itakuwa hivyo hivyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Tano, Kamati ilishauri kwamba Serikali iharakishe mchakato wa kuleta Bungeni marekebisho ya Sheria ya *Parole* Namba 25 ya Mwaka 2002, ili kupanua wigo wa kuwanufaisha wafungwa wengi zaidi watakaoo timiza vigezo na masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali imeeleza kwamba imekwishafanyika tathmini na uchambuzi katika Magereza yote nchini kuhusu namna ya kupanua wigo wa kuwawezesha wafungwa wengi zaidi kunufaika na Sheria hii. Hatua itakayofuata ni kuitisha vikao vya pamoja vya wadau ili kupata maoni yao na hatimaye kuandaa Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ambao utawasilishwa Bungeni kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili Jeshi la Polisi liweze kutekeleza majukumu yake ya kulinda maisha na mali za wananchi kwa ufanisi linahitaji kuwezeshwa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Wizara zimeeleza kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa na Serikali kuliwezesha Jeshi la Polisi kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi mkubwa. Hatua hizo ni pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kulipatia Jeshi hili zana za kazi. Aidha, kwa mwaka 2013/2014, pamoja na bajeti iliyopendekezwa awali, baadaye Jeshi hili liliongezewa shilingi bilioni 33.8 /= kwa ajili ya kununua zana na vitendea kazi. Katika Bajeti ya 2014/2015, Serikali haikuongeza Bajeti ya Jeshi hili katika Kasma ya Matumizi ya Kawaida isipokuwa imeongeza fedha katika Matumizi ya Maendeleo.

Mbili, kwamba Serikali iandae Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa wananchi wanaotaka kufanya maandamano. Kamati ilipendekeza kwamba utaratibu huo uainishe siku ya kuandamana, maeneo mahsusi ya kukusanyika, na muda wa kuandamana ili yeyote anayependa kufanya hivyo, atekeleze haki yake hiyo pasipo kuingilia uhuru wa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Serikali ni kwamba umefanyika uchambuzi kuhusu suala hili na imejiridhisha kuwa utaratibu uliopo bado unafaa, kwani maandamano yote yanaratibiwa kwa kutumia Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuiongezea fedha za Bajeti Idara hii, ili kuijengea uwezo wa kukabiliana na tatizo la wahamiaji haramu. Njia mojawapo kwa Serikali kuongeza Bajeti ya Idara hii ni kuirejeshea gawio yaani *retention* la 61% kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa maelezo kwamba hatua zimechukuliwa za kufikisha Hazina ombi la nyongeza ya Bajeti kwa Idara hii, lakini mafanikio hayakupatikana kwani katika bajeti ya 2014/2015 kiwango cha gawio kwa Idara hii hakikuongezwa.

Mbili, kwamba, ili kukamilisha zoezi la kutoa vitambulisho vya Taifa, kabla ya mwaka 2015, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza fedha kwa Mamlaka ya Kutengeneza Vitambulisho yaani *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015, fedha kwa ajili ya zoezi hili zimeongezwa kutoka shilingi bilioni 151.2 za 2013/2014 hadi shilingi bilioni 160.

Mheshimiwa Spika, Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji. Kwamba, Serikali irudishe gawio la awali la asilimia 70 ili zipatikane fedha za kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Zimamoto na pia kununua zana za kuzimia moto na za uokoaji.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya Wizara ni kwamba yamefanyika mawasiliano ya barua na ya vikao vya pamoja baina ya Wizara hii na Hazina ili kujadili suala hili lakini hadi sasa mafanikio hayajapatikana.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Kabla ya kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa

fedha 2014/2015, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ili kujiridhisha kama fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Wakati wa kupitia Taarifa hiyo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilizingatia mambo yafuatayo:-

Moja, uwiano kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na matumizi yaliyofanyika katika kutekeleza malengo ya Bajeti ya Wizara hii;

Mbili, uhusiano kati ya dhima na dhamira ya Wizara hii na malengo ya bajeti yalivyotekelezwa; na

Tatu, uwiano wa fedha zilizopokelewa kutoka Hazina dhidi ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ulionesha kuwa baadhi ya Taasisi hazikuwa na mwelekeo wa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kama ilivyopangwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kwa mfano, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu ya kipindi cha Bajeti, tarehe 31 Machi, 2013, katika Fungu 29 – Jeshi la Magereza ni asilimia 12 tu ya lengo la makusanyo lilikuwa limefikiwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya  sababu za makusanyo ya mapato kuwa kidogo ni kutokana na kutokamilika kwa mikataba ya baadhi ya malipo kutokana na Taasisi husika kutopokea fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni ukosefu wa nyenzo, mafunzo na vitendea kazi muhimu na vya kisasa. Ni maoni ya Kamati kuwa sababu hizo zikifanyiwa kazi, ukusanyaji wa mapato utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina. Kwa kuzingatia kuwa Bunge kuidhinisha pesa ni suala moja na upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina ni jambo lingine, Kamati ilichambua mtiririko wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa Wizara ya Mambo hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 741,131,000,000/= kwa Wizara hii pamoja na asasi zilizo chini yake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, kiasi cha fedha kilichopokelewa ni jumla ya shilingi bilioni 497,876,000,000/= sawa na asilimia sitini na saba (67%) ya Bajeti iliyoidhinishwa. Pamoja na fedha kutoka Hazina kutofika zote na kwa wakati, Wizara imeweza kutekeleza baadhi ya majukumu yake kama ambavyo walipanga.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Malengo na Kazi za Wizara kufikia tarehe 31 Machi, 2014. Kamati ilipewa taarifa kwamba, Wizara ilifanikiwa kutekeleza kwa viwango tofauti malengo pamoja na kazi zake kupitia idara pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Baadhi ya shughuli zilizofanyika katika kipindi hiki ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Moja, Makao Makuu ya Wizara. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, imeendelea na uchambuzi na tathmini kwa wakimbizi ili kubaini iwapo wapo ambao wana sababu za msingi za kuendelea kuishi nchini. Hadi tarehe 31 Machi, 2014 walikuwepo wakimbizi 97,783 kutoka nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Somalia:-

Wizara imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wakimbizi katika makambi na makazi ya wakimbizi ya Nyarugusu, Mishamo, Katumba na Ulyankulu. Aidha kambi la Chogo limefungwa mwezi Februari, 2014,

Wizara imeendelea na vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa kudhibiti wahusika na pia kuwachukulia hatua mbalimbali za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Operesheni maalum zilifanyika kwa malengo ya kukabiliana na matishio ya amani, kurejesha amani, kuzuia na kudhibiti vitendo vya uhalifu pamoja na vitendo vya vurugu na uvunjifu wa amani kwa sababu mbalimbali.

Uhamasishaji wa wananchi kuhusu shughuli za Polisi Jamii ulifanyika katika mikoa, wilaya, tarafa na kata mbalimbali na Ukaguzi na doria za usalama barabarani zenye lengo la kudhibiti madereva wanaokiuka Sheria za usalama barabarani zilifanyika.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji namba 14 ya Mwaka 2007 umefanyika. Pili, Mafunzo ya kujenga uwezo na kuboresha utendaji kazi kwa maofisa na watumishi mbalimbali wa Jeshi la Zimamoto yamefanyika na tatu, Ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto umefanyika katika mikoa mbalimbali nchini.

1.Ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya magereza umefanyika katika baadhi ya magereza ya mikoa na wilaya nchini;

2. huduma za uangalizi, ulinzi na marekebisho ya tabia kwa wafungwa imeendelea kutolewa kwa wafungwa wote nchini; na

3. kuendeshwa kwa mafunzo ndani ya vyuo vya Jeshi la Magereza kwa maafisa na askari wapya na wa zamani wa vyeo mbalimbali pamoja na watumishi walio nje ya vyuo vya jeshi.

Mheshimiwa Spika, Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*.

1. Idara ya Uhamiaji imewakamata na kuwachukulia hatua mbalimbali za kisheria wahamiaji haramu na wakazi wageni wasio na nyaraka stahili;

2. Huduma na nyaraka mbalimbali za uhamiaji, uraia na Hati za kusafiri zimetolewa kwa wageni na raia wenye mahitaji ya huduma hizi;

3. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* imekamilisha zoezi la utambuzi, usajili na utengenezaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa Watumishi wa Serikali kwa Zanzibar na Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini; na

4. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* imeanza hatua za awali za ujenzi wa kituo cha utunzaji wa kumbukumbu *(Data Centre*), kituo cha uokozi wakati wa majanga (*Disaster Recovery Site*) na ujenzi wa baadhi ya Ofisi ya Usajili na Utambuzi katika Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zifuatazo zilikwamisha baadhi ya malengo ya Wizara kama ifuatavyo:-

1. Upungufu wa rasilimali watu katika idara na taasisi mbalimbali za Wizara;

2. Mtiririko wa fedha kutoka Hazina kutoendana na mahitaji halisi ya Mpango Kazi wa Wizara na Taasisi zake;

3. Ongezeko la matumizi ya teknolojia ya kisasa katika mbinu za uhalifu; na

4. Upungufu wa vifaa vya kuchukulia alama za kibailojia yaani Mobile Enrolment Unit – (MEU) katika Mradi wa Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Randama za Wizara zinaonyesha kuwa, jumla ya shilingi bilioni 665,093,488,000/= zinaombwa kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 216,646,800,000/= fedha za maendeleo kwa mgawanyo ufuatao:-

(a) Fungu 14 – Kikosi cha Zimamoto na UokoaJumla ya Fedha zinazoombwa ni shs. 26,503,375,000/=;

(b) Fungu 28 – Jeshi la Polisi: Jumla ya Fedha zinazoombwa ni Sh.409, 628,142,000/=;

(c) Fungu 29 – Jeshi la Magereza: Jumla ya Fedha zinazoombwa ni Sh. 151,164,544,800/=;

(d) Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi: Jumla ya Fedha zinazoombwa ni Sh. 14,346,014,000/=;

(e) Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji na *NIDA:* Jumla ya Fedha zinazoombwa ni sh. 280,098,216,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia makadirio hayo na kubaini kuwa asilimia 71 ya makadirio inahusu gharama za uendeshaji lakini maendeleo yamekadiriwa kwa asilimia 29 ya Bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Baada ya kueleza uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2013/2014 pamoja na Makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 204/2015, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Mafungu yote matano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji. Fedha za Miradi ya Maendeleo. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halijatengewa fedha za miradi ya maendeleo kwa muda wa miaka minne mfululizo. Ukosefu wa fedha za maendeleo umesababisha miradi mingi kukwama. Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ili waweze kukamilisha miradi yao waliyoianza.

Mheshimiwa Spika, mbili, Ununuzi wa Vitendea Kazi. Kikosi cha Zimamoto kina upungufu mkubwa wa vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, mfano magari ya kuzimia moto na vifaa vya kisasa vya mawasiliano. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kikosi hiki kinapatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na vya uokoaji ili kikosi kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi badala ya kuwa watazamaji kila yanapotokea majanga.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kusitisha Miito ya Uongo. Kamati inakemea tabia ya baadhi ya Wananchi wenye tabia ya kupiga simu za uongo kuita Kikosi cha Zimamoto. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka na kukomesha tabia hii na kununua mitambo ya mawasiliano ya kisasa itakayoweza kuwabaini watu wenye tabia hizi ili waweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi na Vitendo vya uhalifu dhidi ya Polisi. Kamati imesikitishwa na baadhi ya Watanzania kuwashambulia Askari wawapo kazini. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma ili wawatambue Polisi kuwa ni walinzi wao wa amani na waache kuwashambulia Polisi.

Mheshimiwa Spika, mbili, Kukamatwa kwa watuhumiwa waliotenda makosa yaliyovuta hisia za Watanzania. Kumekuwa na vitendo vya uhalifu, kwa mfano, kuwamwagia watu tindikali wakiwemo viongozi wa dini, ulipuaji wa mabomu katika nyumba za ibada na mauaji ya viongozi wa dini kwa silaha za moto. Kamati inasikitishwa na kasi ndogo ya upelelezi wa matukio haya, Kamati inazidi kusisitiza Serikali kuwakamata watu waliohusika na matukio haya ya uhalifu na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, tatu, Adhabu Kali kwa Wanaosababisha Ajali. Kwa kuwa Watanzania wengi wamekuwa wanapoteza maisha kutokana na ajali zinazo sababishwa na uzembe wa madereva wa vyombo vya usafiri. Kumekuwa na malalamiko kuwa baadhi ya madereva huendesha magari wakiwa wamelewa.

Kamati inashauri kuwa Sheria zifanyiwe marekebisho ili wale wote wanaosababisha ajali kutokana na uzembe wapewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, Adhabu kwa Polisi Wanaopokea rushwa. Kamati inazidi kukemea tabia ya baadhi ya Polisi wanaodai na kupokea rushwa. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka na za kisheria dhidi ya Polisi wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Vitendea Kazi. Kwa kuwa Jeshi la polisi linafanya kazi kubwa ya ulinzi wa maisha ya watu na mali zao, linahitaji magari, pikipiki na boti kwa ajili ya kufanya doria. Vyombo vya usafiri vilivyopo vimechakaa na hii inafanya kazi za doria kuwa ngumu. Kamati inashauri Serikali kuwa na mkakati endelevu wa kununua vitendea kazi kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza . Madeni ya Wazabuni na Watumishi. Kamati inasikitishwa kwa uwepo wa madeni ambayo yameshahakikiwa lakini mpaka sasa hayajalipwa. Kufikia Mwaka 2012, madeni ya watumishi yaliyohakikiwa lakini hayajalipwa ni Shilingi bilioni 10,659,463,515/= na madeni ya wazabuni yaliyohakikiwa na kutolipwa ni shilingi bilioni 16,442,569,915/=.

Mheshimiwa Spika, kutolipwa kwa fedha hizi kunasababisha utoaji wa huduma kusitishwa katika Magereza yetu na malalamiko miongoni mwa Askari wetu kuongezeka. Kamati inazidi kuisisitizia Serikali kutenga fedha ili kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Spika, Ununuzi wa Magari. Kati ya Magereza 126 yaliyopo nchini ni Magereza 56 tu ndiyo yenye magari. Kwa kuwa kuna umuhimu wa kuwa na magari kwa ajili ya kuwasafirisha wafungwa na mahabusu kwenda mahakamani, mahospitali na shughuli nyingine za kiutawala, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua magari walau moja kwa kila gereza.

Mheshimiwa Spika, Bajeti Ndogo ya Chakula cha Wafungwa. Kamati imesikitishwa na Serikali kutozingatia ushauri uliotolewa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwamba Bajeti ya chakula cha wafungwa magerezani iongezwe kutoka wastani wa shilingi 500/= kwa siku kwa mtu mmoja hadi walau shilingi 3,000/= kwa siku kwa milo mitatu.

Mheshimiwa Spika, kibinadamu sio sahihi kumlisha mtu kwa shilingi 500/= kwa siku kwa milo mitatu, hivyo Kamati inazidi kuishauri Serikali iongeze Bajeti ya chakula kwa wafungwa iwe wastani wa shilingi 3,000/= kwa siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tatizo sugu la msongamano Magerezani. Kamati inazidi kuishauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo ili kukabiliana na tatizo la msongamano mkubwa magerezani. 1. Sheria ya *Community Service* itumike katika Mikoa yote badala ya Mikoa 18 ya sasa; 2. Sheria ya *Parole* itazamwe upya ili kupanua wigo na hivyo wafungwa wengi zaidi wanufaike; 3. Kamati za kusukuma kesi za ngazi za Wilaya na Mikoa zifanye kazi ya kutembelea magereza na mahakamani ili kusukuma kesi zimalizike haraka; na 4. Wahamiaji haramu warudishwe kwenye nchi zao badala ya kujaza magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji na *NIDA*. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *NIDA* walitengewa kiasi cha shilingi bilioni 151, hata hivyo fedha hizo hazikutolewa zote na Hazina kwani hadi mwezi Machi, 2014 ni shilingi bilioni 35 ndizo zilikuwa zimepokelewa. Kamati inaishauri Serikali kwamba, fedha zilizobaki zitolewe mapema kwani upungufu huu wa fedha utasababisha utoaji wa vitambulisho kutokamilika katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, Ushauri wa Jumla kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi – Fungu 51. Upungufu wa Posho ya Chakula kwa Askari. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Kamati ilishauri kwamba posho ya chakula kwa askari wote chini ya Wizara hii iongezwe kutoka shilingi 5,000/= mpaka shilingi 7,500/=. Hata hivyo pesa hivyo pesa hiyo haikuongezwa na badala yake imebaki kuwa shilingi 5,000/= kwa siku. Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kuwa shilingi 5,000/= kwa siku ni ndogo kwa kuzingatia gharama halisi ya chakula na aina ya kazi wanazofanya. Usajili wa Asasi za Kiraia. Hivi sasa kumezuka uanzishaji wa utitiri wa asasi za kiraia. Kamati inashauri Serikali iwe makini inaposajili asasi hizo na hasa madhehebu ya dini.

Hitimisho. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii inayo ongonzwa na Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa mara ambao umekuwa ukiisaidia Wizara hii kufanya maboresho ya utendaji kazi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa, Anna M. Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Muhammed Seif Khatib. Wajumbe Wa Kamati ni Mheshimiwa Brig. Jen. (Mst.) Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Kapt. (Mst.) John Z. Chiligati, Mheshimiwa, Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa, Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa, Dkt. Donald M. Malole, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mheshimiwa, Rahel Mashishanga Robert, Mheshimiwa Hamad Ali Hamadi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Vincent Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Charles Mloka, Ndugu Theonest Ruhilabake na Ndugu Nesta Kawamala kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi taarifa hii ilipoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hilda Ngoye, Msemaji wa Kamati, kwa niaba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, tunakushukuru sana kwa kusoma vizuri. *(Makofi)*

Sasa moja kwa moja naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naye siyo mwingine ni Mheshimiwa Godbless Lema. Mheshimiwa Lema, tafadhali! *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ninaomba kuwasilisha Bungeni, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *Instrument* ya Serikali inayoainisha majukumu ya kila Wizara, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepewa majukumu ya kushughulikia masuala ya Usalama wa Raia, Uhamiaji na utekelezaji wa Sera za Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama majukumu ya Wizara hii, utaona kwamba, ina majukumu mazito sana yanayohusu usalama wetu sote kama raia wa nchi hii, ni majukumu yanayohusu maisha yetu. Hivyo, Wizara hii inatakiwa iwezeshwe sana kibajeti iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili Wananchi na hata wageni waliopo katika nchi yetu waweze kuishi kwa usalama na amani. Kwa kuwa Wizara hii ina taasisi chini yake zinazohusika na ulinzi wa maisha ya watu na mali zao, hivyo ni Wizara inayotakiwa kufuatiliwa na kusimamiwa kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika wa 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kufanya mambo kadhaa ili kuboresha upungufu tuliouona katika kipindi hicho. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuchukua hatua kali na madhubuti ya kukabiliana na matukio yenye sura ya ugaidi; kwa mfano, kulipuliwa kwa bomu Kanisa Katoliki katika Parokia ya Olasiti huko Arusha, kuchomwa moto kwa makanisa huko Zanzibar na Dar es Salaam, Mapadri kuuwawa na Masheikh kumwagiwa tindikali Arusha na Zanzibar na matukio yanayofanana na hayo. *(Makofi)*

(ii) Kuongeza posho ya chakula *(Ration Allowance)* kwa Askari wa Jeshi la Polisi ili walau posho hiyo ishabihiane na posho ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ili waweze kukabiliana na ugumu wa maisha. Kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*), Waziri wa Fedha wa wakati huo, Marehemu William Mgimwa, alikubali posho ya chakula ya shilingi 225,000/= kwa mwezi kwa kila askari. Taarifa tulizonazo ni kwamba, posho hiyo haijalipwa mpaka leo. Je, askari waandike deni au waandike kwamba wamedhulumiwa? *(Makofi)*

(iii) Kutoa mwongozo kwa Maafisa wa Jeshil la Polisi na Magereza juu ya marekebisho ya sheria kuhusu umri wao wa kustaafu, ambapo marekebisho ya sheria yaliongeza umri wa kustaafu kutoka miaka 50 kwenda miaka 55 kwa Maafisa wa Polisi na kutoka miaka 55 kwenda miaka 60 kwa askari wa Magereza.

(iv) Kujenga nyumba za Askari wa Magereza ili kuboresha mazingira yao ya kazi na kuwafanya wasijisikie kama vile na wao ni wafungwa.

(v) Kuchukua hatua ya kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani.

(vi) Kuboresha lishe na huduma za afya kwa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.

(vii) Kuongeza fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokoaji kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

(viii) Kuacha kulitumia Jeshi la Polisi vibaya kwa ajili ya kulinda masilahi ya kisiasa ya Chama cha Mapinduzi.

(ix) Kuwachukulia hatua kali za kisheria Viongozi wa Jeshi la Polisi na Viongozi wa Serikali waliotoa kauli za vitisho kwa waandishi wa habari walioandika habari za unyanyasaji unaofanywa na Jeshi la Polisi.

(x) Kutoa ukomo wa muda ambapo kila raia wa Tanzania atapatiwa Kitambulisho chake cha Taifa na kuainisha gharama zilizotumika katika mchakato wa kutengeneza Vitambulisho vya Taifa.

(xi) Kudhibiti kuzagaa kwa silaha za moto ambazo hutumika katika matukio mengi ya kijambazi.

(xii) Kuchukua hatua kali kwa watu wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya hapa nchini.

(xiii) Kuchukua hatua madhubuti za kupunguza matukio ya ajali barabarani ambayo yamepoteza maisha ya Wananchi wengi sana wakiwemo polisi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa taarifa ya utekelezaji wa masuala niliyoyataja hivi punde wakati wa majumuisho ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Randama ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi - Fungu 51 na Randama za Taasisi zilizoko chini yake, yaani Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Fungu 29 – Jeshi la Magereza na Fungu 14 - Idara ya Zimamoto, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Wizara na taasisi zilipata mgawo wake wa kibajeti kwa wastani wa asilimia 70 isipokuwa Idara ya Zimamoto na Uokoaji, ambayo ilipata asilimia 46.3 tu ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, kwa mujibu wa Randama ya Jeshi la Zimamoto - Fungu 14, ukurasa wa pili, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014, hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Randama hiyo, huu ni mwaka wa tatu mfululizo kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutotengewa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kutokana na hali hiyo, Jeshi hilo limeshindwa kuendeleza ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu – *TAZARA*, Dar es Salaam, kushindwa kukarabati na kujenga vituo vipya vya zimamoto, kushindwa kununua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo vifaa vya maokozi na vifaa vya kuzimia moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini imeendelea kuwa tete kutokana na sababu mbalimbali. Utafiti wa kiufuatiliaji uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba; sababu zifuatazo zinazorotesha hali ya usalama na amani hapa nchini:-

- Ukosefu wa ajira na kazi zenye kipato kwa jamii. Ukosefu wa kazi na ajira kwa Jamii umekuwa ni sababu mojawapo ya msingi kabisa ya kuendelea kuhatarisha hali ya usalama na amani nchini. Wananchi wengi hususan Vijana, wamekuwa hawana uhakika wa ajira. Mbali na hofu na wasiwasi mkubwa walio nao, vijana hawa kutokana na kutojua hatima ya maisha yao, bado Serikali imeendelea kuwasakama katika shughuli zao ndogo ndogo. Kitendo cha Serikali kuwafukuza mijini Vijana wajasiriamali wanaofanya biashara ndogondogo, kimesababisha Vijana hawa kushindwa kabisa kumudu hata mlo mmoja kwa siku. Jambo hili limewakatisha tamaa Vijana wengi na matokeo yake ni kwamba, baadhi yao wanajiingiza katika matukio ya kihalifu ili waweze kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga mazingira ya usalama, amani na utulivu katika nchi yetu, ni lazima sasa Serikali itambue wajibu wake wa kukuza uchumi na biashara kwa kasi ili kuongeza ajira na kazi zenye tija kwa jamii, kwani kuachia Jeshi la Polisi kudhibiti hali ya ulinzi na usalama katika Taifa ambalo takribani asilimia 80 ya Vijana wake wanarandaranda mitaani bila kuwa na kazi zenye uwezo wa kukidhi mahitaji yao muhimu ni hatari kubwa siyo tu kwa walinzi hawa wa amani, bali pia kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu tukafahamu kwamba, propaganda na tathmini feki kuhusu ukuaji wa uchumi zinazotolewa kila mwaka na Serikali wakati watu wengi wanaendelea kuishi maisha yasiyo na matumaini na wengine wakishindwa kufurahia ajira na kazi kwa sababu ya masilahi duni na mfumuko wa bei za bidhaa unaosababishwa na uchumi kushuka kila mwaka; bila shaka sasa ni kweli kabisa kuwa hali ya usalama Tanzania ni tete na Jeshi la Polisi haliwezi kujipanga kushindana na kundi kubwa la jamii iliyojaa hasira na kupoteza matumaini ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto ni miongoni mwa kundi katika jamii ambalo linaishi maisha ya umaskini wa kupindukia sana. Nyumba zao, mishahara yao na masilahi yao mengine mbalimbali bado ni duni kiasi kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa ni kebehi na dharau kubwa sana kwa Vikosi vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Jeshi ni wito, ni hatari kubwa sana kuwa na Askari ambao wanafanya kazi bila wito, kwa sababu walikosa matumaini kwingineko, hivyo wakachagua kujiunga na Jeshi kama sehemu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, Askari wengi wanafanya kazi kwa moyo uliovunjika na kupondeka. Aidha, wana msongo mkubwa wa mawazo kwa sababu ya ugumu wa maisha. Hali hii inaondoa uimara wa Majeshi yetu haya kwani Jeshi imara siyo tu kuwa na silaha za kisasa peke yake bali ni muhimu pia kuwa na askari wanaoona fahari kulinda raia na mali zao kama wajibu uliotukuka. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutambua na kuthamini kazi inayofanywa na askari wetu ambao ni sehemu ndogo ya jamii iliyojitoa mhanga kufanya kazi za hatari hata kwa maisha yao ili kuwalinda raia na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limekuwa likitajwa kuwa kinara wa rushwa na chanzo cha biashara nyingi haramu. Jambo hili siyo zuri hata kidogo kwa chombo kilichokabidhiwa jukumu la kuwalinda raia na mali zao. Hata hivyo, tafiti nyingi zinaonesha kwamba, mazingira mabaya ya maisha yao yaliyojengwa katika masilahi duni ni miongoni mwa sababu zinazowasababishia kuingia katika tabia hii mbaya ambayo ni hatari kwa usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ndani ya Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama ni majaribu yanayosababishwa na Serikali yetu. Hii ni kwa sababu mishahara na makazi ya askari wetu ni duni, vitendea kazi vichache na duni, jambo linalochangia kwa kiasi kikubwa kuwa na askari wasio na ari na shauku ya kazi ya ulinzi na usalama. Matokeo yake wanakosa nidhamu ya kazi na hivyo kujiingiza kwenye vitendo viovu ikiwemo rushwa na unyanyasaji wa raia.

Ili kuwa na askari wenye nidhamu ya kazi, ni lazima kuwa na Serikali inayojua na kuthamini wajibu mkubwa wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama katika Taifa. Kama ambavyo Serikali inatoa mishahara mikubwa kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Benki Kuu na Wabunge, ili kuwapa motisha wasiibe, vivyo hivyo ingeona umuhimu wa kuwalipa na kuwatunza vyema Askari wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kwa kuwa na askari wanaofanya kazi kwa moyo uliopondeka ni hatari kwa ukuaji wa uchumi na usitawi wa Wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kupuuza masilahi mbalimbali ya askari wetu ni kuwaingiza katika majaribu mbalimbali ikiwemo rushwa, ukandamizaji na unyanyasaji dhidi ya raia wanaopaswa kuwalinda. Ifahamike kwamba, kuwaingiza watu majaribuni ni dhambi. Aidha, majaribu ya kumfanya mtu atende jambo baya yanahesabika kuwa ni dhambi. Katika muktadha huu, hata Bwana Yesu alipokuwa akiwafundisha wanafunzi wake kusali, aliwaambia wamwombe Mungu wakisema "Usitutie majaribuni bali utuokoe na yule mwovu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, dhamira isiyokuwa na utu ya Serikali hii Chama cha Mapinduzi juu ya usitawi wa nchi hii na watu wake, ndiyo chanzo kikubwa cha askari wetu na Wananchi wengine kuingia katika majaribu ya rushwa na aina mbalimbali za uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli inawezekana kabisa binadamu akawa mwadilifu bila kuwa na masilahi bora katika jamii, lakini ni ukweli usiopingika kwamba, umaskini na hali duni ya maisha ndiyo unaochangia kwa kiasi kikubwa, kuondoa uadilifu na uimara wa nidhamu katika kukabiliana vishawishi vya rushwa na mambo mengine machafu yenye sura hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Serikali kuwa ndiyo mlezi wa rushwa, imekosa mamlaka ya kiuadilifu *(moral authority)* kwa kukemea vitendo vya rushwa vinavyofanywa na taasisi mbalimbali zilizo chini yake. Kwa mfano, kwa mujibu wa vyombo vya habari na kwa mujibu wa mjadala wa Bajeti ya Serikali unaoendelea Bungeni, imeibuliwa kashfa ya wizi wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 200, ambapo Viongozi Wakuu wa Serikali wamehusishwa. Katika jambo kama hili, Serikali inatoa wapi nguvu na sauti ya kukemea rushwa katika taasisi inazoziongoza kama vile Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wanaopaswa kukemea na kuzuia rushwa ni wala rushwa, ni wazi moja kwa moja kuwa, utamaduni wa kupokea rushwa na kula rushwa katika Taasisi zote za Serikali ni jambo la kawaida na linaloipendeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hakuna hata Kiongozi mmoja mwenye mamlaka ya kiuadilifu kukemea jambo hili, kwa kuwa familia zao zinaishi, zinasoma na kufurahia maisha kwa ajili ya ufisadi, wizi wa mali za umma na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaikemea Serikali kujenga mazingira ya rushwa kwa askari wetu. Kwa mfano, kitendo cha Serikali hii ya CCM kukigeuza Kitengo cha Askari wa Usalama Barabarani kuwa kitengo cha ukusanyaji mapato kwa makosa ya kutafutiwa na kulazimishwa barabarani ni rushwa iliyowekewa mfumo rasmi. Jambo hili ni hatari sana kwa sababu rushwa ya aina hii haiwezi kumalizika kwa kuwa ina baraka za Serikali.

Hali ni mbaya zaidi kwa kuwa katika kutekeleza jukumu hilo la askari kukusanya mapato, utaratibu umewekwa ambapo kila askari anatakiwa kutafuta kwa bidii, kulazimisha na kukamata makosa yasiyopungua sita mpaka tisa na kuyatoza faini. Mfumo huu mpya wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato umeifanya rushwa barabarani kuwa rasmi. Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kwamba, Serikali imeishiwa fedha, lakini tunaisihi sana isitumie njia za ukandamizaji na uonevu kujikusanyia mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuacha jukumu lao la msingi la kusimamia sheria za barabarani na kuanza kukusanya mapato, ajali za barabarani zimeongezeka sana. Kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2013, jumla ya ajali za barabarani zilizohusisha magari katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Pwani, Kilimanjaro, Arusha na Morogoro zilikuwa ni 459,931 na ajali hizi zilisababisha vifo vya watu 2,408 na majeruhi 16,040. Kwa upande wa bodaboda, watu waliofariki kutokana na ajali ni 1,106 na majeruhi 6,581.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Haki za Binadamu ya 2013, inasema kwamba, nchi inapata hasara ya kati ya asilimia moja hadi mbili ya Pato la Taifa *(GDP)* kutokana na ajali za barabarani. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali wa kukifanya Kikosi cha Usalama Barabarani kuwa Kitengo cha Ukusanyaji Mapato, umekuwa ni hatari kubwa kwa maisha ya raia na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya mahabusu kugoma kula, kuvua nguo hadharani na mambo mengine ya kusikitisha ili kuonesha hisia zao juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa dhidi yao. Madai makubwa ya mahabusu hao ni kwamba, wanapata mateso makubwa gerezani kwa makosa ambayo wengi wao hawajayatenda. Hii maana yake ni kwamba, mahabusu wengi katika magereza yetu wamebambikizwa kesi, jambo ambalo ni kinyume kabisa na Utawala wa Sheria na Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa mwanya uliopo hivi sasa wa Polisi kuwabambikiza raia kesi na kuwaweka mahabusu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ili kuondoa fursa kwa baadhi ya askari wenye nia mbaya kutumia madaraka yao kuwabambikizia watu kesi kutokana na chuki au sababu nyingine. Kwa mfano, kijana mmoja wa Arusha, aliingia katika ugomvi wa mapenzi na askari polisi kwa sababu ya kumgombania binti. Askari yule alitengeneza mazingira kwa kijana yule kumbakiziwa kesi ya wizi wa kutumia silaha na mauaji na kuswekwa rumande. Kijana huyo wakati alipokuwa anaendelea kuteseka mahabusu, yule askari alimwoa yule binti. Baadaye askari huyo na binti huyo ambaye sasa ni mke wa yule askari wakaenda Magereza kumtembelea yule kijana aliyekuwa mahabusu kwa uonevu kama ishara ya kuonesha umwamba!

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo kama haya hayana idadi katika magereza yetu, ni mengi. Uonevu na unyanyasaji unaofanywa na askari wetu katika kila kona ya nchi yetu ulijidhihirisha pia bomu lilipolipuliwa katika Mkutano wa CHADEMA wakati wa kuhitimisha kampeni za marudio ya Udiwani mwaka jana, ambapo watu wanne walifariki dunia na wengine wengi zaidi ya 100 kujeruhiwa vibaya wakiwemo watoto wadogo na Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna ushahidi wa kutosha juu ya ni nani alihusika na mlipuko huo wa bomu. Licha ya kuwa baadhi ya Polisi walihusika na mlipuko huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilimtaka Rais mara nyingi aunde Tume ya Kijaji kwa ajili ya uchunguzi wa suala hili kubwa, lakini hakufanya hivyo mpaka sasa. Badala yake kumekuwa na kejeli nyingi na mizaha juu ya suala hili hatari kwani waliokufa kwenye Mkutano wa CHADEMA wanaonekana hawana tofauti na mbuzi au kondoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi walengwa tuliotaka kuuwawa tunafahamu uchungu na mashaka tuliyonayo dhidi ya maisha yetu. Hata hivyo, mnaweza kuendelea kudharau jambo hili kwa sababu bado Utawala na Mamlaka yenu yanaendela kuelekeza, kupanga na kuendesha nchi. Jambo dhahiri ni kwamba, mateso haya, damu hizi, uonevu huu utafika mwisho na kama ninyi hamtakuwepo basi watoto wenu watakuwepo na ndugu zenu wengine watakuwepo kushuhudia ukomo wa ukandamizaji, utesaji, uuaji na udhalimu huu dhidi ya raia wasio na hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwamba, waliotaka kutuua pia waliendelea kupanga mipango ya kutubambikia kesi hiyo ya mauaji na ugaidi, lakini Mungu akawa mwema, walikamatwa vijana wengi, wamepigwa, wameteswa na wengine sina uhakika kama wataweza kuwa na uwezo wa nguvu za kuzaa tena kutokana na simulizi zao, walivyofanyiwa ukatili wa ajabu na wote walilazimishwa kumtaja Mbunge wa Arusha Mjini, Mheshimiwa Godbless Lema na Viongozi Waandamizi wa CHADEMA kuwa ndiyo waliohusika na mlipuko wa mabomu Kanisani Olasiti na kwenye Mkutano wa kufunga Kampeni za Udiwani za CHADEMA mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijana hawa waliopatiwa mateso makali, baadhi yao walitolewa gerezani wakiwa na kesi nyingine na wakaelekezwa, wakapigwa, wakateswa na wengine kutishiwa kuuwawa, wakubali kuwa mipango ya milipuko ya mabomu Kanisani Olasiti na kwenye Mkutano wa CHADEMA, yaliratibiwa na Mbunge wa Arusha Mjini na Viongozi Wakuu wa CHADEMA. Kwa tafsiri hii, inaonekana waliolipua bomu katika Kanisa la Olasiti, ndiyo hao hao waliolipua bomu katika Mkutano wa CHADEMA. Hii ni kwa sababu badala ya polisi kutawatafuta wahalifu hao na kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria, wanahangaika kutafuta watu wa kuwabambikia kesi ya kulipua bomu kanisani ili wawaunganishe na tukio la mlipuko wa bomu katika Mkutano wa CHADEMA. Kwa sababu wanawatafuta watu wa kuwabambikia kesi, ni dhahiri kwamba, Serikali inajua undani wa tukio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uadilifu wa Jeshi la Polisi umeendelea kuwa mashakani kwani baada ya Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kijana mmoja Kiongozi wa CHADEMA wa Kata ya Usa River, Msafiri Mbwambo, aliuwawa kwa kuchinjwa shingo. Wauwaji wale walikamatwa na Jeshi la Polisi, lakini cha kusikitisha ni kwamba, baada ya muda mfupi wahalifu hawa waliweza kutoroka mbele ya Polisi kwenye chumba cha mahakama wakiwa wamefungwa pingu eti na kufanikiwa kumpora Askari bunduki aina ya *SMG* na kukimbia nayo mpaka leo hawajaonekana wakiwa na pingu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni upumbavu usiofikirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe unaweza pia kuziba masikio yako kana kwamba, hiki kinachosemwa ni *blues* na ngojera, lakini Mungu yule unayemfuata Kanisani kila asubuhi kumwomba amesikia na yuko kazini. *"Only time will tell."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2013, ukurasa wa 22, watu 23 waliuwawa na Vyombo vya Dola kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni, 2013. Kuna mateso makubwa wanayopitia Wananchi kutokana na uonevu wa askari wetu. Wanalia machozi mazito, lakini hakuna msaada kwani Serikali inayopaswa kuwatazama na kuwalinda raia wake dhidi ya ukandamizaji huu, imepoteza ladha ya utu kwa hiyo kelele na mateso wanayopata watu kwa kubambikiziwa kesi na kuwekwa mahabusu na kufungwa miaka mingi na kuuwawa, mateso hayo sasa yamegeuka kuwa laana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba ni vyema kuwajengea Wananchi utamaduni wa kuripoti matukio ya kihalifu kwa Jeshi la Polisi kuliko

kuanzisha taasisi nyingine isiyo rasmi ndani ya Jeshi la Polisi. Tunatambua kwamba, Jeshi la Polisi limeanzisha mfumo huu wa Ulinzi Shirikishi kwa sababu ya uchache wa askari ilionao. Katika Randama ya Jeshi la Polisi, Fungu 28, mojawapo ya changamoto zilizotajwa ni uchache wa Askari Polisi. Kwa mujibu wa randama hiyo, idadi ya askari inayohitajika nchini kwa kiwango cha Kimataifa ni 90,000 wakati waliopo sasa hawafiki nusu ya idadi hiyo. Aidha, Jeshi la Polisi linapata ugumu wa kupata taarifa za kihalifu kutoka kwa Wananchi kwa sababu ya uadui uliojengeka kati ya Wananchi na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuongeza ufanisi katika matumizi yake ya fedha, kuzuia ufisadi na ubadhirifu wa fedha za umma, kuwajengea Wananchi uwezo wa kiuchumi ili fedha zitakazopatikana zitumike kwa ajili ya askari ambao ni wataalam wenye uwezo wa kuwalinda raia na mali zao badala ya kurasimisha mfumo usio rasmi wa Polisi Jamii ambao wengi wao ni *Green Guard* wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani Jeshi la Polisi kupuuzwa huko Zanzibar kwa kuvipa mamlaka zaidi dhidi ya Jeshi la Polisi, Vikosi vya KMKM, JKU na KVZ katika kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama wa Zanzibar. Jambo hili limeondoa mamlaka ya Jeshi la Polisi ambalo lina wajibu wa kulinda raia na mali zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la udini na ukabila katika Taifa letu linaonekana kuendelea kukomaa, lakini tatizo ambalo halitamwacha hata mmoja wetu salama ni tatizo ambalo hakuna mshindi atakayepatikana, ni tatizo ambalo hata kama litaisambaratisha nchi, hata wale watakaofanikiwa kuikimbia nchi, hawatakuwa salama huko wanakokwenda, kwa sababu bado watakakuwa na imani zao na chuki hiyo dhidi ya imani nyingine itaendelea popote watakapokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile jambo hili linatishia usalama mpana wa Taifa hili, ni vyema sasa Serikali ikatafakari upya na kuleta sheria mpya itakayokataza na kuwajibisha kwa nguvu zote wale wote watakaojaribu hata kwa maneno, kueneza chuki au ubaguzi dhidi ya dini, kabila ama rangi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iombe radhi na kuwaondoa madarakani Viongozi wote wa Serikali waliotoa kauli za uchochezi wa kidini, wa kikabila na wa rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano ya Serikali katika biashara haramu ya madawa ya kulevya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina sababu ya kupoteza muda katika eneo hili, kwani ni ukweli usiopingika kuwa, biashara hii inafanywa na Viongozi Wakuu wa Serikali; hivyo basi, waamue wao wenyewe kama wangependa kuwa sehemu ya mateso na mauwaji ya vijana wetu katika jamii ya watu wanaowaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalazimika kufikia uamuzi huu kwa kuwa Viongozi wa nchi hii walishakiri hadharani kuwa, wanawafahamu kwa majina watu wanaojishughulisha na biashara hii. Ni ajabu na kituko kama Rais wa nchi ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama anaogopa kuwataja wafanyabiashara haramu wa dawa za kulevya ambapo alisema kuwa anawafahamu kwa majina. Tunashawishika kuamini kwamba, bila shaka watu hawa ambao hata Rais anagwaya kuwataja, watakuwa na Malaika kutoka mbinguni ama ni Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kama Taifa tukatambua madhara ya madawa ya kulevya kwa vijana wetu ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Kupuuzia na kutokuchukua hatua kwa wahusika wa dawa za kulevya ni kuangamiza nguvukazi ya Taifa. Nguvukazi ya Taifa

ilishaharibiwa na dawa za kulevya, hatuna Taifa tena; hivyo, Serikali ifahamu kwamba, kuendelea kulifumbia macho jambo hili ni kulihujumu Taifa na huo ni usaliti mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2011 katika Hotuba zetu kuhusu Wizara hii tumeendelea kuonesha mauaji ya raia yanayofanywa na Vyombo vya Dola ikiwemo Jeshi la Polisi. Wakati akihitimisha hoja yake hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ingeunda Mahakama ya Korona kwa ajili ya kuchunguza vifo hivyo kwa mujibu wa sheria ya uchunguzi wa vifo vyenye utata *(inquest act)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilirudia kutoa ahadi ya kuanzisha Mahakama hiyo mpya Korona kwa ajili ya kuchunguza vifo vilivyosababishwa na operesheni ya kuwaondoa majangiri na tokomeza, miaka michache iliyopita. Hadi leo ahadi hiyo ya Waziri Mkuu haijatekelezwa na badala yake, Rais ameamua kuunda Tume nyingine huku Bunge lako Tukufu likiwa limewasilisha taarifa kuhusu Tokomeza, jambo ambalo linaonesha Serikali kutokuamini Taarifa ya Kamati ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2013 taarifa zinaonesha kuwa, watu 23 waliuawa na Vyombo vya Dola. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri mwenye dhamana ya Wizara ili kulieleza Bunge lako Tukufu juu ya kukithiri kwa tabia hii isiyokoma mwaka hadi mwaka na ni hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya askari wanaohusika na mauaji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi mpya kuichukulia hali hii kama janga ndani ya jeshi la polisi na hivyo awe na mkakati wa kuzuia hali hiyo.

Katika hali ya kushangaza hata Wananchi wameanza kuchukua sheria mkononi kwa kuwadhuru na hata kuwaua askari polisi. Kwa mwaka 2013, vituo vya polisi takribani vitano vilivamiwa na Wananchi na mali kadhaa za Jeshi hilo kuharibiwa. Aidha, vifo kadhaa vya askari viliripotiwa kutokea maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama matukio haya hayatoshi, Wananchi kwa makundi yao katika maeneo mbalimbali ya nchi, walizidi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaua watu mbalimbali ambapo wametuhumiwa kufanya makosa ya jinai kama vile wizi. Kwa mwaka wa jana pekee, watu 1,669 waliuawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uhalifu mwingine ambao umejitokeza katika nchi yetu ambapo watu wamekuwa wakizikwa hai. Matukio kama haya yametokea katika Wilaya ya Chunya na maeneo mengine katika Mkoa wa Mbeya. Hali hii ya mauaji ya raia inayofanywa na Vyombo vya Dola na pia mauaji yanayofanywa na Wananchi kwa wahalifu na pia kuvamia na hata kuua polisi, si jambo la kulifanyia mzaha kabisa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua hatua za dharura na kutoa taarifa Bungeni; na bila kufanya hivyo, italazimika kuamini kwamba, Serikali iliyopo madarakani imetoa baraka kuhusu vitendo hivi vya kinyama kuendelea kutokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipaka ya Tanzania haipo salama kabisa kwa sababu imeendelea kuwa kichaka kwa wahamiaji haramu. Hali hiyo pia inathibitisha kile kilichosemwa na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imejaa wageni wengi kutoka nchi mbalimbali kama vile Bangladesh, India, China, Pakistani na nchi nyingine za Afrika na Afrika ya Mashariki; wanaofanya kazi hapa nchini katika fani na taaluma ambazo watu wetu wanazo. Kambi Rasmi

ya Upinzani inahoji kama ni Sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutoa kipaumbele cha ajira kwa wageni katika fani au ujuzi na taaluma ambazo Watanzania wanazo. Aidha, tunaitaka Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji na Idara nyingine za Serikali, kupitia takwimu za wageni waliopo nchini na shughuli wanazozifanya ili kuona kama wageni hao wana uhalali wa kuendelea kuwepo na kufanya kazi nchini, ikiwa hakuna kazi inayohitaji taaluma maalum *(Special Skills)* ambazo watu wetu hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila aliyepata fursa ya kusikiliza kwa makini maoni haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, angetaka kuona tunatoa suluhisho gani juu ya nini kifanyike kuhusu mambo haya. Hata sisi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunafikiri ni vyema kushauri na kusaidia kuonesha njia mwafaka ili kuliokoa Taifa letu na mateso haya. Tunapata wakati mgumu kuishauri Serikali ambayo imepoteza thamani ya utu dhidi ya watu wake, hivyo basi, kama kuna mambo ya kushauri basi tungeshauri yafuatayo:-

Moja, Mungu asaidie Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi iondoke madarakani mapema kabla haijaharibu mfumo wa kumpata kiongozi kwa njia ya demokrasia, kwani hali ikiendelea hivi ipo siku watu wataingia barabarani. Hali hii tayari imeshaanza kujitokeza kwani kipindi cha Januari na Desemba, 2013 pekee watu 1,669 waliuawa kwa sababu ya watu walijichukulia sheria mkononi. Tunajua watu watakapojitokeza kudai haki zao na kupinga uonevu, watapigwa mabomu ya machozi, risasi, vitisho na mateso mbalimbali, lakini tunajua hawatarudi nyuma kwani watakuwa wamedhamiria kujitetea na kuwatetea ndugu zao na nchi yao dhidi ya mateso, ukandamizaji, uonevu na dhiki inayotokana na mambo hayo. *(Makofi)*

Kinyume chake, yatakapotokea mambo haya, Serikali itakuwa imetangaza ukomo wa utawala wa kidemokrasia na hilo linaweza kuwa chimbuko la machafuko na umwagaji damu. Hivyo, ni vyema waumini wa imani mbalimbali wafanye dua na sala ili Serikali hii ya CCM iondoshwe madarakani katika Uchaguzi Mkuu ujao kwa ajili ya amani. *(Makofi)*

Pili, siku Serikali ya CCM ikijua kuwa nguvu ya Mfalme ni watu na si bunduki na mabomu ya machozi, siku hiyo ndipo mtakapopata kupata hekima kuheshimu utu wa binadamu na kile kinachoonekana sasa kama mateso, udhalimu na ukandamizaji vinaweza kurekebishwa.

Tatu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutambua kuwa heshima ya Kiongozi haijengwi kwa uwezo wa mali wala utawala bali katika kazi njema, heshima, utu na upendo. Ikiwa Serikali itaelewa hivyo, basi wajibu wake katika kutafuta na kupigania maisha ya mtu mmoja mnyonge, anayeteswa na kudhalilishwa itakuwa ndiyo hazina na heshima kubwa kwa Viongozi wa Serikali na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunafahamu kwamba, ndani ya Serikali kuna watu wengi waadilifu na wenye dhamira njema na nchi yetu. Hata hivyo, wanashindwa kuchukua uamuzi wa kukemea uovu kutokana na utamaduni wa Serikali wa kuwatisha na kuwakemea, kuwawekea vikwazo mbalimbali watu wa namna hiyo. Kutokana na hali hiyo, jamii yetu imejengeka katika fikra za hofu na woga kwa mambo ambayo yanahitaji uamuzi thabiti na kauli za kijasiri ili kulinusuru Taifa letu na maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ijue na Wananchi wajue kwamba, dhambi mbaya na kubwa kuliko zote Duniani ni woga. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaasa Viongozi wachache wenye dhamira njema waache woga, wasimamie misingi ya haki na kweli hata kama gharama zake ni maisha yao kwani msingi wa Taifa letu la kesho unajengwa na Viongozi na Watawala walioko madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godbless Lema, kwa Hotuba yako kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Sasa tunaingia katika utaratibu wa uchangiaji, ambapo mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji ajiandae.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuipongeza Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani na niiombe Wizara ya Mambo ya Ndani iyafanyie kazi yale yote yaliyosemwa na Mheshimiwa Godbless Lema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mimi kulisemea Jeshi la Polisi. Wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana, nyumba zao ni chakavu, askari hawa tukiwa tumelala wao wanatulinda. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie masilahi yao, iangalie nyumba zao. Tumekuwa tukilisema kwa muda mrefu, lakini tunaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ione umuhimu wa kuwatumikia askari hawa wanaofanya kazi kwa mateso makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ninalotaka kulizungumzia, Sheria ya Jeshi la Polisi inaruhusu mikutano ya hadhara pamoja na maandamano, lakini kumekuwa na tatizo kubwa sana hasa kwa Wabunge wa Upinzani; wanapotaka kufanya mikutano yao ya kuzungumza na Wananchi na maandamano, Jeshi la Polisi limekuwa likizuia mikutano hiyo na hasa kwa Wabunge wa Upinzani. Hivi karibuni ilitokea kwa Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa John Mnyika, alipotaka kufanya maandamano kuhusu maji. *RPC* wa Kinondoni alizuia na Wizara imekuwa ikisema kama tunaona Jeshi la Polisi halitendi haki tukate rufaa. Mbunge wa Ubungo alifanya hivyo, lakini mpaka leo hajapata majibu ya rufaa hiyo. Vivyo hivyo, Mbunge wa Arusha Mjini alitaka kufanya mkutano alizuiliwa na *OCD,* lakini *RPC* wa Mkoa wa Arusha aliona umuhimu na akamruhusu Mbunge huyu kufanya mikutano yake. Kwa hiyo, tunaomba wale askari, ninaamini wako wengi wenye nia njema, lakini wako wachache ambao naamini wanatumika aidha kwa masilahi yao au kwa kuhitaji kupata sifa, waache tabia hizo, kwa sababu Wabunge wote wana haki ya kuzungumza na Wananchi wao na si Wabunge wa CCM peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, ningependa kulipongeza Jeshi la Polisi; tumeona kwenye Vyombo vya Habari wakikamata madawa ya kulevya. Ningependa kujua dawa hizi huwa zinahifadhiwa wapi au zinateketezewa wapi? Hivi majuzi kwenye vyombo vya habari tumeona madawa haya ya kulevya yametoweka kwenye kituo polisi. Ningependa kujua sasa yanapohifadhiwa ni wapi na hayo yaliyokuwa kwenye Kituo cha Polisi yalitowekaje na wameweza kukamata askari ambao walipoteza dawa hizo. Kwa sababu, haingii akilini dawa zinapotea kwenye Kituo cha Polisi wakati askari wapo!

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ubambikizaji wa kesi. Wananchi wengi walioko mahabusu leo, kesi ambazo zimewapeleka pale si zao. Kama alivyosema msemaji wa Kambi ya Upinzani, watu wanagombana huku uraiani, kumkomoa yule Mwananchi wanabambikizia kesi. Niombe sana, Waziri atakapokuja hapa atuambie wanachukua hatua gani kwa wale askari wanaogundulika kubambikizia Wananchi kesi, kwa sababu Wananchi wanaumia, wanaacha kufanya kazi zao na wanakaa muda mrefu kwenye mahabusu, mwisho wa siku wanaambiwa hawana kesi ya kujibu. Tungependa kupata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kero ya askari na bodaboda. Vijana wetu wameweza kujitafutia fedha, wamekopa benki wamenunua bodaboda. Leo vijana hao wamekuwa wakinyanyasika sana na Jeshi la Polisi, wameacha kufanya kazi nyingine wanakimbizana na vijana hawa na kuwatoza faini kubwa. Tulikuja hapa Wabunge tukaomba, si

wote wanaoweza kuchukua teksi, si wote wanaoweza kupanda mabasi, lakini hizi bodaboda zimekuwa zikirahisisha sana usafiri kwa Wananchi wetu. Vijana hawa ambao wanataka kujikwamua kutoka kwenye wimbi la umaskini, Jeshi la Polisi limekuwa likiwasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuwaangalie vijana hawa, tukiendelea kuwanyanyasa watarudi mtaani na hali itazidi kuwa mbaya.

Kwa hiyo, ninaomba sana haya niliyoyasema yafanyiwe kazi na kubwa ni hilo la askari, mafao yao yaangaliwe kwa sababu ni vijana wetu, ni watoto wetu, ni baba zetu. Tunajua wana wajibu wa kulinda Wananchi na mali zao, lakini nao basi waangaliwe masilahi yao ili waweze kufanya kazi zao vizuri na hii itapunguza tatizo kubwa la rushwa ambalo askari polisi wanatuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige. Mheshimiwa Sereweji!

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *Bismilahi Rahmani Rahim*. Kwanza, naanza kuchangia kwa kusema kwamba, Wananchi wote wajue kwamba, binadamu ndiye aliyeundiwa silaha na jeshi lolote la polisi au askari wa aina yoyote, ikiwa atachukua silaha yake, aidha maji machafu, akaingia msituni na kwenda kuwinda wanyama kwa kuwamwagia maji machafu au kuwapiga mizinga, huyo ndiye kafanya kosa, kwa sababu mizinga imeundwa kwa ajili ya binadamu. Kwa hiyo, natoa tahadhali kwa Wananchi wote kwamba, wasiwafuate Viongozi ambao wakishawekwa ndani tu Viongozi wanatoka lakini wao wanabaki ndani; watumie akili yao.

Leo sitokoga na kumfukuza mwendawazimu ambaye amechukua nguo zangu, nitachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono Hotuba hii, lakini naliomba Jeshi la Polisi libadili sheria zote zile ambazo zinakandamiza Jeshi la Polisi hasa Jeshi la Polisi wadogowadogo. Sheria ambazo zimepitwa na wakati wazibadilishe na walete hapa watueleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hivi sasa ukitazama mafao ya polisi ni madogo kuliko mafao ya Jeshi la Ulinzi na ukitazama Jeshi la Polisi nao wana kazi kubwa zaidi kuliko Jeshi la Ulinzi. Jeshi la Polisi likitokea tukio lolote la hatari, wao ndiyo wanaokwenda mwanzo na wakienda pale wanaambiwa watumie akili zao na wakifanya kubwa zaidi wanalaumiwa. Lazima waende kiustaarabu, waweke hali ya usalama, wakishindwa wao wanakuja Jeshi la *Field Force*. *Field Force* kwanza wanatoa tahadhali, wakati wakitoa tahadhali pale hatujui Wananchi wale watachukua hatua gani, lakini wakija Jeshi la Ulinzi wao hawana hili wala lile wanafagia tu. Kwa hiyo, ukitazama Jeshi la Polisi wana kazi nzito sana, lazima wafikiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa vyeo; Jeshi letu la Polisi wanasuasua sana kupandishwa vyeo. Ninatoa mfano, kuna askari mmoja anaitwa Haji Maulid, alimuua jambazi mwaka 2005 huko Jumbi, akazawadiwa ukoplo basi mpaka sasa angali koplo, hajapewa cheo chochote tangu 2005 mpaka leo, miaka minane. Asingemuua jambazi mpaka leo angekuwa askari wa kawaida. Kwa hiyo, naomba Jeshi la Polisi watazamwe sana kwa upande wa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye mafunzo; lazima hivi sasa Jeshi la Polisi liende na wakati. Ule wakati kwamba, Jeshi la Polisi kijana mdogo tu anatumia silaha umalizike, lakini inabidi afanye vile kwa sababu hajui kupanga mikono. Yeye akimwendea mtu anataka achukue hatua kubwa tu. Kwa hiyo, namwomba Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, ahakikishe kila Kituo cha Polisi kuna komandoo. Nimekusudia kwamba, kila Kituo cha Polisi awepo Askari wa Polisi mmoja au watatu anayejua kuzipanga. Awe amesomea judo, lakini ikiwa tunakwenda na polisi wetu ambao hawajui judo na hawajui sarakasi, wataadhirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumzia kuhusu Mkataba ndani ya Jeshi la Polisi. Kuna mkataba wa kiinua mgongo na kuna mkataba wa *pension*. Mkataba wa kiinua mgongo ukifika miaka 12 ukiweka mkataba wa kiinua mgongo hata ufanye kazi miaka 40 unalipwa makato, unakuwa huna *pension*.

Kwa hiyo, ningeliomba Jeshi la Polisi, mkataaba wa kiinua mgongo wauondoe, kwa sababu askari wengi wanaweka saini mkataba huo, lakini ukifika wakati hawawezi kuacha kazi mpaka wanafika miaka 40. Wakifika miaka 40 posho wanayopewa ni ndogo sana. Sasa askari yule kama kafanya kazi muda wa miaka 26, ameshafika miaka 26, kafanya kazi miaka 30 wewe unamtegemea kitu gani yule wakati anaacha Jeshi la Polisi anapata kama milioni tatu, milione nne, milioni kumi na huko hana pensheni, asile rushwa atafanya nini?

Tunaomba sheria ile ibadilishwe iwekwe sheria ya moja kwa moja, askari akifika miaka 12 ajitazame, anayetaka kuendelea aendelee na ambaye hataki kuendelea aache Jeshi la Polisi. Akitaka kuendelea moja kwa moja aingie kwenye malipo ya *pension. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Polisi Shirikishi; ningelipenda sana hawa Polisi Jamii …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Sereweji…

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii asilimia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilipotazama upande wangu wa kushoto, niliona walikuwa wanakufuatalia kwa makini. Mchangiaji alikuwa anaongelea mkataba siyo nkataba! Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mhehimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema! *(Kicheko)*

**MHE. CATHERINE VALENTINE MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu wake, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutekeleza majukumu yao wakishirikiana na Wizara ya Ulinzi ambayo ni muhimu sana katika ulinzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zote ambazo zipo katika Wizara hii, ninaomba nielekeze mchango wangu moja kwa moja katika Vitambulisho vya Taifa. Kutokana na umuhimu wa Mradi huu wa Vitambulisho vya Taifa, katika uzinduzi wa Mradi huu, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya M. Kikwete, alitoa ahadi ya kwamba, atafanya kila linalowezekana kuwapatia fedha *NIDA*, nyenzo na rasilimali watu, ili Mradi huu uweze kukamilika kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2013, Serikali ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 150 kwa ajili ya Mradi huu wa Vitambulisho, lakini mpaka sasa watu wengi bado hawajasajiliwa na Wananchi wachache wamepata vitambulisho vyao na hadi sasa tija ya vitambulisho hivi na matumizi yake bado haijaonekana. *(Makofi)*

Mheshimwia Niabu Spika, ninaomba Serikali inipe jibu ni kiasi gani cha fedha, ambazo mpaka sasa hivi *NIDA* wameshapatiwa kwa ajili ya Mradi huu? Je, ni lini hasa Mradi huu utakamilika ili shughuli zake zifanywe kama ulivyokuwa umepangwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa sijautendea haki nisipotambua kazi kubwa anayoifanya Kamishna wa Uhamiaji, Bwana Silvester Ambukile. Idara ya Uhamiaji sasa hivi kuna mabadiliko tangu Kamishna huyu aingie madarakani; Wananchi wamekuwa hawapati usumbufu; *Passport* zinapatikana kwa wakati; na zile foleni na usumbufu wote uliokuwa ukilalamikiwa Uhamiaji umepungua. Kwa hiyo, tunamshukru Mheshimiwa Rais, kwa kumteua Kamishna Ambukile na kweli hakufanya kosa na vilevile, ninaomba Watendaji wengine katika Wizara za Serikali, waige mfano wa Kamishna Ambukile. *(Makofi)*

Mjeshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kuhusu umuhimu wa kulinda mipaka yetu na kutunza heshima ya nchi na kwenda na taratibu za kisasa katika utoaji wa *Passport* za kusafiria; *Electronic Passport* na *Boarder Security*. Kutokana na matatizo ambayo yamekuwa yakitokea ya kughushi *Passport* zetu, nilifarijika sana Msemaji wa Idara ya Uhamiaji, aliposema kuwa, Tanzania tunapanga kubadilisha *Passport* zetu kuwa katika mfumo wa Kielektroniki *(e-Passport)*. Mfumo huu utawezesha alama za vidole, macho na alama nyingine kuwa ni sehemu ya *Passport* ya mtu na mfumo huu, utasaidia sana, vitendo vya kughushi *Passport* havitakuwepo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi mbalimbali zimehamia katika mfumo huu. Ilianza Malaysia na nchi nyingine kubwa sasa hivi zinatumia mfumo huu. Vilevile katika Afrika, Nigeria na Senegal pia wameanza kutumia mfumo huu. Vilevile mwaka huu mwanzoni Serikali ya Guinea imezindua Mradi rasmi kwa ajili ya mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo huu gharama yake ni kubwa sana, wenzetu Guinea, wameamua kutumia mtindo wa *Build, Operate and Transfer (BOT),* ambapo Mkandarasi husika anagharamia katika Mradi huo kila kitu; kujenga mfumo, kuuendesha, halafu mapato kwa kipindi kifupi au ambacho watakuwa wamepanga, wanagawana na Serikali *then* baadaye wanauacha katika Serikali na kunakuwa na Wafanyakazi wa Serikali wachache ambao wamewezeshwa kutumia mfumo huo. Serikali itakuwa inaingiza mapato na mfumo huu unajilipa wenyewe.

Mheshimwia Naibu Spika, naomba nipate jibu la Serikali, inaweza kutuambia mpango huu umefikia wapi na umeanza lini na unatarajiwa kuzinduliwa lini. Je, Mradi huu umetengewa pesa kiasi gani katika Bajeti hili? Wizara imefikia maamuzi gani katika upatikanaji wa gharama za Mradi huu ili utekelezeke kwa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa niongelee Jeshi la Polisi. Nimekuwa nikisikitishwa sana na habari ambazo zimekuwa zikitolewa katika vyombo vya habari mbalimbali kuhusu Polisi wanavyojihusisha na uhalifu. Raia tumekuwa tukipata shida sana, kwa sababu sisi tunategemea Jeshi la Polisi litulinde sisi na mali zetu; lakini polisi wamekuwa wakijihusisha na ujambazi na hivi karibuni tumesikia baadhi ya polisi wamehukumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, polisi wanatuhumiwa kujihusisha na ujambazi, lakini mimi ningelipeda kufahamu, Serikali inajipanga vipi; Askari Polisi wana hali ngumu sana? Mimi ninaiomba Serikali iangalie ni kwa jinsi gani itawasaidia Askari Polisi,

ukizingatia kwa mfano Jeshi letu la Ulinzi, wao wanapewa chakula, wanapewa pesa mbali na mshahara. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia Askari Polisi na wao wakawa wanapata pesa mbali na mshahara au wanagawiwa chakula kama Wanajeshi? Tusiwalaumu Askari Polisi, wanayo maisha magumu sana. Ninaomba Serikali iangalie jinsi gani itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana nitoe pongezi zangu kwa Mkuu wangu wa Polisi wa Mkoa wa Arusha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CATHERINE VALENTINE MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji.

**MHE. DKT. AUGUSTINE LYATONGA MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu wake, kwa ubunifu ambao wameuleta mwaka huu wa motisha kwa ajili ya Polisi, zawadi kwa ajili ya Polisi na Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kupambana na uhalifu, hiyo ndiyo njia mojawapo itakayoweza kusaidia kupata taarifa za makosa na kutambua aina ya uhalifu unaofanyika.

Tunasema Polisi wanaishi katika mazingira magumu, lakini wanaweza kuishi kwa kujengewa mazingira ambayo wanaweza kuongeza pato lao bila kuhitaji kula rushwa wala kushiriki katika ujambazi. Hii inawezekana kabisa. Kwa mfano, Polisi amekamata magendo, sioni ni kwa nini asipewe asilimia kumi ya yale magendo aliyoyakamata. Kwa sababu na yeye anataka watoto wake wasome tena *International School,* ajenge kama tunavyojenga sisi na siyo kumwambia tu ana mshahara. Je, huo mshahara unamuwezesha kuishi? Kwa hiyo, tukifanya hivyo, tukiwapa motisha, kila mbuzi atakula kwa urefu wa kamba yake.

Wananchi na wao kama watatoa taarifa zinazosaidia kufichua uhalifu na wao wazawadiwe. Ndiyo sababu nimefurahi sana Mheshimiwa Waziri kutoa nambari yako ya simu ya kiganjani ambayo ni 0685777222 au 0685777222.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusema hivi na Wananchi wangu wa Vunjo wasikie kwamba, wakisaidiana na Waziri wa Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi, kufichua wahalalifu, wanaweza wakatajirika, wanaweza wakapata kipato bila kulazimika kufanya uhalifu. Mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ninajua mwaka huu umetenga, leo asubuhi nimekusikia kwenye kipindi cha Jambo, shilingi bilioni 3.5. Ninaomba hiyo shilingi 100,000,000 iende Vunjo, watu wangu washirikiane na Serikali na Polisi katika kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninazungumzia nyenzo. Kweli kuna matatizo makubwa. Ninashukuru Waziri, nimeona kwenye Programu ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kuna kama magari 777, kila *OCD, RPC, OCS,* apewe gari tena zuri siyo yale mabovu ya zamani. Hilo umefanya vizuri. Wapatiwe pia mafuta. Matatizo makubwa sana kwa Jeshi la Polisi, tutawalaumu kutoka Kituo cha Polisi kwenye tukio wanasema wanahitaji pesa. Ninashukuru

kwamba, safari hii mmetenga hela za kutosheleza matumizi ya *OCD,* atapata lita 600, ingawa leo asubuhi nimekusikia ukisema lita 400; sasa sijui zimepungua saa ngapi maana jana tulikubaliana lita 600? Nami ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Taifa, kwa hiyo, ninajua ni lita 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezikani Polisi aishi kwa shilingi 5,000 kutwa. Ni nani anayekula shilingi 5,000 jamani? Tulikubaliana tangu mwaka 2013 ya kwamba, fedha hizi ziongezwe mpaka shilingi 7,500. Mimi ninasisitiza kesho kuna Kamati ya Bajeti, tumeitwa Wizara ya Mambo ya Ndani twende tukawatetee Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto, wote wapate *ration allowance* ya shilingi 7,500. Kama Mwanafunzi wa Chuo Kikuu anapewa posho ya shilingi 10,000; Polisi atapewa vipi posho ya shilingi 5,000? Ninaona ni matumizi mabaya ya Jeshi letu la Polisi. Ziongezwe na kufikia shilingi 7500. Ninasikia Jeshi la Ulinzi wanataka kuwaongezea Shilingi 1,000 ili iwe shilingi 8,500. Kwa hiyo, ninaomba na Askari Polisi na wao wafikiriwe pia. *(Makofi)*

Kwa kupanga shilingi 500 kwa ajili ya chakula kwa kila mfungwa kwa kweli tunavunja Haki za Binadamu. Hata kama ni mfungwa asiadhibiwe kwa kunyimwa chakula. Kwa hiyo, bado ninasisitiza iwe shilingi 3,000 kama tulivyopanga. Mwaka 2013 tulisema hata kama hizo shilingi 3,000 hamuwezi kuzitoa, toeni basi hata shilingi 1,500 kwa kila mfungwa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kesho tutaenda wote kwenye Kamati ya Bajeti, tuhakikishe upungufu uliomo katika Wizara ya Mambo ya Ndani unaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanatengeneza hela nyingi kwa njia ya makosa mbalimbali na Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Uhamiaji. Sisi tulikubaliana kwamba, walipwe asilimia 70 ya fedha zote watakazokuwa wametengeneza wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Jimbo letu la Vunjo. Mimi ninaomba, nimeshaongea na Waziri, nilikuomba sana unisaidie Wilaya ile iwe Wilaya ya Kipolisi, *OCD* asikae Moshi akae pale Himo, tena kuna Kituo kizuri sana na tupate Polisi kule Mamba, Marangu, Mwika, Kilema na maeneo mengine wa kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana chonde chonde Polisi wasimkandamize raia, wasitumiwe na watu wenye pesa. Mimi ninaona pale Vunjo, kuna kile kiwanda kilichojengwa Njia Panda, watu wamevunja sharia, wanatengeneza pombe kali, Serikali imesema kiwanda kile kibomolewe, lakini tukisema Polisi wasimamie kibomolewe hilo hamtaki, isipokuwa mnawafuata wale Wananchi wanaolima. Pale Meresini tuna mgogoro wa ardhi. Nilishamweleza Waziri wa Ardhi, hilo suala halijahitimishwa. Jana nimesikia waliwaita watu wakawapeleka Kituo cha Polisi Moshi, wakawahoji. Wanahoji nini kuhusu ardhi? Tangu lini suala la ardhi limekuwa ni la Polisi na wakati Polisi wanazo kazi nyingi za kufanya!

Kwa hiyo, ninaomba yule tajiri kule Vunjo anayetumia Jeshi la Polisi, kwa ajili yake akiwa Njia Panda, hawamkamati yeye, hawamfuatilii, lakini mahindi yaliyoko Menesini, Wananchi wanalalamika wanataka eneo la kujenga shule zao, la kujenga soko. Waziri wa Ardhi anajua, nilikwishamwendea. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri uwakemee leo uwaambie wangoje maamuzi yatakayotolewa na Waziri wa Ardhi, wasifanye biashara hiyo haitawalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nisiseme zaidi, isipokuwa ninachokisema ni kwamba, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi lote la Polisi, ninajua mnafanya kazi katika mazingira magumu, endeleeni kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninauna mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dokta Agustine Lyatonga Mrema. Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Mohammed Bakari.

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kuchangia katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru wewe, wachangiaji ni wengi, lakini pia kwa kuniona na kunipa nafasi hii niweze kuchangia. Ninakushukuru sana kwa kunifanyia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka kuzungumzia suala la mahusiano katika ya Jeshi la Polisi na Wananchi. Kama tutakuwa hatuna mahusiano ya Jeshi la Polisi na Wananchi, kwa kweli hatutaweza kupata amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kuzungumzia Jimbo langu la Mtwara Mjini. Jimbo hili ni tete, matukio makubwa mengi yametokea, lakini mambo yako shwari, baada ya kushirikiana. Ninataka kuwahakikishia pia Mtwara kuna amani, Mtwara kumetulia na Wananchi wa Mtwara wamekwishakuwa waelewa tayari. Tatizo lilikuwa elimu, baada ya Wananchi wa Mtwara kupata elimu, sasa kila mtu ameelewa nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara ni eneo pekee ndani ya nchi hii sasa hivi Wawekezaji ndiyo wanaliangalia. Mtwara Mjini na Mkoa mzima wa Mtwara, kila mwekezaji anayekuja leo, anaangalia katika Mkoa wa Mtwara kuja kuwekeza. Kama tutakuwa hatuna amani katika Mkoa wa Mtwara, hawa wawekezaji tutawapoteza. Mwekezaji hawezi kuja kuwekeza kama amani hakuna.

Mheshimiwa Niabu Spika, tumejaribu kufanya mikutano na kuwaelekeza Vijana, Wazee na Akina Mama wa Mtwara wameelewa. Tatizo linakuja kati ya mahusiano baina ya Jeshi la Polisi na Wananchi; bado Jeshi la Polisi linatumia nguvu kubwa sana dhidi ya Wananchi wa Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunalo tatizo kubwa sana la ajira kwa vijana. Vijana wengi wamejaribu kujiajiri wao wenyewe. Mfano, ulio hai ni kwamba, vijana wengi wameweza kujiajiri kupitia bodaboda. Tunalo tatizo kubwa la mahusiano ya Jeshi la Polisi na Vijana wetu ambao wanaendesha bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita, hali ilikuwa tete Mtwara; ni aibu vitu vinavyofanyika Mtwara na kama kweli hatutaweza kufanya vizuri, tutakuja kusikia sisi tumeshaua watu Mtwara. Ninasema hivi kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo dereva wa bodaboda anampakia abiria anakwenda naye anampeleka anakotaka kwenda, lakini anafuatwa na Maaskari zaidi ya watano na pikipiki. Yule dereva wa bodaboda anawakimbia wale Maaskari wakati amebeba abiria. Wiki iliyopita kuna mama mmoja alipakiwa, bodaboda hiyo ikafukuzwa na Polisi. Dereva wa bodaboda ilibidi aanze kukimbia, yule mama alikuwa anapiga kelele kama anakufa na ni Mungu tu alimsaidia hakuruka kutoka kwenye ile pikipiki. Angelijirusha maana yake kingelitokea kitu kibaya sana kwa mama huyo.

Mimi ninaomba, wale ni vijana wetu, hata majumbani sisi wazee tunao vijana. Vijana wetu wote hawako sawa. Kinachotakiwa ni kuwafanyia *counselling* kukaa nao na kuwaelewesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo madereva wa bodaboda Mtwara wameonesha nia njema; wamekaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, na wamekiri kwamba kuvaa *Helmet* ni lazima, kutii sheria ni lazima, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sharia. Wamekubali kwamba, unapotaka kuendesha pikipiki ni lazima uvae *Helmet*. Baadaye walikaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, wakakubaliana, wakaambiwa waende kwenye redio, wakaenda wakaeleza, lakini bado kile walichokubaliana hakifanyiki; tunashangaa ni kwa nini!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana kwamba, dereva wa bodaboda, avae *Helmet* na abiria naye ni lazima avae *Helmet.* Yule dereva wa bodaboda anakuwa na *Helmet,* anampa abiria avae anakataa anasema tunavaaje *Helmet* moja abiria 10 mpaka 20! Sasa wale madereva wa bodaboda wakaomba wakikamatwa basi sheria ichukue mkondo wake dhidi yetu. Wale abiria kama wanakataa basi sheria ichukue mkondo kwao. Wakakubaliana tayari na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba, abiria kama hatavaa *Helmet,* basi kisheria yeye atapaswa kulipa faini au sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, leo wanakamatwa wale vijana, wanapelekwa kituoni, yule dereva wa bodaboda anawekwa ndani amevaa *Helmet,* ametii sheria zofe. Yule abiria analipa faini na kuruhusiwa aende. Kibaya zaidi kuna madereva wa bodaboda wameshababmbikwa kesi za uchochezi. Kesi za uchochezi zinatokea wapi na kukosa kuvaa *Helmet?* Tunatengenza mtandao ambao tutakosa amani. Tukikosa amani ni kwamba, leo tutakosa wawekezaji kuja Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na hasa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, ndiyo inayotoa maagizo haya. Askari hawana makosa wanaagizwa, wanapoagizwa inabidi wafanye kazi. Mimi mwenyewe nimekwenda kwenye Kikao cha Halmashauri Kuu ya Wilaya, nimekwenda asubuhi Mtwara, siku ya pili yake nimerudi Dar es Salaam. Siku ya tatu yake Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa imeitwa na kusema kwamba, Mbunge amekuja kuwashawishi madereva wa bodaboda. Sijawahi kufanya nao kikao na sijawahi kuzungumza nao, lakini wananishirikisha na mimi! Leo mimi ndiye Mbunge nitakayewasaidia kisiasa kwenda kuongea nao wale. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasnain Murji.

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba vijana wa bodaboda Mtwara watendewe haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Ernest Silinde. Mheshimiwa Faida!

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili ama Wahenga walisema; dua ya kuku haimpati mwewe. Sikubaliani kabisa na Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ya kuiombea Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi eti ianguke. Serikali ya Chama cha Mapinduzi nakwambia

haianguki, inasonga mbele daima. Siyo vizuri wakati wa kutoa Hotuba hapa mtu yeyote, siyo Kambi ya Upinzani tu, Mbunge yeyote kuchochea, tunatakiwa tutetee Maaskari hawa lakini tusichochee, Askari hawachocheleki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuushukuru Uongozi wa Wizara hii akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kufanya ziara Pemba na kwenda kuona maendeleo na changamoto ambazo zinajitokeza.

Napenda kumwomba Waziri Chikawe achukue nafasi maalum ya kuja katika Kisiwa cha Pemba kufanya ziara kuona maendeleo ya Askari wake na vilevile changamoto wanazokabiliana nazo ili kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwajengea nyumba Askari wa Pemba kule Mfikiwa. Miaka kumi sasa hivi nafikiri inakaribia kufika lakini nafikiri *engineering* haikuwa nzuri sasa hivi nyumba zile zinapasuka, zinafanya nyufa. Tunaishukuru Serikali, lakini Askari Pemba hawana nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba, nyumba za Askari Madungu, jamani kila mtu anazijua. Askari Madungu vijumba vidogo, yaani hata havileti raha kwa Askari. Nyumba zina vyumba viwili viwili, watoto walale wapi, mgeni alale wapi na wazazi walale wapi? Chumba hiki wakizungumza mama na baba, watoto wanasikia. Tunaomba Serikali ilifuatilie suala hili, nyumba zile ziongezwe ukubwa ama wajengewe nyingine. Mkoani nyumba za Askari hakuna. Kengeje nyumba za Askari hakuna. Naomba Serikali kila siku nikisimama hapa nazungumzia nyumba za Askari wa Tanzania hii ikiwemo Pemba, mpaka leo naiomba Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi ichukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutujengea Ofisi ya Mkoa pale Chakechake na vifaa vipo angalau siyo vingi, tunashukuru na Maaskari wanashukuru. Ofisi ya Mkoani na Ofisi ya Kengeje jamani zimepitwa na wakati, ofisi zinavuja, mvua ikinyesha Askari hawana pa kukaa. Pale Mkoani kuna mlima mrefu ambao hivi sasa unamong'onyoka, hivi tunataka Askari wetu wapoteze maisha yao? Tunaomba basi kama hawakujengewa sehemu nyingine ile ofisi na zile nyumba Mkoani penye lile lima kubwa linalomomonyoka, wawekewe ukuta wa zege au ile sehemu yote izungushiwe zege.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Tanzania ni wasikivu na watenda kazi lakini jamani kwa nini Askari hawa hawapewi masilahi yao? Masilahi mengi, malimbikizo ya posho za uhamisho, pesa za chakula na kadhalika, wanadai pesa chungu nzima, lakini mpaka leo Askari hawa tunawasemea posho haziongezeki. Tunawaonea huruma, naomba sana watekelezewe mahitaji yao Askari hawa.

Mishahara ya Askari kwa nini itofautiane? Kazi zao ni sawa; kulinda nchi hii asubuhi, mchana na jioni, shida na raha, mvua na jua, lakini kwa nini Askari wengine wapate mishahara mikubwa na Askari Polisi wapate mishahara midogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mishahara ya Askari iongezwe siyo kila siku tunapiga kelele hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi hata kule Pemba hakuna, magari kama ulivyozungumza yamenunuliwa au kama yatanunuliwa naomba Pemba yapelekwe magari na siyo magari tu na mafuta yapelekwe. Inawezekana kuna magari mawili au matatu lakini

mafuta hata ya kwendea kwenye operesheni zao hawana. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri alichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kila mwaka linaajiri lakini Vijana wa Kipemba hawapati ajira zile. Kuna Viongozi wachache wanajifanya wakubwa pale wanachukua watu wao kutoka sehemu mbalimbali wanawafanya eti wale vijana ni wa Kipemba halafu wanawaajiri. Vijana wa Kipemba ambao na wao pia wamesoma na wana sifa zote hawaajiriwi. Naomba kulisemea hili ili wakati wa kuajiri, Mheshimiwa Waziri apeleke Tume kule au Viongozi wakaangalie jinsi uajiri unavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nidhamu katika Jeshi la Polisi ni nzuri, lakini kuna baadhi ya Askari wanachukua sheria mikononi mwao. Wanapopewa pengine kazi na Maaskari wakubwa, mabosi wao wanachukua hatua ya kuwadhalilisha….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakari, ahsante sana.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Faida, kwenye Wizara hii huwa ni mtetezi mkubwa sana.

Mheshimiwa Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo kama manne tu na nitayasema kwa haraka haraka.

Jambo la kwanza, mimi nitaendelea kuishangaa Serikali tunapokuwa na Jeshi la Ulinzi kwenye Taifa ama Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo inahusika na Majeshi haya tunayoyataja kama ya Polisi, Magereza na mengineyo, imeomba shilingi trilioni 1.3, Serikali imekwenda ku-*bargain* ili wawapatie bilioni 800 na ndiyo ipo kwenye *ceiling* kwamba, wanatakiwa wapatiwe bilioni 800 ndiyo kama bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kitu cha ajabu Duniani ambacho hakitokei, huwezi ku-*compromise* kwenye masuala ya usalama. Sasa hivi kuna matishio ya ugaidi na matishio ya usalama wa raia ndani ya nchi na nje ya mipaka yetu. Sasa tatizo la Serikali yetu kila siku haohao wanaokwenda kuonesha maonesho lakini haohao ndiyo wanakuwa wa kwanza kunyimwa bajeti. Sasa hatuwezi kwenda kwa mfumo huu. Kwa hiyo, wanachokiomba kama ni trilioni 1.3 wanatakiwa wapatiwe kama zilivyo. Kwa hiyo, hili nilikuwa nataka niliseme kwa sababu ni aibu, hata Mataifa ya nje wakisikia kwamba, tunaweza tuka-*compromise* eti tunaomba jamani kwa nini msipunguze mpaka shilingi bilioni 800. Sasa hayo ndiyo matokeo ambayo yamekuwa yakitokea na ndiyo maana siku hizi tumekuwa tukiona kila siku na ningependa haya maswali Serikali itujibu.

Polisi kwenda kwenye matukio ya ujambazi, majambazi wameteka benki, majambazi wamekwenda kwenye mipaka kote wameteka Vituo vya Polisi halafu wakishatoweka ndiyo unakuta Polisi wanakuja. Waulize ni kwa nini wanafanya hivi? Ni kwamba, hawana vifaa vya

kwenda kuwa-*attack* majambazi kwa wakati huo? Kwa hiyo, hayo ndiyo maswali ambayo Wananchi wanataka majibu yake.

Vilevile huko vijijini na mimi nizungumzie kijiji kwetu hususan Jimbo la Mbozi Magharibi Momba; kwa mfano, Kamsamba, Kapele na kadhalika. Yanapotokea matukio; kwa mfano, mauaji, Polisi wakipigiwa simu kabla ya kwenda wanawauliza Wananchi mna mafuta? Sasa tuambieni huu utaratibu utakwenda mpaka lini? Wananchi wachangie mafuta ndiyo waende na kama hawana mafuta hakuna Polisi anayekwenda! Kwa hiyo, unakuta mtu amejinyonga, maiti inakaa siku nne mpaka inaoza, watu wanaogopa vilevile kutoa ushahidi. Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo inabidi tuelezwe, ni kwa nini Polisi wawalipishe Wananchi fedha ndiyo waende kule?

Jambo la tatu ambalo limekuwa likilalamikiwa sana ni kitendo cha Polisi kubambikia Wananchi kesi. Sasa hivi tunatakiwa tuiombe Serikali, nafikiri South Africa mambo kama hayo yapo, kunakuwa na Kitengo Maalum ambacho Mwananchi akibambikiwa kesi anakwenda kulalamika kwenye Kitengo kile ili apelekewe Polisi husika. Leo hii Mwananchi anabambikiwa kesi ya kubaka au kesi ya wizi halafu anaambiwa nenda ukashtaki kwa *OCD* au kwa *RPC!* Tangu lini kesi ya nyani akapelekewa ngedere wakati wote ni wezi wa mahindi? Hii haieleweki, haiwezekani na haikubaliki. Kwa hiyo, hili tungependa Serikali sasa ianze rasmi na ianzishe Kitengo Maalum ambacho Wananchi watakuwa huru kupeleka malalamiko yao dhidi ya Jeshi la Polisi ama Askari husika ambao wanawanyanyasa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu limekuwa likizungumzwa hapa na Wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu posho za Polisi na kadhalika. Pamoja na ugumu wote wanaoupata, lakini jamani na wao ni binadamu, wanahitaji wapate angalau masilahi ambayo yanawawezesha. Leo rushwa imekuwa kubwa kwenye Jeshi la Polisi kwa sababu moja tumekuwa tukizungumza ni masilahi madogo. Jambo la pili ni tabia. Sasa tunawaambia miongoni mwa *solution* ukimwuliza mtu kwa nini unachukua rushwa, atakwambia mwanangu hana ada. Serikali kwa nini isichukue jukumu la kusomesha watoto wote wa wafanyakazi kuanzia kwenye Majeshi ya Polisi, Jeshi la Ulinzi na wafanyakazi wengine; Serikali inashindwa hilo? Kutoa *credit* hiyo mnashindwa jamani? Mtakuwa ni Serikali ya namna gani?

Serikali mnashindwa kutoa Bima za Afya? Hiki ni kitu ambacho kinawezekana, mtatoa Bima ya Afya kwa wafanyakazi wote, hakuna mtu ambaye anakwenda pale, maana yake ni lazima uchukue rushwa, mke wako anaumwa au anahitaji operesheni huna fedha unategemea nini? Lazima mtu atakwenda kuchukua rushwa. Hili nalo linawashinda? Watu 450,000 tu hili linawashinda jamani? Ni mambo madogo ambayo mnaweza kuyafanya Serikali ikaaminika, lakini mambo madogo kama hayo mnashindwa! Mnataka jamani tuwaambie nini ili muelewe? Haya ndiyo ambayo siku zote tumekuwa tukiwashtaki.

Twende sasa tukachunguze, rushwa imekithiri, imekithiri wapi? Utashangaa *Traffic* barabarani, rushwa imekithiri kwa sababu faini ya shilingi 30,000 ni kubwa. Mimi nawaambia ukweli, mtu akiambiwa atoe 30,000 na 10,000 atatoa shilingi ngapi? Kwa hiyo, utakuta mwisho wa siku, Serikali badala ya kupata 30,000 Mwananchi anaona ni bora kumpatia Askari 10,000, kwa hiyo, anampa 10,000 gari linakwenda mbele. Matokeo yake mtakuja hapa mwaka kesho mtasema mapato tuliyopanga Serikali ikusanye kutokana na faini na makosa mengine ni shilingi 10,000,000,000, hiyo fedha haitapatikana mtakuja na kigezo kingine, faini iongezeke mpaka shilingi 50,000. Kiukweli siyo hivyo, Wananchi wanaona faini ni kubwa, matokeo yake fedha zote zinakwenda kwa Polisi ndiyo Mapolisi wamekuwa wakiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nalo ni lazima tulizingatie, tunapokwenda kubadilisha *Finance Bill* mwaka huu, miongoni mwa vifungu vitakavyoletwa ni kupunguza faini kutoka shilingi 30,000 mpaka ifike hata shilingi 10,000.

Jambo lingine la kuzingatia ni kwamba, kwenye magari makubwa ambayo sasa yanasababisha ajali kila siku, yamekuwa yakiuwa watu wengine, inatakiwa utaratibu uwe mwingine. Ikiwezekana magari yanayosababisha ajali nyingi, hizo kampuni zifungieni na hao wenye magari makubwa kama yanayobeba watu zaidi ya 50, mkishindwa kuwafungia basi faini zao ziwe hata milioni na kitu. Lazima pia muweke *deadline*, mtu akitoka Mbeya mumpangie kama ni saa 12 basi afike baada ya saa 12. Gari linatembea saa saba kilomita 900 au hata 1000 unategemea watu wakipata ajali hapo wanakufaje? Kwa hiyo, naomba Serikali izingatie na tunawapa mawazo makini ili utendaji wa kazi uwezekane. Kwa hiyo, hayo ni mawazo ya Upinzani naona yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nikuhakikishie tu kwamba, uwepo wako hapo unanipa amani iliyopitiliza kwenye moyo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nataka Mheshimiwa Waziri anieleze katika hizo bajeti zote zinazopangwa ni vigezo gani vinavyomfanya mwanadamu aweze kuishi kwa shilingi 500 kwa siku! Sisi hapa watoto wetu hata wakienda shule huwezi kumpa shilingi 500 ilhali kila kitu anakuja kukikuta ndani. Shilingi 500 kwa wafungwa tunakiuka haki za msingi za binadamu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuridhia sisi wafungwa waendelee kupangiwa bajeti ya shilingi 500 kwa siku hatutendi haki na Mwenyezi Mungu, anatuona tunalolifanya. Mwenyezi Mungu ni mkubwa na hakuna limshindalo, msije mkamlazimisha akaliachia zege hilo likatuangukia kwa dhuluma tunayowafanyia binadamu wenzetu. Anaweza kuliachia hilo likaangukia humu na waja wema kama mimi na wenzangu, tukapata njia ya kutokea. *(Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia Magereza wametengewa magari manane. Jeshi la Magereza Tanzania nzima kuipangia magari manane kwa kweli bado hatuwatendei haki. Wizara ya Katiba na Sheria nasikia wamewekewa magari 218 na pikipiki 200. Tafadhali, hebu tuangalie wale watendaji, ndiyo hayo yanayosababisha Mahabusu kuendelea kurundikana Magerezani hawafikishwi Mahakamani kupata haki zao. Hilo ni jambo la kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siridhiki na posho ya shilingi 5,000 wanayolipwa Askari. Bajeti iliyopita ilipitishwa hapa Askari wapewe shilingi 225,000 kwa mwezi, hilo jambo halikufanyika. Mheshimiwa Waziri wangu Kivuli alilizungumzia hili akauliza ni deni au nini wameandikiwa Askari hao? Tukishakukipitisha kitu hapa lazima kitekelezwe hakuna njia nyingine. Tuambieni malipo tuliyoidhinisha Askari walipwe ya posho ya chakula ni nini hatima ya haki yao hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kitu kingine ambacho kimenigusa sana, nacho ni uchochezi katika nchi hii. Hakuna aliye juu ya sheria katika nchi hii, sote tunapaswa kuitii sheria, nataka Mheshimiwa Waziri unieleze hatua ulizozichukua angalau za kiupelelezi na kufuatilia kwa wachochezi hawa watatu ambao ni hatari kwa Taifa hili. Unipe taarifa ya uchochezi alioufanya Kanisani Mheshimiwa William Lukuvi, taarifa ya uchochezi alioufanya

Mheshimiwa Janeth Mbene Kanisani na uchochezi anaoendelea kuufanya hadi sasa Mheshimiwa Martha Umbulla kule Kiteto. Tunataka kuyajua haya kwa kujua kwamba, hakuna aliye juu ya sheria. *(Makofi)*

Bunge la Katiba tuliwekewa Ukumbi huu tujadili masuala ya Katiba, haikuwa sahihi kwa Mheshimiwa Lukuvi kwenda Kanisani na akahubiri masuala ya siasa Kanisani. Kila mtu ana dini yake na sisi tuna Misikiti yetu, tungeweza kwenda tukafuata kama akili yake yeye sasa hivi ingekuwa ni vurugu ndani ya nchi hii. Leo badala ya kupewa nafasi katika Bunge la Katiba kuondoa angalau kuomba radhi kama uungwana aliounesha jana Mheshimiwa Werema, alikuja kuendeleza uchochezi. Hatuwezi kuridhia uchochezi unaofanywa kwa kutumia mwamvuli wa madaraka walionao baadhi ya watu, hakuna aliye juu ya sheria ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Janeth Mbene, alikwenda Kanisani na vyombo vya habari mbalimbali vilimkariri akisema kwamba, wanaotaka Serikali Tatu wanataka kuleta ushoga! Hii haikuwa sahihi, tunataka tujue Jeshi la Polisi limewahoji? Wamejibu nini na nini kilifuatiliwa? Kuziacha kauli hizi za uchochezi ndani ya nchi ziendelee ni hatari kwa mustakabali wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Bibi Mkubwa Martha Umbulla, matatizo ya Jimboni Kiteto ambayo kila siku tunasikia mauaji kati ya wakulima na wafugaji, hayawezi kuendelea kuvumiliwa. Tunataka kujua Mkuu huyu wa Wilaya mmemchukulia hatua gani angalau za kumhoji na kuieleza nchi hii nini hatima ya mambo anayoyasababisha kila siku. Athari hizo angefanya hukohuko Kiteto, zimekuja mpaka Kibaigwa, sasa ukipita pale Kibaigwa ni lazima uongeze *speed* kwa kuhofia Martha Umbulla kwa fitina na uchochezi wake. Tunataka kujua hatima na mnachukua hatua gani kumshughulikia Mkuu wa Wilaya mchochezi kuliko wote nchi hii Martha Umbulla. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia Vitambulisho vya Taifa kwa upande wa Zanzibar. Hadi sasa tunavyozungumza, zoezi limemalizika Zanzibar likiwa limeacha Wananchi zaidi ya 4,500 katika Wilaya moja tu ya Micheweni hawakupata haki yao hii ya msingi. Katika kutunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba hapa na kura ya maoni, hili jambo tulilisema sana. Maimamu, Mapadri na Masheikh waliotangulia kila mmoja wana warithi wanaowafuatilia kwa nyendo na tabia, lakini Zanzibar kuna Wajukuu wa Firauni wanaitwa Masheha; hawa ni vizazi vya Firauni, wanawatesa na wanawanyima Wazanzibari haki yao ya kupata vitambulisho. Ninasema ni Wajukuu wa Firauni kwa sababu Firauni ni mchochezi na mtendaji vitendo visivyotakiwa kufanyiwa binadamu.

Ninawaambia hivyo wanapata nguvu ya kusimamiwa na Serikali ya SMZ. Nawaonya na ninasema nimeomba hapa jana kwamba, raia wale hawapati Vitambulisho vya Utanzania. Vitambulisho vya Zanzibar wamenyimwa, itangazieni Dunia ielewe kama kuna watu wasiotakiwa na nchi yao kule Zanzibar. Dunia na Taasisi za Kimataifa za haki za binadamu zitajua ziwachukue ziwapeleke wapi watu wale. Hatutakubali, kwa hili hatutasikia la mnadi swala wala la mteka maji Msikitini, hatutasikia la Padri wala mkata bustani Kanisani, lazima Wazanzibari wote wahakikishwe wameandikishwa na hiyo hofu kwamba, ikifika wakati wa kura ya Serikali Tatu iwaondokee kwa sababu hilo halizuiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naonya sana mtupe taarifa ya Martha Umbulla, William Lukuvi na Janeth Mbene hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Idd Azzan. Mheshimiwa Ritta!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na nukuu ya Mchungaji Peter Msigwa wa Jimbo la Iringa Mjini, inasema hivi: "Haiwezekani akili ndogo kutawala akili kubwa." (*Makofi*)

Kwa akili yake hiyo kubwa alisababisha gari la zimamoto Iringa likapigwa mawe, likavunjwa vioo na akafanya uharibifu mkubwa sana wa Jeshi la Polisi. Hiyo ni akili kubwa au ndogo?

**MBUNGE FULANI:** Kubwa!

**MBUNGE MWINGINE:** Ndogo!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, aliahidi kwamba, angeweza kulipa lile gari, mpaka leo hii bado hajafanya lolote na ninasema sheria lazima ishike mkondo wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole nyingi sana kwa Askari wetu wa Jeshi hili la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto, wamekuwa wakifanya kazi kwenye mazingira magumu sana, wamekuwa wakilipwa mishahara duni na wamekuwa wakiishi kwenye mazingira magumu. Makazi ya Askari Polisi kwa kweli yanasikitisha sana. Mimi hapa nilikuwa Diwani katika Kata ya Ukonga, najua hali halisi ya makazi ya hawa askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi hayo yanaweza yakasababisha hata majanga kwenye familia zao, wakaweza kwenda hata kwenye michepuko. Mimi ninaomba jeshi hili liongezewe fedha za kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa kujiamini na kutolaumiwa kwa mishahara midogo wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu uhaba wa Vituo vya Polisi katika Mkoa wetu wa Iringa. Mkoa wa Iringa una uhaba mkubwa sana wa Vituo vya Polisi. Serikali bado haijaweza kuleta fedha ya kutosha katika Mkoa wetu ili kutatua hili tatizo. Kuna changamoto nyingi sana, kuna baadhi ya vituo ambavyo Wananchi wameona sasa walisaidie Jeshi hili, wameweza kutoa nguvu zao, kama Vituo vya Ifunda na Isimani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaishukuru sana *TANAPA*, wameweza kujenga nyumba nzuri sana ya askari pale Idodi, lakini bado hakuna Kituo cha Polisi. Ninaomba leo Waziri atakapokuwa anajibu, aseme ni lini Jeshi hili litaleta fedha ili vituo hivi viweze kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hii changamoto, hata mimi kama Mbunge naomba mchango wangu utambulike, nimejenga kituo cha kisasa katika Jimbo la Iringa Mjini. Kituo kikubwa ambacho kitasaidia Kata karibu nne; Kata ya Kihesa, Mtwilila, Gangilonga na Mkimbizi. Baada ya Bunge hili nitaweza kukabidhi kituo kile ili kuondoa hii changamoto. Pia nitawaomba Wabunge wote bila kujali itikadi zetu, twende pamoja tukafungue kile kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Ofisi ya Wilaya ya Kilolo. Hii Ofisi kwa kweli inatia aibu, taasisi zote zimeshajenga ofisi katika Makao Makuu, lakini Jeshi la Polisi bado halijaweza kujenga Ofisi ya Wilaya. Siku zote Wananchi wanapata shida sana kwenda kwenye Makao Makuu ya Polisi. Ninaomba na hili nalo liwe mwisho, mwakani hatutaki kuzungumzia habari ya kujenga ofisi kwenye Wilaya ya Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie wazabuni kulidai Jeshi la Polisi; ni aibu kubwa sana na udhalilishaji mkubwa Jeshi hili kudaiwa na wazabuni. Hawa wazabuni ni wafanyabiashara wa kati ambao na wao wamechukua mikopo benki, lakini wanakopwa huduma zote; huduma za mafuta, vyakula kwenye Magareza na kila huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wetu hawatendewi haki kwa kutoletewa hizi fedha ili waweze kulipwa. Naomba sasa hivi watuambie ni mkakati gani watautumia kuhakikisha wale wazabuni sasa hawalidai Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sasa kuhusiana na Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto nalo limekuwa likifanya kazi kwenye mazingira magumu kabisa; hakuna magari ya kutosha. Naomba tuletewe magari ya kutosha kwa sababu Mkoa wetu wa Iringa una msitu mkubwa, unahitaji gari likae pale. Mkoa wetu wa Iringa sasa hivi kuna Uwanja wa Ndege, tunatakiwa tupate gari la zimamoto. Mkoa wetu wa Iringa kuna ile Barabara ya Kitonga ambayo mara kwa mara kumekuwa kukitokea ajali, wanatakiwa waletewe fungu la kutosha ili tupate *crane* ya kuondolea magari, kwa sababu kila wakati magari yamekuwa yakiziba barabara na ile ni barabara kubwa ambayo magari mengi yanapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali sasa hivi isifanye makosa, ihakikishe Mkoa wetu wa Iringa unapatiwa fedha za kutosha ili kuweza kuondoa changamoto zinazoukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hawa Wakuu wa Mikoa wa Zimamoto wamekuwa wakikaimu sasa kwa kipindi cha miaka mitatu, watakaimu mpaka lini? Kama wana uwezo kwa nini msiwathibitishe na kama hawana sifa kwa nini msiwaondoe? Hata vyeo vyao vyenyewe havieleweki kuanzia *general.* Naomba sasa hivi jamani hebu angalieni, askari wapeni haki zao, kama ni kupandishwa vyeo wapandishwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niseme kwamba, nimechangia kwa maandishi na nitaleta yote yaingie. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati, kama Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani atasahau kukushukuru, nianze mimi kukushukuru kwa kujenga Kituo cha Polisi cha kisasa pale Iringa Mjini; hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Iddi Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Mama Anna Abdallah!

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana *IGP* ambaye ameteuliwa hivi karibuni kushika nafasi hii, Ndugu Manju. Nina hakika yeye ni Polisi, kwa hiyo, Jeshi la Polisi limepata Polisi wa kufanya kazi vizuri, kupambana na uhalifu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nitamke wazi kwamba, mimi siungi mkono Hotuba ya Waziri pamoja na bajeti yake. Siungi mkono kwa sababu moja kubwa; nimeanza kuchangia Wizara hii katika bajeti na hii ni mara ya tisa sasa na mara zote nimekuwa nikizungumzia suala la nyumba chakavu katika Kituo cha Polisi Magomeni. Mwaka 2011, kwenye bajeti ya 2011/2012 nilimwomba Waziri tufuatane aende akajionee mwenyewe hali halisi, Waziri aliitikia kwa kukubali lakini mpaka hivi leo pamoja na kukumbusha katika bajeti zilizofuatia zote, Waziri hajaja kukagua. Kwa hiyo, hii ni dharau na mimi naona si dharau kwangu tu, bali ni pamoja na kwa askari ambao wanaishi kwenye nyumba zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inanipa nafasi ya kusema kwamba, siungi mkono. Nimezungumzia sana suala la nyumba chakavu na nimeona kwenye bajeti zimejengwa karibu nyumba 350 katika maeneo ya Kunduchi, lakini tukubaline hali ya Dar es Salaam ilivyo, hali ya Kinondoni ilivyo, Wilaya ambayo ina watu takribani milioni mbili, kituo ninachokizungumzia cha Magomeni kinahudumia maeneo makubwa karibu na mikoa mingine katika nchi hii, lakini nyumba za kukaa askari hakuna. Askari wanakaa kwenye hanga ambalo limejengwa tangu miaka ya 1970 mpaka leo. Askari hawa wana familia, wanaishi na familia zao humo, ninarudia tena wanaishi utadhani labda ni kuku wa kizungu wanaofugwa mle, tena siyo wa kizungu wa kienyeji, maana wa kizungu wanamulikwa taa, wa kienyeji wanalala giza tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hali hii hainifurahishi na haiwafurahishi askari ambao wanaishi pale. Kama kweli tunawathamini na wanatufanyia kazi nzuri, lazima pia tuheshimu na tuthamini utu wao. Kuwaweka askari katika maeneo yale, haipendezi. Hizo nyumba 350 mlizojenga Kunduchi mngeweza mkajenga hata nyumba kumi Magomeni, ama mkajenga jengo moja lenye ghorofa tano mkawaweka askari wakakaa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi katika Manispaa ya Kinondoni ni kubwa mno, kwa sababu uhalifu ni mwingi na uhalifu huu unasababishwa na ongezeko kubwa la watu katika wilaya hiyo. Kwa hiyo, kama hatukuimarisha ulinzi, kama hatukuwaweka askari wetu vizuri, ulinzi utakuwa ni wa wasiwasi sana katika maeneo hayo. Ninaomba tena na ninamheshimu sana Mheshimiwa Chikawe, najua utendaji wake wa kazi ni mzuri, amefanya kazi vizuri kwenye Wizara alizopita, ni matarajio yangu baada ya Bunge hili kwisha, tutaungana pamoja twende tukaangalie makazi ya askari katika Kituo cha Magomeni, ili kwa pamoja tuone ni jinsi gani tutaboresha makazi yao, kuliko kuwaacha kama vile walivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujambazi umekithiri, lakini namshukuru sana *RPC* ambaye yupo hivi sasa, aliyeondoka alifanya kazi nzuri, lakini ambaye yupo hivi sasa anafanya kazi nzuri sana. Kazi yake inakuwa haina tija sana kwa sababu ya vitendea kazi; hana vitendea kazi vinavyotosha; hana magari ya kutosha na hana pikipiki za kutosha. Tunafahamu kwamba, wezi wengi hivi sasa wanatumia pikipiki, kwa hiyo, ili askari waweze kukabiliana nao ni lazima askari nao wawe na pikipiki pamoja na magari. Hatutarajii Polisi naye aendelee kutumia *boxer* kama ambavyo wanatumia majambazi hawa, ni lazima itafutwe pikipiki yenye uwezo mkubwa wa kupambana, kufukuza na kukabiliana na majambazi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kama tutapatiwa vitendea kazi vya kutosha, *RPC* na Askari wa Wilaya ya Kinondoni ambao ni Mkoa wa Kipolisi, wataweza kupambana na janga hili kubwa la uhalifu. Kinondoni ndiyo Wilaya kubwa hapa Tanzania yenye watu wengi.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Siungi mkono. Kinondoni ndiyo Wilaya kubwa yenye watu wengi na uhalifu ni mwingi, kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe tunaisaidia. Tofauti na ilivyo kwenye baadhi ya

mikoa, Kinondoni ina watu wengi kuliko baadhi ya mikoa; kwa hiyo, naomba kabisa tupewe kipaumbele katika kupatiwa vifaa na zana za kupambana na ujambazi na uhalifu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyeo, wenzangu wamezungumza; ni kweli askari wanapandishwa vyeo lakini askari hawa wadogo kupanda vyeo ni mbinde. Ukipata Ukoplo wewe basi mpaka utakufa na Ukoplo wato tu, lakini hawa wanaokuja wakitoka shule ana ka-diploma ana ka-digrii basi vinyota vinafukuzana tu mpaka vinaulizana mwenzangu umekuja lini, lakini hawa wadogo kupandishwa vyeo imekuwa tabu. Ninamwomba sana *IGP,* tuwaangalie na hawa askari wadogo jinsi ya kuwapandisha vyeo, angalau wafikie hata kwenye Umeja, pamoja na kwamba mnasema labda elimu zao siyo za kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito tena, kama hawa ambao wana *degrees* na *diplomas* wanaendelea kupewa nafasi ya kujiendeleza kimasomo na hawa wadogo nao wapewe nafasi ya kusoma ili nao waweze kufikia nafasi ya kuwa na vyeo vya uafisa wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la posho limezungumzwa na mimi nasisitiza posho ni ndogo, lakini hata mishahara kwa askari bado ni midogo. Askari hawa wanafanya kazi kubwa sana, kwa hiyo, naomba nao waongezewe posho.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Azzan. Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. ANNA MAGRETH ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Vilevile naungana na wenzangu waliokwishatangulia pande zote mbili, ambao wametetea kwa nguvu zao zote suala la posho ya chakula, vitendea kazi, malazi ya askari, ofisi nadhifu za kufanyia kazi, waliosemea chakula cha wafungwa pamoja na nguo za wafungwa. Vilevile, katika hao wafungwa, wengine wako katika maeneo ya baridi, lazima wafikiriwe kupewa nguo ambazo zitakidhi hali ya hewa ya baridi pale mahali walipofungiwa. Hao wote mimi ninaungana nao mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana mkono sana na wote wanaotetea na waliotetea kwamba, Wizara hii inapaswa kupata fedha zake zote inazoziomba. Mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Ulinzi na Usalama, leo nimepata faraja sana, ukiacha vijineno vya hapa na pale, ninaona sasa humu ndani tunaelewana sana juu ya umuhimu wa Wizara hii. Mimi niwapongeze na ninawashukuru, ninakubaliana na ninyi. Sikukubaliana na maneno yale ya kuiombea CCM sijui ifanye nini, lile kweli ni dua la kuku, kwa sababu mifano ipo. Haya mambo siyo mazuri kwa sababu unamwombea mtu dua halafu inakuja kukupata wewe, baadaye inakuja kuwa tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mambo mawili makubwa na moja dogo. Kwanza, Wizara hii Idara zake zote na kasma zote zinaanza mwaka mpya ujao na madeni makubwa ya nyuma. Hii ni mbaya sana, kwa hiyo, hicho kidogo watakachokipata wataanza kulipa madeni maana yake hawatakuwa na kitu cha kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, fedha za mipango ya maendeleo, nisemee *NIDA* na kuna wengine wamezungumzia, *NIDA* walipangiwa shilingi bilioni 152.2 mpaka mwezi Machi wamepata shilingi bilioni 35 tu, sasa watafanyaje kazi hii muhimu? Haya yako katika Wizara nzima, mwanzo mwisho ndiyo hali ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulisemea ni suala la mafunzo ya askari wote walio katika Wizara hii. Ndugu zangu, Kamati ilikwenda Moshi kwenye Chuo Kikuu cha Polisi. Leo wahalifu wameongeza mbinu za uhalifu, wanatumia TEHAMA hizi hizi ambazo wote tunazitafuta wao wanazitumia. Tulipokwenda kwenye chuo kile tulikuta kompyuta za mafunzo 23 tu, ni aibu. Haki yake kila mwanafunzi pale angekuwa na kompyuta yake, siyo kutumia kwa zamu. Kwa hiyo, suala la mafunzo kwa Idara zote zilizo chini ya Wizara hii, ni muhimu na wajifunze hizi mbinu za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru kwa upande wa Polisi, wameanzisha kile wanachosema wenyewe Kamisheni ya Intelijensia. Hili ni jambo zuri sana, lakini Intelijensia bila kuwa na mbinu na mafunzo ya kisasa haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Polisi Jamii. Polisi Jamii Dunia nzima ipo, pengine sisi ni jina tu, lakini Dunia nzima wana Polisi Jamii; nenda Uingereza wapo, popote pale lazima Wananchi wenyewe washiriki katika ulinzi wa nchi yao. Kwa hiyo, tusidharau Polisi Jamii, wala siyo kushindwa kesi. Hata wale walioendelea sana *concept* ya Polisi Jamii katika maeneo yao ipo. Kwa hiyo, hili ni jambo la kupongeza na liendelezwe na wawezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Mheshimiwa Mrema alipompongeza Waziri, huko nyuma kulikuwa na Tajirika na Mrema. Naomba niseme kwamba, hii Tajirika na Chikawe kazi yake iwe ya kufichua mambo ambayo yanahatarisha amani ya nchi yetu, zitumike vilevile kuokoa mali za umma ambazo zinataka kutoroshwa kama vile meno ya Tembo na vitu kama hivyo. Hawa watu wazawadiwe vizuri ili wengine waone kumbe tukifanya hivi hii ni njia mojawapo ya kutajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; tulikwenda kutembelea Mkoa wa Kilimanjaro, pale Moshi, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wana mpango wa kuwafuatilia *agents* wanaowapokea wahamiaji haramu. Sasa vijana wetu tunawaomba watumie hii Tajirika ya Chikawe wawasaidie kule Moshi na mipakani kule, wale watu wanaowapokea wahamiaji haramu.

Jambo hili ni zuri sana kwa sababu watakaokuwa wanafanya ni vijana, hawa hawa Polisi Jamii na Wananchi wa kawaida. Sasa ile simu ilitajwa na yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri atakaposema hapa atajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninachotaka sasa kumalizia ni kwamba, kwa kweli utaratibu wetu wa kugawa fedha na watu wanakwenda pale Hazina wanajadiliana basi nitakupa kiasi fulani, kuna idara hapa ambazo ukiacha kuzipa fedha hatulali usingizi, ni pamoja na Wizara hii. *(Makofi)*

Mimi ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuungane mkono tuibane Serikali kuhakikisha kwamba, Wizara hii inapata fedha zote inazozihitaji kwa masilahi ya amani na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mama Anna Magreth Abdallah. Mheshimiwa Kange Lugola atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Sururu Juma.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nimejisikia vibaya sana Mheshimiwa Iddi Azzan, alipotaja Kituo cha Polisi Magomeni, wakati mimi niliwahi kuwa Mkuu wa Kituo hicho cha Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni-*declare interest,* nimekuwa Afisa wa Polisi na mpaka sasa mke wangu Mary, Mama Marietha ni Afisa wa Polisi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hongera.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumwuliza maswali Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Chikawe, hivi haoni aibu kuleta bajeti hii inayohusu ulinzi na usalama wa maisha ya watu na mali zao isiyotekelezeka? Haoni aibu kuleta bajeti inayohusu ulinzi na usalama isiyo na mwelekeo wowote wa kutatua matatizo ya makazi duni ya askari? Haoni aibu kuleta bajeti hii katika Bunge hili ambayo haina majibu ya namna gani maslahi ya Polisi yatakavyoboreshwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia haoni aibu kuleta bajeti yenye maneno yaleyale, kwa nini nasema yaleyale na isiyotekelezeka. Mwaka jana aliomba tumpe shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga nyumba za askari Mkoa wa Mwanza, lakini mpaka sasa ninavyozungumza katika shilingi milioni 600, hakuna senti hata moja ambayo imeletwa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninavyozungumza mwaka jana tulimtengea shilingi milioni 600 kwa ajili ya nyumba za Polisi Mkoa wa Mara, ni shilingi milioni 275 tu zimepelekwa na kwa fedheha pia tulitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya makazi ya Polisi Mkoa wa Kagera, hivi ninavyozungumza hata senti tano haijapelekwa. Inakuwaje Wabunge tunaendelea kupiga kelele hapa, hizi ni porojo, Bunge hili lisikubali hata kidogo kukubali bajeti za blaa blaa, bajeti ambazo hazitekelezeki, bajeti za ngonjera, bajeti za ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Askari wa Polisi, Magereza, Uhamiaji. Mishahara imekuwa ni duni, posho zao zimekuwa ni duni wakipanda vyeo hawalipwi. Tumepiga kelele hapa juu ya posho za chakula za askari hawa na mimi huyu huyu akiwepo Mheshimiwa Waziri Nchimbi nilijenga hoja hapa kwa nini Askari Polisi, Magereza na Uhamiaji wanabaguliwa kwenye posho za lishe, posho za chakula. Wanajeshi wanapata shilingi 225,000/= wao wanapata shilingi 150,000/= maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema hizi posho hata ukiwa mkubwa wa ngazi ya juu jeshini unapata sawa na asiye na cheo au mwenye cheo cha chini kwa maana hakuna ubaguzi. Kwa nini posho hizi zinabaguliwa kwenye majeshi. Nikasema kwa sababu ni za chakula, hata kwenye gwaride la Muungano askari wale chini ya Kamanda Mkuu wa Jeshi la Wananchi anawaamrisha wakiwa wamoja, askari hawa wa ulinzi na usalama wote wanageuka kulia na kushoto kwa nguvu zilezile, wote viatu vyao na kofia zinachomoka kwa nguvu zile zile na wote anawaamrisha kutoa heshima ya utii kwa Amri Jeshi Mkuu himahima na wote wanaitikia kwa lishe ya sauti moja Tanzania. Wote wanasogea mbele hatua 15 kutoa heshima, wote wanakwenda wanakanyaga mguu sawa kwa lishe ile ile kwa nini wanabaguliwa. (*Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, leo unaongezea hoja nyingine yalipotokea maafa Zanzibar ile boti ya *Skagit,* nina gazeti hapa la mwananchi *front page* wako Wanajeshi, Polisi, Jeshi la Uokoaji wote wamebeba jeneza, wote wanatumia lishe ile ile na nimeona mikono yao imetuna

misuli kwa maana kwamba wanafanya kazi moja ya kutumia misuli na nitaomba Mheshimiwa Chikawe nikukabidhi gazeti hili ili uone jinsi walivyobeba jeneza wakati wanaopoa maiti wakati ilipozama boti kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu kwa wavuvi Ziwa Victoria. Kwenye bajeti humu hakuna mikakati yoyote ya namna ambavyo Polisi watapambana na uhalifu Ziwa Victoria kwa wavuvi wetu na ndio sababu wavuvi hawachangii pato la Taifa kwa kiwango kinachotakiwa. Wanaingia mikopo, nyavu zao zinaporwa, injini zinaporwa na wao wanauawa au kujeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwaje Mkoa wa Mara kuna kituo kimoja tu cha *Marine* pale Sota kitahudumiaje Wilaya sita ndani ya Ziwa Victoria. Ukienda Mwanza kuna kituo kimoja tu cha *Marine* kitahudumiaje Wilaya sita ndani ya Mkoa Mwanza, vivyo hivyo na Kagera kule Kerebe, Goziba, Ukerewe na Irugwa. Irugwa mwezi Aprili wavuvi wamenyang'anywa injini sita ikiwemo ya Josephat Kusekwa Masururi pamoja na Dewji Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Ukara mwezi Mei tarehe 2 wamenyang'wanywa mashine sita katika Kijiji cha Chifule, Chibasi lakini hawana msaada wowote ndani ya Ziwa Victoria. Ukienda Sota boti wanayotumia ni *old model* inatumia mafuta lita 3,000 na mwendo ni wa kusuasua wa kinyonga, watakwendaje mpaka kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalishauri Jeshi la Polisi, fungueni vituo vya *Police Marine* kila Wilaya ili wakiwa na vituo vya Polisi kwenye Wilaya itakuwa ni rahisi kukabiliana na uhalifu ndani ya Ziwa Victoria. Mwibara pale tumeomba Wilaya ya Kipolisi mpaka sasa Mheshimiwa Chikawe naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gereza la Bunda ukienda pale ni aibu, hivi sh. 500/= wanakula wafungwa, sh. 500/= wanakula mahabusu. Mahabusu hajatiwa hatiani na yeye mnam-*subject* kula sh. 500.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono bajeti hii mpaka nipate majibu ya uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Chikawe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Sururu Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said!

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisimamisha hapa nikiwa na afya na mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono Wizara hii kwa asilimia mia. Pili, napenda kuwapa pole Masheha wote wa Zanzibar kwa kuitwa vijukuu wa Firauni. Tuliokuwepo hapa tunasema tusiitane majina yaliyokuwa sio mazuri, sasa nashangaa kwa nini wanaitwa majina hayo wakati tukijua kwamba *firauni* ni *finnari jahannam*. Kwa hivyo, nawapa pole Masheha wote wa Zanzibar, hayo ndiyo maneno ya wanasiasa na mimi kwa niaba yao nawaomba radhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Bububu kuna jengo la makazi ya Polisi la siku nyingi ambalo limejengwa karibuni miaka minne lakini nasikitika hadi leo halijamalizwa jengo lile. Limefikia hatua nzuri tu, lakini bado askari wale hawajaanza kutumia kwa ajili ya kuishi. Hivyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii kufanya jitihada za ziada kuweza kulimaliza ili

askari wale wapate kuishi. Tayari jengo lile limeshaezekwa, limeshatiwa madirisha, kilichobaki ni kutiwa sakafu, vyoo, mifereji na milango ya ndani. Kwa hivyo, naiomba Wizara kulikamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Jimbo langu niliwahi kuomba kituo kidogo cha Polisi, *Police Post* katika eneo la Kijichi. Jimbo langu limekaribiana na Jimbo la Dole. Kwa hiyo, kituo kile kidogo kinaweza kusaidia masuala ya ulinzi katika eneo la Bububu, Dole, Kizimbani na kadhalika. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwa mwaka huu waweze kuanzisha kituo kile ili ulinzi na usalama uimarike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisiwa cha Zanzibar kimezungukwa na hoteli nyingi za kitalii na katika harakati za Zanzibar inatakiwa ulinzi na usalama uwe wa hali ya juu wa saa 24, lakini cha kusikitisha ni kwamba, Zanzibar imekosa vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya ulinzi huo wa utalii. Hivyo, naiomba Wizara itilie mkazo vifaa hivi hasa kwa upande wa Paje, Nungwi na Matemwe waweze kupatiwa usafiri wa gari lililokuwa madhubuti kwa ajili ya ulinzi liweze kusaidia katika doria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Zanzibar inakuwa inatoa huduma ya ulinzi katika majengo mbalimbali, ofisi za Serikali na kadhalika na ulinzi ule unakuwa masaa 24. Kwa bahati nzuri taasisi zile zinafanya malipo lakini kupitia Makao Makuu ya Polisi, Tanzania Bara. Je, nataka kuuliza malipo yale yanarejeshwa kule Zanzibar kwa ajili ya huduma ile na kama hayarejeshwi kwa sababu gani na huduma inatokea kule na ikijulikana kwamba Zanzibar ina upungufu mkubwa wa fedha za matumizi katika kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika kazi ya doria kumekuwa na upungufu mkubwa wa mafuta, kwa hivyo, kazi inakuwa ngumu katika kuhudumia kazi hiyo. Nataka kujua je, Wizara ina mgao gani wa mafuta kwa kila *zone* maana yake kila tukiuliza kule Polisi wanaambiwa mafuta yamekuwa kidogo, vifaa hatuna, je, Serikali ina mkakati gani katika kuongeza kasi ya ulinzi Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maslahi ya Askari Polisi. Naungana na wenzangu katika kuwaombea maslahi haya yaongezeke hasa kwa wale askari wenye *rank* ya chini. Nasikia wale wa *rank* ya chini wanapewa pango ya sh. 15,000/=, je. inatosha jamani?

**MBUNGE FULANI:** Haitoshi.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Siku hizi kuna nyumba gani ya sh. 15,000/= kwa mwezi?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Kwa hivyo, tunawaombea wazidishiwe maslahi ili wapate kujenga maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Jimbo la Dole kule kuna Kituo cha Polisi cha Mwera na Mchomeke. Vituo hivi ni vya siku nyingi vinahitaji ukarabati mkubwa zaidi kwa sababu ndio kinahudumia katika Mkoa wa Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, sina zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi. Mheshimiwa Mwanakhamis!

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru nami kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Kwanza nisije nikasahau naunga mkono Wizara hii. Wenzangu wengi waliotangulia wamezungumzia kuhusu Askari Polisi, matatizo yao na kero zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwuliza Mheshimiwa Waziri na suala hili nataka anijibu kwa sababu nilishawahi kuliulizia hapa. Askari Polisi wanapokuwa kazini kama kwenye mikutano ya kisiasa, wanapopigwa wao huwa tunakimbilia kwenye ukumbi huu, tukadai haki za binadamu, lakini hawa Askari Polisi walio ndugu zetu, kaka zetu, dada zetu wao haki ya binadamu hii haiwagusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumegeuza jengo hili kama ndio ukumbi wetu wa siasa sio wa kuwatetea wananchi walioko nje na tunapenda wenzetu waliokuwa hawawezi kuingia humu kufika huwa tunawatukana sana kwa sababu tunajua kwamba tuna hakika wao kuingia humu hawawezi. Askari wetu wanafanya kazi nzuri sana katika nchi hii. Wana upungufu wao kama binadamu, lakini wanafanya kazi ya usiku na mchana, hawana Jumapili hawana Jumatatu. Askari wetu kufanya kwao kazi katika maeneo yao ni kwa hali ngumu sana, kwa sababu hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sisi Wabunge unapotoka hapa saa 11.00 alfajiri unaelekea Dar es Salaam, kila unapopita kuanzia saa 11.00 alfajiri askari wetu wako barabarani, si huku tu na kwingineko. Hawana mwamvuli, hawana kibanda, hawana chochote wao wako katika kazi. Leo kuja kumsakama binadamu mwenzio walio ndugu zetu, maana yake wanawaona kama nafikiri Askari Polisi hawana haki ya nchi hii, hiyo si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi unamwambia aende kwenye mkutano wa kisiasa, sasa hivi ndugu zetu wamekuwa ni woga sana. Unamwambia Askari Polisi aende akalinde mkutano na huku Vyama vya Siasa wamepanga magaidi yao, wakishafanya ugaidi wao husukumia wakasema ni Askari Polisi na Polisi huyu anapokwenda pale hana hata karatasi mkononi ile kalamu anaambiwa asiende nayo na unafika hapa unamnyanyasa kweli ni ubinadamu huu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kiongozi yeyote wa siasa baadhi yao ndio wachochezi wanaowachochea wananchi wa kuwapiga askari wetu na tunasema hii haikubaliki. Tunataka sheria ije hapa ya kumlinda Askari Polisi akajitetee wapi hiyo haki ya binadamu. Ukasema kama ni rushwa, nafikiri ni Tanzania nzima, kila Wizara inanuka rushwa tunayoizungumza hapa. Kwa hivyo, kama mtu anafanya rushwa huo ni ubinadamu wake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina salamu zangu maana yake nasikia kengele inalia. Sasa hivi tunaona tunafanyiwa uchochezi Wazanzibari, tena uchochezi mkubwa sana kwa kusingizia Katiba. Tunasema Mheshimiwa Tundu Lissu amezoea Wazanzibari kututukana, kutunyanyasa, kutudhalilisha, ametuita majina yote anayoyajua yeye, lakini na sisi tunasema ole wao, tutakapokuja tukazozana Wazanzibari kupigana, basi Mheshimiwa Tundu Lissu ndio Mhaini wa mwanzo tutakuja kumkamata hata ikiwa amejitia kwenye tundu la nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Kamshina wa Jeshi la Polisi, Zanzibar, muda mdogo tu baada ya kuingia yeye pale, amefanya kazi nzuri na anaendelea vizuri na

mabadiliko yanaonekana na askari wanaendelea vizuri. Tunaloomba Zanzibar vitendea kazi katika vituo vyetu vya Polisi hamna.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yao ya kazi Askari Polisi ni mabovu, majumba yanavuja, mashimo, vitendea kazi hata ile karatasi unakwenda hawana, viti hawana, magari hawana. Naomba Mheshimiwa Waziri sisi tunajua yeye ni mgeni ameingia juzi, haya mambo mengi ameyakuta, lakini tunajua atafanya kazi vizuri na aendeleze pale alipofika mwenziwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwape pole Masheha wetu Zanzibar walioitwa firauni. Mimi nasema waendelee na kazi wasiogope, wasitishike, wafanye kazi kama tulivyowaelekeza ndio hivyo hivyo. Hawa ni kelele zao wamezoea na mimi kumsikia mwanamume anakuja hapa anatukana maneno mara lile, mara vile, alisema hapa Mheshimiwa Tundu Lissu au alitaja na lile jina lakini silijui alivyosema, lakini nasema huwezi mwanamume kukaa hapa ukawa unatukana matusi tu wewe ni nani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanakhamis a nakushukuru. Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. AMINA N. MAKIILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nilijiandaa vizuri sana kuwatetea baba zangu na naomba nichukue nafasi hii kwa kweli kutangaza kwamba mimi ni familia ya Askari Polisi, tena kwa upande wa baba na mama, kwa hiyo mimi ni tunda la askari. Nimezaliwa kambini, nimekulia kambini, nimesomeshwa kambini na hata leo na nafasi yangu ya Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na malezi niliyopewa na Jeshi la Polisi mpaka nikafika hapa nilipo, nikajenga nyumba yangu nzuri lakini bado mimi nalala *Line Police*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nakupongeza wewe ni kombania *one*.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Amina, ahsante. Kwa hiyo, unapozungumzia matatizo ya askari kwa kweli unakonga moyo wangu na kwa kweli nayajua kuliko unafikiri Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kulipongeza sana Jeshi letu la Polisi na Majeshi ya Magereza, Uhamiaji, Zimamoto kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Unajua kama uko nje unaweza ukasema mengi, lakini sisi ambao ni familia ya askari, ambao *bigura* ikilia, tarumbeta ikilia, king'ora kikilia, mzazi anaondoka bila hata kuwaaga anakwenda wala hamjui anarudi lini.

Anakaa huko miezi mitatu, anaacha familia nyumbani bila ya kujua kesho mtaamkaje. Kwa kweli ninaposikia mtu anadhalilisha askari wetu hawa, huwa najisikia vibaya sana. Na kwa kuwa huwa ninajua kwamba akutukanaye hakuchagulii tusi na ukiwa kwenye maji unaoga akija mwendawazimu, haumfukuzi, unachutama kwenye maji, unamsamehe tu maana hajui atendalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwenye mchango wangu. Naomba niungane na Kamati ya mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Anna Abdallah, kueleza kwa hisia kwamba bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ni finyu sana. Pia naomba niungane na mapendekezo ya Kamati kwamba sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuisaidie Wizara hii ipate fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina changamoto nyingi sana, unamwambia askari atoke pale Musoma akafukuze majambazi, ametia lita 10 za mafuta, anafikiri atawakuta Makutano, anakwenda anaambiwa jambazi amekimbilia Kenya, anaongea na Kamanda anasema endelea mpaka umpate, anafikaje Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo madeni mengi sana ya Askari Polisi wanaofanya kazi katika mazingira magumu, tunawalipa fedha kutoka wapi kwa bajeti hii? Kuna matatizo mengi, *uniform* zao, maisha yao ya kujikimu, madeni ya wazabuni wamefanya kazi, lakini hata wazabuni huko wanalalamika wanaopeleka vitu katika majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niungane na Mheshimiwa Anna Abdallah na Kamati yake kwamba, sisi sasa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na najua tunaweza tukithubutu, tuwasaidie wapate fedha na siyo kuwasaidia tu kupata fedha, vile vile zitoke. Maana kuna vitu vinaitwa *exchequer* wakati mwingine zinakaa hewani hapa hata hazifiki katika hayo majeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu hebu tujaribu kuona, leo tuthubutu, tuongee wote tushikane kama tulivyoshikana kwenye bajeti ya maji, tuwatetee watu wetu hawa waweze kupata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze maslahi ya Askari Polisi na nimeanza kueleza kwamba mimi kila siku nalala *line police*, hata jana nimelala *Field Force*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nyumba za Askari Polisi kwa kweli zinatisha. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kukarabati nyumba za askari wetu na siyo Polisi peke yake, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto hali bado ni mbaya. Lakini askari wetu hawa ambao tunawategemea wanaishi na raia. Huko wanakokwenda kupanga nyumba kwa mwezi anatakiwa alipe 30,000/= mpaka 50,000/= mpaka 60,000/= kwa chumba. Kwa mshahara wa askari anapata wapi fedha ya kulipa kodi na kama hataingia katika vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanalala kwenye majumba, yanaitwa *full suit*, mabati. Unajua nazungumza hapa, mimi nimelala kwenye *full suit*, mimi nimelala mpaka kwenye handaki. Kuna mdogo wangu *WP* Jema Makilagi yuko Ofisi ya *RPC* Mwanza amezaliwa kwenye handaki anaitwa Mwamvita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninapozungumza matatizo ya Jeshi la Polisi na ndiyo maana leo nikasema niseme kwa uchungu kwamba, hebu Serikali iwaangalie vijana wetu hawa na wanafanya kazi nzuri, wanapigwa madongo, wanafanya kazi haithaminiki, hawatambuliwi. Sisi leo Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuenzi kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi yao katika posho inaitwa *ration* na hapa nilikuwa naongea nao, maana ni ndugu zangu, mbali na kuzaliwa na askari, lakini asilimia 80 wote ni askari, mimi peke yangu ndiyo niko huku Bunge. Wananiuliza mama sh. 5,000/= kwa siku, chakula cha wapi? Naomba niungane na Kamati ya Mama Anna Abdallah, hebu tuwapandishe tuwape 10,000/= kwa mwezi na inawezekana kama tulivyofanya katika taasisi zingine. Kama wanafunzi wetu wa vyuo vikuu wanaweza kupata 10,000/= wakiwa shuleni, tunashindwaje kuwasaidia askari wetu hawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la askari wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Kule mipakani wanafanya kazi katika mazingira ya kuhatarisha maisha yao,

wanalinda usalama wetu. Kama walivyosema wachangiaji wenzangu, lakini anapomaliza kazi anachofanya ni kupiga *salute* na mzee anasema ahsante, anakwenda nyumbani. Hebu tuwaangalie vijana hawa ili kuwatia moyo, ili kuwapa nguvu waweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie utaratibu wa kupandisha vyeo askari wetu. Utaratibu ni mzuri sana, lakini naomba utazamwe upya. Kama walivyosema wachangiaji wenzangu, unakuta askari ametumikia jeshi hili miaka nenda rudi, lakini anakuja kijana amesoma vizuri anakwenda haraka zaidi. Ni vizuri zaidi kwa sababu tunataka tupate jeshi la wasomi ili tujenge Taifa ambalo ni salama, lakini naomba huu utaratibu pia uangaliwe vizuri ili vijana wetu waliotumika kwa muda mrefu na wenyewe waweze kupanda vyeo kama wenzao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mwisho, ooh, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Makilagi, tunakushukuru sana kwa historia hiyo iliyosheheni uzoefu mkubwa wa masuala ya Polisi. Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Hussein Mzee.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami pia napenda kuchukua fursa hii kuipongeza hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Pia naomba kusisitiza kwamba ile kero ya bodaboda imezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ni kweli tunaomba Serikali iifanyie kazi, vijana wetu wasinyanyasike. Kwa sababu ya muda siwezi kuzungumzia kwa ndani kuhusu vijana wa Mara na hasa wa Tarime wanavyonyanyaswa na suala zima la bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka pia nizungumzie maslahi ya askari wetu, yamezungumzwa kwa upana wake na niseme athari ya kutoimarisha maslahi ya askari inapelekea, hauwezi kuweka kwa ujumla wake kwamba inawezekana ni tabia ya mtu, lakini pia inakuwa ni kigezo kimojawapo cha kusababisha rushwa katika Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nimeingia Bungeni hapa kwa kiasi kikubwa sana nimekuwa nikisimamia haki ya wananchi hasa wale ambao wanauawa, wanauliwa na baadhi ya askari wa jeshi la Polisi. Tumekuwa tukishuhudia mauaji kwa takriban kila wiki lazima mwananchi atauawa katika mgodi wa *North* Mara au maeneo yanayozunguka mgodi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa Serikali ituambie ni lini watasitisha, kwa maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba wataunda sijui ni Tume kuchunguza maskari wanaosababisha mauaji katika mgodi ule, lakini mpaka leo hii hamna chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi juzi tu, wiki iliyopita kuna kijana aliuawa, tena wanapigwa risasi siyo kule kwenye maeneo yanayozunguka pale. Mbaya zaidi wakimkuta mwananchi anatembea barabarani wanamkamata, anapata kipigo, wanakwenda kwenye makazi ya wananchi, wanawakamata wananchi maeneo ya Kipimio, Nyakungulu, Namrito na kwingineko. Wanakwenda mpaka kwenye sehemu za starehe wanawakamata, wanawapiga. Wakiulizwa kosa ni nini, "ukishafika kituoni usipotoa rushwa, niliandika hata jana kwenye Katiba na Sheria, usipotoa rushwa unaandikiwa *robbery, murder*. Tunapelekea wapi Taifa letu, tunaua vijana ambao ni nguvu kazi, ina maana unajenga ombaomba kwenye Taifa, unaacha wajane. Napenda majibu katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa haraka haraka nafikiri mtakumbuka wote kwamba yalitokea mauaji Tarime, kuna mtu alikuwa anaitwa Kinonke. Kusema ukweli Tarime

tulifedheheshwa sana na tuliathirika kwa kiasi kikubwa sana, siyo tu kupoteza ndugu zetu ambao hawana hatia, lakini pia shughuli za kimaendeleo kwa maana kiuchumi zilisitishwa kwa muda, takriban zaidi ya wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunashuhudia Jeshi la Polisi likitoa taarifa zingine ambazo ni za kufedhehesha kwamba, wanaouawa wale ni kwa sababu ya mahusiano ya kimapenzi, ugomvi wa kimapenzi na hata mwanafunzi wa shule ya msingi alipigwa risasi, nikasema mwanafunzi wa shule ya msingi Kinonke alimpiga risasi! Huyu mwanafunzi wa shule ya msingi ni mtoto, mahusiano ya kimapenzi wapi na wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hiyo, naomba jamani, baadhi ya askari tunawapenda, lakini mtende haki, muwalinde wananchi na mali zao na mtende haki, msitoe taarifa za kupotosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha zaidi tuna Kanda Maalum ya Tarime/Rorya na maaskari wengine, lakini mpaka tulipopata watu kutoka Makao Makuu ndipo huyu bwana Kinonke akapatikana. Kwa hiyo, naomba tuwe *serious* kwenye *issues* ambazo zinaathiri Taifa na uchumi wa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia pia mauaji ya wanawake kule Butiama, inasikitisha sana, tuna Jeshi la Polisi na Intelijensia zote. Mbaya zaidi, Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Mheshimiwa Anjela akasema kwamba, mwanamama kwenda shambani au kwenda kuchota maji lazima aende na mume wake au *partner* wake. Kwa mazingira ya kule kwetu Mkoa wa Mara unakuta mwanaume ana wanawake hata wanne, atajigawa vipi aende shambani na hao wanawake wana mashamba tofauti na yeye mwenyewe, ina maana huyo mwanaume asifanye kazi zingine?! Kwa hiyo, majukumu mengine ambayo ni ya Jeshi la Polisi tusiwatwike. Mkuu wa Wilaya anasema kabisa kwamba ikitokea mwanamke ameuwawa, huyo mwanaume atakuwa *held responsible*. Hii hatuwatendei haki, tuwe tunaangalia na tamaduni na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhusu mauaji ya Albino. Ni kitu cha kufedhehesha sana. Tumeshuhudia ndugu zetu hawa wanaendelea kuawa, takriban zaidi ya watu 80 mpaka sasa hivi wameuwawa. Lakini Serikali imeendelea kufumbia macho hiki kitu, ndugu zetu wanaendelea kuawa na wanasema ni mambo ya ushirikina. Chukueni hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia Tume nyingi zinaundwa, lakini siyo za mauaji ya *Albino*. Kwa nini msiipe uzito hawa ndugu zetu *Albino* wasiendelee kuawa. Pia tumeshuhudia kesi zikipelekwa Mahakamani zinaishia hata hatuoni zinakwenda wapi, watu wanahukumiwa kunyongwa, lakini hatujui ni nini hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa harakaharaka ni kule Mwanga, Kilimanjaro kuna Kata ya Jipe, Kitongoji cha Ruwi. Inasemekana kwamba kuna Watanzania wanakamatwa na askari kutoka Kenya wakati wanafanya shughuli zao za uvuvi, wanapelekwa upande wa pili wa Kenya, wakifikishwa kule wanashtakiwa na kufungwa miezi sita au wanaambiwa watoe rushwa ya laki sita. Wakishindwa, ndiyo hivyo wanafungwa. Sasa nataka nijue je, Serikali inalitambua hili? Kama inalitambua imefanya mpango gani wa kiulinzi kuhakikisha wale wananchi wa Kata ya Jipe hawapati hii adha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuhusu *barriers* za barabarani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Ya kwanza nafikiri. *Barriers* za barabarani?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Eeh?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimeambiwa ni kengele ya pili. Ahsante sana Esther Matiko,. Mheshimwa Mussa Hussein Mzee!

**MHE. MUSSA HUSSEIN MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Natoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa kawaida katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani kupatiwa fedha ambazo ni kidogo sana, hazikidhi mahitaji yao. Kwa hiyo, naomba wapatiwe fedha kwa ajili ya kupata mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Jang'ombe sehemu kubwa imezungukwa na boma ambalo ni kituo cha Polisi. Hapo zamani lilikuwa boma kweli kwa sababu lilikuwa lina uzio wa chuma na ukitaka kuingia ndani mpaka upitie katika milango miwili mikuu ambayo ina askari, lazima uonane na askari ili upate kuingia ndani. Lakini sasa hivi boma hilo limekuwa siyo boma tena kwa sababu lina matundu mengi sana unaweza ukapita popote ukaingia ndani, na hii ni hatari sana kwa Kituo cha Polisi ambacho kinategemewa ambacho kina *history* kubwa sana, kuwa na matundu unaweza kufika mpaka ndani bila kupitia waliko askari. Zamani kulikuwa na waya mzuri umezunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoomba, Wizara iongeze bajeti yake kwa upande wa Zanzibar kuzungusha ukuta wa matofali kwa sababu hapo zamani palikuwa hapana nyumba nyingi katika eneo lile, lakini sasa hivi imezungukwa na nyumba nyingi sana. Kwa hiyo, kuzungusha senyenge inakuwa ni tatizo, sasa inabidi Wizara ifanye mpango wa kupeleka mafundi wake wazungushe matofali kulihifadhi lile boma ili liwe na hadhi yake kama boma lilivyokuwa zamani, mtu akitaka kuingia apitie kwenye milango mikubwa badala ya kupenya vichochoroni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamezungumzwa kuhusu askari na lote hili linatokana na tatizo la kutokuwa na fedha za kutosha ili kuwahudumia askari hao. Askari wanafanya kazi nyingi tena muhimu kwetu sisi. Sisi tunalala ndani wao wako nje wanafanya shughuli zao. Kwa hiyo, naunga mkono yote yaliyosemwa kwa ajili ya askari hawa, bajeti yao iongezwe kama walivyoomba ili wafanikishe kazi zao za ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza ni matumizi ya *CCTV* na kuepusha na kuhami uhalifu. Kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu katika nchi yetu hii, mfano wizi katika mabenki, ulipuaji wa mabomu, kumwagiwa *acid* (tindikali), yote haya yanatokea wakati askari wanafanya kazi zao za upelelezi, lakini muda mwingi ushahidi haupatikani kwa sababu hakuna anayejitokeza kutoa ushahidi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba teknolojia hii itumike kwa ajili ya kuwasaidia askari kufanya kazi zao, wataweza kuepusha matukio kabla hayajatokea na yanapotokea inakuwa ni rahisi kwao kufanya uchunguzi wakitumia hiyo CCTV. Pia naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutupa ufafanuzi kwa nini mpaka leo hii Wizara yake haijaweza kufunga *CCTV* ambazo ulimwengu mzima zinatumika kusaidia mambo ya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumza lingine kuhusu usalama barabarani. Moja kati ya kazi muhimu wanazofanya askari wa usalama barabarani ni kuzuia ajali, lakini imekuwa kuna matatizo ya kutokezea ajali nyingi sana ambazo zinasababishwa na malori, madereva wa mabasi, kila mtu anaendesha anavyotaka mpaka bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linasababisha ongezeko la vifo na ongezeko la walemavu. Ongezeko hilo linatokana na uzembe wa madereva. Sasa ninachomwomba Mheshimiwa Waziri atueleze, kaweka mikakati gani katika kuzuia na kupunguza vifo vya watu barabarani katika ajali hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Hussein Mzee. Uchangiaji wetu utaendelea jioni ambapo Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu na wengine watachangia jioni.

Mheshimiwa Mangungu upo? Kwa dakika moja!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), naomba Mwongozo wako kama Kanuni ya 46(1) inavyotamka kwamba: "Waziri aliyeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama alivyoulizwa".

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi wakati anajibu swali Namba 69 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi kwa niaba ya Mheshimiwa Faith Mitambo, alitamka kwamba Serikali haina mpango wa ujenzi wa barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya majibu haya yanakinzana kabisa na maelezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa Mjini Njinjo mwaka 2009 wakati anakwenda kuzindua Kambi ya *Selous* pale eneo la Miguruwe ambapo alitoa agizo na barabara hii ilijengwa kilomita 1.8 kwa kiwango cha lami.

Mwaka 2010 alitoa maelezo kwamba, barabara ile sasa ifanyiwe tathmini, ijengwe kwa kiwango cha lami. Mwishowe, mwaka 2012 kwa mapenzi yake ya watu wa Lindi, Mheshimiwa Rais alifanya ziara kwa njia ya barabara kutoka Liwale hadi kufika Nangurukuru na alitoa maelezo kwa Wizara kushughulikia haraka barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelezo yanayotolewa na Mkuu wa Nchi yanakuja kupingana na maelezo yanayotolewa hapa Bungeni. Sasa naomba Mwongozo wako kwamba, je, Serikali hii inafanya kazi tofauti au inafanya kazi kwa mujibu wa mwongozo wa pamoja? Kwa sababu hakuna kauli zinazowiana na hamna *consistency* ya utatuzi wa matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ili tuweze kujua nini hatima ya ujenzi wa barabara hii na ikiwezekana Serikali itupe gharama za ujenzi wa barabara hii, wananchi watakuwa wako tayari wenyewe kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa uchungu na hisia za Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mangungu. Ninachoomba tu ni kwamba, tutakwenda kuangalia *record* ya vielelezo vyetu hizo ahadi za Mheshimiwa Rais. Lakini kama ana vielelezo hivyo vya ahadi za Mheshimiwa Rais, naomba atupatie ili tuweze kuchukua hatua tuweze kulinganisha na kufanya marekebisho ya majibu yetu kwa mujibu wa vielelezo vitakavyokuwepo.

Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mangungu ana vielelezo vya ahadi hizo za Mheshimiwa Rais, tungependa kuviona ili tuweze kulinganisha na maelezo haya. Hata hivyo, kama Serikali tutakaa pamoja na kupitia ili tuweze kufanya marekebisho muhimu kwa majibu yaliyotolewa leo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida, samahani sana. Haya, kwa muda mfupi sana!

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Mangungu. Nikiwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa, Mheshimiwa Rais mara mbili tukiwa naye katika mzunguko anatamka kuwa barabara ya Nangurukuru – Liwale ijengwe kwa lami. Tulikuwa katika msafara huo na Naibu Waziri wa Miundombinu wakati huo Mheshimiwa Makongoro Mahanga, akitoa hilo tamko mbele yake. Yeye Waziri akamwambia simama uongee, akasema kuwa mimi nipo hapa na nitasimamia barabara ya kutoka Nangurukuru mpaka Liwale iweze kukamilika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri wanapojibu maswali tuwe tunasikiliza vizuri ili hata pale tunapotaka kubisha jibu, basi tuwe angalau tumelisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi jibu lake alilolisoma ambalo nakala yake ninayo hapa, inasema ifuatavyo:-

Barabara ya Nangurukuru – Liwale ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 231 inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS*. Barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum kila mwaka kulingana na bajeti inayotengwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haina mpango wa kuijenga barabara ya Nangurukuru – Liwale kwa kiwango cha lami, kwa sasa. Hata hivyo, Serikali itaangalia uwezekano wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami katika mipango ya muda mrefu.

Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni ambapo tutaendelea na uchangiaji. Waliokuwa kwenye orodha wasiwe na wasiwasi watapata nafasi. Ahsanteni sana.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa hadi Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea kwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mathias Chikawe na tuko kwenye hatua ya uchangiaji ambapo mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Jabil Marombwa. Mheshimiwa Ramadhani Saleh! Mheshimiwa Abdul Jabil Marombwa ajiaande Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nianze kwa kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani kwa mafuriko makubwa yaliyowapata katika Wilaya zake karibu zote, Mungu akipenda nikiwa kama Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Pwani tumejipanga kuona tutafanya nini ili kuhakikisha kuwa Mkoa wetu unarudi katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ilikuwa niiombe tu Serikali, kwetu sisi Rufiji mwaka wa mafuriko ni mwaka wa neema pamoja na kuwa watu watakuwa wamepata shida kwa miezi mitatu, lakini mara baada ya mafuriko kutoka uwezekano wa kupata mazao mengi na kutumia mwaka mzima ni mkubwa. Naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ipeleke mbegu sasa ili kuwasaidia wale wakulima walioathirika waweze kupanda kwa msimu huu wa masika yanapokwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa mara ya kwanza naikataa au naipinga kabisa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Niseme tu kwamba, katika Wilaya ya Rufiji na hasa katika Jimbo la Kibiti kwa miaka mingi tumelizungumzia suala la upatikanaji wa Kituo cha Polisi pale Kibiti. Kwanza kipo kwenye *Road Reserve,* lakini la pili, kile kituo hakikuwa ni kituo kilichojengwa kwa madhumuni ya kuhudumia Polisi ilikuwa ni kambi ya Idara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipoondoka ndipo wao wakaamua kuchukua jengo moja wakalifanya hilo ni jengo la Polisi, lakini niseme tu kwamba, jengo lile ni chakavu sana na nimelizungumza ndani ya Bunge hili kwa mara zaidi ya saba, jengo lile ni chakavu sana, lakini kwa bahati mbaya Serikali haijatoa lolote la kuamua kuwa tunaisaidia nini ili angalau kulikarabati lile jengo liweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelizungumza mara nyingi na Mheshimiwa Waziri, unapita katika eneo lile unaliona kila siku ya Mungu, nakuomba uende ukalione mara hii ili uone ni namna gani askari zaidi ya 43 wanavyoteseka kwa kuishi kwenye jengo lile. Kwa mfano mwezi huu wa tano, wakati mvua nyingi zilipokuwa zinanyesha katika Wilaya ya Rufiji na Mkoa wa Pwani, nilikwenda kutembelea lile jingo, tena nilikwenda siku mvua inanyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule Mkuu wa Kituo cha Polisi alikuwa amesimama wima hajui mahali pa kukaa anasema Mheshimiwa Mbunge nikuweke sehemu gani jengo lote linavuja hakuna sehemu isiyovuja na pale kuna askari zaidi ya 43 wanaokaa kwenye jengo hilo tumelizungumza kwa muda mrefu hata kama liko kwenye *Road Reserve* na hata kama hamna uwezo wa kulihamisha kwa sasa hivi, likarabatini ili wale askari wakae mahali pazuri, lakini Serikali bado haijasikia hili ombi, wafanye nini wale askari wanakaa pale kwa ajili ya kazi tu, lakini tukimweka Mheshimiwa Waziri kukaa kwenye lile jengo, hawezi kukaa hata kwa dakika moja, jengo chafu, la siku nyingi, halikarabatiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, hebu iangalie uwekano wa kulitengeneza lile jengo hata kama mnashindwa kulihamisha kwa sasa basi tafuteni hela angalau mkalinyayue kidogo ili liweze kutumika vizuri, wale askari wetu waweze kulitumia jengo lile vizuri. Hili la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la Gereza la Kibiti. Naishukuru sana Serikali imefanya kazi kubwa ya kujenga jengo lile la kukaa wale wafungwa na mahabusu, wana jengo zuri wametengenezewa, lakini nyumba wanazoishi Maafisa wa Polisi, jengo la Utawala la Maafisa wa Magereza wale na jengo la utawala la Gereza lile, huwezi hata kuliangalia, lina nyufa kila kona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza lakini hakuna kinachoendelea. Majengo yale ya askari yote ni matope matupu, hakuna jengo hata moja la simenti, majengo yote ni matope yalijengwa toka miaka ya sabini mpaka hivi leo. Sasa naomba sana Serikali iweze kuhakikisha kuwa angalau pale napo panaangaliwa, lakini pamoja na kuangaliwa kilio chao kikubwa wale askari wa Magereza pale lile ni Gereza la Kilimo lina zaidi ya hekta 5,000 au 6,000 za eneo la kilimo, lakini hawana trekta, hivi kweli hata Serikali inashindwa kuipatia Magereza trekta? Tena yule Mkuu wa Gereza anasema sisi tunaweza hata kununua, tukopeshwe tutarudisha kwa sababu lile ni Gereza la Kilimo, wana ardhi ya kutosha, tena eneo lile mvua ni za kuaminika sana, tunashindwa hata kuwapatia trekta moja ili waweze kujitegemea? Ndiyo maana nikasema siungi mkono hili mpaka niweze kuambiwa na Mheshimiwa Waziri ni nini kinachojiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwalimu Marombwa. Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis!

**MHE.VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia Wizara yetu hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri ripoti yake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wenzake wote walioandaa taarifa ya bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kupunguza uhalifu mkubwa wa unyang'anyi na inaonesha kabisa kwamba wanafanya kazi yao vizuri, wanashirikiana vizuri katika mpango mkakati wa Polisi Jamii, lakini pia naomba niwaambie waendelee kukaza mkanda wa kudhibiti wale watu wakiwemo Wanasiasa pia, wachochezi ambao wanakuja kuleta vurugu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijakwenda katika eneo lingine nataka niulize kwa Mheshimiwa Waziri, huko nyuma katika Hotuba za Waziri wa Mambo ya Ndani miaka miwili ya nyuma walitenga fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Polisi, Wilaya ya Namtumbo na ilikuwa imetengwa na bajeti yale, lakini mpaka leo hii kile Kituo cha Polisi cha Wilaya hakijajengwa, watu wa Idara ya Ujenzi ya Polisi walikuja wakakagua na tukawaonesha mpaka eneo ambalo tulilowagawia wajenge, lakini hakikajengwa, sasa nataka Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kufanya majumuisho atueleze na awaeleze wananchi wa Namtumbo Kituo kile kitaanza kujengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kuzungumzia suala la ajali za barabarani. Ajali za barabarani zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka na hata ukisoma katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri unakuta ni hivyo hivyo ajali zimekuwa zikiongezeka. Nilitoa ushauri huko nyuma na nitaendelea kutoa ushauri huu kwamba, haya magari yanayopata ajali hasa makubwa; mabasi, malori yote haya ni *second hand,* magari ambayo mengi yao yametumika nje ndiyo tunanunua yanakuja hapa yanasafirisha mizigo, yamechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio nikasema kwamba, Polisi peke yake hawana ule uwezo wa kuyakagua haya magari na Sheria inasema kwamba, magari haya yanakaguliwa na Jeshi

letu la Polisi. Sasa niliomba, Wizara ya Mambo ya Ndani wakae na Wizara ya Usafirishaji watengeneze Sheria ya kuhakikisha kwamba magereji au gereji za watu binafsi washirikishwe katika mpango wa kuyakagua magari haya, kujua kila baada ya kilomita kadhaa, vipuri kadhaa vinabadilishwa. Hii ni kwa sababu matajiri wa magari haya wakiona wakiwasha *starter* likiwaka, yeye analituma tu safari, anachojali ni fedha, mpaka gari liharibike ndiyo linakwenda gereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tutengeneze utaratibu wa kuleta Sheria ya kuhakikisha kuwa kila baada ya muda fulani au kilomita kadhaa magari yanakaguliwa, kunakuwa na *Compulsory Motor Vehicle Inspection* hasa kwa hawa wanaosafirisha malori na wanaosafirisha raia kwa maana wanaosafirisha mizigo na raia. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ilizingatie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Idara zingine za Wizara hii, Magereza nilikuwa natazama Hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona mpango mkakati wowote ambao unaelezea askari wa Magereza watajengewa na wao nyumba lini, kwa sababu kwa *structure* ya Magereza au *command structure* yoyote ni kwamba, lazima askari wakae katika kambi. Wanapokuwa *scattered* au wanapokuwa mbalimbali inapotokea dharura inakuwa ni vigumu sana kuwakusanya na magereza inatunza wale wahalifu wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliona kwenye miaka 50, ni jinsi gani wale wanapochachamaa na wanavyoitwa wale kuja kuwasaidia, kama watakuwa na wao wanakaa mbalimbali itakuwa ni vigumu sana kuwasaidia au kulisaidia Jeshi hili la Magereza. Kwa hiyo, tunaomba pia Mheshimiwa Waziri watengeneze mkakati wa kusaidia pia Magereza zetu zile kubwa kuwajengea nyumba za kuishi askari hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Uhamiaji na *NIDA*; Uhamiaji huko nyuma walikuwa wanapata *retention* ya 70%. Ukitazama katika kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri utaona hapa mbele kuna picha ya Jengo la Uhamiaji, Zanzibar, lakini pia kuna Makao Makuu hapa Dar es Salaam, wametuonesha kwamba ile 70% ya *retention* waliyokuwa wanaipata ilisaidia katika mipango yao ya maendeleo, lakini leo zimepunguzwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar!

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuwasilisha vizuri Hotuba yake, lakini ninataka kuzungumzia NIDA. Vitambulisho vya Watanzania ambavyo tayari vimeanza kutolewa, naipongeza Serikali kwa kazi na juhudi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Wizara kwa usimamizi wake mzuri, kwa sababu kuna vitambulisho aina kumi na mbili. Kimoja katika hicho kama utakuwa nacho wewe unapata utambulisho wa Mtanzania na kama hukuwa Mtanzania, unapata cha ukaazi na kwa vyovyote tukubali kwamba Serikali ilitenga fedha kidogo. Sasa hawa wengine wanaosema bado hawajafanikiwa, watafanikiwa kwa sababu hii kazi bado itakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara wanataka kuweka vituo katika Wilaya, basi tusipige kelele jua kwamba kazi hii ni endelevu na wewe ni Mtanzania na vitambulisho vilivyotajwa, ikiwa una kimojawapo, jua kuwa utapata. Tusiwaonee Masheha, wanafanya kazi kwa taratibu za Sheria ya nchi, huwezi ukamwambia kuna watoto wa Firauni, basi Sheha watoto wa Firauni, hapana, hiyo tunafanya kufuru, huwezi kumwambia binadamu mwenzio maneno hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe kuna maneno aliyozungumza Mzee Ali Hassan Mwinyi, ukitaka kujibu tusi usiseme tusi, mwambie mwenyewe, sasa ukisema mwenyewe inakuwa lile tusi lote alolimwambia mwenzie, limemrejea yeye mwenyewe. Sasa ikiwa ni hilo, watoto wa Firauni basi na yeye yumo, asiwaambie wenziwe, kwa sababu maneno mengine ukisema jifikirie na wewe ukiambiwa, itakufurahisha? Maana yake tusizungumze maneno tukatoka katika mipaka ya mazungumzo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia mishahara duni ya askari wetu, mavazi chakavu kwa askari wetu, wanaokwenda mafunzoni wakirejea wanakaa mwaka mzima hawajalipwa, Makoplo hivi karibuni Zanzibar wamepandishwa vyeo, hadi hii leo hawajalipwa. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri hili aliangalie na waweze kulifanyia kazi na hawa watu walioko chini ndiyo muhimu wakawatazama kwa sababu hawa ndiyo wanawatuma, wao wako juu, kikitokea kitu wanatoa amri. Sasa hizi amri wanazozitoa na hawa wanaowapa amri pia wawe wanawaangalia na wanawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia lingine kuhusu bodaboda. Bodaboda zinafanya kazi nzuri, lakini wakati mwingine zinakera, unaweza kuwa umepanda kwenye gari, bodaboda inapiga muziki kama wa *Ambulance, wuuu wuuu*, sasa wewe inabidi ukae pembeni upishe, kumbe inapita bodaboda, sasa wewe unashangaa. Hii siyo ajali? Kwa sababu wakati wewe umesimama ghafla unamwona yeye anapita, wewe unachukia mtasababisha ajali, mtaondoa usalama, mnaleta matatizo kwa sababu wakati mwingine inaweza ikawa ni *Ambulance* wewe ukafikiri ni bodaboda usipitishe, kumbe kweli inakuja *Ambulance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ingefaa na hii milio ya bodaboda iangaliwe iwe na nidhamu, ijulikane ni milio gani ya kupiga wao na kutembea nayo mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja tena kwenye Polisi Jamii. Polisi Jamii inafanya kazi nzuri, hata mimi kwa Zanzibar ni mlezi wa Polisi Jamii, lakini kinachosikitisha ni elimu yao bado hawana elimu ya kutosha, utamkuta Polisi Jamii anachukua madaraka ambayo yanapitiliza na ilivyotakiwa afanye. Unakuta Polisi Jamii anagombana na Jamii, sasa ningeomba wapate elimu, waambiwe mipaka yao iko wapi, sisemi kama ni wabaya, ni wazuri, wanafanya kazi nzuri, lakini wanavuka mipaka ya kazi zao, badala ya kuwa watu wafurahie kazi zao, inabidi wanakereka na kazi zao. Sasa hayo ndiyo nalitaka kuyazungumzia, Mungu ajaalie muwe mmenisikia na muweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa uchakavu wa majengo. Majengo ya Polisi ni machakavu kwani ukienda Polisi hali utakayoikuta viti, meza, sehemu wanazofanyia kazi na wakati mwingine utamkuta askari nadhifu, lakini sehemu aliyokaa hairidhishi, lakini afanye nini, hakuna budi, ni lazima afanyie kazi pale. Pia wewe unayekwenda pale, mwenyewe umekwenda nadhifu, unahangaika wapi ukae, lakini ikiwa mwenzio umemkuta amekaa pale, itabidi na wewe ukae palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba hilo waliangalie na kama hawawezi kuzitengeneza, angalau wazipake rangi kama hawawezi kutengeneza, angalau viti vingine waviwekee misumari ili wakifika watu wajue kuwa hiki ni kituo, kinaheshima na waliopo wanaheshimika na wewe unayekwenda pale utakuwa na heshima yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis. Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Salim!

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia angalau kwa uchache katika Hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kunipa afya njema na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia angalau machache kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani kwa Hotuba yake nzuri, imesheheni ahadi nzuri, lakini siungi mkono hoja. Nitasema ni kwa nini siungi mkono hoja. Sitaunga mkono hoja mpaka hapo atakapokuwa amenipa majibu ya kuniridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ambazo zinafanywa. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri kwa kuimarisha ulinzi na mali za wananchi. Jeshi la Polisi tumekuwa tukililalamikia mambo mengi; linakula rushwa, wanapokea rushwa, tuangalie chanzo ni nini? Tusiwanyooshee kidole, tuangalie kwanza chanzo ni nini hata kama ni wewe Mheshimiwa Naibu Spika utakapokuwa umepewa kitu kidogo na ukawa unakisimamia kitu kikubwa, ni lazima utapata kishawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, lakini kipato chao ni kidogo, waboreshewe mazingira yao, wapewe mishahara mizuri, ninahisi suala la rushwa linaweza likapungua ama likafutika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi hususan Wilaya ya Nyanghwale, wanafanya kazi nzuri ya usalama na ulinzi wa mali za wananchi, lakini Jeshi hili kwa Wilaya ya Nyanghwale, linafanya kazi katika mazingira magumu, kwa upungufu wa zana, mfano, magari hawana, lipo gari moja kwa Wilaya nzima na gari lile lina upungufu wa matairi, mafuta, hata likitokea jambo sehemu fulani inabidi waanze kuchangisha mafuta. Suala hili si zuri. Utakapokwenda kumwomba mtu mafuta, siku ana tatizo lazima umwangalie usoni, ndio mwanzo wa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya majengo, Ofisi kwa Wilaya ya Nyanghwale ambapo ndio Makao Makuu ya Wilaya Karumwa, jengo ni bovu na dogo, mahabusu ya kubeba watu wane, wanaingizwa mpaka watu kumi. Mahabusu mbovu, kuna jengo liko pale limejengwa leo lina zaidi ya miaka kumi na tano nami nikiwa mdau nimechangia zaidi ya milioni tatu, lakini jengo hilo mpaka leo halijakwisha.

Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa kwamba kuna majengo yatakayojengwa ya ofisi kila Tarafa, je, Tarafa hiyo ya Msalala na Tarafa hiyo ya Nyanghwale imo kwenye bajeti hii? Kama ataniambia bajeti hii yamo hayo majengo, nitaiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Jeshi la Polisi kwa Wilaya ya Nyanghwale, upungufu niliousema naomba sasa kwenye bajeti hii wapewe gari, nyenzo zingine ndogondogo kama vile pikipiki, waboreshewe ofisi zao, wawekewe samani pamoja na silaha hazitoshi, wajengewe mahabusu. Kwa kweli nitaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda nizungumzie suala moja, mahusiano si mazuri kati ya Jeshi la Polisi la wananchi katika Jimbo la Nyangwale. Kuna baadhi ya askari walio wachache na majina ninayo, vijana hawa wanasumbua wananchi kwa kujifanya wao ni *TRA*,

Mabwana Mifugo, wanajifanya wao shughuli zote ni zao kwa kuwasumbua wananchi na kuwaomba rushwa. Kwa kweli imefikia sehemu, siku moja wananchi walitaka kuwapiga na bahati nzuri wale jamaa kwa sababu wameshapitia mambo ya kijeshi waliweza kukimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wapo wawili, naomba majina niyataje na naomba vijana hawa wahamishwe ili lisije likatokea tatizo la wao kugombana na wananchi. Vijana hawa mmoja ni binti, anaitwa Doto na wa pili ni kijana, anaitwa Frank. Nimeweza kufanya mkutano wa hadhara karibu Kata tatu, wanawalalamikia na nikaweza kupiga kura kwenye Mkutano wa hadhara kwamba jamani hawa Maaskari mnaowalalamikia hebu toeni maamuzi mnasemaji.

Mikutano yote waliweza kunyanyua mikono wananchi na kusema waondoshwe. Sasa kwa sababu wananchi tayari hawana mahusiano mazuri na hawa vijana wawili hawa, tunaomba hawa vijana wahamishwe, vinginevyo litakuja litokee tatizo na hilo tatizo wananchi wakishachukia na mahusiano yakawa si mazuri kwa kweli mazingira yatakuwa si mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, sitaunga mkono hoja mpaka hapo nitakapojibiwa yale ambayo nimechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Amar. Mheshimiwa Masood Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Murtazar Ali Mangungu.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu, hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa hiyo, nitakuwa na maelekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mishahara ya Polisi, mishahara ya Magereza na Zimamoto. Mishahara ya Polisi imekuwa ni midogo sana kulingana na hali ya maisha ilivyo na mishahara hii hailingani na ukali na kupanda kwa gharama za maisha. Kwa msingi huo, kuna haja hasa ya kuweza kuboresha mishahara ya Jeshi la Polisi, lakini pia kuboresha mishahara ya Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza mishahara yake ni midogo sana. Tuangalie namna gani ambavyo Jeshi la Magereza linavyofanya kazi, lakini Jeshi hili limedharauliwa, limetupwa, haliangaliwi kwa hali yoyote. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani wewe binafsi nilikuona kwenye Jambo Tanzania ukilalamikia hili hili, kwa sababu wewe ni sehemu ya Serikali tunakwambia kwamba bajeti hii haitakaa vizuri kama hutaboresha mishahara ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na zima moto pamoja na uhamiaji kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya chakula kwa majeshi yetu haya ni shilingi elfu tano kwa siku, haitoshi ni kidogo sana kutokana na kupanda kwa gharama za maisha. Hili nasema kwamba, ni vyema tuangalie upya angalau ifike elfu nane kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kuchekesha kabisa inakuwaje leo Magereza 129, mnakwenda mnatoa bajeti ya kununua magari nane? Magari nane hamna kitu. Leo hii mkienda kwenye Mahakama mnakwenda kununua magari 218, sawa! Lakini kwenye Magereza mnatenga pesa za magari nane tu. Hii ni aibu, Serikali imechoka nini jamani? Hii ni aibu ya mchana kweupe bila giza. Tukubali kama mmechoka mtuambie na dalili zinaonesha kwamba mmechoka, Mheshimiwa Lukuvi yupo! Mmechoka Serikali ya Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili chakula cha Wafungwa wanapewa shilingi mia tano tu kwa siku, ndio mlo wao, hata katika haki za binadamu ni hatari sana. Ukienda Magerezani ni aibu kupita kiasi. Tumepiga makelele zamani mafungu tumesema yawekwe, lakini wanasema wakubwa Hazina hawataki kuzipeleka fedha. Mfungwa wa Tanzania shilingi mia tano jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, akifanya majumuisho alieleze hili Bunge Tukufu, ana mkakati gani wa ziada wa kuhakikisha kwamba fedha angalau za chakula kwa mfungwa na mahabusu zinafikia angalau elfu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Vituo vya Polisi. Kituo cha Polisi cha Kingeja ni kibovu tangu ukoloni, mmerithi majengo ya ukoloni, kuyatunza hamwezi aibu tupu. Hata ukoloni hamwenzi kuyatunza yale ya ukoloni, askari wanataka kufa! Tumekuwa na Naibu Waziri pale Mheshimiwa Pereira akaangalia mna askari na familia zao. Nyumba za ukoloni kuzitunza hamuwezi! Halafu mnasema ndio utawala bora, mimi sikubaliani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahakikishe kwamba askari wale Kengeja kama watapata madhara yoyote ya kuangukiwa na lile jengo, basi hapa patakuwa hapatoshi. Jengo la Kituo cha Polisi la Mkoani nalo ni bovu kwa Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani na Konde nako halikadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie atakapofanya majumuisho na Mheshimiwa Waziri kwa ujumla wake, wana mkakati gani wa kuweza kufanya ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Kengeja, Kituo cha Polisi cha Konde, kufanya jengo jipya la Mkoani na maeneo mengine ambayo hali imekuwa ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamiaji haramu, wameanza kurudi. Wilaya ya Karagwe wameanza kurudi, katika Wilaya ya Misenyi na wanaorudisha ni Watendaji wa Vijiji na Vitongoji na sio siri kwamba ni wa CCM, ni wa Chama cha Mapinduzi ndio mliowachia kule Karagwe, Misenyi wanachukua rushwa mnafumbia na macho, mafisadi na ushahidi huu upo. Hasa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kwa fedha zile za walipa kodi maskini mkaachia leo wanarudi kule kule, wanachukua rushwa wanarudi. Wamechoka, tatizo ni nini? Mtuambie dalili zinaonekana mmechoka. Serikali ni vyema muondoke mapema madarakani amesema Mheshimiwa Lema hapa nampongeza sana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la Kituo cha Polisi Mkokotoni. Mmetenga shilingi milioni 450 mwaka jana, fedha za Mkokotoni hamkotoa na mara hii mmetenga shilingi milioni 300 tu kwa Zanzibar zima ukarabati wa majengo, fedha hizi ni ndogo sana zinafaa ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, watuambie sababu gani za msingi wakifanya majumuisho, ni nani asiyepelekea fedha shilingi milioni 450 za jengo la Mkokotoni mwaka jana kwa nini zitolewe? Nani kazuia nani mwenye ubavu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inachosha na inasikikitisha kweli, askari wako katika hali ngumu kwelikweli na wala hawawezi kugoma, kila kitu wanaonewa tu na hawa hawa mara nyingine mnawatumia kwa shughuli nyingine. Hii Serikali jamani! Hamuondoki mnabakia mnafanya nini? Ondokeni!

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEC* na *NIDA* wananunua vifaa vya pamoja na kununulia vifaa vya kuchukulia alama za vidole, hili ni suala kubwa sana na Mheshimiwa Waziri anajua, ili kusiwe na *duplication* juu ya jambo hili, kuna haja ya *NEC* na *NIDA* wakae pamoja, ili kuepusha mpangilio huu wa pamoja ambao unaweza kuligharimu fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masood nakushukuru sana. Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza ningependa nimwambie Mheshimiwa Masood bin Abdallah bin Salim ambaye ni Mbunge pia ni Mjumbe kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, Chama kinachoongoza nchi hii kipo imara na ndio maana wao wameamua kuungana ili kuweza kupambana nayo na bado hawatoweza. Maana Waswahili wanasema, wafu wanakokotana!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba ambazo wenzetu wamezichangia na baadhi ya Wajumbe ambao walitangulia kuchangia, ni jambo la kusikitisha na kustajabisha sana pale ambapo sasa tumeelezwa kwamba nchi yetu haina usalama na hali ya mipaka yetu ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote sisi ni mashuhuda, tumekuwa tukifanya kazi kubwa sana ya kuwapokea wenzetu ambao nchi zao si salama, wanakimbilia hapa Tanzania kwa sababu wanaamini kabisa, kuna usalama na bado tunao watu hao katika maeneo ya Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo tabia ambayo imejijenga hivi sasa na inazidi kukomaa. Lazima tuseme ukweli kwamba hii ni tabia mbaya kuvitukana, kuvishutumu, kuvilaumu na kuvisingizia vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Kama hatutejenga mfumo wa kuwaaminisha wananchi kuviheshimu vyombo hivi, hatuwezi kuwa na nchi ambayo itakuwa salama kwa kipindi kifupi kinachokuja.

Ni kweli kwamba yapo maeneo ambayo Polisi na lazima hili tulijue, Sheria ya Polisi na askari wote wameruhusiwa kuua. Pale ambapo unashindwa kutii amri watakuua kwa sababu wanapewa silaha na zile silaha si kwa ajili ya kuwindia, bali ni kwa ajili ya kulinda usalama na yule ambaye anakiuka *measures* zile za kiusalama atapigwa risasi na wakati mwingine atakufa.

Kwa hiyo, nasema tu kwamba, wanasiasa wenzangu na Wabunge wanzangu, lazima tujenge mfumo, hivi vyombo tuviheshimu vifanye kazi zake kwa kadri ya kiasi ambacho kinatakiwa. Tukiwa ni viongozi, tukiona hawa wanafanya makosa, wana viongozi wao, kuna utaratibu uliowekwa kuweza kuwaelimisha na wale ambao wanabainika kwamba wamefanya makosa, basi watachukuliwa hatua ya kinidhamu kwa sababu hakuna Jeshi lolote lile ambalo linaundwa bila kuwekwa misingi ya kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kiusalama inategemea na mambo mengine pia. Nimeleta mchango wangu wa maandishi hapa kwamba bado idara zetu za kazi, *immigration* hawafanyi kazi ya kutosha kwenye kudhibiti wimbi la Wageni wanaokuja kuvamia ajira za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimetoa mapendekezo hapo, kianzishwe kitengo maalum ambacho kitashughulika na hili kwa sababu haiwezekani tukawa na mamlaka zinakinzana kwenye kutoa vibali vya watu kufanya kazi hapa nchini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningependa na nitafurahia sana kama utatupa majibu nini ambacho Serikali inakusudia

kufanya ili kuweza kudhibiti wimbi hili ambalo limekuwa ni kero kwa Watanzania na limekuwa linahatarisha hali ya kiuchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia jambo moja kwamba ukipitia ile *Police General Orders* kwamba kwa kipindi cha miaka kumi na mbili, mtu ambaye amechukuliwa na Jeshi la Polisi, anakuwa bado hajapata ajira ya kudumu, sasa ni lini mtabadilisha mfumo huu ambao ulikuwa umewekwa katika misingi ya kikoloni na kuli-*modernize* hili Jeshi ili mtu anapoanza ajira yake basi awe na uhakika, huu mpango wa miaka mitatu mitatu mpaka ifike miaka 12 ndio aje kuwa na *option* ile ya aidha kwenda kwenye gratuity au kuchukua pensheni yake ndio aajiriwe moja kwa moja naamini kabisa ni jambo ambalo inabidi mliangalie kwa uharaka ili uweze kutatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, wenzetu hawa wanaofanya kazi kubwa ya kulinda usalama wa nchi yetu, wanapata kazi pia kuweza kubajeti jinsi ya kuishi na familia zao. Ni lini hasa Wizara mtaleta mpango mkakati kuboresha maslahi ya askari hawa? Sio tunakubali tu kupokea saluti zao bila kuwaboreshea maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, litakuwa ni jambo la busara sana, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hapa awe amelielezea hilo kwamba ni jinsi gani ambavyo atafanya maboresho kwa Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji pamoja na vikosi vingine ambavyo wanashirikiana navyo katika kulinda usalama na kusimamia shughuli zingine za usalama wa kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilisema kwamba kumekuwa na tatizo kubwa sana la hawa wenzetu *Traffic Police* wanapowakamata watu wanaokiuka, wanapokuwa wanasimamia misafara ya magari, tabia hii ya watu kukimbizana na Mheshimiwa Fakharia bahati nzuri amelisema hapa kwamba, wanapoongoza misafara watu wengine wanaunga msafara na *ambulance*, wengine na gari la viongozi. Sasa utaratibu huu akikamatwa mtu, tayari ameshapigiwa simu Waziri, Mkuu wa Mkoa, hebu tuache hao wenzetu wafanye kazi zao vile ambavyo inatakiwa. Mambo ya simu haya tuache! Tunatunga Sheria humu watu watozwe faini, waache wakifanya makosa watozwe faini, tuache mambo ya kutoa toa amri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika sana kwa maelezo ya mtiririko wa uchangiaji wa Wajumbe wengi, kuhusiana na hali ya usalama katika eneo lile la Kiteto na wenzetu wa Kongwa. Hivi ni kweli Wizara ya Mambo ya Ndani na Serikali mmeshindwa kutafuta suluhisho la mgogoro huu? Ni kweli kabisa hamna namna ya kuweza kudhibiti hali ya mauaji katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita, ni kweli kabisa vurugu zilifanyika pale Kibaigwa na wengine tulikaa barabarani kwa zaidi ya masaa matano kutokana na tatizo hili. Ni kwa nini Waziri hapeleki namna ya kuweza kutatua matatizo yanayowakabili wananchi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabisa ningependa kwamba, wenzetu wa *NIDA* ambao wamekabidhiwa jukumu la kutengeneza vitambulisho, kasma ya bajeti ili wapelekewe na majibu ya maelezo ambayo nimeyatoa ni muhimu na yanahitajika na asipoleta majibu haya Mheshimiwa Waziri sio kwamba tutatoa shilingi, bali tutafuta kabisa mshahara wake na wa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Hamis Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Chiku Abwao na Mheshimiwa Kidawa Salehe ajiandae.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza dakika zangu Mheshimiwa Mangungu ameanza kuzila. Nianze kwa kusema kwamba, hakuna nchi ambayo haina usalama kama Tanzania na nasema hivyo nikiwa na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya *Albino* yamechukua muda mrefu sana, *Albino* wamepoteza maisha, wamepoteza viungo vyao na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali katika mauaji haya. Ningeomba Serikali itoe tamko ni lini itaunda Tume ya Kuchunguza Mauaji ya *Albino* Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, siwalaumu ndugu zetu wa Jeshi la Polisi, najua wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa sheria, ninaowalaumu ni Viongozi wa nchi ambao wanalitumia vibaya Jeshi hili. Kwa mfano, hivi karibuni tuliomba kufanya mkutano Zanzibar Jeshi la Polisi lilikuwa tayari limeshakubali, lakini Viongozi wa Serikali wakawatumia taarifa kwamba wasiruhusu kufanyika kwa Mkutano ule. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo ni Mkutano upi huo, ule wa UKAWA au?

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mkutano wa Kibanda Maiti, UKAWA, sawasawa, wala hakuna ubaya. Si huo tu, lakini hata Pemba haukuruhusiwa kufanyika, niseme kwamba woga wa Viongozi wa Serikali ndiyo ambao unachochea kuleta uvunjifu wa amani ndani ya nchi hii. Ninasema hivyo nikiwa na ushahidi, Kanda hii naomba ifike mezani kwako, maelezo haya ni ya Mheshimiwa Lukuvi, nina hakika amekwishaipata, lakini naongeza hii hapa, aliyoyatoa Kanisani kuhusu kuwabagua Watanzania katika misingi ya udini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna watu ambao wanatakiwa kuchukuliwa hatua, basi yeye ni mmojawapo, kwa sababu kama alikuwa na chochote alitakiwa akizungumze ndani ya Bunge siyo Kanisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Mheshimiwa Janet Mbene, mimi sitaki kumsema mtu kama hayupo, amezungumza kanisani. Vile vile Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, amefanya kikao, lakini usiku kukatokea mauaji, sasa tuulize hapa palikuwa na masuala gani? Ni mkutano wa UKAWA huu? Ule wa Kanisani ulikuwa mkutano wa UKAWA?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la nafasi za ajira. Hakuna nchi ambayo haina ubaguzi kama Zanzibar, kuna watu ambao wameshtuka kwa kuambiwa kama Zanzibar watapata asilimia 21 ya nafasi za ajira katika Muungano. Nafasi zile za ajira zinazotoka kule katika Muungano basi kama utafanya utafiti na uchunguzi Wazanzibari hasa wanaopata nafasi zile hawafiki asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nataka ufanye utafiti, ndani ya Baraza la Wawakilishi kuna Watanganyika wangapi waliochaguliwa wakawa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao ni Watanganyika, ndani ya Bunge hili, kuna Watanganyika wangapi ambao wamechaguliwa kuwa Wabunge kutoka Zanzibar na wao wanawakilisha Zanzibar na wao ni Watanganyika? Hivyo ni kuonesha dhahiri kwa Wazanzibari hawana ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Kituo cha Matangatwani, kituo kile hakina hata choo, hakina hata umeme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kombo. Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Chiku ujiandae!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Mheshimiwa Kombo na mwenzake leo wameniota hawa. Nataka tu kusema kwamba haya maneno yanayosemwa nilishayatolea maelezo baada ya Mheshimiwa Lipumba kuyasema kwenye Bunge la Katiba nami ndani ya Bunge lile lile nikayajibu. Sasa nakushauri Mheshimiwa Kombo na mwenzako mkitaka maneno haya kama mna ubavu mje kwenye Bunge la Katiba, nitawajibu tena, lakini msitumie Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yangu ni wazi tu, Waasisi za siasa za udini ndani ya nchi hii ni ninyi, kama mnabisha wewe una *video* moja, mimi ninazo 20 hapa na bahati mbaya sana zina sura za Viongozi wako, sitaki kusema mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia tu kwa ufupi kwamba, yaliyosemwa kwenye Bunge la Katiba na bahati nzuri wapo watu walijitokeza kutishia nyau kwamba watakuja kukata rufaa, tunawasubiri. Mheshimiwa Kombo nataka kukwambia kwamba, hata haya machache nilikuwa nisikudokeze kwa sababu nawaheshimu wakubwa zako walinipigia simu nisiseme zaidi na mimi sisemi, kwa sababu vinginevyo itabidi muanze kuombana radhi hata ndani ya UKAWA. Kwa sababu mmetumia Misikiti kusemana hata na wenzetu wa Vyama vingine ndani ya UKAWA. Ndugu zangu tusichokoze mambo, ukinyoosha kidole kwa Lukuvi angalia hivi vinne vinakutazama wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako lisitumike kuchokoza mambo ambayo hayana utafiti, wana hiyo kanda moja, lakini mimi nilialikwa, wako watu wanajipeleka wenyewe kutaka midahalo kwenye maeneo ya ibada, unawajua? Hivi mpaka mmekuja hapa hamkufanya hata utafiti kidogo? Masoud wewe una akili hukusema!

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa maneno hayo mnayoendeleza kuyasema ndiyo mnashabikia uchochezi. Siku nyingine nawaombeni, msije humu ndani mkazungumza mambo hamna uhakika yanakoanzia na mwisho wake, ni mabaya, mtakuja kuchukuliwa hatua za kinidhamu huko kwa wakubwa zenu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Salehe na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani, Kamanda Godbless Lema ameongea vizuri sana, ametuwakilisha vizuri na namuunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia wamekuwa wakilalamika jinsi Askari wetu wanavyoteseka. Naamini hata wale ambao hawajachangia, mawazo yao yanafanana, wote wana uchungu kuona Askari wetu wanaishi maisha yasiyoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nimekuwa Mbunge mwaka 1995 mpaka 2000, nimechangia Wizara ya Mambo ya Ndani kila mwaka na hata niliporudi sasa toka mwaka 2010 mpaka leo, kila mwaka bajeti hii huwa nachangia Wizara ya Mambo ya Ndani na kilio kikubwa ni kuwasaidia Askari wetu ili waweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kushangaza pamoja na malalamiko yote na masikitiko yote ya Wabunge wote baadaye bajeti inapitishwa mia kwa mia. Naomba kusema pamoja na kwamba tunawatetea sana Askari tunawapigania wapate haki, lakini kuna wengine humu ndani wanafanya usanii kuwatetea Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema wanafanya usanii kwa sababu wana uwezo wa kuwafanya waishi vizuri, wana uwezo wa kukwamisha bajeti ili iongezwe. Nashukuru kuna baadhi ya Wabunge hapa wametoa mfano wa bajeti ya Wizara ya Maji ambapo mwaka jana tuliweza kuizuia, wote kwa umoja wetu ndani ya Bunge hili bila kujali itikadi zetu, tulilalamika, tukaiomba Serikali na mwisho tukakwamisha bajeti na hatimaye ikaongezewa pesa. Sasa nasme kama kweli wote tuna kauli moja na wote tuna masikitiko na uchungu na Jeshi la Polisi leo Bajeti hii isipite, irekebishwe iongezwe ili Askari wetu waweze kuboreshewa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu usanii wa kusema tu mnajionesha kwa Jeshi la Polisi kwa kuwa wanawaona, mnajidai mnawatetea, lakini ndani ya mioyo yenu hamna dhamira, huu ni unafiki na hii haikubaliki kuwachezea watu ambao tunawatumia kwa gharama kubwa sana ya uhai wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi wana shida, Askari wa kima cha chini wanateseka vibaya sana, maisha yao ni duni wanapata tabu sana. Hata kama wakitaka kuomba kwenda kusoma hawapati likizo ya kwenda kusoma, hata wakijitolea wenyewe wajisomeshe au familia zao ziamue kuwasaidia waweze kusomeshwa wananyimwa ruhusa, wakihamishwa hawalipwi posho ya uhamisho. Kuna waliohamishwa hata zaidi ya mara ya tatu hawajapewa posho yao ya uhamisho. Wanadai posho hizo mpaka wanakufa, wana shida sana watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Uniform* zao zinatolewa kwa tabu, wenyewe wanasema wanabaguliwa kwa mashtaka wanayoniambia, Mheshimiwa wewe unatutetea kila mwaka, sisi tunabaguliwa, kupewa *uniform* kwenyewe hatupewi wanavaa wakubwa, lakini naamini si kama wanabaguliwa, hawapati hizo *uniform* hazitoshi, ruzuku inayotolewa kwa Jeshi la Polisi haitoshi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama kweli Wabunge wenzangu hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mlio wengi ambao mna uwezo wa kubadilisha chochote tukidhamiria kushirikiana humu ndani, hii bajeti leo isipite ili kweli tutimize dhamira yetu ya kuwatetea Askari hawa, waweze kunufaika kwa sisi kuwawakilisha ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Askari hawa wanateseka, mengi yamesemwa, lakini pia pamoja na kuwatetea sana Askari wetu, wapo Askari ambao hawawajibiki vizuri, wapo Askari ambao wanafanya kazi kwa ubaguzi. Mimi kama mkazi wa Iringa…

**MBUNGE FULANI:** Lukuvi!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Lukuvi sina shida naye safari hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mkazi wa Iringa Askari wamenilalamikia sana na mimi pia nimelalamika juu ya Jeshi la Polisi kwa askari ambao hawawajibiki vizuri. Iringa kuna kesi

chungu nzima za kubambikiwa tu hasa kwa vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, wanakamatwa bila sababu wanawekwa ndani, wakati wa chaguzi ukifika ni vitisho kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi wa juu Iringa mimi sina matatizo nao, lakini kuna mmoja ambaye anaitwa Wakya alikuwa *RCO* wa Iringa, huyu Wakya ni tatizo kubwa sana na nimemshuhudia mwenyewe akifanya kazi akiwa amelewa kabisa anapepesuka, anachukua magongo ya kupigia ng'ombe anapigia binadamu bila hatia yeyote na nilimwambia Bwana Wakya nitashuka na wewe Bungeni. Akasema usinibabaishe wewe, mimi nina wakubwa hutanifanya chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda mpaka kwa *RPC* ambaye yupo sasa hivi Iringa nikamweleza matatizo ya huyu Bwana. *RPC* kwa kweli alisikitika sana ila akasema nitafuatilia nipate ukweli wa hayo unayoyazungumza. Ukweli ni kwamba, huyu Askari anafanya vitu vya ajabu Iringa, Wapinzani amewageuza kuwa maadui, anaacha kufanya kazi yake ya Kipolisi, anaingilia mambo ya Vyama vya Siasa na chuki kubwa ni kwa Wapinzani, vijana wengi wamefunguliwa kesi Iringa ambazo hazina hesabu. Akitimka tu, akiwaza vibaya amelewa kwenye baa amewakuta pengine wamemzidi wanakunywa zaidi yake, kesho anawakamatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ukweli kabisa, wananchi vijana wa Iringa wamepata shida sana kwa huyu Wakya. Nashukuru baada ya malalamiko mengi sijui, nafikiri kama alifuatiliwa ama hakufuatiliwa au ni ile ile staili ya kuwahamisha tu watu, huyu bwana amehamishiwa Temeke, amehamishwa juzi tu Iringa baada ya uchaguzi wa Kalenga, lakini ukweli ni kwamba, huyu ni mtu ambaye hawajibiki na hafai kuwa Kiongozi na hafai hata hicho cheo kuwajibika nacho kwa sababu anakitumia kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu ana uchungu na Jeshi la Polisi, hakika mimi nimekuwa nikiwaonea huruma na nimekuwa nikiwatetea kwa nguvu zangu zote, naamini kama Chama changu kingekuwa ndiyo kimeshika madaraka, Askari hawa wangekuwa wameshaboreshewa maisha, lakini hatuna uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuungane wote, si tunawatetea sana, Wabunge wote tumeonesha dhamira ya kuwatetea Askari, bajeti hii ni ndogo na imeonekana wazi hakuna aliyesifia hata mmoja, tukwamishe hii bajeti, leo ili Askari wetu waongezewe, waweze kupunguza matatizo waliyonayo ingawa hayatakwisha kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao nakushukuru sana Ahsante.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana, lakini leo nitatoa shilingi kama Wabunge wa CCM mtaendeleza usanii wenu wa kupitisha hii bajeti sitakubali kabisa, lakini nawaomba kutoa shilingi haitoshi, tushirikiane tuwe kitu kimoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Leo Mheshimiwa Chiku Abwao ana hasira kweli kweli. Mheshimiwa Kidawa Salehe atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kunipatia nafasi na naanza kwa kuunga mkono hoja kabla sijachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haiondoki, itakuwepo na itaendelea kuwepo kwa sababu inachaguliwa na wananchi kila baada ya miaka mitano, inapata kura nyingi na Watanzania walio wengi wana imani na Chama cha Mapinduzi wataendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwa kupongeza kazi nzuri ya Jeshi la Polisi kwa kulinda usalama wa raia na mali zetu, wakati sisi tumelala wao wanaendelea kuchapa kazi. Napenda kusisitiza kwamba Jeshi la Polisi liendelee kufanya kazi kama watu ambao ni *neutral* ambao hawafungamani na itikadi ya upande wowote na hivyo ndiyo itaweza kutenda haki kwa Watanzania wote na kwa wale ambao wanavunja sheria wachukue jukumu lao la kuwaadhibu kisheria kuwapeleka Mahakamani wote wale bila ya ubaguzi, hapana msalie Mtume kumwachia huyu ni wa Chama gani, wala huyu wa Chama gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa vibali vya mikutano na maandamano. Hili ni suala la kisheria, wamepewa wao uwezo wa kutoa vibali na waangalie kabisa mazingira na wakati muafaka wa kutoa vibali. Wakiona kama kuna mazingira ya kuweza kuvunjika amani ndani ya nchi hii, waendelee kutotoa vibali kwa sababu jambo la muhimu katika nchi yetu ni kuendelea kuwa na amani na usalama. Kama wanaona kutatokea uvunjifu wa amani vibali visitoke, tena kwa vyama vyote siyo kwa Upinzani tu wala siyo kwa CCM, wao ndiyo waangalie hali halisi ilivyo ya mazingira ya wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za uchochezi zinazotolewa na viongozi. Kuna Viongozi ambao kwenye majukwaa ya kisiasa na majukwaa mengine wanatoa kauli za uchochezi ambazo zinaashiria kuvunja amani ndani ya nchi yetu. Nchi yetu ni ya amani na tunaomba tuendelee kuwa na amani, hatupendi kuvurugwa. Wengine Viongozi watu wazima, miaka 75 na kwenda juu, wameshaishi maisha yao, wanataka kutuvurugia nchi watoto wetu wasiweze kuishi kwa amani kama tunavyoishi sisi kwa maslahi yao wenyewe.

Hili tusilikubali, Jeshi la Polisi msiwavumilie watu kama hawa, tumieni utaratibu wa kisheria, hakuna mtu ambaye yupo juu ya sheria, wote inabidi tuadhibiwe kulingana na sheria ilivyo! Hakuna kumwachia mtu ambaye mnahisi atatuvurugia nchi, Jeshi la Polisi msivumilie, tumieni sheria ya kufanya shughuli zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakuja Polisi Zanzibar; nampongeza Kamishna mpya ambaye ameteuliwa hivi karibuni, anafanya kazi zake nzuri, ana ushirikiano mzuri na Maafisa wake, kazi mpaka sasa zinakwenda vizuri, Mwenyezi Mungu amsaidie, lakini kuna matatizo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni Kaskazini Unguja, Makazi ya Polisi; Kaskazini Unguja kuna Askari karibu 400, lakini wanaokaa katika nyumba za makazi ya Polisi ni 30 tu, wengi wao wanakaa nje ya Mkoa mitaani huko. Hili jambo lina athari kubwa, kuna vishawishi vingi katika mitaa. Hivyo tunaomba sana Bajeti ya Wizara hii iongezwe ili hao Polisi waishi katika nyumba za Staha.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Kaskazini Unguja tu, hata hapa Dodoma ukizunguka katika zile nyumba, sisi tunaopita tunaona aibu, sembuse wao wenyewe wanaoishi mle? Hawa ni watu, walinzi wa amani, wanatulinda, lazima waishi katika nyumba za heshima. Naomba wafikiriwe pale wanapolala. Wasiishi tu kama wanapolala watu wengine wengine tu wa kawaida, hawa ni walinzi wetu wa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoa gari kule Nungwi. Gari hiyo imepatikana na inafanya kazi nzuri ya kulinda amani hasa katika ule ukanda mzima wa utalii wa Kaskazini, kwa sababu hapo nyuma tulikuwa tunaulizia suala hili.

Sasa taarifa iliyokuwepo, gari ipo na inafanya kazi. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutumiza ahadi yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu Kituo cha Polisi cha Mkokotoni. Japokuwa Jimbo lake lipo Mtambile, Pemba lakini kama Mbunge, naye, amelizungumzia suala hili. Niliuliza swali hapa kwamba Kituo hiki kitamalizika lini? Nikaambiwa kiko katika hali nzuri ya kujengwa, *fine!* Lakini kumbe hela hazikutolewa! Mkandarasi yuko pale, anadai. Mwaka huu zimetengwa Shilingi milioni 300. Kipindi kilichopita cha mwaka huu tunaoumalizia Shilingi milioni 450 zilitengwa, haikutoka hata senti moja. Yule aliyepewa ile kandarasi ya kujenga, ale nini na watoto wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, picha hii haionyeshi kwa Kituo cha Kaskazini Unguja tu pale Mkokotoni, lakini maeneo mengi ni hivi hivi. Lazima Serikali ijipange, itengeneze bajeti, bajeti itoke, Wakandarasi walipwe, waendelee kuishi vyema na watoto wao na wawe na hamu ya kufanya shughuli nyingine za Serikali. Vinginevyo, hawa hawatatusaidia, maana hatuwalipi. Nani anayefanyishwa kazi bure halafu ataendelea tu kupenda kufanya kazi kwenye Serikali? Siyo rahisi kitu kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hapa kuhusu mbwa wa Polisi kule Zanzibar, nikaambiwa mbwa yule amekufa, naye ndiye aliyekuwa anatumika kwenye viwanja vya ndege kuchunguza madawa ya kulevya. Nikaambiwa mbwa amekufa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kidawa!

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Muda umekwisha?

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Naendelea kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Ester Bulaya hayupo, badala yake namwomba Mheshimiwa Deo Sanga achukue nafasi hiyo, na mchangiaji wetu wa mwisho kwa wachangiaji atakuwa Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla, Naibu Waziri wa Afrika Mashariki.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wenzangu kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naungana na wenzangu vile vile juu ya Jeshi letu la Polisi, Magereza na kadhalika kwamba ni vizuri zikaongezwa fedha kwa ajili ya Jeshi hili ili liweze kufanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Waziri ambayo alikuwa ameiwasilisha jana, alizungumzia habari ya kujenga Vituo vya Polisi kila Tarafa. Sasa katika Jimbo langu la Njombe Kaskazini, Tarafa ya Lupembe, tumeshajenga Kituo na kinafanya kazi kwa muda mrefu. Ombi langu ni kwamba tunaomba tupewe Askari wa kutosha kule Lupembe, tupewe vitendea kazi ili kazi ya Polisi kule Lupembe iweze kwenda vizuri kwa ajili ya wananchi wa Lupembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Lupembe mpaka Njombe ni kilomita takribani 70. Kwa hiyo, ni mahali parefu sana, kutoka Lupembe kwenda Wilayani.

Vile vile katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alizungumzia habari ya kununua magari, vitendea kazi katika vituo mbalimbali. Ombi langu ni kwamba, pale Makambako ni *Centre* ya Kituo kikubwa kabisa katika Wilaya ya Njombe. Ni kituo kikubwa! Naomba sana katika magari haya yatakayonunuliwa, gari moja waligawe katika Kituo cha Makambako ili Polisi wafanye kazi zao za doria vizuri ipasavyo. Ombi lingine katika Kituo hiki cha Makambako, kwa sababu ni Kituo kikubwa, kiwe ni Kituo cha Kiwilaya Kipolisi pale Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri jana, amezungumzia juu ya madeni mbalimbali ambayo wananchi walio-*supply* vitu katika Jeshi la Polisi wanadai. Kule Njombe kuna mtu mmoja anaitwa Msigwa; zaidi ya miaka minne amekuwa akihudumia Magereza pale, hajalipwa mpaka hivi sasa. Mtaji wake amefilisika!

Kwa hiyo, naiomba sana Wizara iweze kumlipa. Najua kwa suala kama hili la Msigwa, Njombe, wako wengi ambao wamefilisika kwa namna walivyokuwa wanahudumia nchi nzima. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ichukue jukumu la kuwalipa ili waendelee kuhudumia Jeshi letu la Polisi, Magereza na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije upande wa boda boda. Ni vizuri Taasisi hii ya vijana wetu wajasiriamali wa boda boda, elimu ziwe zinatolewa mara kwa mara kuliko wanavyonyanyaswa, namna ambavyo wanakimbizwa, ni hatari! Mtu mmoja alichangia hapa kwamba kuna mtu mmoja alikuwa aanguke namna alivyobebwa yule abiria kwa sababu ya kukimbizwa. Nilidhani ni jambo zuri ili hawa watu wa boda boda wafanye kazi zao vizuri, wapewe elimu mara kwa mara, ni jinsi gani wanatakiwa kuendesha boda boda zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja alikuwa anachangia hapa, akasema safari hii wanaweza kuingia msituni.

Ndugu zangu naomba sana, amani hii ambayo tunayo katika nchi yetu, sisi viongozi tusiwe kama watu wa kuchochea. Naiomba sana jamii ya nchi ya Tanzania, tusikubali watu wanaochochea kwamba wataingia msituni. Huko msituni waingie wao Viongozi, wawaache wananchi wetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mjumbe mmoja katika kuchangia kwake amesema anashukuru sana *AG* namna jana alivyoomba radhi, na akamtaja Ndugu Lukuvi.

Sasa mimi niseme, mbona wao jana wamesema maneno mabaya juu ya Spika, hawakuomba radhi? Tusiwe wa kwanza kunyoosha kidole! Tuangilie vidole vingapi vinakuangalia wewe!

Mheshimiwa Naibu Spika, wameelezea habari ya Mheshimiwa Lukuvi kwamba amekwenda Kanisani kuzungumza vitu tofauti; ndugu zangu, kama nilivyosema, tusiwe wa kwanza kunyoosha kidole! Tena Kiongozi wao wa ngazi ya juu kabisa ndiye amekuwa Kiongozi wa kuchochea suala la kidini. Amani hii ndugu zangu, Wabunge wenzangu ni lazima tuendelee kuienzi, ni lazima sisi kama Viongozi tusimamie jambo hili vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri sana ya kutulinda sisi na mali zetu. Nimpongeze sana *RPC* katika Mkoa mpya wa Njombe, anafanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Ndugu zangu, nimalizie kwa kusema, Waheshimiwa Wabunge wote wa itikadi mbalimbali tuhakikishe tunaunga mkono bajeti hii ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri wamefanya kazi vizuri na Katibu wao Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Ahsanteni sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Kwa ombi maalum, kwa dakika za Meza, namruhusu Mheshimiwa Tundu Lissu halafu atafuata Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika mjadala huu. Kwa kuwa muda ni mdogo sana, naomba nizungumzie suala moja tu la Jeshi la Polisi na Mikutano ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni ya Vyama vingi. Angalau tangu mwaka 1992 Katiba yetu na Sheria mbalimbali zimeruhusu Mfumo wa Vyama vingi. Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 imetoa haki kwa Vyama vya Siasa. "Haki," siyo fadhila; imetoa haki kwa Vyama vya Siasa kufanya Mikutano ya kisiasa ya hadhara na maandamano. Naomba nirudie, ni "haki".

Mheshimiwa Naib Spika, Sheria hiyo hiyo imetoa wajibu kwa Jeshi la Polisi kulinda Mikutano ya Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, Vyama vya Siasa vina haki ya kufanya mikutano na maandamano na vile vile Jeshi la Polisi lina wajibu wa kulinda mikutano na maandamano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la kutekeleza maagizo hayo ya Sheria ya Vyama vya Siasa na hasa kwa Jeshi la Polisi na kwa Vyama vya Upinzani. Tangu zitokee vurugu zinazohusiana na gesi Mtwara na Lindi, Vyama vya Siasa vya Upinzani vimepigwa marufuku kufanya mikutano ya kisiasa katika hiyo Mikoa miwili na mpaka sasa hivi haijulikani nani ambaye amepiga marufuku kufanyika kwa mikutano ya Vyama vya Siasa katika hiyo Mikoa miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofahamu ni kwamba Serikali haijawahi kutangaza hali ya hatari katika hiyo Mikoa miwili. Haijawahi kutangaza *State of Emergency;* haijawahi kutangaza *State of War;* haijawahi kusema kwamba ni *Civil Liberties,* haki za kiraia, kama kufanya mikutano imekatazwa katika hii Mikoa miwili kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Vyama vya Upinzani ndiyo vinakatazwa. Chama cha Mapinduzi, Chama tawala kinaruhusuwa *somehow* kufanya mikutano katika hiyo Mikoa miwili. Miezi miwili, mitatu iliyopita walifanya maandamano wale waliokuwa wanaunga mkono kupinduliwa kwa Rasimu ya Warioba humu ndani, yakapokelewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, anaitwa Salma Kikwete. Wakafanya maandamano na wakafanya mkutano wa hadhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefuatilia, tumeuliza, nani aliyeruhusu maandamano na mkutano wa hadhara uliofanywa na Salma Kikwete Mkoa wa Mtwara ili tujue, kwa nini Vyama vingine vya Siasa vinakatazwa? Mpaka sasa hivi hatujapata jawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ni muda muafaka kuambiwa mbele ya Bunge hili Tukufu, ni wapi ambapo imeandikwa kwamba Salma Kikwete na CCM yake wanaruhusiwa kufanya Mikutano ya Hadhara katika Mikoa ambayo Vyama vingine vya Siasa vimepigwa marufuku? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusiana na suala hili la Mikutano na Maandamano ya Vyama vya Siasa vya Upinzani, mwaka 2013 mwanzoni, niseme hapa kwamba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Tume ya kikatiba ambayo Makamishna wake wote wameteuliwa

na Rais. Hawa sio watu wa upinzani, sio wana-CHADEMA wala wa *CUF,* ni watu ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imesema mwaka 2013 kwamba Jeshi la Polisi linakiuka Sheria. Linakiuka Sheria pale inapozuia Mikutano ya Vyama vya Siasa vya Upinzani halafu linaruhusu Mikutano ya Vyama vya Siasa, Mikutano ya CCM na mfano walioutoa ni huu ambao Vyama vya Siasa vilikuwa vinapigwa mabomu kama Iringa, Nyololo na kwingineko wakati CCM wanafanya kampeni mahali kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuzungumzi kwa sababu ni kitendo kibaya tu kwetu sisi, tunazungumza kwa sababu vitendo kama hivi, ubaguzi wa wazi wazi namna hii ndiyo ambao mara nyingine unasababisha watu kuchoka na kuamua kuvunja amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni kwamba Jeshi la Polisi lifanye kazi yake *with even handedness,* kwa haki. Kama wanazuia Mkutano wa Vyama vya Siasa, wazuie Mikutano ya Vyama vya Siasa vyote. Siyo wanakataza Wapinzani halafu akiingia Salma Kikwete kwa sababu ni mke wa Mheshimiwa Rais, wanamruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndiyo vitu ambavyo vinasababisha nchi inaingia kwenye matatizo ya uvunjifu wa amani na wengi hapa wanasema kwamba tusingependa kuelekea huko. Kama kweli hatupendi kuelekea huko, ni vizuri Jeshi la Polisi likatenda haki kwa Vyama vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hapo kwa kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri kwa kuteuliwa katika Wizara hii. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri, kwa utendaji wake mzuri katika Wizara hii. Naipongeza sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, iliyojaa au kusheheni kila eneo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyokamilika, bado naomba Wizara hii iongezwe fedha ili kukidhi mahitaji ya Wizara, itekeleze majukumu yake. Naishauri Serikali isiweke ukomo Bajeti ya Wizara hii sawa na kuwapa mwanya maadui wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la masilahi ya askari wetu ni muhimu sana. Naomba Wizara iangalie suala hili kwa uzito wake kwani linachangia sana kushawishi rushwa kwa askari wetu. Ushawishi huo unawaponza pia wale askari waadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tena sana, Wizara hii ipewe pesa kama ilivyoomba ili waweze kukidhi mahitaji yao. Malalamiko kwa Wizara hii hayataisha kama hawatapewa pesa hizo walizozihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala posho kwa askari wetu liangaliwe upya, shilingi 7,500 ni ndogo sana. Ningeomba Wizara iliangalie suala hili la posho kwa askari wetu angalau wapewe shilingi 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari wetu kwa kweli zinavunja hadhi na heshima yao mbele ya jamii. Ningeomba sana, Wizara waongee na Mashirika ya *NSSF, PPF PSPF* na mengine pia hata *National Housing*, waweze kuwajengea nyumba askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kwa Wizara hii ni usafiri, kwani magari mengi yamechakaa na yanawatia hasara Wizara kwa kufanyia ukarabati. Naishauri Serikali angalau kila mwaka wapate magari si chini ya matatu. Naomba angalau kila kituo kidogo wapewe pikipiki tatu ili waweze kukidhi huduma hii kwa Wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha kwa kusema tena kuwa, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wazidi kuiomba Serikali wapewe haya mahitaji ya bajeti kama walivyoomba. Nasema hili ili wasipate Mawaziri lawama na kuwapongeza *IGP* na *DCI* kwa kuteuliwa kushika wadhifa huu mkubwa na wenye majukumu mengi.

**MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR**: Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya walemavu wa ngozi, vikongwe na wanawake katika Mkoa wa Mara, yanalitia doa Taifa letu lenye amani na utulivu. Eneo la haki za binadamu nalo lilitia doa katika Ripoti ya Mpango wa Afrika wa Kuthamini Utawala Bora *(APRM)* hasa mauaji ya walemavu wa ngozi.

Naomba unapohitimisha utoe tamko la Serikali kutokana na mauaji haya ya kikatili. Hawa wanaohusika na mauaji haya wachukuliwe hatua za haraka.

**MHE. IGNAS ALOYCE MALOCHA**: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana na hasa ukiangalia maendeleo na kujua kuwa, Dunia kwa sasa ni kama Kijiji, kutokana na mawasiliano yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyohiyo na uhalifu, uvunjifu wa amani na ujambazi umeongezeka. Wananchi kwa kutambua umuhimu wa Polisi katika kulinda usalama wao na mali zao, wameamua kujenga Vituo vya Polisi kwa nguvu kazi, wanaomba Serikali iwaunge mkono, kumalizia majengo yao kwa kutoa mabati, sementi na thamani mbalimbali. Maeneo hayo ni Muze, Mtowisa na Ilemba.

Pia kipo Kituo cha Polisi kilichojengwa kwa asilimia mia moja kwa nguvu za Wananchi, kwa sasa kimechakaa kinahitaji ukarabati. Naomba Serikali iwasaidie Wananchi kwa kukarabati Kituo hicho kilichopo Kata ya Milepa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naviomba vituo vifuatavyo vipewe pikipiki kwani viko mbali sana na Makao Makuu ya Polisi Sumbawanga. Vituo hivyo ni Milepa, Ilemba, Mtowisa na Kipeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Laela umepanuka sana, hivyo umekuwa na changamoto nyingi, Serikali inatakiwa kupeleka gari kwa ajili ya kuwawahisha Polisi kukabiliana na uhalifu mbalimbali unaotokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Nianze mchango wangu kuhusu ushirikiano wa Polisi na Wananchi.

Polisi hawezi kufanya kazi yake bila ushirikiano wa Wananchi. Ushirikiano huu hauwezi kutokea bila kujaribu kutoa hofu inayojengeka kutokana na Polisi kuwakamata Wananchi na wakati mwingine kupigwa.

Askari wakikaa barabarani wanafanya kazi nzuri kwani kuna magendo mengi yameshikwa kutokana na kazi yao. Tatizo ni pale wanapodai kitu kidogo na wakati mwingine Wananchi huandaa fedha za hongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukizungumzia Kituo cha Polisi Wilaya ya Longido. Kituo hiki ni cha zamani, tangu enzi ya ukoloni. Kituo hiki ni kidogo kulingana na ongezeko la shughuli zinazoendelea na wingi wa matukio kwenye Wilaya hiyo.

Pili, Wanannchi wamejenga Kituo cha Polisi cha Gilay Lumbwa, lakini hakuna nyumba ya askari. Je, lini Serikali itakubali ombi la Wananchi wa Longido wanaoomba kila mwaka wajengewe nyumba za watumishi? Kituo cha Gilay Lumbwa kimejengwa kutokana na majangili wengi wa Kisomali waliowanyanyasa Wananchi mpaka Wananchi wakachukua uamuzi wa kujenga Kituo tangu mwaka 2000, kilichobaki ni nyumba za maaskari. Kituo hicho kipo mbali na Wilaya, ni kilometa 93 toka Longido na ni mpakani mwa Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya ya Longido. Hakuna kituo kingine kilicho karibu kwani Kituo cha Loliondo ni mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Longido ni Wilaya ya pembezoni na mpakani. Kituo cha Namanga kilichoko mpakani hakiwezekani kulinda Mpaka wote, kinahitajika kituo kingine.

Naomba kueleza kwamba, nimeomba Kituo hiki kwa muda wa miaka mingi, lakini hakikumbukwi. Nifanye nini wewe Waziri pamoja na Wakuu wengine mnikubalie ujenzi wa nyumba hizi ili Wananchi wapate ulinzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo nipate majibu ya Wizara, nakosa imani na Viongozi wa Wizara hii.

**MHE. ZARINA S. MABABIDA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana kwa usalama na utulivu wa nchi yetu, Serikali ni lazima wavingalie Vitengo vyote kwa umuhimu wa kipekee ili waweze kutimiza wajibu wao na kuwaondolea vishawishi mbalimbali wanavyokutana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie upya marupurupu yafuatayo:-

Naomba Serikali iwajengee nyumba siyo tu za makazi, lakini pia za kwao binafsi ili wakopeshwe na kukatwa kwenye mishahara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itawahakikishia maisha bora baada ya kustaafu. Hali ilivyo sasa, wengi wanakuwa katika hali mbaya sana wanapofikia kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Mabatini Kijitonyama ni mateso kwa Polisi wetu. Kila mtu anafahamu jua na joto la Dar es Salaam! Ni vipi mtu anaweza kuishi kwenye nyumba *(full suit)* la bati? Hivi anawezaje kuwa na vitu kama *fridge,* pasi na vifaa vingine vya umeme? Ni vipi huyu baba au mama wanalala ndani na watoto humohumo; heshima iko wapi? Hivi huku siyo kuvunja haki muhimu za binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo zamani walikuwa wakikaa kwenye nyumba za pamoja, lakini sasa wengi wanakaa uraiani ambako kuna maisha mengi ya anasa. Kwa kuwa askari wengi mishahara yao ni midogo sana, hawawezi kumudu anasa nyingi za huko uraiani, inaleta ushawishi tofauti na kama wasingeishi huko uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingerudisha hamasa kwa Polisi kwa kutoa motisha kwa Polisi yeyote anayekamata aidha mali ya umma iliyoporwa, kama vile madawa ya kulevya, wizi wa mabenki, lakini hata kwa jamii. Hii ingepunguza rushwa kwa Polisi na ingeongeza hamasa kwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *fine* za papo kwa papo zingeondolewa; kwa mfano, Wiki ya Usalama kinachotokea ni uuzaji wa stika kwa sababu hakuna ukaguzi wowote wa magari bali ni uuzaji wa stika tu. Tena kunakuwa na mashindano ya vituo kuuza stika hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachotokea ni kuendelea kuwa na magari mabovu yanayohatarisha maisha ya watu wasiojua hali halisi ya magari yabayowabeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza zetu ziko katika hali mbaya sana na hii inatokana na mlundikano wa mahabusu. Kwa nini Serikali isiangalie upya kulundika mahabusu? Hivi huyu kibaka anayedaiana na mwenzie ni kwa nini wakae mahabusu?

Mimi nashauri mahabusu wabaki wenye tuhuma zinazoeleweka za madawa ya kulevya, unyang'anyi wa silaha, mauaji na siyo ya kubambikwa na watu wa nje ambao labda kuna wasiwasi wa kutoroka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iiangalie sana suala la kubambika kesi za mauaji, dawa za kulevya na uhasama wa kimapenzi na kisiasa.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii kuhusu Bajeti ya Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikusudia kujenga Kituo cha Polisi Mjini Itigi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alichangia Sh. 2 ml. kama kianzio. *IGP* Said Mwema alifika na kuhimiza, lakini Kituo hicho mpaka sasa kimefikia hatua ya msingi kutokana na mchango wa nguvu za Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kutosha walau Sh. 30 ml. ili kwa kushirikiana na nguvu za Wananchi, tuweze kujenga Kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwahi kutoa haki kwa ajili ya kazi za Polisi Kituo cha Itigi, kukabiliana na wimbi la uhalifu Tarafa ya Itigi yenye ukumbwa wa kilometa za mraba 17,000. Cha kusikitisha ni kwamba, gari hili ni bovu, halifanyi kazi kwa ufanisi. Naomba gari jipya litolewe kwa ajili ya Kituo cha Itigi. Hali ya usalama eneo hili pana ni tete, Wananchi wanaendelea kuporwa mali zao mchana kweupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO**: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazingira duni wanayoishi askari wetu (Polisi, Magereza na FFU) ni ya kusikitisha sana tena ya kudhalilisha utu wao. Nikianza na mazingira yao ya kazi ni mabovu, hawana vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi, hivi sasa uhalifu unafanyika kisayansi kwa mbinu za hali ya juu; je, askari wetu wanavyo vifaa vya

kutosha kwa sababu kila kukicha askari wetu wanauawa sana katika matukio mbalimbali hususan ya kijambazi? Serikali inunue vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi wanayoishi ni aibu nyingine ya hali ya juu, maeneo ya mijini mmejenga maghorofa, je, walioko Mikoani hususan Wilaya ya Kibondo ni lini watapatiwa makazi bora? Hii ni kwa Polisi, Magereza na FFU, maana hakuna aliye na nafuu. Tunataka makazi bora kwa askari wetu hao mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa maana ya mishahara ni aibu nyingine katika Taifa hili. Ukiangalia kazi wanazozifanya na ujira wao inasikitisha sana na ndiyo maana wanapokea rushwa, wanatorosha wafungwa au mahabusu na mambo mengine yanayofanana na hayo. Serikali iliangalie hili, mishahara yao iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kwa upendeleo katika upandishwaji vyeo pamoja na nafasi za kwenda kusoma ili kujiendeleza kielimu, hili ni wazo kubwa tunaitaka Serikali itende haki, wenye sifa wakasome na vyeo wapandishwe inavyostahili. Haya niliyoyaeleza yakishughulikiwa, askari wetu watafanya kazi kwa moyo na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Chikawe, kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii ambayo ina changamoto kubwa; ni wajibu wako kuinusuru kwa kuisafisha Wizara hii ili kurudisha imani kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kuwa, wahamiaji haramu wameanza kurudi nchini, katika maeneo ya Karagwe na Misenyi na kusemekana kuwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji huchukua rushwa na kuwakaribisha tena hapa nchini, pamoja na Serikali kutumia gharama kubwa katika Operesheni Kimbunga. Je, Serikali kupitia Wizara hii inaweza kutuambia ni mkakati gani ambao wanao na kuhakikisha kuwa waliorudi wanaondoka na ambao hawajarudi wasifanikiwe kurudi?

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ndogo wanazopewa askari ndiyo hasa kichocheo cha rushwa, kwani ni lini hasa posho zao zitaongezwa? Pia wanatumwa kazi, mfano wanapotumwa kufanya kazi na *SUMATRA* au *TRA,* wenzao hulipwa lakini askari wanakopwa. Hii ni dhuluma maana hayo madeni huwa hawalipwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubambikizwa kesi, Wananchi hata kwa kesi ndogo tu wanakaa rumande kwa muda mrefu na kusema ushahidi haujakamilika. Hii inanyima haki kuwa mtu kupoteza muda mrefu rumande hata kama hana kosa la msingi. Pia ningependa kujua mna mpango gani wa kufunga *CCTV* katika Majiji kama vile Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga na Mbeya. Hii itasaidia kupunguza uhalifu na pia kupata ushahidi wa haraka na kumaliza tatizo la kurahisisha upelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua ni lini Serikali hii kupitia Wizara hii mtaleta tochi za uhakika ambazo zinaonesha spidi inayokwenda gari hilo, picha ya waliomo ndani, pia namba ya gari hilo, ili kuondoa utata na rushwa za askari wa barabarani kama ambavyo Naibu Waziri aliahidi wakati ananijibu swali langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waziri na Naibu Waziri, wawaangalie sana hawa askari wa barabarani wanaotumiwa na mabosi wao, kutaka wapelekewe pesa. Wakitambua kuwa askari hawa hawana shamba wala soko, huku sikuwaomba watafute rushwa na

kuwapelekea wao? Huu ni udhalilishaji na uvunjaji wa sheria. Hii ni aibu, ni wazi waache kufanya hivyo. Ahsante.

**MHE. MARIAM NASSORO KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na napongeza juhudi za Serikali kupitia Viongozi wetu ambao ni Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, wamejitahidi sana kufanya kazi na hasa katika kupambana na uhalifu katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi mazuri lakini changamoto haziko Serikalini katika utendaji au maendeleo ya nchi. Kubwa kwangu ni Ofisi ya Polisi ya Wilaya ya Mbagala, ina Wananchi 582,000 na katika Wilaya ya Temeke Mbagala ndiyo eneo lenye matukio mengi ya kihalifu. Askari wanakaa nje hawana pa kufanyia kazi na hali ni mbaya sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Ofisi ni mbaya sana na nyumba zilizopo pale za makazi ya Polisi hao ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha hayo ni magumu na yanakatisha tamaa askari hao wanakosa moyo wa kufanya kazi kabisa. Nawapongeza askari wanafanya kazi kama kawaida bila kukata tamaa na waendelee kuwa na moyo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mnipe maelezo ya kutosha vinginevyo mtoe Wilaya ya Polisi ya Mbagala maana hakuna sifa japo kinatusaidia sana. Msipofanya hivyo nitatoa shilingi na sitairudisha tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza askari kuwekewa maduka yenye bidhaa zenye bei nafuu, ni jambo jema tunapongeza juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Magereza ni mbaya, mahabusu wamejaa Magerezani na huduma ni finyu sana. Nyumba za Askari Magereza Keko zinatisha, wanaweka watoto kwenye vibanda vya kuku, mabati kama wanalala kuku, ni aibu na huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti za wakuu wa Magereza. Bajeti wanayopewa ni ndogo sana kulingana na changamoto zilizopo magerezani naomba sana waangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri pia ni tatizo japo niliona Gereza la Keko lilipewa gari. Gari moja halitoshi, waongezwe mahabusu wanaugua usiku na wengine kupigana, wapewe magari ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahamiaji haramu na wasio haramu wamezidi Mkoa wa Dar es Salaam. Wahindi, Wachina na Wakenya, wamejaa viwandani, hali inayopelekea Vijana wetu wa Kitanzania kukosa ajira na watu wa nje kuhodhi ajira katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *Passport* na utoaji wa huduma katika Makao Makuu ya Uhamiaji ni mzuri sana; nawapongeza na waendelee hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, zimamoto ndiyo hali mbaya sana. Natambua changamoto za ufinyu wa bajeti tuliyonayo, lakini tuangalie kwa umakini maeneo ambayo hali ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kufanikisha kuleta Hotuba ya Wizara hii ndani ya Bunge lako Tukufu ili nasi tutoe maoni yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kutoa Vitambulisho vya Taifa ni kweli litafanikiwa kabla ya Uchaguzi Mkuu 2015? Sasa ni takribani miaka mitatu vitambulisho vilivyotolewa ni vichache sana ukilinganisha na idadi ya Watanzania wanaostahili kupata vitambulisho hivyo. Je, mpaka sasa *NIDA* wamepewa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu mbovu wa kutowalipa kwa wakati askari wake pesa zao wanazodai ambazo ni haki yao. Kwa mfano, askari polisi anatumwa kwenda safari bila ya kupewa pesa za kujikimu. Je, askari huyu anaenda kuishi vipi huko anakotumwa aende kufanya kazi? Tunaitaka Serikali kuthamini Jeshi la Polisi kama wanavyowathamini Jeshi la Wananchi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni takribani miaka miwili tangu 2012/2013 - 2013/2014, nimekuwa nikiomba Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kulipatia pesa Gereza la Mng'aru, Rufiji, Mkoa wa Pwani ili kuweza kutekeleza Mradi wao wa Ufugaji wa Samaki kwani wana chanzo kizuri cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu utawasaidia wafungwa na askari wetu wanaofanya kazi hapo kupata kitoweo. Kubwa zaidi, kujiongezea kipato katika Gereza hili ili waweze kukidhi ama kutatua matatizo madogo madogo yanatokea Gerezani hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni uchakavu wa nyumba za askari magereza katika Gereza la Mng'aru, Rufiji, nyumba zimejengwa miaka mingi, mabati yamechakaa, zinavuja na hazifai kwa makazi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali kuboresha makazi ya askari maregeza ili nao wasiwe wafungwa ila wawe waangalizi wa wafungwa wetu na waweze kuwarekebisha vijana wetu.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyotengwa ni ndogo sana hasa kwa Miradi ya Maendeleo, shilingi bilioni 6.8 kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujenga Vituo vya Polisi katika kila Tarafa limekuwa ni hadithi ya kuwahadaa Watanzania kila mwaka kuwa mmetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, lini Vituo vya Polisi Bassotu, Endasak na Balangdalalu Wilayani Hanang vitajengwa? Kituo cha Polisi Bassotu ni cha miaka mingi, tangu 1964 kituo hicho kipo kwenye nyumba za Mission RC hawana Ofisi wala nyumba za watumishi. Hamwoni kuwa sasa ni wakati wa kujenga vituo hivyo na nyumba za watumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi hawana zana za kufanyia kazi na vitendea kazi mfano; usafiri, mafuta na fedha za matumizi. Polisi katika Wilaya zetu wamekuwa ombaomba kutaka usafiri panapotokea uhalifu, wanashindwa kufika kwa wakati magari hayana mafuta. Fedha zitolewe ili *Post* zote ziwe na pikipiki za kutosha na magari. Vilevile nashauri posho ya askari iwe zaidi ya shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi ni walinzi wa amani kwa umma, lakini hutumika vibaya au hutumiwa vibaya na Viongozi wa Serikali; mfano, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kwa ajili ya masilahi yao na Serikali iliyoko madarakani.

Unyanyasaji wa Wananchi kwa kubambikiziwa kesi kama yalivyotokea Hanang, Babati, kukamatwa Wananchi wa Galapo, Mamire, Vilima Vitatu, Bassotu na maeneo mengine mengi. Migogoro inaweza kuwa ni ya ardhi lakini kesi inabadilishwa kuwa ya ujangili au uvuvi haramu wakati mtu huyo si mvuvi!

Mimi mwenyewe yalinikuta Kalenga Mkoani Iringa, nilitekwa na *Green Guard* ya CCM na kupelekwa Makao Makuu ya CCM. Baada ya kutafutwa na wenzangu, polisi walifika Makao Makuu ya CCM kuniokoa. Matokeo yake sikupata huduma kwa polisi kutonipa *PF3* kwa ajili ya matibabu kwani walininyang'anya, walinipa ambayo haikujazwa na Daktari. Je, huoni kuwa hawafanyi kazi yao ipasavyo?

Wananchi wa Kijiji cha Mulbadaw eneo la Ghama, Wilayani Hanang, walichomewa nyumba na Viongozi wa Kijiji na Kata wakisimamiwa na Wilaya na Polisi. Je, huo si ukiukaji wa haki za binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi hutumika vibaya na Vyombo vya Serikali; hilo liangaliwe kwa uangalifu. Rushwa kutolewa au kupokea ni kutokana na fedha ndogo inayotolewa na Serikali kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeni fedha kwa polisi.

**MHE. MOZA ABEID SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hulazimika kila mwaka kutenga bajeti ya fedha Bungeni kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Polisi; na kwa kuwa zinalenga ukarabati; je, ni lini Vituo vya Polisi Mkoa wa Dodoma na nyumba za Askari Polisi vitajengwa ili askari wapate nyumba nzuri kuliko vibada walivyojijengea hasa hapa mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini kunakuwepo mgao wa nyumba bila kujali askari huyo ana familia au hana? Inadhalilisha sana kuona askari wetu na familia zao wanaishi chumba kimoja au kwa kuwa hamna jinsi ya ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, uajiri katika Jeshi hili hufanyika kwa usiri kwani imekuwa ya upendeleo, haiko wazi, ukabila na udini umedhihiri ndani ya Jeshi hili; sasa ni lini ubaguzi huu utaisha? Hamwoni madhara yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati wa uwazi na ukweli na Ulimwengu huu ni wa Sayansi na Teknolojia, twende na wakati tulionao kwani Dunia nzima wanafunga *CCTV Camera* kutambua wahalifu. Je, ni kwa nini raia hawaelezwi faida kama hiyo ya *camera* ili wale wanaovamiwa kwenye nyumba za wageni majumbani kubaini kwa urahisi wahalifu? Nashauri Jeshi lichukue *tender* hiyo ya *camera* na kutoa elimu kwa raia ili kupunguza ongezeko hili la uhalifu. Mahabusu ni wengi mno, ni gharama kusubiri upelelezi wakati tunaweza kama ilivyo nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi karibuni limeanza zoezi la Vitambulisho vya Taifa, kumekuwa na manung'uniko kila maeneo, watu wengi hawajapata Vitambulisho

vinavyotolewa kwa taratibu sana. Lini watu wote watapewa Vitambulisho hivi na tunaelekea Uchaguzi Mkuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Vyuo vya Polisi vinatoa askari kila mwaka; lini sasa mtapeleka askari wa kutosha kwenye vituo vilivyo na upungufu wa Askari Polisi hasa Wilaya ya Bahi na Chamwino ili kuwapunguzia adha polisi wanaolinda vituo vidogo vya Mtungutu kulazimika kukaa wiki mbili eneo hilo? Kufanya hivyo pia si sahihi sana na si kuwatendea haki kwa kuwatenganisha wiki mbili na familia zao. Naomba hilo liangaliwe.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, Wizara na Askari wote chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri ya kudumisha amani na utulivu tuliyonayo hapa nchini. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni yafuatayo:-

(a) Kituo cha Polisi cha Wilaya (Manyoni) ni kidogo na chakavu, hakina hadhi ya kuwa Kituo cha Wilaya. Kwa kutambua umuhimu wa kujenga Kituo cha Kisasa, tayari *Plot* ya kujenga kituo kipya imepatikana (eka 20). Pili, Wananchi wakiongozwa na Mbunge wao, wameanza kufyatua matofali ya ujenzi. Hadi sasa matofali takribani 5,000 yamefyatuliwa.

Tunaomba Serikali kupitia Wizara hii, ituunge mkono ujenzi uanze. *IGP* aliyepita aliandika barua akiahidi Jeshi la Polisi lipatiwe fedha ili kuunga mkono jitihada za Wananchi, kwa bahati mbaya ahadi hiyo bado haijatekelezwa hadi sasa. Nazidi kuomba Serikali iunge mkono Mradi huu kwa kutenga fedha katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 za kuanzisha ujenzi wa Kituo hiki.

(b) Nyumba za Askari Polisi na Magereza zilizopo Manyoni ni chache na chakavu sana. Ombi ni kwamba, nyumba zilizopo zikarabatiwe na pili uanzishwe mpango wa kujenga zingine mpya.

(c) Uhaba wa *Radio Calls* Vituo vya Vijijini. Kituo cha Polisi cha Wilaya hakuna mawasiliano na Vituo vya Vijijini hasa maeneo ambayo bado mtandao wa simu za mkononi haujafika. Kwa hiyo, Vituo vya Polisi vya maeneo hayo vipatiwe *Radio Calls* ili mawasiliano yaweze kupatikana. Vituo hivyo ni vile vya Makonda, Heka na Seuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kurudia kusema kwamba, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. EMMANUEL J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mathias Chikawe, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wengine, kwa utendaji wao mzuri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kushauri mambo machache yafuatayo:-

Kwanza *NIDA* inasikitisha kuwa Mradi wa Vitambulisho haupewi uzito wa kutosha. Natambua kazi kubwa inayofanywa na Waziri na wenzake, lakini Wizara ya Fedha imekuwa haitoi ushirikiano wa kutosha. Kwa mfano, Mwaka wa Fedha 2012/2013 fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huu ni bilioni kumi, lakini zilizopokelewa ni chini ya bilioni tano. Hii ni pamoja na mahitaji halisi ambayo yalikuwa bilioni 150. Mwaka wa Fedha 2013/2014 fedha zilizotengwa ni bilioni 150, lakini zilizopokelewa ni chini ya bilioni 40. Hili ni jambo la aibu na halikubaliki.

Pili, posho za Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto zimeendelea kuwa chini, wanalipwa shilingi 5,000 kwa siku. Kamati ya Bajeti katika uwasilishaji wake katika Bajeti

2013/2014, iliamua posho hiyo iongezwe. Naishauri Serikali ihakikishe posho hii inaongezeka ili askari wetu waweze kutimiza wajibu wao vizuri.

Tatu, ili Taasisi zetu ziweze kujitegemea ni muhimu zipewe uwezo. *Retention* ya Uhamiaji na Zimamoto ziongezwe, lakini pia Jeshi la Magereza lipewe mtaji ili liweze kutekeleza Miradi ya kisasa ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji na hivyo, kutekeleza nia ya kujitegemea kwa Magereza na kusaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemalizia kwa kuwatia moyo Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake na kuwahakikishia kuwa, tutaendelea kuwaunga mkono.

**MHE. WILIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kituo cha Polisi Kimende na Dodi. Isimami tumeanza kujenga, naomba ushiriki wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale Polisi wanaofanya kazi kwenye maeneo ya Vijijini kama Pawaga au Idodi na Ismani, angalau wakopeshwe pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa umakini na uhodari wao wa kuhakikisha usalama wa nchi na raia unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekumbwa na wingi wa waingiaji haramu kwa makundi kutoka Ethiopia, wanakamatwa na wanashtakiwa. Wengine wanalipa faini na wengine wanafungwa, lakini wanapomaliza kifungo wanabaki magerezani wanaongeza msongomano. Tunashuhudia wengine wanagoma kula kwa kudai kurudishwa kwao. Nataka kujua kwa nini Serikali hailishughulikii tatizo hili la kuwarudisha hawa wahamiaji haramu nyumbani kwao; kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wanaostaafu au wanaofariki wakiwa kazini wamekuwa wanadai mafao yao kwa muda mrefu bila ya kulipwa. Hii inasababisha maisha yao yawe duni pamoja na kazi kubwa waliyoifanya ya kudumisha ulinzi na usalama wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanadai zaidi ya miaka kumiwanakwenda na kurudi bila mafanikio na wakati mwingine wanaambiwa mafaili hayaonekani wanateseka. Je, ni lini Serikali itafanya mabadiliko ili mafao haya yapatikane?

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kuna matatizo makubwa ya magari ya *escort* kwa Viongozi. Magari haya hayafai kabisa kutumika, ni aibu na hata wakati mwingine yanagoma njiani. Magari haya yamekuwa yakitumika kwa muda mrefu; hivyo, hayafai kutumika, lakini pia na vitendea kazi kama *radio call* kwa *traffic* zimechoka wanatumia simu zao za mkononi kwa mawasiliano. Tunaomba Waziri achukue hatua za haraka katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Mazizini – Magharibi, Serikali iwatafutie gari la kudumu pamoja na kujenga nyumba za wafanyakazi katika Kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu, kwa Hotuba nzuri. Uwezo wa Jeshi la Polisi kifedha bado ni mdogo katika ngazi ya Wilaya na Kata. Bado shughuli za Polisi

zinakwama kwa sababu ya uhaba wa fedha. Fedha ziongezwe katika bajeti ili Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi ya ulinzi na usalama wa watu na mali zao kwa ukamilifu. Aidha, siyo vizuri raia kuchangia fedha yoyote katika operesheni na shughuli za Jeshi la Polisi, kwani inawanyima haki baadhi ya watu wanaozozana katika migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yatolewe kutoka ngazi ya juu kwa Polisi Mkoa wa Manyara na Jeshi la Polisi Wilaya ya Kiteto ili kumaliza mgogoro wa ardhi ndani ya Hifadhi ya Emboliye Mwitongos na kurejesha amani. Kama hukumu ya Mahakama ya Rufaa inavyoelekeza, sheria iwafikie na kuwabana wahalifu wakubwa ambao ni wakulima wakubwa, walioshikwa na kufungwa ni vibarua tu, matajiri wao hawajaguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgogoro wa Mwitongos Kiteto, Polisi wasimame wima bila kuegemea upande wowote katika mgogoro husika. Mgogoro huu ni wa rasilimali ardhi na una pande nyingi. Uhalifu na makosa pande zote za mgogoro. Kwa sasa picha inayojitokeza ni Polisi kuwalalia wafugaji zaidi. Wanaoshikwa na kubambikizwa kesi ni wafugaji. Mgogoro wa ardhi ya Mwitongos Kiteto umekuwa mradi mkubwa kifedha kwa polisi Kiteto. Hili likemewe lisiendee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ya Silanga Kiteto ijengewe Gereza sasa badala ya kuendelea na jengo la muda linaloendelea kutumika kama Gereza.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka pale Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani, atakaponipatia maelezo ya kina kwenye maeneo yafuatayo:-

- Kuendelea kwa mauaji ya *albino* nini juhudi za Wizara ya Mambo ya Ndani kukomesha mauaji hayo sanjali na mauaji ya wanawake kule Butiama?

- Kama imeshindikana Wizara iombe msaada wa Polisi wa Kitaifa ili watoe ushirikiano kama wanavyoshirikiana kukamata magari yaliyoibiwa nchi mbalimbali.

- Inakadiriwa kuwa zaidi ya *albino* 80 wamekwishauawa na wengi kuongezewa ulemavu, zaidi ya ule walionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani anipe maelezo ni kigezo gani kilichotumika kumwacha nje bila kesi Mchungaji aliyeamuru waumini wake kuchoma moto Kiwanda cha kupiga chapa Vitabu vya Dini ya Kiislam kule Mikocheni na kuendelea kuzuiliwa dhamana kwa Sheikh Ponda Issa Ponda? Kama hoja ni uchochezi, ule wa Mchungaji ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Lindi wanaishi kwenye magofu, jambo ambalo ni hatari. Je, kuna juhudi gani zinafanywa kuwaondolea adha hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi hukatwa Sh. 5,000 kila mwezi kwa ajili ya mfuko wa kufiwa lakini pale Polisi anapofiwa pesa hutolewa kwa kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri alijulishe Bunge lako Tukufu ni fedha kiasi gani zimekusanywa kupitia Mfuko huo. Ni kiasi gani kimetumika na kiasi gani kimesalia kwenye Mfuko huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii haitekelezeki hata kidogo kwani ya mwaka jana haikutekelezwa. Hii ni aibu kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja.

**MHE. CHIKU ALFAH ABWAO**: Mheshimiwa Naibu u Spika, pamoja na kuchangia na kuwatetea askari kwa matatizo wanayoyapata kutokana na ukali wa maisha, bado naendelea kuiomba Serikali iwaangalie na kuwasaidia askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nimetoa malalamiko juu ya *RCO* Wilaya jinsi alivyowatesa vijana wengi wa Mkoa wa Iringa. Iringa Mjini - Jimbo la Ismani, Kilolo, Kalenga na Mufindi, vijana wengi wanateseka kwenda kwenye kesi zisizoeleweka na wengine baada ya kufunguliwa kesi wanasoteshwa mahabusu na baadaye wanatolewa kwa kuonekana hawana kesi na baada ya malalamiko mengi wanahamishwa. Pia nimelalamikiwa kuwa ni mlevi wa kupindukia, anafanya kazi akiwa analewa saa za kazi, anafanya kazi kwa vitisho. Hivi ana sifa gani ya kuwa askari?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nitatoa shilingi, natoa shilingi si kwa kuwa Waziri ndiye tatizo, yeye ameyakuta matatizo mengi, lakini ndiye aliyepo ambaye tunatoa malalamiko ili arekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo katika nchi hii ya Jeshi la Polisi yanatokana na Viongozi kutumia vibaya Jeshi la Polisi, vitisho vingi kwa Vyama vya Upinzani, ubaguzi wa kiitikadi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shilingi ili aone uchungu nilionao juu ya matatizo yaliyopo ayafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema.

**MHE. HAJI KHATIBU KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Muumba wa Mbingu na Dunia, kwa kuniamsha salama siku ya leo na nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandikishaji wa Vitambulisho vya Taifa ni jambo jema sana kwa Wananchi hasa pale Wananchi wanapotaka kusafiri kwenda sehemu yoyote ikiwa ndani ya nchi au hata nje ya nchi. Inakuwa vigumu kwa safari hiyo endapo Mwananchi hana kitambulisho; hivyo ndiyo maana Wananchi wamejitokeza kwa wingi katika zoezi hilo si Zanzibar wala Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la uandikishaji wa Vitambulisho vya Taifa wiki moja iliyopita lilikuwa likiendelea katika Kisiwa cha Pemba kwenye Wilaya zote za Pemba. Zoezi hilo lilianza katika Wilaya ya Mkoani Pemba. Katika Wilaya hii, zoezi lilipangiwa wiki mbili na lilienda vizuri kiasi kwamba, Wananchi wote waliojitokeza waliandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi hili Wilaya ya Mkoani Pemba, zoezi lilihamia Wilaya ya Chakechake Pemba, nako zoezi lilienda vizuri na Wananchi wote waliojitokeza waliandikishwa ndani ya wiki mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya zoezi kukamilika katika Wilaya Chakechake lilihamia Wilaya ya Wete, ndani wiki mbili nako hali ilienda vizuri kama Wilaya zilizotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, zoezi hili la uandikishaji wa Vitambulisho vya Taifa lilimalizia Wilaya ya Micheweni. Wilaya ambayo kwa masikitiko makubwa zoezi hilo lilipangwa kufanyika kwa wiki moja, jambo ambalo lilisababisha Wananchi walio wengi hawakuandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo iliyojitokeza Wilaya Micheweni hasa kule Jimboni kwangu Micheweni, nitamtaka Mheshimiwa Waziri, wakati wa kufanya majumuisho, aniambie ni sababu gani na kigezo gani kilichotumika Wilaya ya Mkoani, Wilaya ya Chake na Wilaya ya Wete, zipangiwe wiki mbili na Wilaya ya Micheweni ipangiwe siku mbili; jambo ambalo lilisababisha Wananchi wengi kukosa kuandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi waliopandishwa vyeo mwaka 2002 hadi sasa wanalipwa mshahara ambao walikuwa wakilipwa kabla ya kupandishwa vyeo vyao vya sasa, jambo ambalo linawasononesha askari hawa. Naomba Mheshimiwa anipatie ufafanuzi wa jambo hili ni kwa nini hadi sasa askari hawa hawajalipwa mishahara kulingana na vyeo vyao vya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 Bunge lilipitisha posho ya Askari Polisi Sh.225,000, lakini hadi sasa Askari Polisi wanalipwa posho ya zamani ya shilingi 150,000 kwa mwezi. Naomba wakati wa kufanya majumuisho jambo hili litolewe ufafanuzi linawasononesha sana askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari Polisi Wilaya ya Micheweni imekuwa ni kero kubwa kwa askari wa Kituo Kikuu cha Wilaya ya Micheweni. Baadhi ya askari wa Kituo hiki Kikuu cha Wilaya ambacho kipo Jimboni kwangu, wanalazimika kuja na kurudi kila siku kwa sababu ya kukosa makazi ya kuleta familia zao kwenye sehemu ya kituo chao cha kazi. Naomba wakati wa kufanya majumuisho nipewe ufafanuzi wa ni lini nyumba hizi za askari hawa zitajengwa wakati ardhi ya kujenga nyumba hizo ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa gari kwa Ofisi ya Uhamiaji Wilayani Micheweni ni jambo la msingi sana na muhimu, kwani Wilaya hii ya Micheweni, Jimboni kwangu, ambako ndiko iliko Ofisi ya Uhamiaji Wilaya, Ofisi yenye changamoto nyingi ambazo utatuzi wake unahitajika usafiri wa gari na siyo pikipiki kama ilivyo sasa.

Wilaya hii imezungukwa na madiko mengi sana na vilevile Wilayani hii ipo pembezoni mwa bahari iliyopakana Kenya. Tukizingatia wakati huu ambao magaidi wa Kisomali na hali halisi ilivyo sasa Nchini Kenya, ni vyema Askari wa Uhamiaji wa Wilaya ya Micheweni wapatiwe gari kwa ajili ya operesheni badala ya pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupatiwa usafiri wa gari Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni siyo jambo geni, kwani Mheshimiwa Naibu Waziri alipofanya ziara katika Wilaya ya Micheweni, tulikutana na tulizungumzia suala hili na yeye binafsi alilikubali na alitoa maelekezo kwa Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, lakini hadi leo hakuna utekelezaji. Ninakuomba wakati wa kufanya majumuisho nipewe ufafanuzi wa jambo hili na Wizara ni lini Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni itapatiwa gari kwa ufanisi wa kazi zake badala ya pikipiki iliyopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inaendelea kukumbwa na matatizo mbalimbali ikiwepo:-

- Uhaba wa nyumba za askari.

- *Budget* ndogo ya Wizara.

- *Ration Allowance* kubakia Sh. 15,000 kwa mwezi na hali ya maisha kuendelea kuwa ngumu.

- Askari kutopandishwa vyeo mpaka wanakuwa *frustrated* na *OCDs* wengi wamebakia na vyeo hivyo kwa miaka kadhaa. Kwa mfano, *OCDs* wa Kanda ya Kati.

- Askari kutokwenda kozi kwa muda mrefu, jambo ambalo linaua uzalendo wa askari wetu.

- Kero nyingine ni askari wa barabarani kupewa kiwango cha kesi ambazo wanatakiwa kukamata barabarani kwa mwezi na kwamba, zisipungue 60 na wapeleke faini ya shilingi 1,800,000 kwa mwezi. Askari atakaeshindwa masharti hayo, huvuliwa kofia na kuondolewa barabarani.

Sasa nataka kujua ni lini Wizara hii itashughulikia kero hizi na kuziondoa au kuzipunguza?

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba, bajeti ya Jeshi la Polisi na Mambo ya Ndani ni ndogo. Naomba Serikali iangalie kwa kina masilahi ya Askari ya Polisi na Magereza. Askari hawa wanaishi maisha magumu.

Naomba Serikali inipe maelezo ya kina kwa nini kuanzia 2010 hadi sasa Polisi wanatumia nguvu ambazo siyo za kutuliza maandamano na kuumiza watu wengi wengine? Polisi hawaoni sehemu nyingine Duniani ambapo vurugu zinatulizwa bila kutumia risasi za moto?

Jambo la pili ni kuhusu *parking* nyingi, kwani Polisi wameamua kazi hii ya kisheria ifanywe na watu binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nakumbusha Gari la Polisi kwa Kituo cha Haydom na Dongobesh katika Wilaya ya Mbulu pamoja na mawasiliano ya *radio call* kwa Tarafa ya Nambis, Yaeda Chini na Daudi.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, pole na majukumu. Huu sasa ni mwaka wa 12 toka wananchi wa tarafa ya chipanga Wilaya ya Bahi walipokamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi kwa kujitolea hadi kukikamilisha wakati huo kwa takribani Sh. 30,000,000/= lakini hadi leo Kituo hicho cha Polisi hakijapewa Askari wala hakuna dalili za kukifungua licha ya mimi mwaka 2012 kumwomba aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Shamsi Nahodha kutembelea kituo hicho; na alipotembelea alishangazwa sana na kupuuzwa kwa juhudi za wananchi kushirikiana na Polisi katika kuimarisha usalama na akaagiza Kituo hicho kikubwa, kizuri na cha kisasa kifunguliwe mara moja. Lakini hadi leo Kituo hicho hakijafunguliwa.

Hata hivyo sikuchoka, nililalamika kwa Waziri aliyemfuatia Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi na akanitaka nimwandikie barua na nilifanya hivyo, lakini hadi anaondoka hakuwahi kujibu barua hiyo au kutoa maelekezo yoyote ili kituo hicho kifunguliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuandika maoni yangu hayo nikikuomba uchukue juhudi ili kituo hicho sasa kifunguliwe kabla ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kupata majibu yako wakati ukijibu hoja hii ya bajeti ya Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Swaila katika Wilaya ya Nkasi ina matukio mengi sana ya uhalifu hasa ya mauaji na vijiji vyake vina miundo ya barabara ambayo siyo mizuri Korongwe. Kata ya Korongwe kijiji cha Korongwe kiko mwambao mwa Ziwa Tanganyika.

Hii Kata ya Korongwe kila mara inavamiwa na maharamia toka *DRC Congo* bila woga wowote ule na kurudisha maendeleo ya kijiji hiki kudumaa kiuchumi. Naomba Wizara yako itume hata wataalamu wako wakachunguze ukweli huo katika vijiji hivyo vya Makao Makuu ya Kata ya Swaila na Korongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine nyeti kabisa ni kuhusu kujenga mahabusu ya washitakiwa katika Mji wa Namanyere. Kwanza kabisa nashukuru sana Wizara ya Sheria na Katiba kutupatia Hakimu wa Wilaya, sasa kuna usumbufu mkubwa sana kwa washitakiwa wa Wilaya ya Nkasi, maana mara baada ya kuahirisha kesi inabidi washitakiwa wote wapelekwe Sumbawanga kilometa 100 kwenda tu, sasa ni gharama sana kwa Serikali yetu, na kama gari lipo, mafuta hakuna. Pia ni hatari washitakiwa kusafiri kila mara umbali wa kilometa 100. Kwa hiyo, naomba Wizara yako kwa hilo, maana kiwanja kipo cha muda mrefu sana.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuweza kujenga Kituo cha Polisi cha Mkokotoni. Ni matumaini kwamba Serikali itaweza kulimaliza jengo/kituo hicho kwa wakati na nategemea pesa zitatengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Jimbo langu la Tumbatu limo katika Wilaya ndogo ya Tumbatu Zanzibar. Vile vile Tumbatu ni kisiwa na kiko katika bahari. Kutokana na uhalisia huo, naomba Serikali kutuwekea Kituo kidogo cha Polisi ili kiweze kusaidia masuala ya ulinzi na usalama na kuzuia uhalifu.

**MHE. ABUU HAMOUD JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha nami kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2014/2015.

La pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuandaa bajeti nzuri yenye kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ulinzi shirikishi ulipoanzishwa ulikuwa na maana kubwa sana ya kushirikisha raia ili washirikiane na Polisi wetu katika kuleta utulivu katika maeneo mbalimbali, ila sasa imeibuka dhana tofauti ya utaratibu huu kwa Polisi Jamii kugeuza kazi hii kama ni mtaji kwao ya kujipatia fedha kwa kuomba rushwa, kutembea na pingu kwa kuwatisha wananchi na wakati mwingine kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wananchi pindi wanapowakamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo geni, kwani bado linaendelea kutendeka, Polisi Jamii wamekuwa wakifanya hivyo nyakati za usiku na hata wakati mwingine nyakati za mchana. Wananchi wamekuwa wakilalamikia sana hali hiyo na hivyo kuwapelekea kutotoa ushirikiano wa kutosha kwa Polisi Jamii na kutokuwa na imani nao.

Naliomba Jeshi la Polisi kupitia Serikali kutoa mafunzo kwa Polisi Jamii ili waweze kufuata sheria za nchi kama zilivyowekwa kwa mujibu wa Katiba na siyo kujichukulia sheria mikononi.

Kufanya hivyo ni kukiuka na kuvunja sheria za nchi. Naomba Mamlaka husika kuweka utaratibu wa kuwachunguza Polisi Jamii hawa kabla hawajajiunga na utaratibu huu kwani wengi wamekuwa na rekodi mbaya kwa jamii, hivyo hujiunga na Polisi kama tu kuficha matendo yake.

Vile vile kuna tatizo la kutokuwa na Askari waaminifu. Hapa nazungumzia askari wetu wa usalama barabarani, wamekuwa wakila rushwa pasipo kuzingatia maadili na sheria za kazi, kupitia hizi faini za barabarani zinazotozwa na Jeshi la Polisi. Chombo hiki kingeweza kuliingizia Taifa hili fedha nyingi sana na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu, ila Jeshi la Polisi limekuwa likipoteza fedha nyingi sana kwa kuwa na Askari wasiokuwa waaminifu. Naishauri Serikali kuchukua hatua kali sana kwa Askari wake ambao siyo waaminifu, kwani wamekuwa ndiyo chachu ya kuinyima Serikali fedha zitozwazo kama faini ya makosa mbalimbali yanayofanywa barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wamekuwa wakiishi katika hali duni sana na hivyo wangine kupelekea kujiingiza katika matukio ya kihalifu. Mifano ipo mingi sana ambayo imeshawahi kutokea na hivyo tunatakiwa kujifunza kupitia makosa. Askari wetu wamekuwa wakipata mishahara midogo, marupurupu hakuna, pia wamekuwa wakiishi katika maisha duni, hawana nyumba nzuri za kuishi, hivyo kuwafanya wapate majaribu na ushawishi mkubwa wa kutaka kujiongezea kipato ili waweze kuishi maisha mazuri. Maboresho hayo pia yafanyike katika kuwapatia *uniform* za kutosha na kuondokana na zile chakavu, vitendea kazi vya kutosha kama magari, virungu, pikipiki na mambo mengine ambayo yatawarahishia kufanya kazi bila shaka,

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barua yangu ya awali niliyoiandikia Wizara mnamo tarehe 10/3/2011 na kupokelewa. Nilielezea kwa urefu matatizo yanayotukabili Jimbo la Kibaha vijijini, lakini kati ya maeneo ambayo niliyaandikia na kuyaelezea katika barua hiyo kwa Wizara ni Kata ya Magindu. Katika ziara zangu ninazoendelea kuzifanya bado naona matatizo yanazidi kukua hususan ya usalama wa raia na mali zao. Wamekuwa wakiishi kwa mashaka kwa kukosekana gari la Polisi katika Kituo cha Polisi Mlandizi, ambalo lingesaidia sana kufanya doria za kila mara.

Ikumbukuwe kuwa Jimbo la Kibaha vijijini liko katika Wilaya mpya ya Kibaha vijijini ambayo ni Wilaya kubwa na changa ambayo inakuwa kwa kasi kimaendeleo, na ukilinganisha kwa hivi sasa ongezeko la rasilimali watu, limezidi kuwa kubwa. Watu wengi wamekuwa wanakuja kuwekeza Wilayani kwetu. Jimbo la Kibaha vijijini tuna kituo kimoja tu cha Polisi kilichojengwa Mlandizi karibu na barabara ya kwenda Morogoro.

Kituo hiki kinatoa huduma mbalimbali na muhimu kwa wananchi, pamoja na kazi kubwa nzuri waifanyayo askari wa kituo hiki, lakini bado kiutendaji wanakwamishwa na tatizo la kutokuwa na gari la Polisi kutokana na matukio mengi yanayotokea katika njia hii.

Askari hawa wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu bila kuwa na usafiri yaani gari la Polisi kupelekea kufanya shughuli zao katika mazingira magumu. Hivyo tumekuwa tunauhitaji wa gari tena ikiwezekana hata zaidi ya moja ili iwarahisishie Polisi wetu kiutendaji. Baada ya kuiandikia Wizara barua hizo za kuomba Serikali kutupatia gari, hatimaye walinijibu kwa barua kumb. Na CAB 85/127/01/33 mnamo tarehe 03/09/2013, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri (kuwa barua yangu imepokelewa na Waziri na kuthibitisha kuwa ni kweli Kituo cha Polisi Mlandizi hakina gari na kwa kuwa Jeshi la Polisi linatarajia kununua magari mapya, basi Kituo cha Polisi Mlandizi kitapewa kipaumbele mara tu magari hayo yatakapopatikana. Mwisho wa kunukuu).

Sasa naiomba Serikali kuhakikisha katika bajeti hii, basi ahadi ya Serikali inakamilika kwani wananchi wamekuwa wakiishi kwa mashaka sana na mali zao, kwani raia na mali zao

wakiwa katika hali ya mashaka na kutokuwa na usalama wa kutosha, basi wale wote wenye nia mbaya wanaweza kutumia fursa hii mbaya kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Jimbo la Kibaha vijijini limekuwa na tatizo la kutokuwa na Vituo vya Polisi vya kutosha na kufanya mianya ya uhalifu kufanyika na kuwazuru watu wetu, naomba Serikali kutujengea Kituo cha Polisi Kata ya Magindu, kwani kikishakamilika kitakuwa na msaada mkubwa kwa wananchi na kupunguza uhalifu na kuimarisha ulinzi katika Jimbo la Kibaha vijijini, ingawa tuna maeneo mengi hatuna Vituo vya Polisi na hivyo wananchi wamekuwa wanapata shida kwani vitendo vya uvunjifu wa sheria vimekuwa vikifanyika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ruvu haina Kituo cha Polisi kwani Kata hiyo ina wananchi wa kawaida, wakulima, wafugaji na wafanyabiashara. Kata hii inazidi kukua kulingana na maendeleo yanavyokuja kwa kasi katika Wilaya yetu, kwani kuna stesheni kubwa ya Reli ya Kati (*Ruvu junction*) stesheni hii, ndipo mabehewa ya treni za mizigo na abiria zinazokwenda na kutoka Bara zinabadilisha mzigo. Kwa umuhimu wake, ni sehemu ambayo Jeshi la Polisi linaweza kujenga Kituo cha Polisi na nyumba za Askari na hivyo kufanya eneo hilo kuwa la usalama zaidi kuliko ilivyo sasa.

Vile vile tumeanza ujenzi wa awali wa Vituo vya Polisi kupitia mfuko wa Jimbo na ujenzi huo tumeanza katika Kata ya Gwata, Kata ya Magindu na Kata ya Soga, hivyo tunaomba Serikali ituunge mkono kwa kuja kututembelea na zaidi kutusaidia kwa kumalizia vituo hivi, kwani kama nchi tukifanikiwa kuwa na Vituo vya Polisi kila Kata itatusaidia sana kuwa na mazingira ya amani na raia kuwa salama na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa jitihada kubwa katika kukabili changamoto hasa kwa Jeshi la Polisi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu nchini kumekuwa na jitihada za kuinua na kuboresha hali za kiuchumi kwa wananchi wa Tanzania. Tatizo kubwa ni jinsi mamlaka zinaposhindwa kusimamia ipasavyo ulinzi wa ajira dhidi ya wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya kwanza duniani ambayo mamlaka zake zinashindana kutoa vibali kwa wageni bila ya kuzingatia vigezo na masharti ambavyo wageni wanatakiwa kukidhi kabla ya kupewa vibali vya kufanya kazi. Kwa uthibitisho, kwa baadhi ya waajiriwa wageni, hawana taaluma na ujuzi kuwazidi Watanzania ambao wana ujuzi na uzoefu. Taasisi na vyombo husika vimeshindwa kuchukua hatua ya uhakika wa vyeti vya taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la ajabu zaidi ni kwa hivi sasa wageni wengi wanaingia nchini kama watalii na baadaye wanajiingiza katika kushiriki kufanya biashara na hata shughuli za uchuuzi. Hii ni hatari sana kwa ustawi wa jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ichukue hatua za haraka kudhibiti hali hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha kitengo maalum kitakachohusika na utoaji wa vibali kwa wageni ambapo kitengo hiki kinatakiwa kiwe kimehusisha pia Idara ya Uhamiaji, Polisi, Jeshi, Usalama wa Taifa na Idara ya kazi. Kikosi hiki kifanye kazi pia ya uhakiki wa wageni waliopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti hali ya uhamiaji nchini, naishauri Serikali kuanzisha *immigration card* yaani Kadi ya Uhamiaji ambayo itabeba kumbukumbu muhimu kwa wageni wote nchini. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe uanzishaji wa *electronic Visa* kwa ajili ya kukuza utalii nchini.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Mambo ya ndani, Naibu wake na Watendaji wote kwa kukabiliana na changamoto zilizoko Wizarani na zile za Taasisi wanazosimamia. Baada ya utangulizi huo, naomba kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, mwezi Februari, 2012 Ofisi ya *OCD* Tandahimba ilichomwa moto. Mengi yalisemwa, lakini hatimaye iliundwa Tume kuchunguza chanzo na sababu ya kadhia ile. Kwa bahati mbaya sana tangu Tume ile iundwe hadi leo Wanatandahimba hawajapata ripoti na taarifa ya yaliyojiri. Naomba sana Wizara itoe maelekezo kwa yeyote mwenye sifa na wajibu wa kutoa ripoti ya yaliyobainika na Tume yatolewe kwa wananchi kwani maswali ni mengi kwa sisi Viongozi wao wa ngazi ya Wilaya. Aidha, ni vyema ripoti itolewe ili mwisho wa jambo hili ufikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wilaya ya Tandahimba haina Ofisi ya Magereza na Polisi hawana nyumba za watumishi. Napenda kupata maelezo ni kwa namna gani Wizara imejipanga kuondoa shida hizi? Halmashauri ya Wilaya huko nyuma iliwahi kutoa Shilingi milioni 10 kusaidia kulipia fidia ya mkorosho kwa kiwanja cha Ofisi ya *OCD*, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Tafadhali ondoeni kero hizi ili wananchi wapate ustawi na maisha yenye amani na upendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu iko katika zoezi la uandikishwaji wa urai wa Tanzania kwa kupitia *NIDA*. Hivi karibuni zoezi hilo limekamilika huko Zanzibar lakini kwa bahati mbaya zoezi hilo limeacha athari kubwa kwa baadhi ya wananchi kutoandikishwa wakati ni wazaliwa wa Zanzibar, ambayo ni muhimu kwa nchi inayoitwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mkoani iliyoko katika kisiwa cha Pemba Mkoa wa Kusini, ina Majimbo matano ambayo zoezi la uandikishwaji wa uraia wa Tanzania umeshakamilika. Kwa bahati mbaya wako wananchi ambao kwa tabia ile ile ya uandikishaji wa kitambulisho cha Uzanzibar ukaazi wamekoseshwa hali hiyo ya kuandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi waliokoseshwa fursa hiyo ni idadi kama ifuatavyo: Jimbo la Mkoani 527, Jimbo la Chumbani 700, Jimbo la Kiwani 330, Jimbo la Mitambile 870 na Jimbo la Mkanyageni 280. Athari ya kutoandikishwa wananchi hao ambao pia wawezekana hata kitambulisho cha Uzanzibar hawana, wananchi hao wamewekwa njia panda, wao siyo Wazanzibar bali pia siyo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuelewa Waziri atasaidia vipi katika suala hilo ili wananchi hao wapate haki hiyo? Je, Waziri yuko tayari kwa wakati muafaka na wa karibu kufanya ziara huko Pemba katika Wilaya ya Mkoani ili kujionea mwenyewe hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Pemba ina Mikoa miwili; Mkoa wa Kaskazini na Kusini. Pemba Mkoa wa Kusini una Wilaya mbili; Chake chake na Mkoani. Katika Wilaya ya Chake chake tayari Wizara imeshajenga nyumba za Askari Polisi pamoja na Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kusini Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha, kwa muda wote wa Muungano miaka 50 Wilaya ya Mkoani haijajengwa nyumba wala Ofisi inayohusiana na Polisi. Kwa ufupi ni kusema

nyumba na Ofisi za Polisi Wilayani Mkoani, zimejengwa na Wakoloni. Hivi sasa hali ya Polisi Mkoani, Kengeja na Mkandile hali ni mbaya zaidi, Polisi Wilaya ya Mkoani ambapo ndiyo Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya makaazi ya Polisi Mkoani ni mbaya sana. Pia Ofisi ya Polisi Wilaya ya Mkoani iko pia katika hali mbaya. Ni lini Wizara yako itatua kero hiyo?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Waziri, kumekuwa na sera za ubaguzi na mauaji ya kikatili mno ndani ya Wilaya ya Kiteto.

Sera hizo zinasimamiwa na Viongozi wa kuchaguliwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto na hasa baadhi ya Madiwani wanaosaidiana na mchaguliwa wa Jimbo hilo na pia kuungwa mkono na mchaguliwa wa Viti Maalumu katika Ubunge wa eneo hilo, ambaye kwa bahati mbaya sana amepewa wadhifa wa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto. Kwahiyo, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaouawa wengi ni wananchi wa Wilaya ya Kongwa wanaoishi na kulima kwenye Wilaya ya Kiteto. Kwenye mauaji yote ambayo yametokea Viongozi hao wa Kiteto hawajawahi:-

- Kutembelea wafiwa;

- Kutoa salaam za rambirambi kwa jamaa wa wafiwa wala Viongozi wa Kongwa;

- Hawahudhurii mazishi ya waliouawa;

- Hawafiki hata *mortuary* ya Kiteto Kibaya kuona mauaji ya kikatili;

- Hawatembelei majeruhi waliolazwa kwenye hospital ya Wilaya pale Kibaya au Kongwa; na

- Hawatoi "pole" kwa Mbunge wa Kongwa hata tunapokutana nao hapa Bungeni, hawanisalimii.

Mheshimiwa Waziri, mauaji yanayoendelea Kiteto ni ubaguzi wa kikabila na siyo vinginevyo na wanaoua ni watu wanaokodiwa kwa madhumuni ya kuua kwa kutumia sime, mikuki, visu na bunduki za vita, wauaji wakiwa wamevalishwa mavazi ya kifugaji lakini nyuso zao, tabia, mwenendo na matamshi siyo ya wenyeji.

Mheshimiwa Waziri, kuhusu ombi, kwanza, Polisi wachunguze kwa undani nani wafadhili wa mauaji haya? Nani wanaoua wenzao?

Pili, Polisi Kiteto watende haki. Pamoja na maagizo ya kibaguzi wanayopewa na *DC* wa Kiteto kama kukamata wakulima na kuwafunga hadi sasa zaidi ya 60 wamefungwa mwaka mmoja hadi miwili.

TAtu, kipelekwe kikosi kulinda amani. Nne, *DC* Kiteto hana sifa ya kuongoza Wilaya hiyo.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hotuba nzuri, pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara pamoja na watumishi wote kwa kazi nzuri ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara muhimu sana, kwani inasimamia ulinzi na usalama wa raia. Nilipokuwa naipitia bajeti hii ya mwaka 2014/2015 katika Idara ya Jeshi la Polisi sijaona mpango wowote unaolenga moja kwa moja katika uanzishwaji wa Mikoa mipya. Mikoa mipya ukiwemo Mkoa wa Geita tunahitaji kujengewa makazi ya Askari kujengewa Ofisi na kuletewa vitendea kazi, hivyo basi, kwa mchango huu nahitaji kupata maelezo na ufafanuzi juu ya namna Wizara ilivyojipanga juu ya kupeleka huduma muhimu katika Mikoa mipya hasa katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Idara ya Zimamoto na Uokoaji katika Mkoa na Geita tunahitaji vitendea kazi, tunahitaji majengo ya Ofisi na Vituo vya Zimamoto. Vile vile tunahitaji ujenzi wa makazi kwa Askari wetu. Katika Wilaya ya Geita, tuna Gereza la Butundwe linalojishughulisha na kilimo. Gereza hili linakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na vitendea kazi. Hakuna matrekta wala vifaa vya kisasa vya kilimo. Gari lao pia linahitaji matengenezo. Naiomba Serikali iangalie namna ya kuboresha utendaji kazi katika Gereza hili kwa kuleta vitendea kazi muhimu.

Gereza hili pia linakabiliwa na changamoto mbalimbali, kwani hakuna maji, hakuna umeme, hakuna usafiri. Naiomba Serikali ieleze ni lini sasa itapeleka huduma muhimu katika Gereza hili. Sambamba na huduma za kijamii katika hotuba hii, nimeona namna ambavyo Serikali imeanzisha matumizi ya nishati mbadala Magerezani kwa ajili ya kupikia chakula, nishati mbadala *(Biogas)* katika Gereza la Butundwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nahitaji usafiri wa gari na pikipiki katika Vituo vya Katoro, Rwamgasa, Nyarugusu na Bukoli. Vituo vya Polisi hivi, viko katika maeneo ya machimbo ya dhahabu ambako kuna watu wengi sana. Penye watu wengi pia pana mengi. Hivyo vitendea kazi ni muhimu sana, Serikali itufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Askari, naomb Serikali iangalie upya maslahi ya Askari nchini. Ni muda mrefu sana wameishi kwa shida japo wanafanya kazi ngumu na nzuri ya kulinda wananchi na mali zao, ningependa kufahamu ni lini Askari watalipwa posho ya chakula ya Sh. 225,000/= kwa mwezi kwa kila askari? Jambo hili limejadiliwa sana ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wanadai vitu vingi ikiwemo pesa za safari, uhamisho; huwa hazilipwi kwa wakati pamoja na madai ya posho zao mbalimbali. Kwa ujumla, Serikali ione umuhimu wa kuwalipa posho zao zote stahili kwa Askari wote nchini ili wafanye kazi zao kwa moyo na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Askari, mkakati gani unafanywa ili watumishi hawa waishi katika nyumba nzuri zenye staha? Serikali itueleze ina mpango gani kuhakikisha Askari Magereza na Askari Polisi wanajengewa nyumba? Nyumba za bati juu hadi chini na mateso makubwa kipindi cha jua joto kali, kipindi cha baridi ni baridi kali, kwani bati linachemka na kupoa kulingana na hali halisi iliyopo kwa wakati/majira yaliyopo. Mikoa ambayo ina nyumba za Askari, nyumba zimechakaa na ni ndogo sana, zimepitwa na wakati. Wakipata posho yao wakaishi nyumba zenye staha, watafanya kazi nzuri kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi, pamoja na kwamba Askari ni wachache, hawaendani na hali halisi ya wingi wa Raia, hivyo kazi huwaelemea, lakini pia hawana vitendea kazi vya kutosha. Nashauri Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha za

kutosha kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki na maboti kwa maeneo yenye Maziwa kama Kigoma, Mwanza na Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Magereza, Magereza karibu zote nchini zimechakaa sana, lakini pia Magereza yamejaa sana. Idadi ya wafungwa na mahabusu haiendani na hali halisi. Naishauri Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria waangalie jinsi gani wataweza kupunguza mahabusu kwa kusikiliza kesi haraka, lakini pia sheria ya *parole* ifanye kazi kwa zile kesi ndogo ndogo ili kupunguza mlundikano wa mahabusu Gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu faini za makosa ya barabarani, nashauri faini za makosa ya barabarani zilipwe ofisini ili kupunguza uwezekano wa rushwa kuendelea kutolewa barabarani, kwani wanapata fursa ya ku-*bargain*. Nchi nyingine kuna sheria inayolazimisha kila mmiliki wa gari au magari, kukaguliwa kila mwaka. Hali hii inasaidia kwanza kuongeza mapato, lakini pia kuongeza nidhamu ya madereva, kwani atakayekaguliwa akakutwa gari lake bovu sana, hapewi kibali cha kuendelea kulitumia gari hilo ili kuondoa gari chakavu, lakini pia uchafuzi wa mazingira. Pia hapewi kibali cha kuendelea kulitumia gari lake kama ana *notifications* alizoandikiwa kwa makosa mbalimbali barabarani na hakwenda kuzilipa kwa wakati. Hivyo, analipa *fine* zaidi kwa kutokulipa *fine* zake mapema.

Hivyo basi, kila anayekamatwa, taarifa zake ziandikwe sawasawa, apewe *notification* pale anapokosa na kutakiwa kwenda kulipa maeneo/ofisi zitakazopangwa. Ikitokea hakwenda kulipia siku ya ukaguzi wa gari lake asipewe kibali mpaka alipe faini hizo na faini za kuchelewa kulipa. Hii itasaidiakuongeza nidhamu barabarani, tutaondoa magari chakavu lakini tutaongeza mapato. Nashauri tufuate utaratibu huo mzuri. Nchi za Uarabuni mfano Dubai wanatumia mtindo huo.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Waziri na Naibu wake, napenda pia kuipongeza Wizara na Watendaji wake kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kutokana na vurugu za mara kwa mara katika mpaka kati ya Wilaya ya Chemba na Kiteto ambapo watu kadhaa wamepoteza maisha yao, naomba Wizara ipeleke Askari wa kulinda amani katika eneo hilo pamoja na lile la Kiteto na Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda raia na mali zao katika mazingira tofauti na kudumisha amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa Vituo vya Polisi, naipongeza jitihada ya Wizara kwa kuendelea na ukarabati huo, lakini naomba Kituo cha Polisi Dunga Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini – Unguja, kiangaliwe, kwani hivi sasa Kituo hicho kinahatarisha uhai wa Askari, kwani kuta zake zote zimepasuka na wakati wowote zinaweza kuwaangukia. Hivyo ni bora kukinga kuliko kutibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kudumisha amani ni la wananchi wote. Hivyo Jeshi la Polisi liwe tayari kusimamia amani hii na lisikubali kuwaachia watu/vikundi vyenye nia ya kuvunja amani kwa visingizio vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika kwa vijana wanaoajiriwa Jeshi la Polisi kufanyiwa uchunguzi wa kina kabla ya kushiriki kozi (mafunzo) kwani kwa taarifa za hivi karibuni toka vyanzo mbalimbali vya Magazeti, ni kwamba vijana ambao tayari wameshapata mafunzo hufukuzwa katika ajira na sababu ya kufukuzwa kwao ni kughushi vyeti vya kumaliza shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja bajeti hii *with my few observations*/*comments.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni nyeti, kwani ndiyo imebeba usalama na amani ndani ya nchi na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza nchini imekuwa ni tatizo kutokana na mlundikano wa mahabusu/wafungwa. Utaratibu uwekwe ili kuwe na mpango mkakati wa vifungo vya nje ambavyo vitawadhibiti ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya watumishi wa Magereza yamekuwapo tangu enzi za mkoloni, yamechakaa sana, watumishi wanaishi maisha ya kusikitisha sana, hususan Gereza la Ruanda Mbeya, ambalo pia Gereza hili limekuwa likibeba hadi mahabusu/wafungwa toka Chunya, Kyela ambako hakuna Magereza ya uhakika, hivyo kusababisha mlundikano kwenye Gereza hilo na kuwa kero kubwa kwa pande zote mbili wafungwa/mahabusu na Askari Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Polisi kwa Polisi Jamii. Hata hivyo, tukio linapotokea mahali, Jeshi la Polisi huwa linasuasua kufika kwenye eneo la tukio. Kwa hiyo, waongezewe usafiri hata kama ni wa pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa imekithiri sana katika Jeshi la Polisi, kama watunza amani na usalama, tutafika? *Integrity* imepotea kabisa ufanisi haba. Itolewe adhabu kali kwa Polisi wote wanaopokea rushwa ili iwe fundisho kwa wengine. Pia adhabu kali sana itolewe kwa madereva wote wanaosababisha ajali, *seriousness* iwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi inakuwaje Polisi wanajihusisha na uhalifu/ujambazi? Zamani katika watu/watumishi wanaoishi katika mazingira magumu licha ya Askari Magereza ni Jeshi la Polisi ambao wao wapo uraiani, hivyo kufanya hayo matendo ya uhalifu. Licha ya kuwa hili ni kosa kubwa sana kwa Askari, lakini pia maisha ya Askari Polisi ni magumu sana, *yet* wana vishawishi vikubwa. Mnategemea nini? Matokeo yake ndiyo hayo; rushwa, uhalifu na kadhalika. Jeshi la Polisi lipewe/liongezewe *incentives* na uzalendo zaidi, wathaminiwe kuongezewa kipato, *hence* morali ya kazi iwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ikifanya vizuri amani itakuwepo nchini, na haki itatendeka ziko tuhuma nyingi za Polisi kudai rushwa na wakati mwingine kushiriki katika matukio ya wizi, mfano wizi wa Shilingi milioni 150 za Kariakoo. Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua kuwafukuza kazi na nashauri Serikali isiwaonee haya askari kama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo kubwa la ajali kutokea katika barabara zetu hasa nyakati za usiku kwa sababu ya magari mabovu yaliyosimama. Mfano, ajali iliyoua wasanii iliyotokea mwaka 2012 eneo la Mikumi na ajali iliyotokea mwaka 2013 na kuua watu tisa na

kujeruhi wengine, iliyokuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama mwaka 2012, tuliwahi kuishauri Wizara iliondoe tatizo la magari mabovu kusimamishwa barabarani na kusababisha ajali.

Wajumbe wa Kamati tulishauri Wizara iweke mpango Wakuu wa Polisi wa Wilaya, wachukue jukumu la kuondoa magari hayo kila watakapoona gari imeharibika na ni ngumu gari hilo kuondoka usiku huo, na ma-*OCD* waliondoe kwa gharama za mwenye gari (*OCD* akachukua *breakdown* akasogeza gari hilo, gharama zote zilipwe na mwenye gari).

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halikufanyika na bado ajali zinasababishwa na magari mabovu yaliyosimamishwa barabarani. Napenda Serikali itueleze ina mkakati gani katika kuzuia na kuondoa magari mabovu barabarani ili kuzuia ajali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu safari za usiku za mabasi yaendayo Mikoani zirekebishwe, mabasi yasafiri mpaka saa 1.00 jioni au saa 4.00 na siyo mpaka saa 6.00 usiku. Usiku haushoni nguo. Madereva wanachoka, mabasi yaendeyo mbali kama Kigoma, madereva wakifika Dar es Salaam, kesho yake iondoe gari *team* nyingine. Wenye mabasi walazimishwe wawe na *team* mbili, na sio *team* moja kama ilivyo sasa. Haiwezekani dereva aendeshe gari mpaka saa 6.00 usiku, asubuhi saa 12.00 aondoe gari Ubungo (Kituo cha Basi) kupeleka Kigoma.

Naelewa *SUMATRA* wanapanga ratiba, lakini Wizara hii inaweza kutoa mchango mkubwa Idara ya Polisi ina *syndicate* kubwa ya kuleta wahamiaji haramu nchini, kupitia Ofisi zake zilizoko katika Mikoa ya mipakani wako watu (wafanyabiashara) wanafanya biashara hii na wanashirikiana na Polisi. Kila mhamiaji haramu analipa USD 5,000. Nashauri Serikali ifanye uchunguzi, ifanye upelelezi katika Mikoa ya mipakani. Hata wananchi wa kawaida wanawafahamu, yumkini wanafahamu wanakolazwa, wanaowapikia na kadhalika. Uhamiaji wanalalamika kuwa hii ni biashara ya vigogo wa Polisi na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Polisi waliamua tatizo hili liishe; litakwisha. Nashauri Serikali iwatafute wafanyabiashara hao na askari wanaoshirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuepuka ajali za barabarani *Traffic Police* wahakikishe namba za simu za Polisi zinaandikwa katika kioo cha mbele cha basi na namba hizo ziwageukie abiria ziandikwe kwa herufi kubwa na abiria yeyote aweze kuzisoma anapoona uendeshaji wa basi hauridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Okaeni Wilaya ya Moshi Vijijini kiko Kituo cha Polisi kilijengwa na mpaka sasa mkandarasi anadai Shilingi milioni 90. Waziri aliyekuwepo Emmanuel Nchimbi na *IGP* aliyekuwepo waliahidi fedha hiyo ingelipwa na Serikali kuu. Mpaka sasa bado Serikali ina mkakati gani wa kuondoa deni hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Moshi vijijini, Jimbo la Vunjo Kata ya Mwika Kaskazini wananchi walianza kwa nguvu zao kujenga Kituo cha Polisi. Mpaka sasa wamejenga msingi na wameweka kama kipaumbele Sh. 39,970,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo hicho. Je, fedha hizi zimejumuishwa katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani? Kama hapana, ni lini Serikali italiwekea kipaumbele tatizo hili la Kituo cha Polisi cha Mwika Kaskazini Wilaya ya Moshi Vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya karibuni mpaka sasa nchi yetu imeshuhudia matumizi haramu na ya nguvu za kijeshi ambayo hayajawahi kufanywa kwa wananchi tangu nchi hii ipate uhuru wake mwaka 1961. Nguvu hizi za kijeshi zimekuwa zikionyesha kwenye *operations* mbalimbali mfano *Operation Kimbunga* na Tokomeza Majangili. Nia ya *Operation Kimbunga* ilikuwa ni kuwaondoa wahamiaji haramu hasa kutoka Mikoa ya mipakani mfano Kagera na Kigoma inayopakana na Burundi na Rwanda.

*Operation* hii imepelekea kuuawa kwa raia wengi wasio na hatia, watu waliporwa mali, fedha, mifugo na makazi yao kuharibika. Pia watu walidhalilishwa na kuteswa kwa kiwango cha kutisha. Swali la kujiuliza, ni kwa nini *Operation* hii haikufanywa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Rukwa, Mtwara, Mbeya na Ruvuma ambayo inapakana na nchi jirani za *DRC*, Kenya, Malawi, Msumbiji na Zambia ambayo nayo pengine ina wahamiaji haramu? Ni kwanini nguvu kubwa kiasi hicho itumike kwa suala ambalo linahitaji mazungumzo na njia ya kisayansi zaidi? Serikali ni lazima sasa iache uharamia huo wa kutumia nguvu za kijeshi hata pale pasipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya tindikali na uchomaji moto nyumba za ibada, ni kwa nini bado kuna matukio ya uchomaji moto Makanisa na umwagiaji watu tindikali hususan viongozi wa dini zote? Ni kwa nini Serikali haiwakamati wahusika mpaka sasa, kama kweli iko makini na ulinzi wa watu wake? Kama kweli *TISS* inafanya kazi yake sawasawa na haifanyi kazi yake kufuatilia njama ya upinzani kwa kusingizio cha habari za kiitelijensia (ambazo ni uzushi wa kuminya demokrasia kwa Vyama vya Siasa hasa Upinzani) ni kwa nini imeshindwa kuzuia matukio haya kabla ya kutokea Mikutano ya Vyama vya Upinzani? Ni kwanini *TISS* imeshindwa kuwabaini na kuwakamata watu hawa wahalifu ambao wamefikia hatua hata ya kumwagia watalii huko Zanzibar tindikali na kulichafua Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulipuaji wa mabomu kwenye Mikutano ya Vyama vya Siasa, ni muda mrefu sasa, kumekuwa na matukio ya ulipuaji wa mabomu hasa kwenye Mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa vya Upinzani, hususan CHADEMA. Ni kwa nini kumekuwa na matumizi makubwa ya silaha za kivita kwenye Mikutano ya Wapinzani ilhali Mikutano ya CCM huwa inalindwa na kutoingiliwa kwa lolote? Ni kwanini Askari wamekuwa wakilazimishwa kutumia silaha za moto kwenye kusanyiko hata bila sababu za msingi?

Serikali itoe tamko la kuzuia matumizi hayo ya silaha za moto maana matokeo yake ni kupoteza maisha ya watu wasio na hatia hususan watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Askari, ni lini Serikali itachukua hatua mahsusi ya kujenga nyumba za Askari ambao wanaishi kwenye nyumba kama viota vya ndege? Serikali itoe majibu ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya wafungwa Magerezani ni hali ya kutia aibu kwa nchi yenye kujitawala kwa zaidi ya miaka 52 sasa wafungwa wake kukosa hata *uniform* za kuvaa. Ukitembelea Magereza karibu yote katiak nchi yetu, kuna kilio kikubwa cha wafungwa kukosa nguo *(uniform)* za kuvaa kiasi ambacho wafungwa wengine wanashindwa kutoka nje. Hii ni kwa nini?

Hazina ya Serikali itaanza ulazima wa kutoa fedha zinazotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya Magereza zetu ili kuondokana na adha na aibu hii mbaya? Ni kwanini mpaka leo ni 5% tu ya fedha zilizotengwa kwenye kasma hii ndio zimetolewa? Serikali itatoa lini fedha zilizotengwa ili

kufanya kazi iliyokusudiwa? Ni aibu kwa Taifa lenye umri wa miaka 52 kukosa fedha kwa ajili ya watu inaowafunga. Pia kasma ya chakula cha wafungwa haitoshi kabisa, iongezwe ili kunusuru maisha ya wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo jambo la kushangaza kwa wakati huu kuona Jeshi la Polisi kwa maelekezo maalum, kuzuia haki ya msingi ya Mikutano ya Vyama vya Upinzani kwa kisingizio cha sababu za kiintelijensia. Sababu hizi kwa kiasi, hazina uhakika unaoweza kuielezea, wakati Jeshi la Polisi linaweza kuruhusu Mikutano ya CCM leo mahali pale pale, lakini kesho likazuia Mikutano ya upinzani. Hali hii ni kuminya demokrasia ya Vyama vingi na kupendelea CCM.

Wajibu wa Jeshi la Polisi ni kulinda Mikutano ya Vyama vyote na kuzuia uhalifu wowote unaoweza kujitokeza badala ya kuzuia Mikutano ambayo ni haki ya kisheria kwa Vyama vya Siasa. Ni wakati sasa kwa Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria bila upendeleo wowote kwa mtu yeyote na kwa Chama chochote ili kuleta amani na mshikamano wa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la matumizi mabaya ya silaha kwa watu wanaozimiliki kihalali kuzitumia kuwaua ndugu zao, wapenzi au wachumba zao. Mifano iko mingi na Polisi wana ripoti za mauaji haya. Ni kwanini sasa Serikasli isione kwamba kuna umuhimu wa kuanza kupitia upya Sheria ya Umiliki wa Silaha ili kuongoza masharti magumu ya kuwabana wale wote wenye nia ya kumiliki silaha hizi?

Naishauri Serikali kuanza mchakato wa kuwatambua watu wote wanaomiliki silaha na ikiwezekana ianze mchakato mwingine upya wa utoaji silaha ili kunusuru mauaji ya watu wasio na hatia. Itakuwa ni busara pia kuwanyang'anya wale wote wanaomiliki silaha baada ya kuwabaini kuwa hawana mfumo mzuri wa maisha. Hili siyo gumu ukizingatia kwamba Jeshi la Polisi lina njia nyingi za kuwabaini watu wenye historia inayotia shaka. Serikali ijiondoe kabisa na suala la rushwa katika jambo hili nyeti ambalo linaweza kuwa janga kubwa la Taifa miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vurugu na matukio ya kutisha wakati wa kampeni za Uchaguzi, kumekuwa na matukio ya kutisha mpaka ya mauaji katika Mikutano mingi ya kampeni za Uchaguzi miaka ya hivi karibuni. Wananchi wamekuwa wakipigwa, kuteswa, kudhalilishwa na kumwagiwa tindikali katika Mikutano hii ya kampeni ilhali Jeshi la Polisi lipo ili kulinda wananchi. Mfano halisi ni katika kampeni za Uchaguzi za Kalenga ambapo Mheshimiwa Rose Kamili Salum alitekwa na wanachama wanaodaiwa ni wa CCM na kuteswa, kudhalilishwa mbele ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa kwa kosa lisiloeleweka mpaka sasa, kwa sababu yeye ni mwanachama na Mbunge wa CHADEMA. Kama hali imefikia hivi kwa watu ambao ni Viongozi, tena Wabunge, kuteswa na kupingwa; ni kwa vipi demokrasia ya Vyama vingi itastawi?

Je, hali hii siyo kuwatisha wanawake ambao wana nia ya kuingia kwenye siasa ili kuiingia kwenye vyombo vya maamuzi? Kama Jeshi la Polisi halina Chama, ni kwanini linaachia mateso haya kwa wanachama wa Vyama vya Upinzani ilhali lipo kwa ajili ya kulinda amani kwa wananchi wote? Naitaka Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru unyanyasaji na udhalilishaji huu wa wananchi hasa kwenye kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu biashara ya dawa za kulevya kumekuwa na kasi ndogo ya kuwakamata watu wanaomiliki biashara hii ya madawa ya kulevya, lakini wale wanaotumika (pindi) ndio hukamatwa na kubebeshwa mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Mheshimiwa Rais pamoja na wahusika wamekalia majina ya (wauza unga) wamiliki wakubwa wa biashara hii na kuendelea kuwalinda kwa kuwaomba na kuwasihi waachane na biashara hii badala ya kuwachukulia hatua za kisheria? Ni kwanini Serikali haiko *serious k*uhakikisha biashara hii haramu inakomeshwa, wakati watumiaji ambao wengi ni vijana wakiendelea kuangamia na Taifa kupoteza nguvu kazi yake? Kama Serikali haihusiki na biashara hii, ni wakati sasa wa kuwataja kwa majina na kuwachukulia hatua madhubuti ili Taifa liweze kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wa Wizara kwa juhudi wanazofanya ili kuona Wizara hii inatimiza malengo yanayohitajika yapo katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, fedha za ukarabati wa Vituo vya Polisi, kwanini hazipelekwi wakati kila mwaka hutengwa bajeti (fedha) kwa ajili ya ukarabati wa Vituo? Mwaka 2013/2014 Bunge liliidhinisha kiasi cha Sh. 450,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mkokotoni Unguja, hadi leo hii hakijajengwa. Je ni sababu zipi zilizopelekea hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu urasimu juu ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa, ni lini zoezi hili litaanza katika Wilaya hasa kule Pemba? Kwani katika Vituo kulikuwa na usumbufu mkubwa wa kudaiwa vitambulisho aina kwa aina. Tatizo la vyeti vya kuzaliwa ambavyo vingi vimeambiwa ni feki: Je, watengenezaji ni nani hata adhabu iwafikie wananchi wasiokuwa na uwezo wowote katika kutengeneza vyeti? Tunaomba *NIDA* ipunguze vikwazo, kwani hii ni haki ya kila raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukabiliana na uhalifu huu, sasa ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, ni lazima twende na wakati tulionao kwani dunia nzima sasa wanafunga *CCTV Camera* kwa ajili ya kuwatambua wahalifu. Wananchi wanaendelea kudhalilika kwa kuvamiwa ovyo ovyo na Askari wetu wanapata shida sana katika suala hili. Hata barabarani pia tufunge *CCTV Camera.* Tutapunguza muda wa upelelezi, gharama na pia tutapunguza msongamano wa mahabusu kwenye Magereza yetu na ufuatiliaji wa kesi utakuwa wa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubaguzi wa uajiri ndani ya Jeshi la Polisi, uajiri hauko wazi katika Jeshi letu la Polisi na hasa kule Pemba, kwani vijana wenye sifa na wale ambao wametokea JKU wanaachwa na badala yake wanachukuliwa vijana kwa kujuana kupitia Sheha wa Shehia. Mpaka lini tutakwenda na utaratibu huu mbovu usiokuwa na tija? Matokeo ya ubaguzi huu ndiyo yale yaliyotokea kule Moshi, vijana 221 wamerejeshwa kutoka chuo cha Moshi cha Polisi kwa kugundulika kuwa na vyeti feki. Hii imetokana na kuchukuliwa vijana kwa itikadi za Vyama. Hili halitusaidii katika ujenzi wa Taifa letu.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia mambo machache katika Wizara hii ya Mambo ya ndani kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Karatu haina Kituo cha Polisi zaidi ya makazi ambayo yalikuwa Ofisi za Mkuu wa Wilaya zamani, Ofisi za Kata ambayo haina hadhi ya kuwa Kituo cha Polisi. Naomba kuuliza kuwa Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Karatu?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya karatu haina mahabusu kwa wahalifu, wanaosubiri kesi zao. Ni lini sasa Serikali itajenga mahabusu Karatu?

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi hawana makazi, hupangisha Mitaani kitendo ambacho ni kinyume sana na maadili ya kazi zao. Sasa ni lini Serikali itajenga makazi ya Askari Polisi Karatu?

Vile vile nashauri mishahara ya Askari Polisi iboreshwe. Hii itaondoa tamaa mbaya ya askari wetu kuingia katika majaribu ya kupokea rushwa ndogo ndogo hasa Askari wa Barabarani (*traffic*). Suala la uadilifu kwa Askari wetu lidhibitiwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Karatu ina mamlaka yake kamili, ina Mahakama, ina Polisi; cha kushangaza ni pale wananchi wa Karatu wanapodaiwa kuwa wahalifu katika eneo la mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kwa upande wa Karatu na kuwapeleka Loliondo zaidi ya 200 mpaka 300. Haya ni mateso makubwa sana kwa wananchi wa Karatu ilhali Karatu kuna Polisi na Mahakama:

Je, ni lini basi Serikali itawaondolea mahangaiko wananchi wa Karatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza, Mang'ola ina matatizo ya maji safi na salama na nyumba za Askari Magereza ni mbovu sana, nyingine ni za makuti: Je, Serikali itatatua lini matatizo hayo ya Magereza Mang'ola?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni upatikanaji wa miundo mbinu ya Jeshi la Polisi Karatu. Hawana magari ya kutosha na hata wakiwa nalo moja hakuna mafuta. Hili ni tatizo kubwa kwa Polisi Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yao ipate kuongezwa ili waweze kulinda raia na mali zao vizuri.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kuchangia kwa utumwa niliopewa na wananchi wa Jimbo la Rahaleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wanalalamika kwa tatizo la kuwasindikiza waandamanaji ikiwa haramu au halali hali ya kuwa utamaduni umeonyesha kuwa mengi yao hayaishi salama. Wanashangaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu limekuwa kama *story* ya mbwa na mchaichai maana maskani hutiwa moto kwetu, barabara na matairi kwetu, maduka kuvunjwa kwetu na waandamanaji matembezi ya vurugu huanza mbali sana. Hivyo, tunakiomba Kitengo cha intelijensia kiimarishwe kabla matokeo makubwa kutokea. Lakini wakianza shughuli huwa shughuli kweli na tunawapongeza kwa kazi zao, ila kidogo wananchi wanasema huwa wanachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakipongeza kitengo cha *Interstate Security Committee (EA Peace and Security)* kimefanya kazi nzuri ya kupunguza silaha, madawa ya kulevya na hata ushirikiano wa kuondoa ugaidi. Nawapeni pole sana, lakini sisi tulioko jikoni tunaona jitihada zenu na tunawapeni *Big up,* hayaishi lakini tuyapunguze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Maafisa wa Uhamiaji kwa kudhibiti uingiaji holela wa wageni. Tunakubali kuwa mipaka yetu iko *proms'* yaani ina njia za panya nyingi lakini uimara wenu na kushirikiana na wenzenu wa *EAC* tuendelee kuwabaini hawa wahamiaji

haramu. Naomba Kitengo cha *Investigation* kiimarishwe zaidi kwa zana kazi ili waweze kufanya *penetration* wakishirikiana na vitengo vingine vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri ya kutoa *permit* na kutoa wepesi kwa pasi kwa wajasiriamali wadogo na wakati ni jambo ambalo tunazidi kulisisitiza ili watu wetu watumie fursa za mtangamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masheikh, wapo kisheria na sheria hiyo imetungwa na Baraza la Wawakilishi na wanaongozwa na usimamizi wa *GNU* lakini pia wao ndio *Custodian* wa maeneo yetu tunayokaa katika sekta zote; maji, usalama, uhamiaji na uendeshaji kiutawala. Sasa leo kuwalaumu huwa hatuwatendei haki na hasa kama wanafuata sheria kihalali na sehemu ya kuwashtaki ndani ya *GNU*. Nawapa pole, mimi nawaambia tu wachape kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kuwa na jela maalum ya watoto, lakini pia ya akinamama Wajawazito na wanaonyonyesha ili wale watoto nao wasijisikie kuwa nao ni wafungwa au mahabusu na mama zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wa Usalama Barabarani Zanzibar waongezewe *radio call*. Watanganyika wangapi wamo BLW? Wazanzibari wangapi wamo Bungeni? Kauli inanisikitisha na AH! Kaka yangu kwamba hii ni kauli ya Ubaguzi. Naomba tusiendelee na masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiunge mkono hoja. Sasa kama hatujaunga mkono, watapataje pesa? Hivi mwezi wa Julai, tutaendaje?

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kulinda usalama wa watu na mali zao, hali ya usalama nchini imekuwa ni tete sana kiasi cha kuwa wananchi wanaishi kwa wasiwasi mkubwa, vitendo vingi sana vya kihalifu vinatokea mara kwa mara katika jamii zetu. Hivyo basi naishauri Serikali iwaandae askari wetu ili waweze kupambana na changamoto zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niishauri Serikali iangalie maslahi kwa Jeshi letu la Polisi ili waweze kufanya kazi zao kwa utulivu. Bila ya kuangalia maslahi ya askari wetu ipasavyo, basi ni kuwajengea mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ipambane na wale wote wanaoleta uchochezi wa kidini na kikabila katika Taifa letu. Tatizo hili linaonekana linaendelea kwa kasi kubwa sana na kama Serikali haitalikemea, basi litaisambaratisha nchi hii. Jambo hili linaleta chuki na ubaguzi wa kidini, ukabila na rangi. Serikali itafakari upya na kuleta sheria mpya Bungeni ambayo itakataza na kuwawajibisha baadhi ya viongozi ambao watajaribu kujenga chuki na ubaguzi wa kidini na ukabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba, ni vyema mambo haya, Serikali ianze kuyakemea mapema kabla athari zake hazijatumaliza na kuisambaratisha nchi yetu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, janga la UKIMWI limeathiri sana maisha ya wananchi walio wengi. Elimu ya kujikinga na VVU/UKIMWI iongezwe na kurudiwa mara kwa mara katika maeneo ya makazi ya Askari wetu kwani bado wanaishi katika msongamano wa nyumba jambo ambalo ni kivutio na vishawishi vinaweza kutokea kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya askari wa barabarani wanafanya kazi yao wakiwa na msongo wa maisha kutokana na hali ngumu ya kazi kutokana na ukosefu wa vifaa vya kisasa, mishahara ya kuridhisha na makazi ya kisasa. Hasira waliyonayo humalizikia barabarani kwa kuwanyanyasa madereva kwa kuwabambikizia makosa alimradi wajipatie fedha kidogo ili kupata mlo wa siku pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi linalofanywa na askari wa barabarani la kupata makosa sitini (60) kwa mwezi sawa na shilingi milioni moja na laki nane, je, zoezi hili ni halali au ni mradi wa askari wachache? Askari asipoweza kukusanya kiwango hicho cha fedha huwa katika hatari ya kuondolewa barabarani. Hii ni kutokana na utafiti niliofanya nilipokuwa safarini kutoka Dodoma – Dar es Salaam).

Mheshimiwa Naibu Spika, je, askari wa barabarani wamegeuka kuwa *TRA*? Uwekwe utaratibu wa kulipa faini za barabarani kwa *M-PESA* kwani utaratibu uliopo hivi sasa unaweza kuweka mwanya wa makusanyo kutofikishwa yote au kutofikishwa kabisa katika ofisi ya fedha ya Serikali au kule zinakotakiwa kupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tochi nyingi za barabarani hazifanyi kazi, ukishikwa na askari barabarani unaweza kuambiwa unakwenda kasi ya kilomita fulani kwa saa, kwa mfano, kilomita 120 kwa saa, Askari akimaanisha kwamba dereva amezidisha mwendo hasa katika maeneo yenye tahadhari. Dereva anapohisi, madai ya kuzidisha mwendo sio ya kweli na kudai kuiona tochi ya askari ili kujiridhisha na namba iliyopo kwenye tochi, ni masikitiko kwamba tochi nyingi hazifanyi kazi. Askari hudai malipo ya kuzidisha mwendo ili kufikia lengo la kukusanya makosa 60 kwa mwezi. Wizara ifuatilie jambo hilo kwani linaondoa amani na kujenga uadui kati ya watumiaji wa barabara na askari walioko zamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu sana kwa sababu imebeba majukumu yanayoigusa jamii moja kwa moja. Watumishi wa Wizara hii wanayo kazi kubwa sana ya kupambana na wahalifu katika taasisi na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi hawa hawalipwi posho wanazostahili kwa nini? Mfano, stahili yao ni kupata posho ya jumla ya sh. 7,000/= badala yake wanalipwa sh. 5,000. Hii sio kweli tunaomba wapewe stahili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano Magerezani, kumekuwa na ongezeko la wafungwa na hivyo magereza kufurika. Baadhi ya Magereza kutokamilika kujengwa, mfano, Gereza la Mbarali halijakamilika ujenzi wake na hivyo wakubwa na wadogo hurundikwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibiwe ni lini ujenzi wa Gereza la Mbarali utakamilika ili wakubwa na wadogo waweze kutenganishwa. Gereza la Mbarali, halina huduma muhimu kwa maisha, hakuna nyumba za kutosha, maji, umeme na kadhalika. Ulinzi na usalama wa raia unaanza kuingia shaka, matukio ya uharibifu yanaongezeka, hasa kupigwa mabomu Makanisani na mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua hatima ya mwananchi aliyeuawa Mbarali Kata ya Mbaruku kwa kupigwa risasi na askari na hatimaye kufa. Ikumbukwe kuwa watu binafsi ndiyo waliojitolea kuhudumia familia. Kwa nini askari walifanya kosa la jinai, hachukuliwi hatua za kisheria kama inavyofanywa kwa raia, mfano, muuaji na kujeruhi wananchi Kata ya Ubaruku,

taarifa ambayo niliitoa hapa Bungeni nikimtaja mwananchi aliyeuawa na aliyejeruhiwa wakati wananchi wao wanapinga uonevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari Polisi na hasa Wilaya ya Mbarali hazijajengwa hadi sasa pamoja na ahadi ya Serikali kuwa itatenga fedha kwa ajili hiyo. Matumizi mabaya ya askari ambapo baadhi ya taasisi au watu wenye fedha kuwatumia askari katika kuwakandamiza wananchi wasio na hatia na kuwabambikizia makosa ya uongo raia wasio na hatia, nini tamko la Serikali katika kuzuia hali hii.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Kituo cha Polisi Vwawa, Mbozi ambacho ndicho kituo kikubwa cha Polisi, Wilayani Mbozi kipo katika hali mbaya sana ya majengo ya ofisi na nyumba za askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009 niliuliza swali hapa Bungeni nataka kujua ni lini majengo ya kituo hicho yatakarabatiwa au kujengwa upya. Katika majibu yake Wizara ilisema kituo hicho kimejumuishwa katika mpango wa miaka mitano wa Wizara wa kukarabati na kujenga majengo ya Polisi. Hadi sasa miaka mitano imepita, bado Kituo kipo vile vile!

Ni vizuri Wizara ijue kwamba Kituo hicho kilijengwa mwaka 1960, kilikuwa Kambi la kukusanya vibarua wa kwenda mashamba ya mikonge ya Wakoloni! Naomba kujua ni lini sasa kituo hicho kitakarabatiwa au kujengwa upya rejea ahadi ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Gereza la Vwawa sio zuri, pamoja na ukweli kwamba Gereza hili siyo la siku nyingi, lakini majengo yake yapo katika hali mbaya. Nyumba za askari Magereza ziko chache, lakini pia katika hali mbaya. Naomba Wizara ichukue hatua za haraka ili kurekebisha hali hiyo. Aidha, kwa muda mrefu gari la Gereza limekuwa bovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimamoto na kozi ya mashamba, Kikosi cha Zimamoto nchini kimeanza utekelezaji wa sheria inayolitaka Jeshi hilo kutoza kodi ya mashamba na kadhalika. Hata hivyo, sheria hiyo bado haieleweki vizuri kwa wananchi wengi.

Pili, viwango vinavyopaswa kulipwa bado haviko wazi. Tatu, ni wakulima na mashamba ya ukubwa gani wanaotakiwa kulipa kodi hiyo. Nne, kodi hizo zinatozwa bila kutoa vifaa vya zimamoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara itoe elimu ya sheria hiyo kabla utekelezaji wake haujaanza.

(ii) Viwango vinavyopaswa kulipwa viwekwe wazi.

(iii) Ukubwa wa mashamba yanayolipiwa kodi uwe wazi.

(iv) Vifaa vya kuzimia moto vitolewe kwa wakulima watakaolipa kodi hiyo.

(v) Kodi itozwe katika kipindi ambacho wananchi wana pesa. Rejea pia rai ya Waziri Mkuu aliyowahi kuitoa huko nyuma kwamba wananchi walipe fedha za michango mbalimbali wakati wa mavuno/mauzo ya mazao yao. Wananchi wasivamiwe; wapewe notisi ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa wameshindwa kufikia malengo waliyojiwekea kutokana na ufinyu wa bajeti. Mamlaka ina majukumu makubwa ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wote wanapata vitambulisho, lakini Serikali imeshindwa kutoa fedha kwa wakati na kukwamisha shughuli za mamlaka. Ni lini Serikali itatoa fedha kwa mamlaka bila kukwamisha shughuli za mamlaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa kesi husababisha mrundikano wa mahabusu Magerezani, pia harufu ya rushwa. Jeshi la Polisi liweke utaratibu wa kumaliza kesi kwa haraka pale ambapo ushahidi ni dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maaskari wengi hufanya kazi katika hali ngumu, pamoja na hali ngumu ya kulinda usalama wa raia, maisha yao kimaslahi siyo mazuri. Posho zao hazilipwi kwa wakati, nyumba wanazoishi (baadhi yao) ni za kutisha. Wengine hulala chumba kimoja baba, mama na watoto wao wakubwa waliovunja ungo; hii ni aibu na fedheha kwa Jeshi letu. Serikali iwajengee maaskari nyumba za kuishi nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madereva wa bodaboda bado ni tatizo. Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuufuata kwa madereva wa bodaboda nchi nzima, baadhi ya Mikoa madereva wa bodaboda hulazimishwa kulipa ushuru na kadhalika. Hata hivyo, wengi wao hawana mafunzo ya udereva wala leseni, matokeo yake ajali za bodaboda zinatishia maisha ya raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za chakula cha Askari Polisi, Magereza, Zimamoto ni kidogo sana ambapo ni Shilingi elfu tano tu (5000). Napendekeza kiwango hiki kiongezwe hadi Sh. 8,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula cha mfungwa na mahabusu ni kidogo sana hakikidhi haja ya chakula kwa siku kwani wanapata Sh. 500/= kwa chakula kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri kwa Jeshi la Magereza ni tatizo. Magereza mengi hayana magari ya usafiri na mengine yaliyoko ni mabovu, huku mahabusu na wafungwa wanahitaji usafiri. Bajeti ya 2014/2015, Magereza wametengewa fedha za kununua magari nane tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahamiaji haramu wameanza kurudi katika Wilaya za Karagwe na Misenyi, hivyo watendaji wa vijiji katika maeneo haya wanachukua rushwa kuingiza wahamiaji haramu nchini jambo ambalo ni hatari sana. Hivyo naishauri Serikali kuangalia upya namna ya watendaji wa vijiji na vitongoji wanaovuruga sheria na hatua kali ichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NIDA* na *NEC,* waangalie utaratibu wa kununua mashine za kuchukua alama za vidole kwa pamoja kwani kazi inayofanyika ni moja, hivyo kusiwe na *duplication* katika kazi hiyo ili kuokoa fedha kutotumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madeni ya Askari Polisi, Zimamoto, Magereza yamekuwa makubwa, hivyo ni vyema walipwe fedha zao. Madeni ya wazabuni yamekuwa ni makubwa, hivyo naishauri Serikali kulipa fedha za wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Kengeja, Jimbo la Mtambile ni kibovu kinavuja na ni hatari sana kwa maisha ya askari na familia zao, hivyo nashauri Serikali kukarabati Kituo cha Polisi Kengeja – Mtambile. Naomba kuwasilisha.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Chikawe kwa kazi nzuri, yeye binafsi kwa muda huu mfupi ila pia nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi nzuri katika mazingira magumu ya kifedha pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Malemi, Watendaji wote walio chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Afande *IGP* Mangu kwa uteuzi, hakika Rais hakukosea kwani uwezo wake tunaufahamu, na umakini wake haupimiki. Niwapongeze Makamishna Wasaidizi wote akiwemo Mheshimiwa sana Mtweve, Chagonja, Andengenye, Mngullu na kadhalika na Ma- *RPC* wote nawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia katika masuala yafuatayo:-

(1) Pamoja na kwamba nimekwishatoa kilio changu Polisi, naomba nisisitize kuwa naomba sana kadri itakavyowezekana nipatiwe *OCD* angalau mwenye maadili ya Polisi.

(2) Wilaya ya Kilindi tuliahidiwa kujengewa ofisi. Hivi sasa pamoja na kuwa na kiwanja kikubwa na kuahidiwa kujengewa Kituo cha Polisi cha Wilaya, hadi leo hakuna chochote kinachotumika ni *post,* hakika ukifika utashangaa. Karibuni Kilindi naamini mtaona aibu mkifika.

(3) Magari, tuna gari moja chakavu na moja ni zima kiasi, lakini kutokana na ubovu wa barabara magari yote yako juu ya mawe.

(4) Vitambulisho, kama tuko *serious about* ongezeko la mapato mkombozi pekee ni vitambulisho ndiyo suluhu. Wizara inafanya jitihada gani kusaidia hilo. Tunaomba kabla ya Desemba zoezi liwe limekamilika.

(5) Maaskari wanatakiwa kuhamishwa hamishwa kila mara ili kuondoa mazoea katika sehemu moja. Labda pawe na Kamati ya kufanya *monitoring* ili waliokaa zaidi ya *three years* wahamishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru, naomba majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho za Polisi, Polisi nchini wanafanya kazi kubwa na kwa kujitolea, tena katika mazingira magumu. Umuhimu wa Polisi katika usalama na amani ya nchi hii ni jambo lisiloweza kupuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho wanazolipwa maaskari hapa nchini ni ndogo sana ukilinganisha na kazi na majukumu waliyonayo. Ni kwa nini Serikali haitoi kipaumbele kwa posho za maaskari hapa nchini? Ni kwa nini umuhimu wao hauthaminiwi na kutiliwa mkazo? Ni kwa nini wanasiasa wanapata posho nzuri na maslahi mazuri kuliko Mapolisi ambao wanajukumu kubwa hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli na majibu ya Serikali kwa jambo hili la maslahi na posho za Polisi hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Polisi; kuna uhaba na uchakavu wa Vituo vya Polisi hapa nchini na hakuna mkakati na jitihada za dhati za Serikali kuhakikisha kuwa Vituo vya Polisi vinajengwa na kukarabatiwa.

Suala la ujenzi huu wa Vituo vya Polisi na au ukarabati unaweza kufanywa na wadau mbalimbali katika maeneo hayo endapo kutakuwepo na uwazi/ushirikishwaji wa wadau husika. Hii ni kutokana na majibu ya Serikali mara zote kuwa bajeti ni finyu, pale ambapo bajeti haijitoshelezi wadau washirikishwe kwa ukamilifu na hasa kwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni letu sote.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Serikali ituambie vita ya kudhibiti madawa ya kulevya ni waagizaji na wasambazaji wangapi wamekamatwa na fedha kiasi gani zimeingizwa kupitia faini wanazotozwa wahusika wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika Hotuba yake ukurasa wa 15 ameelezea mradi wa ujenzi wa Vituo vya Polisi katika kila Tarafa hapa nchini. Katika mradi huu naomba kujua ni fedha kiasi gani zimepangwa kuboresha majengo ya Polisi katika Ofisi ya *RPC* Mwera katika Mkoa wa Kusini Unguja, vile vile naomba kujua Wizara ina mpango wowote au ina mpango gani wa kujenga majengo ya Polisi katika Kituo cha Mwembemchomeke kilichopo katika Jimbo la Dole. Kituo hiki kimepandishwa hadhi na kuwa Kituo Kikuu cha *Traffic* katika Wilaya ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niombe maelezo ya Serikali kuhusu ajali nyingi zinazosababishwa na madereva wazembe. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuleta Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani ili Bunge lako litunge Sheria kali dhidi ya madereva wazembe. Kwa kufanya hivyo tutaweza kulinda na kunusuru maisha ya Watanzania. Watanzania wengi wamepoteza maisha, wengine wamepata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kujua ni kesi ngapi ziko Mahakamani kule Zanzibar dhidi ya watu waliochoma moto nyumba za Ibada. Serikali ina mpango upi kuwafidia wananchi walioharibiwa nyumba zao za Ibada. Vile vile naomba kujua uchunguzi umefikia hatua gani kuhusu watu waliomwagiwa tindikali, viongozi wa dini na wale waliojeruhiwa kwa risasi. Padri Ambrose Mkenda pia yule aliyempiga risasi na kumuua Padri Evaristus Mushi wa Kanisa la Katoliki Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kujua ni fedha kiasi gani zimetumika kuwatibu wahanga wote wa tindikali huko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kushukuru Wizara hii kwa kuruhusu kisima cha maji cha eneo la Kituo cha Polisi Muheza kuboreshwa na kutumika kwa pamoja; kwa Polisi na wananchi wa Kata ya Genge. Wizara ya Maji (Serikali) imetoa Shilingi 100 milioni na Halmashauri imeweka pampu ya nguvu za sola na maji yamepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naipongeza Serikali kwa kuanzisha ujenzi wa Vituo vya Afya katika maeneo makubwa ya makazi ya Polisi kama pale Kilwa *Road* – Dar es Salaam. Tunaomba mpango huu uendelezwe katika Mikoa na Wilaya zote hata kwa ngazi ya Zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Wizara juu ya ahadi zifuatazo zilizotolewa muda mrefu tangu alipofika Waziri wa Mambo ya Ndani zaidi ya miaka minne iliyopita Mheshimiwa Chiligati.

(i) Ujenzi wa nyumba za Polisi, eneo la Kituo kipya cha Polisi Genge, Muheza. Nyumba za zamani zilikuwa mali ya Shirika la Reli la Afrika Mashariki na baadaye Shirika la Reli Tanzania na ni Magofu makubwa na chakavu. Wilaya mpya zinapata vituo vipya na nyumba mpya ila Wilaya ya zamani ya Muheza kubaki katika magofu.

(ii) Uboreshaji wa Kituo cha Polisi cha Tarafa ya Amani, Muheza. Kituo kipo zaidi ya kilomita 35 kutoka Muheza Mjini, katika maeneo ya Mlima mkubwa wa Amani wenye mashamba makubwa ya chai, miwa, na eneo kubwa la Hifadhi ya msitu na kivutio kikubwa cha utalii. Licha ya Taifa kunufaika na mapato ya amani bado Kituo hakina usafiri wa uhakika pia uhaba wa watendaji. Ahadi za awali za uboreshaji wa kituo hiki zimekuwa hadithi na hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri (sasa amebadilishwa) ya kutembelea Muheza na Kituo hicho cha Amani haikutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji wa mishahara ya Polisi, kumetokea ucheleweshaji wa mara kwa mara wa mishahara ya Polisi wa Muheza. Nini tatizo? Je, ni Wizara ya Fedha au tatizo lipo ndani ya mfumo wa Wizara? Ni vema hili lifanyiwe kazi ya kuliondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Kituo cha Zimamotom Mji wa Muheza ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza, ambapo hakuna Kituo cha Zimamoto. Vitu vinavyosaidia Muheza ni Zimamoto kutoka Jiji la Tanga zaidi ya kilomita 30 au Kituo cha Zimamoto, Korogwe zaidi ya kilomita 35.

Hali hiyo ni ngumu na mbaya sana kwa ajili ya moto unaotokea Muheza kwani magari yanachukua muda mrefu kuwasili Muheza, hivyo kukuta nyumba zimeshateketea. Je, ni lini sasa ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Muheza kitajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vidogo vya mafuta kwa matumizi ya Polisi na *Patrol;* Polisi wanashindwa kufanya *Patrol* kwa ufasaha kutokana na uhaba wa mafuta. Serikali ifanye jitihada kuongeza viwango vya mafuta na kuhakikisha fedha za mafuta zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha Polisi kupambana na mbinu za majambazi wanaojiandaa na pia kuwezesha *Patrol* kufanyika ili kupunguza uwezo na hila za majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kusisitiza kwamba fedha za bajeti zinapatikana kwa wakati.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hotuba ya Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la ulinzi na usalama liko katika Kata mbili za pembezoni mwa Jimbo la Igalula, Tura (upande wa Mashariki) na Loya (upande wa Kaskazini).

Majambazi na waporaji wanafanya uhalifu wa kila aina. Loya sasa tunashirikiana na Waziri wa nchi kujenga Kituo cha Polisi. Tunaomba Wizara pia ichangie ujenzi huu. Pia Tura tuna mpango wa kujenga Kituo cha Polisi pamoja na Goweko (Makao Makuu ya Biashara) Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madeni ya Polisi kwa Raia Wazabuni baadhi, ni muda mrefu sasa hayajalipwa. Mpiga kura wangu Bwana Mukesh anaombwa alipwe madeni yake ya muda mrefu sasa. Simu yake 0784 304047.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nawasilisha.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba pia kumpongeza sana *IGP* ndugu Mangu kwa kuteuliwa kushika Wadhifa huo, naamini kuwa ni mchapakazi na atazidi kuliimarisha Jeshi la Polisi, kulinda kupambana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara iangalie kwa namna ya pekee Wilaya/Mkoa wa Kinondoni kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wakazi, hivyo pia kuwa na uhalifu mkubwa wa aina mbalimbali, Serikali isaidie kwa ukaribu vitendea kazi mbalimbali, yakiwemo magari ya doria, pikipiki na kadhalika ili kukabiliana na ongezeko la uhalifu, ujambazi, wizi, ubakaji, madawa ya kulevya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi liangalie kwa ukaribu sana maeneo ambayo vijana wanayatumia kuvuta Shisha, ziko taarifa kuwa baadhi ya maeneo ya *Restaurant* zinauza shisha, kuna mchanganyiko pia wa matumizi ya bangi na madawa ya kulevya, Polisi iyafanyie uchunguzi wa kina maeneo hayo ambayo yako mengi katika Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza sana *RPC* wa Kinondoni ndugu Wambura kwa ushirikiano na ushupavu wa kupambana na uhalifu Wilayani/Mkoa wa Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada inayofanywa na Jeshi la Uhamiaji kudhibiti wahamiaji haramu kama vile raia wa Ethiopia, lakini bado udhibiti haujafanikiwa. Katika Hoteli moja katikati ya Jiji la Dar es Salaam eneo la Kariakoo wapo Wasomali wageni wengi sana, kila siku wanaingia. Siamini kwamba, uhamiaji hawajui hilo wala hawawaoni Wasomali hao. Inasikitisha sana sana. Naomba wasomali wadhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Jeshi la Zimamoto nchini na hasa mijini unajulikana lakini Serikali hailipatii umuhimu Jeshi hili. Jeshi hili halina vifaa na hasa magari ya zimamoto hayapo na yale yaliyopo ni mabovu. Kuna haja ya kuweka mkakati kati ya Serikali na Halmashauri za Manispaa na Miji ili ununuzi wa magari ya zimamoto ufanyike na uwe endelevu, aidha, tabia ya askari wa zimamoto kwenda katika matukio ya moto bila ya maji linahuzunisha sana. Wanapoulizwa wanasema eti kwanza wanakuja kuangalia hali ya moto, kisha ndio waje wazime moto. Hii ni aibu na fedheha, naomba Jeshi hili lipewe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Polisi nashauri Bajeti inayopitishwa na Bunge iwe inapelekwa ili kuwezesha Jeshi hili kufanya au kutengeneza majukumu yao ipasavyo. Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani makazi yao ni duni, Posho ni ndogo ya dharura, *uniform* zimechakaa na vitendea kazi havitoshi na ni duni. Lakini na Polisi wenyewe nao watakiwe kutunza vifaa hasa magari, pikipiki na kadhalika. Nasisitiza nyumba za Polisi zijengwe ili askari wakae makambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza pia linafanya kazi katika mazingira magumu, Jeshi limeongezewa majukumu, lakini bila ya kuongezewa fedha. Naomba Magereza nao wathaminiwe.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa maoni katika bajeti ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hali duni ya maisha inayowakabili watumishi na wafungwa katika Wizara hii. Wafungwa hupewa chakula cha sh. 500/= tu kwa siku. Mheshimiwa Spika ni wapi duniani mtu anaishi kwa Sh. 500/= kwa siku kwa chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wanalindwa na haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Magereza wafungwa hawana nguo za kuvaa na wengine zimekwisha kabisa hata wanashindwa kutoka nje kufanya kazi wanazotakiwa kufanya wakiwa kifungoni. Lakini je, wafungwa hawawezi kuwekewa utaratibu wa kushona nguo zao wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero kubwa ya vizuizi vya Polisi barabarani ambavyo ni kero kubwa kwa wafanyabiashara ya usafirishaji. Kuna zaidi ya vizuizi 60 kutoka Dar es Salaam – *DRC* na lori moja hutumia takriban mwezi mmoja kumaliza *route* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za *fine* zinazokusanywa na askari wa barabarani zinapelekwa wapi? Ni kiasi gani kimeingizwa kwenye pato la Taifa kutoka fungu hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lilipitishwa sheria ya *road licence* ili ipelekwe *fire* hadi mwaka unakwisha ni kiasi gani cha fedha hii kutoka *TRA* kimepelekwa *fire*? Maana tunajua kuwa hali ya kikosi cha *fire* ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza zaidi, Wizara hii ya Mambo ya Ndani imekuwa na ombi la Shilingi 47.7 ili wanunue magari 777 kwa ajili ya misafara ya viongozi wakuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu kwa nchi iliyo na matatizo lukuki na ya msingi kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa rehema na neema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa katika Polisi, kuna msemo usemao "mtoto hufuata kisogo cha mzazi wake." Kwa mantiki hii ni kuwa rushwa ndani ya Jeshi la Polisi inasababishwa kwa kiasi kikubwa na kufuata wakubwa wao. Kwa kuwa Jeshi la Polisi

limeshindwa kuwachukulia hatua stahiki wala rushwa wakubwa, wabadhirifu wa mali za umma na mafisadi kwa maelekezo ya waliowaweka madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ovu kabisa ndio limesababisha kujengeka "*chain*" ya rushwa katika ngazi mbalimbali za Jeshi la Polisi. *Chain* hii ndio imesababisha pia wale Polisi wa vyeo vya chini waanzishe mfumo wa kuwabambikizia kesi wananchi wanyonge ili kujipatia rushwa ya kujikimu. Ndio maana wanasema kila mtu anakula pale alipo. Kwa sababu hii ndio Polisi ikawa na mfumo wa maonevu dhidi ya jamii. Pamoja na mishahara midogo na marupurupu madogo yanayolipwa, lakini hili la kulindana ndio sababu kubwa zaidi kwani ndani ya Jeshi la Polisi kumejengeka woga kuwa "ukimwaga mboga na mimi nitamwaga ugali."

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa, Serikali ni lazima ilifanyie kazi zoezi hili kwa uadilifu ili kulinda haki za raia wote bila ya ubaguzi wa dini, kabila, rangi, jinsia au kwa itikadi za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dalili za wazi na wasiwasi mkubwa kuwa zoezi hili kule Zanzibar na hasa Pemba linaendeshwa kisiasa. Watu wananyimwa vitambulisho kwa sababu tu ya Masheha kukataa kutoa barua ya utambulisho kwa wananchi wa Shehia yake kwa sababu tu ya itikadi za kisiasa. Hili ni jambo baya na la hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya chakula kwa wafungwa, kuna utaratibu unaofanywa na baadhi ya nchi na sisi ni vyema tukaiga kwani ni wa busara sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwapeleka wafungwa kufanya kazi za kuzalisha mali ili mapato yanayopatikana yasaidie kutumika katika bajeti yao ya chakula. Utaratibu mzuri unaweza kuandaliwa ili badala ya wafungwa kusubiri ruzuku ndogo ya Serikali wazalishe mali katika kilimo au katika sekta ya ujenzi na ufundi, ambazo Jeshi la Magereza lina vitengo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Ugaidi na uchochezi wa kidini, naomba nipewe ufafanuzi au tafsiri iliyo wazi ya neno Ugaidi, kwani matukio ya kihalifu yanayofanana moja huambiwa ni la kigaidi na lingine ni uhalifu wa kawaida tu. Napata wasiwasi sana juu ya matamshi ya msamiati huu. Bila ya Serikali kuweka bayana matumizi ya neno ugaidi kuna wasiwasi mkubwa wa kuzidisha chuki na uhasama katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni ya hatari sana na ni wajibu wa Serikali kuzingatia na kuweka wazi na bayana matumizi ya neno ugaidi hasa katika wakati huu ambao dunia nzima imo katika taharuki ya mizozano ya wenyewe kwa wenyewe au na majirani zao aidha kwa kimaslahi au kwa kiitikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina umuhimu mkubwa wa kuendeleza ustawi wa Taifa, Serikali ina wajibu wa kuwa wazi katika utendaji kazi wa Wizara hii na kuiepusha na kuiingiza katika itikadi za siasa. Ni lazima Wizara hii isiegemee upande wowote ifanye kazi kama Jeshi la Polisi ilivyo nembo yake "Usalama wa Raia na Mali zao" na isiwe balaa ya raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Mawaziri wote na watendaji wa Wizara hii, kwa kuwasilisha bajeti yao ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia uwezo mkubwa wa kumwandaa askari mmoja kulitumikia Taifa zaidi ya miaka 30. Askari wanaandaliwa kwa ajili ya usalama wa raia na ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona Serikali kila mwaka imekuwa ikitenga bajeti ndogo sana kwa ajili ya Wizara hii. Naomba kutoa ushauri kwa Serikali, hebu ijaribu kuangalia unyeti wa Wizara hii ni kutenga bajeti ya kutosha ili kuisaidia Wizara kutatua changamoto nyingi zilizo katika Idara mbalimbali zikiwemo za Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Polisi na uchakavu wa makazi/ofisi. Jeshi hili lina changamoto kubwa sana ya uchakavu wa makazi. Changamoto hii inakuwa ni ya muda mrefu haitatuliki, inasababisha hata askari wengi kuishi uraiani. Tunaomba sasa Serikali itupatie mkakati wa kuhakikisha kuwa makazi ya askari yanaboreshwa katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa Vituo vya Polisi, Mkoa wetu wa Iringa bado unao uhitaji mkubwa sana wa Vituo vya Polisi ambao Serikali bado haijaweza kuleta pesa ya kutosha ili kutatua tatizo hilo. Kutokana na changamoto hiyo kuna baadhi ya vituo vinajengwa na nguvu ya wananchi kama Kituo cha Polisi Ifunda na Isimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru *TANAPA* wamejenga nyumba nzuri sana ya Polisi yenye thamani ya Sh. 72,000,000/= Idodi, lakini bado kituo hakijajengwa pia vituo hivi bado havijakwisha. Serikali itambue ni lini italeta pesa ili kuunga mkono juhudi hiyo ya wananchi ili kutatua changamoto katika hayo maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambaba na hilo hata mimi mwenyewe kwa kuiunga Serikali mkono na kutatua changamoto hiyo nitajenga Kituo cha kisasa cha Polisi chenye thamani ya milioni 40 katika Kata ya Kihesa, kituo hiki kitakapofunguliwa kitasaidia wakazi wa Kata nne, Kata ya Nduli, Kihesa, Mtwivila, Gangilongana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hicho nimekijenga kwa kutumia mkopo kupitia posho hizi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu huu utambulike na baada ya Bunge hili niweze kukabidhi rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Ofisi ya Wilaya ya Kilolo, taasisi karibu zote zimeshajenga ofisi zao katika Makao Makuu ya Wilaya hii isipokuwa Jeshi la Polisi tu. Makao Makuu yapo mbali hivyo kusababisha adha kubwa sana kwa wananchi kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini ofisi hii itajengwa, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, basi anipatie majibu sababu kero hii ni ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazabuni kulidai Jeshi la Polisi ni aibu kubwa sana, chombo kama hiki kudaiwa. Tunaiomba Serikali ituambie mkakati wa kulipa wazabuni hao sababu wametishia mpaka kukatiza huduma katika Jeshi letu, kwa kuwa wao wamechukua mikopo katika mabenki hivyo wanatishiwa kuuziwa dhamana zao na kweli nisipopata jibu nitatoa shilingi katika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto katika kipindi cha miaka minne hawajapatiwa pesa ya maendeleo, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana kwa mfano, hawana ofisi, hawana kabisa nyumba za kuishi, hawana magari ya ofisi, magari ya kuzimia moto hayatoshi na hawana vifaa vya maokozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata vyeo vya Jeshi hili havina mtiririko kuanzia Kamishna *General* mpaka cheo cha chini kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania nzima Makamanda wa Mikoa wanakaimu, sasa sheria inasemaje, watakaimu mpaka lini? Kama hawana sifa watoeni, hawana hata posho za madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mkuu wa Jeshi la Zimamoto, Kamanda Nyambega kwa kutumia juhudi binafsi ya misaada ya magari yanayoletwa mikoani kwetu kama Mkoa wa Iringa, japo uhitaji ni mkubwa sana sababu tuna msitu wa Sao *Hill*, tuna kiwanja cha Ndege cha Nduli, tunahitaji *Crane* kwa ajili ya kukwamulia magari katika Mlima Kitonga.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa ya kutoa maoni yangu juu ya Wizara hii ambayo lengo, dhumuni, nia na dhamira ya kuundwa kwake ni kusimamia usalama wa raia na mali zao, kulinda haki za binadamu, kulinda fursa na uhuru wa kutoa mawazo iwe kwa faragha au hadharani alimradi mtu awe havunji sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Siasa vilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria Namba Tano (Na. 5) ya mwaka 1972, sheria ambayo inatoa fursa kwa Vyama kutoa taarifa katika Jeshi la Polisi na sio kuomba kibali, ni kutoa taarifa, lakini sheria hii hii watawala wanaitumia vibaya kwa kuwashinikiza Polisi kuivunja sheria hiyo kwa visingizio visivyo na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni binadamu tunaelewa kwamba Polisi hawazuii baadhi ya mikutano au maandamano yanayokusudiwa kufanywa na Vyama vya Siasa bali ni mbinu na njama za makusudi zinazofanywa na watawala wa CCM ili sisi tuwaone Jeshi la Polisi kwamba hawavitendei haki Vyama vyetu ili tuwachukie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano hai ni hivi, miezi ya karibuni, vyama vilikoseshwa haki ya kisheria na kikatiba ya kufanya mikutano ya hadhara Lindi na Mtwara kwa kisingizio cha kiusalama, lakini wakati huo huo CCM inafanya mikutano yake nchi nzima popote pale na kuhubiri matakwa yao na hatujaona uvunjifu wowote wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hivi karibuni CCM walifanya mkutano wao katika Wilaya ya Temeke wakihubiri namna wanavyojipanga kutetea mfumo wa Serikali mbili jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Namba 83 ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 inayotaka uwepo wa mfumo wa Serikali tatu. Kama kuna chama ambacho kinahubiri kuwepo kwa uvunjifu wa amani ni CCM lakini msajili wa Vyama vya Siasa amenyamaza kimya kama hayupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha hivi karibuni Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ulitaka kufanya maandamano na Mkutano katika viwanja vya Kibanda Maiti, mjini Zanzibar, taarifa zilipokelewa na Jeshi la Polisi na Polisi waliridhia lakini kwa nia ile ile na dhamira ile ile ya kutaka kutujengea chuki baina ya Jeshi la Polisi na Vyama wakatakiwa waandike barua ya kuzuia maandamano na mkutano kwa kisingizio cha kiusalama wa nchi. Hivyo, niulize baada ya wiki iliyofuata mkutano ulifanyika ni matokeo gani mabaya ya uvunjifu wa amani yaliyoripotiwa kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu, wamekuwa ving'ang'anizi wa madaraka na kwa sababu hiyo hufika mahali tukajiuliza hivyo hawa wenzetu wamelikosea nini Taifa hili mpaka wakawa wagumu wa kukubali mabadiliko? Wanafanya hivi kwa kuhofia nini? Kuna dhambi gani kubwa ambayo wameitenda na wanahisi kwamba hakuna toba ambayo wangeweza kuiomba ikubalike kwa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kazi ngumu na mishahara ya Polisi. Jeshi la Polisi linaingizwa katika makundi na taasisi ambazo zinapokea rushwa kama vile Mahakama kutokana na mishahara midogo ambayo haikidhi hali ya maisha. Jambo hili huchangia Jeshi letu la Polisi kulifanya chombo cha ombaomba na kushusha heshima za kiutendaji katika kutimiza wajibu wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka jana 2013/2014, katika Bunge hili, Jeshi la Polisi lilitengewa kiasi cha Sh. 200,000 kila askari na kwa kila mwezi kama ni *ration allowance*, kiasi ambacho ni kidogo sana, lakini hata hicho kidogo hawapewi wanapewa laki moja tu, hivyo tutegemee kufanya nini askari kutokana na udhalilishwaji huu wanaofanyiwa na Serikali kama sikuvunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, uajiri katika Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, Uhamiaji na takriban sekta zote za ulinzi hawaangalii vigezo bali wanaangalia zaidi huyu ni nani, wazazi wake ni wafuasi wa Chama gani na anatoka wapi. Mfano, mara nyingi nafasi za ajira za Jeshi la Polisi zinapokuja Pemba huchukuliwa vijana kutoka Bara, wakachukulia nafasi hizo za ajira Kisiwani Pemba na kuachwa kwa makusudi vijana wa Pemba katika nafasi za ajira katika jeshi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mauaji yote ya *Albino* yanayofanyika mpaka sasa Serikali haijaunda Tume ya Kuchunguza Mauaji ya *Albino* jambo ambao ni kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Matangatwani, Pemba, Wilaya ya Micheweni, ni kituo ambacho hakina umeme wakati umeme upo karibu hauwafikii. Hawana choo wanajisaidia porini, hivyo ni kwa nini wanadhalilishwa kiasi hicho. Hivyo, askari hawa wa kituo cha Matangatwani wamekosa nini mpaka waachwe katika hali hiyo.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafedheheka sana kila ninapoona wananchi wanachukua sheria mkononi ambapo watuhumiwa wakati mwingine hupoteza maisha au kupata ulemavu au majeraha makubwa na hakuna hatua zinazochukuliwa baada ya tamko la Kamanda wa Polisi kusema "wananchi wenye hasira kali", ni dhahiri Polisi wameshindwa kusimamia ipasavyo kukomesha hali hii na kujenga tabia ya watu kuheshimu sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyakati matukio yanarekodiwa na vyombo vya habari na kuonesha jinsi wananchi wanavyotekeleza hasira zao, lakini Polisi hawachukui hatua ya kuwahoji na kuwafikisha katika vyombo vya sheria hao wenye hasira kali ili sheria ichukue mkondo wake na waadhibiwe kwa kiwango cha makosa yao ili watu waheshimu utawala wa sheria. Polisi wakiamua kusimamia jambo hili wanaweza, naamini hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuamini aliyoyasema Hayati Baba wa Taifa kwamba watabinafsisha hata Magereza kwa mwelekeo na mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ukurasa 39, matarajio ya kuingia ubia na sekta binafsi ni hatua ya awali ya kubinafsisha Magereza. Niitake Serikali kwa ujumla wake kuangalia eneo hili na kuwekeza mtaji wa nyenzo kwa Magereza badala ya kutegemea mtaji kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara imekata tamaa kuendeleza Magereza ya kilimo likiwemo la Kalilaukukulu, Mkoani Katavi, hivyo basi Gereza liwe tayari kuwarudishia wananchi wa Kijiji cha Kawanzige ardhi yao ambayo Magereza iliihodhi na haiendelezwi, ni vema kuwapatia wakulima wadogo wadogo maeneo kuliko kufikiria kuingia ubia na mtu

mmoja mmoja. Kwa kufanya hivyo, wananchi wengi watapata maeneo kwa ajili ya kilimo kwa ustawi na maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa mipya ambayo ina changamoto nyingi ikiwemo makazi ya askari, ofisi na vitendea kazi ni matarajio yangu, Wizara itatoa kipaumbele maalum katika mikoa hii pamoja na kuwa na ikama stahiki ya askari. Pia kwa unyenyekevu mkubwa Wizara itupatie gari ya zimamoto katika Uwanja mpya wa Ndege Mpanda ili huduma za usafiri wa kibiashara uweze kuanza mapema iwezekanavyo, kikwazo ni gari ya zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali barabarani ambazo Watanzania wengi wamepoteza maisha ni mali, ningependa kupata maelezo juu ya ubora na usalama kwa mabodi ya mabasi ya abiria, inaelekea mabodi ya mabasi hayazingatii usalama kwa abiria, pia yapo matumizi mabaya ya taa kali (*spot light*) katika magari, hizi ni taa za ziada katika gari lakini matumizi mabaya ya taa hizi ni kisababishi cha ajali na kwa kuwa taa hizi ni za ziada na zinatumika vibaya tufikie maamuzi ya kuziondosha kutumika, nchi nyingi wamefanya. Hivyo, ni matumaini yangu utaangalia ipasavyo juu ya ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakimbizi; tunahitaji kujua hatima ya wakimbizi wa Burundi katika yaliyokuwa makazi ya Katumbo na Mishamo ambao ilikuwa ifikie tamati miaka kadhaa iliyopita. Nini mpango mkakati wa kuwaondosha na nimesikitishwa sana Serikali sasa ndio inafikiria suala la kuchukua picha na alama za vidole wakati wakimbizi hawa wamezagaa nchi nzima hasa katika miji mikubwa. "Tunakumbuka shuka wakati tayari kumekucha" Naomba kuhakikishiwa ni namna gani zoezi hili litakavyofanikiwa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu katika Wizara hii kwa kuongelea hali ya Kituo cha Polisi Wilaya ya Biharamulo. Kituo hiki kipo katika hali mbaya sana. Jengo dogo kuanzia paa hadi sakafu lipo hoi kiasi cha kukatisha tamaa ya kulitumia kufanyia kazi. Si kwa Askari tu bali hata raia wanaokwenda pale kutoa kero zao au kujibu mashtaka yao, hakika wana kosa amani ya kupata haki yao au kutendewa haki, mvua ikinyesha inakuwa balaa kubwa. Tafadhali sana Serikali ifanye utaratibu wa kujenga kituo kipya na cha kisasa. Jambo la kukatisha tamaa ni kwamba kituo hakina hata choo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kina uhaba mkubwa sana wa nyumba za watumishi. Leo Polisi wengi wanapanga mitaani kwetu na huko mitaani ndiko kuliko na mengi, wahalifu wapo mitaani na raia wema wachache nao pia wapo huko. Leo hii tunawalaumu kuwa wanapokea rushwa lakini ni kutokana na kuwaweka Maaskari hawa wema na raia wabaya ambao lazima watapenyeza ushawishi ili wapokee rushwa na kuhalalisha uhalifu. Haiwezekani upate mshahara kidogo, maisha magumu wakati umepanga kwenye nyumba ya tajiri anayejihusisha na magendo na kesho hiyo aweze kumdhibiti mhalifu huyo. Polisi hana uhakika wa mlo wake wakati nyumba jirani kuna mziki na nyama choma, atakuwa mvumilivu kiasi gani? Niombe Serikali iwajengee nyumba na kuboresha hadhi ya Kituo cha Polisi Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la vijana hawa kunyimwa fursa za kujiendeleza. Ikumbukwe kuwa kujiendeleza sehemu ya kazi ni haki ya msingi ya mwajiriwa na ni jukumu la mwajiri kumsaidia na kumwendeleza mwajiriwa. Kuna Askari wanaomba kubadilisha vitengo ndani ya idara lakini suala hili linazusha mgogoro mkubwa kwa wakubwa wao kazini. Leo hii kama Askari Polisi akitaka ajira yake iingie ukakasi basi aombe kubadili kitengo kwenda masomoni. Ili kutekeleza suala la utawala bora ni vema masuala haya yakapewa kipaumbele, watendeeni haki Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usafiri kwa Vituo vya Polisi ni tatizo kubwa sana. Kila mara utakuta kituo kikubwa cha Polisi cha Wilaya kina gari moja, gari hilo alitumie *OCD* au wasaidizi wake au ndio liende doria na kama haitoshi kwenda kwenye matukio mbalimbali. Niombe Serikali iangalie suala la usafiri kwenye vituo hivi na hususani Wilaya ya Biharamulo ambako suala la ujambazi, ujangili, unyang'anyi limejitokeza sana. Pori la Akiba la Burigi na Kimisi limekuwa likitumiwa na majambazi hawa kuwadhuru watu. Hivyo, inahitajika nguvu ya Jeshi, mafuta ya kufanya doria yanahitajika na magari pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali ifanyie kazi hoja hizi za msingi. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja naomba yafuatayo yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi bado wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, mishahara haitoshi, posho ndogo, kazi ngumu zenye hatari, makazi yao ni duni hasa Wilaya ya Nkasi. Naitaka Serikali kutoa majibu kuwa mambo haya yataboreshwa lini kama kila siku bajeti inayoletwa haitoshi namna hii, ni chanzo cha Polisi kuomba/kupokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ofisi za Polisi (vituo vya Polisi), wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini wamejitolea kujenga vituo vya Polisi maeneo kadhaa vikiwepo vile vya vijiji vya Kate na Mpasa. Nawapongeza wananchi, naomba Serikali iwasaidie ukamilishaji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto lina jukumu la kukusanya maduhuli ya Serikali ni vema lakini katika Wilaya ya Nkasi wananchi wanalalamika kuwa kwa nini hakuna Kituo cha Zimamoto ili kuwafanya waridhike na yanayotolewa na Jeshi hili. Nataka maelezo ni lini Kituo cha Zimamoto kitaanza Namanyere Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa na Jeshi la Polisi. Kutokana na umuhimu wa Jeshi hili na kutokana na changamoto zinazolikabili, nashauri utafiti/*research* ifanywe ili rushwa itoweke kabisa katika Jeshi hili muhimu. Naamini kama Askari watathaminiwa na kulipwa vizuri, wakipewa marupurupu mazuri, wakitambuliwa na jamii umuhimu wao, wakionekana kama ni sehemmu ya jamii yetu, naamini rushwa ingekwisha. *Study* ifanyike duniani kote kuona lipi lifanyike waache kupokea rushwa na inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ya Kitete, Wilayani Nkasi. Magereza haya yana matatizo makubwa. Licha ya kuwa katika eneo zuri kwa kilimo bado hawana makazi bora ya Askari, gereza pia sio la kisasa nadhani ni la muda tu. Naiomba Serikali iboreshe hali ya Magereza ya Kitete. Magereza haya hayana zahanati nzuri ndiyo wako kwenye ujenzi kwa kujitolea na mimi kama Mbunge niliweza kuwachangia Tshs. 2,000,000/= kupitia Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo katika Magereza haya. Kutokana na ardhi hii kuwa nzuri, kilimo kinakubali sana, naomba waboreshewe kwa kupewa trekta zuri kupitia SUMA JKT. Wana uwezo wa kulipa, ni suala la kuwapa zana na wanaanza kuzalisha mwaka mmoja au miwili tu wataweza kulipa deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji ya albino. Polisi komesheni jambo hili. Hili jambo linatakiwa likomeshwe kwa gharama yoyote kwani ni kinyume na utu. Mimi nina mtoto anaitwa Judith Mipata, ni albino, natambua sana namna familia zenye albino wanavyoishi kwa shida kubwa duniani, nani wa kusaidia, ni sisi Bunge, ni ninyi Serikali, ni Wizara hii na mtuambie leo

mauaji haya yatakwisha lini? Tafadhali naomba komesheni mauaji ya albino, tunapata shida hawa ni binadamu.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia hotuba hii kwa kutoiunga mkono hadi hapo Serikali itakapotoa ufafanuzi wa kuridhisha kuhusu hoja zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni Kituo cha Polisi Kibiti ambacho kwa muda mrefu kimetelekezwa na Serikali. Kituo hiki ambacho kipo kwenye *road reserve*, hakijafanyiwa marekebisho na paa lake lote linavuja. Askari wa kituo hiki wakati mvua inanyesha husimama wima na wengine hukimbilia maeneo ya nyumba za jirani ili kujisitiri wasilowe. Aidha, kituo hiki kwa kuwa kipo kwenye *road reserve* Serikali inakataa kukifanyia marekebisho/ukarabati kwa madai kwamba ni la muda tu wapo mbioni kujenga jengo lingine na la kudumu. Ni lini hili jengo lingine na la kudumu litajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Kibiti wana mahusiano mazuri na Askari Polisi na Wizara ya Mambo ya Ndani, mwananchi mmoja ametoa ekari mbili ili kujenga kituo hicho kipya. Naoimba Serikali ikae na iangalie uwezekano wa kujenga kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo hiki ndicho kinachohudumia Jimbo zima la Kibiti lakini hakina gari la kufuatilia pindi matatizo au uhalifu unapotokea. Naiomba Serikali iweze kuangalia kwa makini suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Gereza la Kilimo Kibiti. Naishukuru Serikali kwa kujenga jengo la kukaa/kulala wafungwa la kisasa. Pamoja na ujenzi huo lakini nyumba za Maafisa wa Gereza hilo ni chakavu na ni za udongo. Pamoja na uchakavu, nyumba hizo pia hata jengo la utawala nalo limepasuka na wakati wowote litadondoka. Naiomba Serikali iende ikaone gereza hilo na watafakari kwa kina namna ya kuliboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, gereza la Kibiti ni la Kilimo. Gereza hili lina eneo kubwa sana la kilimo na ardhi yake ni nzuri. Miaka ya nyuma gereza hili lilikuwa linazalisha chakula ambacho kilikuwa kinatosheleza si Gereza pekee bali pia hata kwa maeneo mengine ya Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati gereza hili kipindi hicho lilikuwa na trekta ambalo kwa kiasi kikubwa lilichangia kupata mazao ya ziada kwa sasa gereza hili halina trekta na maendeleo yake yamerudi nyuma sana. Kilio kikubwa cha Mkuu wa Gereza na *staff* wake pamoja na wafungwa wake ni kukopeshwa trekta. Wao wapo tayari kukopeshwa trekta ili liwasaidie katika kuimarisha kilimo gerezani hapo. Naiomba Serikali ilifikirie kwa makini suala hili ili wakopeshwe trekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa upo mchakato wa kupeleka umeme kata ya Dimani kupitia *REA*. Naiomba Serikali nayo iingilie kati ili umeme huo pia upelekwe kwenye gereza hilo. Toka mahali ambapo umeme utapita ni kilomita tatu tu kufika gerezani Kibiti. Ni vizuri Wizara ikaanza sasa mazungumzo na *REA* ili wahakikishe kuwa mradi huo ukianza basi ujumuishe gereza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu nategemea kupata majibu mazuri ya kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wa Wizara hii kwa kuwapatia *facilities* waweze na wao kujiona ni watumishi wa Wizara hii kinyume chake siungi mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufumbuzi juu ya hoja ya msingi ifutayo:-

Wilaya ya Kisarawe haina Kituo cha Polisi kinachoeleweka kwani hadi *OCD* hana ofisi, ofisi ya *OCD* ameazima kichumba katika ofisi ya Mtandao wa Vijana Kisarawe (KIYODEW). Je, kwa nini Serikali haijengi Kituo cha Polisi Kisarawe? Jengo bovu linalotumika kwa sasa lisilo rasmi kiasi hata nyaraka hazina pa kukaa. Ni lini ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wanalalamika sana kwa kutolipwa haki zao za uhamisho na madai mengine. Kwa nini Serikali isiwalipe Askari Polisi madai yao ya uhamisho na madai ya posho mbalimbali ili kuwasaidia Askari wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapatiwa ufumbuzi wa maeneo haya mawili. Kama sitapata ufumbuzi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Kisarawe nakusudia kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya Polisi yanachukua muda mrefu sana. Baadhi yao wanapostaafu na kurudi uraiani wanakuwa wanalipwa 50 kwa mwezi hiyo pesa inakuwa haikidhi mahitaji yao. Vilevile 50 inachukua muda mrefu mpaka walipwe, ukiangalia askari huyo anaishi kwenye mazingira magumu, baadhi wanaishi kwenye nyumba za kupanga, bado hawajasomesha watoto na kadhalika, ni lini Serikali italipa mafao ya Askari kwa wakati muafaka na kuwaongeza posho ya kustaafu ukilinganisha na maisha yalivyopanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi ya Askari, hili ni tatizo sugu kwa Maaskari kwani wanaishi katika nyumba zilizochakaa (chakavu) hili ni tatizo la Askari wote wa Tanzania kwani Askari hawa wanaishi katika mazingira magumu, vyumba vyao ni vidogo, vilevile baadhi ya Askari hawa wanakuwa wana familia kubwa. Ni lini Serikali kupitia Shirika la *NSSF* itawajengea nyumba bora za makazi Askari wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itahakikisha inatoa posho za Askari kwa kiwango ambacho kinaendana na maisha tuliyokuwa nayo ili Askari hawa waache kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa, ulinzi, kuvunja haki za binadamu na vitendo ambavyo haviendani na maadili ya askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *traffic*, ukusanyaji wa mapato barabarani umegubikwa na rushwa kubwa sana. Kuna baadhi ya *traffic* wanachukua rushwa na kuyaruhusu magari hata kama mabovu na kusababisha ajali barabarani. *Traffic* hawa wanapenda kuwakamata raia hata kama hawana hatia ili mradi wapate rushwa kupitia raia hawa. Naiomba Serikali iangalie kwa umakini hili suala la *traffic* kwani limekuwa likileta usumbufu sana hasa kwa wananchi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamiaji haramu, mipaka yetu ya Tanzania haiko salama kwani hili tatizo ni la kila siku na wahamiaji haramu ni wengi sana hasa kwenye hoteli za kitalii. Baadhi yao wanachukua kazi za Watanzania (ajira), wahamiaji hawa wameshatujua udhaifu wetu. Ni lini Idara ya Uhamiaji watafanya makao kwenye hoteli za kitalii na kuwakamata wahamiaji haramu (wageni) ambao wameingia nchini kinyume cha sheria?

Kwa mfano, nchi ya Malaysia haitoi ajira kwa wageni, inawapa kipaumbele wananchi wake. Ni vizuri tukaiga mfano wa nchi za wenzetu kwa kufanya msako mara kwa mara wa kukamata wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la magereza (wafungwa). Kuna baadhi ya wafungwa wananyanyaswa, wanaishi katika mazingira magumu, wanakosa haki za binadamu, watoto waliofungwa wanachanganywa na watu wazima, kufanya *sex* ya jinsia moja.

Naomba kuuliza wafungwa huwa wanalima vile vyakula wanavyolima vinaenda wapi? Ni kwa nini wanakula mlo ambao hauridhishi? Mbona nchi za wenzetu wanawathamini wafungwa wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanandoa wafungwa ni kwa nini wasijengewe sehemu ya faragha waweze kukutana na wanandoa wenzao kama China? Hii itapunguza maradhi ya zinaa, mapenzi ya jinsia moja ndani ya magereza na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watoto walioko jela wajengewe sehemu zao maalum kama nchi za wenzetu, hii itapunguza watoto kuharibika kimaadili/kisaikolojia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya wafungwa wamekuwa wanasoma ndani ya magereza, wengine wanasoma mpaka digrii ya sharia. Napenda kujua ni wafungwa wangapi waliomaliza kifungu chao na wakapatiwa ajira Serikalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba magereza yakarabatiwe pamoja na vituo vya Polisi na Serikali iongeze bajeti ya kutosha katika Wizara hii.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, posho za Polisi, jambo hili limekuwa kero kwa Askari na sisi tunaoishi mitaani tumesikia/tunasikia kero hii. Hii ni kero namba moja kwa Askari wa Jeshi la Polisi. Wanafunzi wasio na familia wanalipwa Tsh.7,000 wakati Polisi wanalipwa Tsh.5,000. Kiwango hiki hakitoshi, naomba maelezo lini watapandishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hawapandishwi vyeo na wakipandishwa hawalipwi fedha kulingana na cheo. Askari wengine wanakaa hadi miaka 6 hadi 7 bila *increment*. Nashauri walipwe mapema ili kuongeza morali ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Polisi Ileje. Nyumba ziko tatu zilijengwa enzi za miaka ya 1980, zimechakaa sana, hazina *ceiling board*, popo wanazaliana ndani ya majengo haya. Nyumba hizi ni kero kubwa kwa Askari. Ni lini Askari hawa watapatiwa makazi ili waishi kama binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pensheni, nashauri sheria irekebishwe haraka ili pindi Askari anapoingizwa katika *payroll* aanze kukatwa na kutunziwa *pension* yake katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kidogo cha Polisi Isoko. Aliyekuwa *IGP* wa Polisi aliyemaliza muda wake Said Mwema, mwaka jana aliniahidi kwamba kituo hiki kitajengwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Naomba juhudi zifanyike ili kuwaondolea adha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Magereza Itumba – Ileje. Nyumba zote zimebomoka hazifai kwa maisha ya binadamu. Naomba kupatiwa maelezo.

**MHE. MADGALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya vituo vya Polisi kwenye Wilaya karibu zote hapa nchini ni mbaya. Hakuna vifaa na vitendea kazi kwa Polisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Mtuhumiwa anatakiwa anunue karatasi ili Askari watumie kuandika tuhuma. Hakuna viti vya kukalia, Askari wale wanafanya kazi wamesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi cha Wilaya Mpya ya Kaliua hakina hadhi ya Wilaya, hakuna ofisi za Askari kufanya kazi, kachumba kadogo sana, kinatumiwa kwa

kupokezana *OCD, OC-CID*. Hakuna samani mfano meza, viti, makabati na makaratasi kwa matumizi ya ofisi. Kituo hakina nyumba zaA hata moja hata Mkuu kituo analazimika kufanyia kazi kwenye nyumba ya wageni *(guest house)*.

Serikali ina mpango gani kwa kituo hiki kinachohudumia zaidi ya kata 19 na ni maeneo ya mpakani mwa nchi ambapo kuna uhalifu mkubwa sana kiwe na hadhi ya kituo cha Wilaya kwa kukipatia fedha za kupanua kituo na kujenga nyumba za watumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza lina malalamiko mengi sana kuhusu stahili zao. Askari Magereza wanacheleweshewa posho zao kwa muda mrefu sana na hali ya maisha ni ngumu. Wenzao Polisi wanaweza kulipwa posho zao tarehe 15 ya mwezi husika wakati Magereza wanapata tarehe 7 mpaka 10 ya mwezi unaofuata. Serikali itoe ufafanuzi ni kwa nini hawa Magereza wanacheleweshewa posho zao tofauti na Polisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, posho ya Sh.5000 kwa siku kwa Askari wetu ni dhambi kwa Mungu kazi wanayofanya ni kubwa sana na haitoshi katika maazingira magumu sana. Posho iongezwe ifike angalau Sh.10,000/= kwa siku. Sahani ya chakula ni Sh.5,000 na hapo hujanywa chai. Serikali inajua gharama za maisha iwatendee haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Magereza wanayo malalamiko yao ya likizo na nauli za kuwalipia kwenda likizo wao na familia zao kwa miaka zaidi ya mitatu. Askari anaambiwa ajilipie usafiri kwenda na kurudi atarejeshewa matokeo yake hawalipwi. Huku ni kuwaonea, Serikali itenge fedha za kutosha kulipa malimbikizo ya Askari, tusiwavunje moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa na mahabusu ni binadamu kama wale walioko uraiani. Kitendo cha Serikali kutenga Tshs. 500/= kwa mfungwa kwa siku ni kuwatesa, mlo mmoja kwa siku haukubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani hazitoweza kupungua nchini kama Serikali haitatafuta mikakati ya kuondoa rushwa katika Jeshi la Polisi wakiwepo Askari wa usalama barabarani *(traffic)*. *Traffic* wanakusanya fedha barabarani bila aibu. Hata kama ni kiongozi akikusimamisha anakuomba hela kweupe, hili ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha polisi kipya cha Kona Nne, Kata ya Sasu, Tarafa ya Ulyankuru Kaliua kilipokelewa kwa furaha sana na wananchi walishiriki kukijenga tena kwa kujitolea kwa hali na mali. Hata hivyo, Askari wa kituo hiki wanawatesa sana wananchi, wanawabambikia kesi, wanachukua rushwa kwa kutetea wahalifu. Serikali ichunguze Askari wote wa kituo hiki na kuwapa adhabu kwa dhuluma wanazowafanyia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora haswa Wilaya ya Kaliua na Urambo, matukio ya uhalifu yanaongezeka sana kutokana na kuwepo kwa silaha nyingi zinazouzwa kama njugu mpakani. Tarehe 5/4/2014, Askari Magereza Coplo Liberatus No.B.2590 amekamata silaha imebebwa kwenye pikipiki, silaha aina ya bastola na simu za mikononi 39, zilikuwa zimewekwa kwenye begi, silaha hizo zimekabidhiwa kwa *OCD* Urambo kwa uchunguzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imuangalie Askari huyu aliyepambana na jambazi na kufanikiwa kunyang'anya bastola pamoja na simu 39 za wizi kwenye begi. Askari huyu atendewe haki na uchunguzi ukikamilika atangazwe wazi kwenye vyombo vya habari ili wengine waige mfano wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora uangaliwe kwa kipekee kudhibiti uhalifu unaoendelea kutokea kila leo hivyo kujenga hofu kubwa na kuhatarisha maisha ya watu.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu kwa hoja zifuatazo:-

(i) Kumekuwa na tatizo la mahabusu Meatu kutokana na ukweli kwamba Gereza la Meatu limekamilika lakini bado uzio tu kwa thamani ya takribani milioni 100. Matokeo yake mahabusu wote hupelekwa gereza la Maswa umbali wa 90km na kuliongezea Jeshi la Polisi gharama ya kuleta mahabusu Mahakamani.

Je, ni lini sasa gereza hili uzio wake utakamilika? Niko tayari kuchangia shilingi milioni 30 toka Mfuko wa Jimbo kama Serikali itaamua kutoa fedha.

(ii) Askari walipanda vyeo tangu mwaka 2010 ni lini wataanza kulipwa stahili zao kwa mujibu wa *PGO*?

(iii) Kuna magari matatu yaliyotolewa na kampuni ya uwekezaji ya Meatu mwaka 2012. Kampuni ilitoa magari matatu, magari mawili yapo lakini moja tulinyang'anywa na Mkoa, tunataka gari letu haraka ili tulitumie.

(iv) Bajeti ya kutengeneza magari ya Jeshi la Polisi Meatu tunapata Shs.98,000/= kwa magari matatu ambazo hazitoshi. Tunaomba bajeti hii iongeze fedha.

(v) Kuna Askari wanaotumwa kwenda operesheni maeneo mengine nje ya vituo vyao vya kazi. Wakimaliza kazi na kurudi madai yao huandikwa kwa jina la *OCD* lakini fedha hizi huwa hawapati. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa madai haya yawe yanakuja na majina ya Askari husika na siyo kwa jina la *OCD*?

(vi) Naomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI kuwapatia Askari (W) mafuta angalau lita 1000 kwa mwezi badala ya kiwango cha sasa cha lita 500.

(vii) Hakuna *sentry box* nyumbani kwa *DC* Meatu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni ufinyu wa bajeti. Bajeti ni ndogo, naishauri Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ikiwemo kulipa madeni ya wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni maslahi ya watumishi yaani Askari Polisi, Magereza na Uhamiaji, posho zao ni ndogo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza *ration* (fedha ya chakula) kutoka Sh.5,000 kwa siku hadi Sh.10,000/=?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Askari wanaofanya kazi katika mazingira magumu, wako katika mazingira hatarishi mfano Tarime, Kagera na kadhalika. Ni lini watapewa posho ya mazingira magumu na fedha za vocha kwa ajili ya mawasiliano?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni nyumba za wafanyakazi. Wafanyakazi hawa hawana nyumba za kuishi, je, ni lini watapatiwa nyumba Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto kwani zilizopo zimechakaa na wengine hawana. Pia nyumba za Askari Polisi na ofisi ya *OCD*

Karagwe zinavunjwa kupisha ujenzi wa barabara ya lami. Serikali ifanye juhudi za dharura kujenga nyumba hizo na ofisi ya *OCD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, utaratibu wa kupandisha vyeo. Nashauri utaratibu huu uangaliwe upya ili kuwapandisha Askari waliotumikia kwa muda mrefu ili kuwaongezea ari na morali ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita ni kuhusu waendesha pikipiki. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafundisha na kuwapa leseni waendesha pikipiki?

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wakuu wote kwa hotuba nzuri. Wizara hii ina majukumu mengi na taasisi nyingi zilizo chini yake. Wizara hii inatakiwa kuhakikisha usalama na ulinzi wa Watanzania wote na vitu vyao. Hili ni jukumu kubwa sana lakini bajeti wanayotengewa ni ndogo, haikidhi utekelezaji wa majukumu makubwa ya Wizara hii. Naomba Serikali ilione hili na kuiongeza fedha kwenye bajeti ili kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko makubwa kuona wanawake wanavyozidi kuuawa. Ni muda mrefu sasa tangu wanawake, wazee wenye macho mekundu kuanza kuuawa. Je, Serikali imechukua hatua gani au ina mpango gani wa makusudi wa kukomesha ukiukwaji huu wa haki za binadamu? Wanawake mkoani wamekuwa wanauawa kinyama na siku za karibuni wanawake wanauawa wakiwa mashambani wanalima ili wapate chakula cha familia zao na nchi nzima. Kwa ujumla wake katika kipindi kifupi wameuawa wanawake wengi kwa imani za kishirikina. Naomba kumuuliza Waziri ni mpango gani kabambe uliopo kwa kutumia intelijensia kuwabaini wauaji hawa na kukomesha vitendo hivi vibovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Pereira Silima na Watendaji Wakuu kwa kazi kubwa na ngumu wanayofanya. Nawapongeza pia *IGP* na Wakuu wa Vitengo vyote vya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye eneo la maadili ya Askari na Maofisa wa Jeshi la Polisi, Magereza na kadhalika; kwenye masuala ya kushugulikia watuhumiwa na wahanga wa uhalifu na kuboresha mifumo ya usalama barabarani na mambo yanayohusiana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani zingedhibitiwa vizuri na kupunguzwa kama kungekuwa na ukaguzi mzuri wa magari, leseni kutolewa kwa watu waliofuzu na kwa vipimo vya mara kwa mara vya macho vya madereva na vilevile kuwa na mfumo wa adhabu kali kwa madereva wanaosababisha ajali kwa uzembe. Vilevile kuweka kamera zinazojitegemea maeneo mengi barabarani ili kufuatilia mwenendo wa madereva na Askari Polisi wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi ulioletwa na mwekezaji toka Marekani ambaye angejengea uwezo TEMESA wa kukagua magari na kuwajengea Askari wa Usalama barabarani uwezo na kuwapa vifaa bora vya ukaguzi ili wafanye kazi kwa ufanisi. Mradi ungejumuisha Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Uchukuzi na Mambo ya Ndani. Rais alikutana na mwekezaji *WEP* na wawekezaji walishaleta pendekezo kwa Serikali, je, mradi huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi watenge kitengo cha kushughulikia madai ya wahanga wa ajali barabarani ili waweze kurahisisha madai yao dhidi ya bima za wenye magari ya usafirishaji abiria na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Polisi wa kila ngazi wanaomba/kushinikiza rushwa hata pale ambapo hakuna kosa. Hii siyo siri na hawajali cheo cha mtu wala hawana aibu. Hii imefanya wananchi kukosa imani na Polisi katika kuwategemea kwa ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wanatumika kuwalinda wahalifu na wavunja sheria mbalimbali kwenye makazi, biashara na kadhalika. Kuna haja sasa kuanzisha chombo maalumu (*ombudsman)* kitakachosimamia ukiukwaji wa maadili ya Askari na kuwachukulia hatua stahiki. Hii itaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa ukiukwaji wa maadili ya kazi kwa Askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wachache wapewe mafunzo maalum ya kushughulikia masuala ya makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia na kinyume na maumbile ili wawe *sensitive* kwa saikolojia na athari ambazo zimewapata wahusika na kuzingatia usiri unaohitaji katika kuficha *identity* ya wahanga wa uhalifu huo. Hii itawafanya wahanga wengi kujitokeza kutoa taarifa dhidi ya wahalifu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mauaji ya vikongwe, wenye ulemavu wa ngozi na kadhalika mara nyingi uhalifu huu umehusisha waganga wa jadi. Ni wakati muafaka sasa wahalifu hawa wakawataja waganga hawa nao kuunganishwa kwenye kesi hizi kama washiriki ili wachukuliwe hatua husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubakaji wa watoto wachanga, vikongwe na kadhalika, hali kadhalika umehusishwa na imani za kishirikina. Hapa pia wahusika wabanwe kwa kutumia Polisi waliofunzwa saikolojia hadi wataje hao waganga waliowashauri kufanya hivyo ili nao pia washtakiwe na kuchukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa wa Polisi wengi wamenenepa mno na kuwa na vitambi vikubwa na hii haitii moyo kuwa maafisa hawa wana stamina ya kutosha kushughulikia kazi zao kwa ukakamavu na ukamilifu. Kuna haja ya Maafisa na Askari kufanyiwa upimwaji wa afya na kushauriwa kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili wawe na afya imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi wengi bado wanaishi katika nyumba duni, kwa nini Jeshi lisitumie *Mobile Building Unit* iliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya JWTZ na ambayo haitumiki ilhali ina uwezo wa kujenga nyumba takribani nane (8) kwa siku na ina uwezo wa kuzunguka maeneo yoyote yanayohitajika kwa Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza lingetengeneza kitengo kitakachojiendesha kibiashara zaidi na kiombe tenda za ujenzi, useremala kwa ajili ya shule, taasisi za umma, ofisi za Serikali na kilimo na ujenzi ili waweze kutunisha mfuko na kuweka fungu dogo la kuwalipa *allowance* ndogo wafungwa wanaoshiriki ili wakitoka wawe na pesa kidogo ya kuanzia maisha baada ya kutumikia kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani iungane na Wizara ya Viwanda na Biashara kushinikiza Serikali na Taasisi zake zote kutumia bidhaa za ndani kama samani, makapeti na vifaa vya ujenzi vinavyotumia mbao kama milango na madirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari na Polisi *Traffic* wamekuwa wakichukua pesa toka kwa wananchi bila kutoa stakabadhi na ni dhahiri hii pesa hairudi Wizarani. Nitoe rai kuwa *fine* zote

ziwekwe kwenye mfumo wa elektroniki ili mtu akalipe benki *fine* yoyote anayodaiwa. Mfumo utengenezwe, kwa hili pesa nyingi itapatikana kwa njia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linashauriwa kuanzisha tovuti kupokea malalamiko ambapo watu watakuwa wanatoa taarifa kutaja tukio, wapi na namba au jina la Askari husika, kwa kuombwa rushwa wapi, kiasi gani na kwa kosa gani au kupigwa au kufanyiwa jambo lolote la ukiukwaji wa haki na Askari basi watajwe kuaibishwa na huku wakipeleleza na kuchukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu Uhamiaji. Pamekuwepo na wageni wengi sana wanaofanya kazi ambazo zingefanywa na Watanzania. Unakuta raia wa kigeni wanauza vitu barabarani kama Wamachinga, *garage* nyingi za Kichina wanafanya kazi za kuosha/kukwangua magari rangi, wengine kutoka India pale *Shopaz Plaza Supermarket* wanafanya kazi za ulinzi. Ni kigezo gani wanachotumia kuwapa watu kama hawa vibali vya kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu maslahi ya Askari. Askari wengi wanadai malimbikizo ya posho zao na bado mpaka sasa wanalipwa posho za Sh.150,000/= tu hii haiwapi motisha ya kufanya kazi na kupelekea kuwashawishi kupokea rushwa. Ni lini Serikali itawalipa malimbikizo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu makazi ya Askari. Makazi ya Askari ni jambo la kusikitisha pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa joto ni kali sana mpaka sasa hapa Dodoma bado Askari wanalala kwenye nyumba za mabati zijulikanazo kama *(full suit)*. Tukumbuke Askari nao ni binadamu, wana familia, wanatakiwa wawe na afya njema badala ya kulala ndani wanalala nje sababu ya joto wanaumwa na mbu, ni lazima waugue. Ni lini nyumba zitajengwa kwa matofali hapa Dodoma? Ni aibu kwenye karne hii bado Askari wetu wanalala chumba kimoja na familia watu 3 – 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni Kikosi cha Zimamoto. Mji wa Dar es Salaam unajengeka sana na majengo yenyewe ni maghorofa marefu sana. Nilichotaka kujua ni kwa kiasi gani Jeshi hili limejiandaa na magari yanayoweza kuhimili majanga ya moto kwa maghorofa marefu, magari hayo yanaweza kufikia ghorofa ya ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni mauji ya raia na Polisi. Taarifa zinaonesha watu 23 waliuliwa na Jeshi la Polisi mwaka 2013. Zaidi ya hayo, kuna mauaji yaliyotokea wakati CHADEMA ikifanya mikutano ya kampeni za Udiwani Arusha. Watoto wadogo na watu wazima waliuwawa. Je, mpaka sasa hivi uchunguzi wa mauaji haya umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, hali ya usalama. Katika nchi yetu hakuna amani kabisa ila tuna utulivu tu. Pamekuwepo na matukio ya kutisha ya mauaji ya watu wasiokuwa na hatia mfano albino, vikongwe kwa visingizio vya uchawi, Makanisa kutupiwa mabomu, watu kumwagiwa tindikali na kadhalika. Jeshi la Polisi lina mikakati gani ya kuhakikisha raia wake wanapata usalama?

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Askari wa Usalama Barabarani. Pamekuwepo na ajali nyingi barabarani zinazohusisha mabasi ya raia na kupelekea raia wengi kupoteza maisha. Ajali

nyingi husababishwa na mwendo kasi na vilevile aina ya mabasi. Mabasi mengi yanatumia *chasis* za maroli halafu wanazijengea bodi. Serikali ilikuwa ikague mabasi yote yenye *chasis* za malori ili yasiwe barabarani. Je, ukaguzi huu umefikia wapi? Malori yalikuwa yasafiri usiku lakini sasa hivi yanasafiri mchana, je, tamko lile limeishia wapi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na usalama na wananchi na mali zao nchini ni muhimu kwa ustawi wa watu na maendeleo ya nchi. Hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 katika mafungu matano ya Wizara ni muhimu kupimwa kwa kuzingatia umuhimu wa mahitaji hayo. Kipimo hiki kwa mafungu yote ya: Jeshi la Polisi (Fungu 28), Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji (Fungu 14), Jeshi la Magereza (Fungu 29), Idara ya Uhamiaji (Fungu 93) na Wizara ya Mambo ya Ndani (Fungu 51). Kwa upande wa Jimbo la Ubungo, naomba Wizara katika majumuisho itoe majibu ya masuala mbalimbali ambayo nimeyahoji kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2011 na 2013 na Wizara kutoa ahadi za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na michango mingine ya Mbunge tumekuwa tukichangia usalama wa raia kwenye ujenzi wa vituo mbalimbali vya Polisi mfano ujenzi wa Kituo cha Polisi Mavurunza (Kimara), Msewe (Ubungo) na Sinza. Kwa vituo hivi ambavyo viko katika hatua mbalimbali Wizara katika mwaka wa fedha 2013/2014 imetoa mchango gani na kuunga mkono jitihada hizo? Naomba katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara na Jeshi Polisi washiriki katika kuunga mkono jitihada za ujenzi na Kituo cha Polisi katika Kata ya Goba eneo ambalo liko pembezoni na kuna matukio ya ujambazi, uvamizi na uhalifu mwingine. Kiwanja kwa ajili ya ujenzi kimepatikana na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo tayari umeshatenga shilingi milioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono jitihada za Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi na vyombo vingine vilivyo chini ya Wizara katika masuala ya usalama wa Taifa, baadhi ya viongozi wa Wizara na Askari wa Jeshi la Polisi wamekuwa wakikiuka misingi ya uwajibikaji, utawala bora na haki. Waziri wa Mambo ya Ndani anapaswa kueleza ni hatua gani imefikiwa na amechukua uamuzi gani juu ya rufaa niliyokata dhidi ya aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni Charles Kenyala (kwa kuvamia mkutano wa Mbunge na wananchi kwa sababu zisizokuwa za msingi).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara izingatie pia kuwa Polisi walizuia maandamano ya madai ya maji. Ikiwa Wizara itaendelea kutoeleza maamuzi ya rufaa hiyo na barua ambayo nimemuandakia Waziri wa Mambo ya Ndani, nitaandaa maandamano dhidi ya Waziri wa Mambo ya Nandi kwa kutokuheshimu utawala wa sheria. Pia Waziri katika majumuisho atoe maelezo ya chanzo cha bomu lililolipuka katika mkutano wangu katika Kata ya Mabibo nikiwa jirani na gari la Polisi na hatua zilizochukuliwa kwa aliyehusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa 2013/2014 juu ya hali ya usalama kwenye aya ya 12, ukurasa wa 7, Waziri ameeleza warsha iliyoandaliwa na Jeshi la Polisi tarehe 15 Februari, 2013. Hata hivyo zipo Wizara nyingine ambazo ilikuwa ni muhimu kuhusishwa kwa kuwa zinasimamia sekta au masuala ambayo ni vyanzo vya migogoro ambazo ni muhimu katika kufanya suala usalama kuwa kipaumbele cha cha Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hizo ni pamoja na Wizara yenye dhamana ya kazi na ajira, Wizara inayoshughulikia masuala ya Vijana, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara yenye dhamana ya Mifugo, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Maji. Hivyo, katika makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa 2014/2015, Jeshi la Polisi likutane na awamu ya pili ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha maazimio ya warsha ya kwanza hayajitoshelezi, awamu ya pili itoke na maazimio ya kina zaidi na Wabunge tupewe nakala ili tuweze kushauri na kusimamia utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo katika Jiji la Dar es Salaam ambalo idadi yake ya watu ni zaidi ya asilimia 10 ya wananchi wote wa Tanzania Bara lina vyanzo au viashiria vifuatavyo ambavyo Polisi wanapaswa kushirikiana na Wizara nyingine zenye dhamana kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Matatizo ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, udhaifu katika utekelezaji wa mgawo wa maji, biashara harumu ya maji inayoambatana na uharibifu wa miundombinu kama mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Operesheni Safisha Jiji *(Smart Area)*. Suala la usafi binafsi naliunga mkono. Hata hivyo, operesheni zinatekelezwa vibaya kwa kushughulikia matokeo badala ya vyanzo na kuleta migogoro inayoweza kupeukwa. Mfano katika Jimbo la Ubungo palishakuwa na makubaliano ya kutafuta eneo mbadala la wafanyabiashara ndogondogo (Wamachinga), simu 2000 na wengine kabla ya operesheni ili zoezi kuwa endelevu. Hali hii iko vilevile kwa mama lishe na wanawake waliojiajiri.

Hata hivyo, Polisi kwa kulipwa fedha za ziada na *TANESCO* ama vyanzo vingine au mamalaka nyingine wanashirikiana na mgambo kufanya operesheni zenye kuchochea migogoro. Wizara ya Mambo ya Ndani izingatie kwamba ukosefu wa ajira kwa vijana na umaskini wa kipato kwa wakazi wengi wa Dar es Salaam ni bomu la wakati, Wizara na Jeshi la Polisi wasishiriki kulilipua na badala yake washauri vizuri katika muktadha wa kiusalama na Wizara nyingine kushughulikia chanzo badala ya matokeo. Operesheni hii imehusisha pia kuzuia bodaboda kuingia katika maeneo yanayoitwa katikati ya Jiji, Ubungo, Mwenge, Buguruni, Tazara na kadhalika huku Polisi wakishiriki kunyanyasa na kuchukua rushwa.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maandishi nichangie hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni moja ya Wizara muhimu zenye jukumu la kulea na kutunza amani ya Taifa letu. Wizara hii ni jicho na sikio la Taifa katika mustakabali mzima wa ustawi na utulivu wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua rasilimali kidogo zinazotengwa kwa ajili ya Wizara hii lakini pamoja na hali hiyo naandika kuelezea hatarisho *(risk)* linalolikabili Taifa kutokana na jinsi Mkoa wa Kagera kutawaliwa. Mkoa huu uko karibu na nchi tano na zote kwa kiasi kikubwa hali yake ya usalama si nzuri. Mikoa hiyo ni Rwanda, Burundi, DRC – Congo, Uganda na Sudan hali zao kiusalama si nzuri. Wananchi toka nchi hizo kwa nia nzuri au ovu wamekuwa wakiingia nchini kupitia Mkoa huu bila kudhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa huingia na kutoka katika nchi yetu kwa kiasi kikubwa na huwezi kuwalaumu watendaji. Mkoa wa Kagera una mpaka mrefu sana ukihusisha misitu, milima, maji ya ziwa na mito mikubwa. Kwa rasilimali tulizonazo kama Mkoa si rahisi kudhibiti mpaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia bajeti hii, naishauri Serikali kwa hatua ya dharura kuutangaza Mkoa wa Kagera kuwa Kanda ya Kiusalama. Nashauri Kagera iwe Kanda na Wilaya zake ziwe Mikoa ya kiusalama. Napendekeza Kanda ya Kiusalama kwa kulenga kuwa na watendaji wa hadhi hiyo kwa upande wa Jeshi la Polisi na upande wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya utaratibu wa kanda tunalenga kuwa na rasilimali nyingi za kiutendaji. Wilaya ya Muleba tu ina eneo la kilomita za mraba 7,000 za Ziwa zenye visiwa zaidi ya 30. Eneo hili linahitaji boti ziendazo kwa kasi zisizopungua tano ili kudhibiti eneo hili. Mpaka sasa hakuna hata boti moja ya aina hiyo acha Muleba hata Kagera nzima. Tunayo misitu mikubwa na hifadhi za Taifa ambazo zimekuwa zikitumiwa na raia wa nchi jirani kama maficho hasa wale walioasi kwao. *OCD* au Afisa Uhamiaji mwenye eneo la utawala kama hilo si busara kumtengea rasilimali kama zinazotengwa sasa. Ni kwa vigezo hivyo, naishauri Serikali kwa hali ya haraka ianzishe Kanda ya Kiusalama Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, niifikirishe Serikali yetu juu ya utaratibu wake katika uajiri wa watendaji wa Jeshi la Polisi na Uhamiaji. Utaratibu wa sasa unahimiza kuchukua vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa yaani kijana apitie mafunzo ya JKT kwa kipindi cha miaka miwili au mitatu na ndipo apate fursa ya kujiunga. Ushauri na hofu yangu ni kuwa kijana aliyepata mafunzo ya kijeshi barabara kwa miaka takribani mitatu utendaji wake utakuwa wa kijeshi zaidi.

Mtendaji mwenye uzoefu wa kijeshi kupewa jukumu au shughuli za kiraia utekelezaji wa majukumu yake utakuwa na walakini. Ipo haja ya kuwaandaa vijana ikiwemo kuwachuja kutokana na unyeti wa majukumu yao. Nashauri zoezi lifanyike bila kuwapatia fani ambazo zitaathiri utendaji wao. Wahitimu wa JKT ni sawa kwenda Jeshi la Wananchi kwani huko ndiko muelekeo wa mafunzo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo ya kuwa na Kanda ya Kiusalama, niishauri Serikali kudhibiti hali ya usalama katika Ziwa Victoria. Limekuwepo wimbi la uvamizi wa wavuvi na wananchi wanaoendesha shughuli za kiuchumi katika Ziwa. Wavuvi hunyang'anywa zana zao za uvuvi ikiwemo injini ambazo zimepatikana kwa fedha nyingi tena kwa mikopo. Hatari zaidi ni kuwa majambazi hawa hutumia silaha za kivita na mitumbwi iendayo kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Jeshi la Polisi Mkoani Kagera wamekuwa si wa msaada kutokana na rasilimali duni walizonazo. Ili kuepuka magaidi na waasi katika nchi zao hushirikiana na wahalifu wa Kitanzania kuligeuza Ziwa nchi ndani ya nchi, nashauri haraka jitihada zifanyike kudhibiti watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu Kituo cha Polisi Wilaya ya Kilombero kilichopo Ifakara. Kituo hiki kiko kwenye hali mbaya na ngumu kiutendaji na utunzaji wa nyaraka kwa sababu kila mwaka wakati wa mvua panakuwa na mafuriko ya muda mrefu.

Kibaya zaidi mwaka huu hatari kubwa imetokea na kusababisha kazi kutofanyika kabisa kama vile kukosa eneo la kuwahifadhi mahabusu, ofisi za kufanyia kazi na kuharibika nyaraka pia eneo la kuhifadhi. Serikali itoe jibu ni hatua gani za dharura na haraka zitafanyika ili kuhamisha kituo hicho ili kuboresha utendaji kazi na haki kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero yenye Kata 23 zenye wakazi wasiopungua 407,220 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 inakaribiana na ya wakazi wa Mkoa wa Katavi ambao wapo wakazi 500,000. Ni hatari kutotenga fedha za kutosha na kupelekea Askari kufanya kazi kwenye mazingira magumu na kuhamasisha vitendo vya rushwa kuzidi kushamiri na wananchi kukosa haki. Hivyo napenda kupata majibu ni lini Serikali itatenga bajeti kulingana na ukubwa na idadi ya watu na miundombinu ya eneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu ni lini itapeleka gari kituo cha Polisi Mlimba pamoja na kukosekana majengo na kujibanza katika majengo ya TAZARA? Wafanyakazi wanafanya kazi kwenye mazingira magumu kwa kukodi magari kwa gharama kubwa na kuazimwa na raia ambapo ni hatari kwa usalama wa wananchi na haki. Mlimba hadi Kituo cha Wilaya Ifakara ambako ndiko kuliko Mahakama ya Wilaya ni kata 14 na miundombinu ya barabara ni mibovu kwa mwaka mzima wakati wa mvua ndio hatari zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vingi vya Polisi havina majengo wala vyombo vya usafiri hata pikipiki, wananchi ndio wanasaidia mara zote vituo hivyo. Mfano Kituo cha Mbingu pamoja na wananchi kujitolea kujenga ofisi lakini hadi leo hakuna choo. Je, ni lini sasa Serikali itaunga mkono nguvu za wananchi kwa kupeleka pesa za ujenzi wa choo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Askari wa Barabarani *(Traffic)* kuwapa masharti ya kuandika faini mbili kila siku na kila Askari kila siku akusanye fedha hizo? Je, hii ni kwa sababu zipi na inasaidia nini katika kukomesha rushwa? Hii sio kuonea na uvunjaji wa haki za raia kwa Askari kulazimisha makosa mliyompangia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isianzishe Kanda Maalum Musoma Vijijini kuimarisha ulinzi ili kuokoa maisha ya wanawake wanaouawa wakiwa shambani wakitafuta chakula cha watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Mzungumzaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** *Bismillah!*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi angalau nichangie kidogo katika bajeti hii ambayo ni muhimu kwa ajili ya usalama na amani ya nchi yetu. Naanza kwa kusema kwamba naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia. Kama sijaunga mkono, basi sijui usalama utapatikana vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningependa sana nizungumze niliyotumwa na wapiga kura wangu wa Jimbo la Rahaleo Mjini Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kufanya hivi kwa sababu walishaniambia kwamba Mbunge wetu uende ukazungumze na sisi tumechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli kubwa iliyokuwa pale inazungumzwa ni kwamba kule Zanzibar huwa kunafanyika kitu sisi tunaita mitingi. Hufanyika mitingi, tena hufanyika kwa salama sana. Ni mikutano! Lakini mwisho wa habari wa ule Mkutano huwa kunafanyika matembezi na mengi huwa siyo ya halali. Sisemi kwamba ni maandamano, lakini mwisho wake ni pale Jimboni kwangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu limekuwa kama mchaimchai na kuna mnyama mmoja anaitwa mbwa. Ni lugha ya Kiswahili, nzuri, ni fasaha. Kwamba mwisho wake wakifika pale, barabara zinachomwa. Pale kwenye Jimbo la Rahaleo maskani zinachomwa, watoto wanapotea pale Rahaleo, wenye magonjwa ya pumu, mabomu pale Rahaleo; maduka, pale Rahaleo!

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wananchi wa Rahaleo wamechoka. Sasa wanachoniomba tu, wamewapa hongera sana Askari Polisi. Walifanya kitimutimu pale siku mbili, taabani sote! Siyo Rahaleo tu, mpaka Kwamtipura na kwingine kulikuwa taabani! Hali ilikuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lao wanasema kwamba tusifike huko. Kitengo cha Intelijensia (na hapa ndiyo kwenye suala) cha Jeshi la Polisi lifanye kazi ili hali hii isitokezee mapema na ili watu waishi kwa amani. Hilo ni ombi ambalo wamelitoa na imenibidi leo nisimame nilizungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni Masheha. Masheha wamechaguliwa na *GNU*. Sheria ipo ya Baraza la Wawakilishi! Wanafuata Sheria ile. Ile Sheria inasema wakikosea, basi washitakiwe au wahukumiwe kutokana na Sheria ambayo inawalinda wao.

Sasa inakuwaje leo tunatoka hapa tunawashambulia wale wazee kama hawafanyi kazi, hawalali kucha kutwa wale wazee, wanatazama usalama wetu, siye tumelala, Masheha anaamka usiku; mtu mwanawe ameumwa na pumu tu, anamwendea Sheha ampeleke Hosopitali. *(Makofi)*

Leo tunakaa tunawashambulia wale wazee! Mimi naona hatuwatendei haki. Mimi nahisi tu kama kuna matatizo yametokezea kwa Masheha mahali basi tuwashitaki katika sehemu husika ili nao washughulikiwe kuliko kusema maneno mabaya juu yao. Nawaheshimu na nawapa pole kama wenzangu wengine walivyowapa pole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kuna mambo yanatendeka nyuma ya pazia, lakini ndugu zetu Polisi hawa hawaonekani. Lakini kwa kila anayemwona nina hakika atawapongeza. Nawapongeza sana watu wa *Inter State Security Police* wa Afrika Mashariki, wamefanya kazi kubwa sana, mimi ni shuhuda. Wamezuia *small armament* hizi silaha ndogo ndogo nyingi sana kutoka katika nchi za jirani. Wamezitia katika *Data Base* na sasa hivi imepungua. Haijamalizika najua, lakini natoa hongera kwa Polisi hawa na waendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hilo halitoshi, Polisi hawa hawa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ndio wanaoshirikiana nasi kuzuia madawa ya kulevya; ndio wanaoshirikiana nasi katika mambo ya kuzuwia ugaidi. Wana Kitengo chao muhimu sana ndani. Mungu atupishie mbali, yaliyotokea kwingine pengine yangetokea kwetu, lakini ni ushujaa wao. Kwa hiyo, nawapongezeni. *IGP* Mangu, najua wewe mwenzangu sana, ulini-*serve* sana siku ile ya ajali, nakushukuru sana kwa kazi nzuri unayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo hatoshi na wale wa *Immigration* nao ndio vilevile, hawalali! Kuna kikundi fulani cha *Investigation* cha *Immigration* kwa kweli wanatia huruma. Tena naomba vilevile niwaombee mishahara itaongezwa, lakini vitendea kazi. Kuna wengine wanatumia pikipiki, wanatumia zana maalum wenyewe wanazijua, waongezewe. Mshahara vilevile, najua Serikali yangu hii sikivu, itawaongezea. Sio kwa wao tu, kwa watumishi wote wa Jeshi hili la Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu katika Mitaa yetu tunaishi watu wengi sana, tena wa hulka tofauti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Dakika zetu zimekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Nategemea sana kwamba Jeshi letu litapata nguvu na mishahara ya hali ya juu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Dkt. Abdulla Saadalla, Naibu Waziri wa Afrika Mashariki. Huu ndiyo mwisho wa uchangiaji wetu wa jumla, sasa tunaingia katika awamu ya uhitimishaji; naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, atatumia nusu saa. Mheshimiwa Pereira!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu katika hoja hii. Kabla sijafika mbali naomba nitangaze kwamba, naiunga mkono mia kwa mia na nawaomba wenzangu Wabunge wa pande zote mbili tuiunge mkono ili tuweze kupata hizo fedha na twende tukafanye kazi tunayotaka kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wengi sana wamechangia. Tunawashukuru wote, wale ambao wametia maoni, wale ambao wametushauri, ni kwamba ushauri huo tunauchukua na tutaufanyia kazi. Wale ambao walikuwa wanataka ufafanuzi, tutajitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo kwamba, kwa sababu ya kuhamasika Wajumbe katika kuchangia kwa njia zote za maandishi na za kuongea, michango imekuwa ni mingi sana. Kwa nusu saa hii na nusu saa ya Mheshimiwa Waziri, hatutaweza kutoa majibu ambayo yataweza kumridhisha kila mtu.

Niseme tu kwamba, mjue lengo letu ni kutoa majibu ambayo yatatoa ridhaa na yatatosha katika hoja hizi, lakini baada ya hapo, tutatayarisha Bango Kitita ambalo tutalisambaza kwa Wabunge ambao majibu yao wanaweza wakayakuta humo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivysosema, kulikuwa na hoja nyingi na hoja ziko kwenye mafungu yote ya Wizara hii. Naomba nianze kutoa mchango wangu kwenye baadhi ya hoja zilizoelekezwa kwenye Jeshi la Polisi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo nafikiri ni la umuhimu sana ni suala la Sskari kulaumiwa kwamba wanachukua rushwa. Hili kwa kweli, halipendezi, ni aibu, ni kinyume na utawala bora. Watu wengi walilikemea na kutaka lifanyiwe marekebisho ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, jitihada kubwa zinafanywa. Katika kufanya hivyo, tunafika hatua ya kuwafukuza Askari na Maafisa wengi ambao wanaonekana pengine wanapokea rushwa. Baada ya hapo, wale watuhumiwa baada ya kuwaachisha kazi, tunawapeleka kwa hatua zaidi za vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tushirikiane kwa sababu taarifa ndiyo mwanzo wa kuchukua hatua zenye maana. Tupeane taarifa ili wale ambao tunawashtakia na wale wenye ushahidi tuwachukulie hatua na tusikamate ambao hawahusiki na kuwavunja moyo ambao ni waadilifu katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilihusu Serikali kuwa na mkakati endelevu wa vitendea kazi kwa ajili ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Jeshi la Polisi kama yalivyo kwenye majeshi mengine Wizara ya Mambo ya Ndani ni mengi, lakini tunajitahidi kila siku kwa bajeti na uwezo wa Serikali inayotupatia kuyatatua matatizo tuliyonayo. Katika siku hizi za karibuni, hasa kwenye vitendea kazi, kama ilivyoonesha bajeti yetu tunategemea kupata magari, 777 kuongeza kwenye magari kama 600 ambayo ni mazima na 300 ambayo hayafanyi vizuri. Tunaamini kwamba wale wote ambao wanalalamikia magari kwenye Wilaya zao tunaweza tukawasaidia na tukawa na usafiri wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ambayo lazima niseme hii ni hoja iliyochangamkiwa na Wajumbe wengi, Wabunge wengi wamesikitika sana kama tunavyosikitika sisi kwamba Askari wetu bado wana maslahi duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru sana kwa kuona uchungu na suala hili. Serikali imeendelea kujitahidi kuyarekebisha maslahi ya Askari katika nyanja zote. Hata hivyo, inawezekana kwamba *speed* ni ndogo na pengine hili tatizo bado linasumbua. Tutachukua hatua zinazowezekana kwa msaada wenu na msaada wa Serikali kwa kujenga hoja ili tuweze kuyarekebisha kama bajeti zinavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kupunguza uhalifu kwenye Ziwa Viktoria. Ni kweli kwamba kuna uhalifu siyo tu Ziwa Viktoria, lakini pia tatizo hili linawakuta wavuvi wa Ziwa Tanganyika na maziwa mengine, hata wengine walikuwa wanataja Ziwa Jipe. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo tunalifanyia kazi, tumepata baadhi ya vitendea kazi vya msaada na tayari tumevipeleka kwenye maeneo kusukuma mambo haya. Ni tamaa yetu kwamba tuendelee kusaidiana pale ambapo pengine kuna tatizo, lakini tunashukuru sana kwa ushauri huu ambao siku zote tunaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilijitokeza ni suala la ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba tunapoteza watu wengi sana, lakini pia tunapoteza mali na tunawatoa wengine kutoka kwenye wanadamu ambao wana viungo kamili kuwapeleka kwenye ulemavu. Hili ni jambo ambalo sote tukishirikiana tunaweza tukalipunguza, kwa sababu kama sio dereva utakuwa abiria na kama sio abiria utakuwa mtu ambaye unaona kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pendekezo la sheria mpya kwa ajili ya kupunguza ajali barabarani, lakini hilo halitasaidia kuliko au kuongeza viwango vya adhabu kuliko kila mtu kuchukua akafanya wajibu wake.

Kuna mapendekezo ya kutumia *CCTV* katika maeneo ya mjini ili yadhibiti madereva kama hawa, lakini pia wahlifu wa aina nyingine; hili jambo tunalifanyia kazi na tutafika mahali ambapo nchi yetu itapata *coverage* yakutosha.

Katika ajali pia kuna suala la kubandika namba za Viongozi wa Polisi; hilo tunalifanya na pengine zinasaidia katika kupunguza ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na tatizo la uhalifu wa tindikali, mabomu, uuaji wa Viongozi wa Dini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, upelelezi umefanywa katika kila tukio na tumewakamata watu wengi, wengine wamehojiwa, wakaachiwa, wengine wamehojiwa

wakaendelea kuchukuliwa hatua nyingine. Wapo ambao majalada yao yamefika kwenye Ofisi ya *DPP* na wengine wameshafika mpaka Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na lingine kwamba kuna matukio yaliyoorodheshwa ya Polisi kuchukua uhai wa binadamu pasipo sababu. Haya yote yameripotiwa na tunaendelea kuyafanyia kazi. Kama ilivyosemwa kwamba, kila mahali inapotokea upelelezi unafanywa na hatua dhidi ya wahusika zinachukuliwa, ikiwemo kuwafukuza kazi na wengine kuwapeleka kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Al-Shymaa la hawa walemavu wa ngozi. Jjtihada nyingi tumefanya na kwa kweli tulikuwa tayari tumeondokana na jambo hili kwa siku nyingi. Hata hivyo, tatizo la ushirikina limerudi na linaendelea kutuathiri, siyo tu kwa hawa walemavu, lakini pia kuna mauaji ya wanawake ambayo kwa kweli hatuwezi tukayavumilia. *Task Force* tumezipeleka huko na zinafanya kazi, tutapata matokeo na kazi kubwa itafanyika baada ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Jeshi la Polisi nilisema zilikuwa nyingi, nyingine zitaandikiwa na nyingine Mheshimiwa Waziri, atazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hoja ya kwanza, ilikuwa ni masikitiko kwamba Jeshi hili halipatiwi fedha za maendeleo. Hiyo ni kweli, na kwa kweli kuna mambo mengi ambayo Jeshi hili Jipya lingefanya kuliko kuendelea kuhangaika. Kuna masuala ya ujenzi wa Makao Makuu, kuna ujenzi wa Vituo mbalimbali, kuna ununuzi wa magari ambavyo kwa kweli hatuwezi tukavifanya bila ya kuwa na kasma ya maendeleo. Matatizo haya tumeyafikisha kwenye Kamati ya Bajeti, lakini pia tumeyafikisha kwenye Serikali kwa maana ya Hazina na tuna tamaa kwamba kunaweza kukatokea marekebisho baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa wengi tu waliomba kuwa na Vituo vya Zimamoto na wengine magari; yote tuombe na tusaidiane tuweze kufanikisha katika kuongeza au kulipatia Jeshi hili fedha za maendeleo ili tuweze kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni vitendea kazi ambalo halina tofauti na maelezo niliyotoa. Zikipatikana fedha na bado tuna jitihada nyingine za kidiplomasia, tunapata misaada. Hivi karibuni tulipata magari matano ambayo tumeyapeleka Mikoani, lakini pia tumepata boti za uokoaji ambazo nazo tayari tunazitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la maghorofa marefu, hasa Dar es Salaam, na uwezo wa Jeshi la Zimamoto kuweza kuyafikia kama moto utatokea kwenye maeneo ya ghorofa za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba uwezo wetu kwa sasa haufiki, lakini bado kuna hatua ambazo zinafanyika kwenye majengo marefu kuweza kuwanusuru watu ambao wako kule pamoja na mali ambazo zipo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya kuchukua hatua za haraka kukomesha tabia ya wananchi wanaopiga simu za uwongo. Ni kweli baadhi ya Watanzania wanapata furaha na wanaridhika wakipiga simu Zimamoto kuwaambia kuna moto ambao haupo. Hili jambo linaleta usumbufu mkubwa siyo tu kwa Askari, lakini pia watu ambao wanatumia barabara, lakini pia na hasara katika kile kidogo ambacho tunacho. Ni vyema tujione kwamba, anayepiga simu ana umri wa kiutuuzima na tabia hizi za kitoto siyo vizuri kufanywa na watu ambao wana utu uzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine ambazo zilikuwa kwenye Jeshi la Magereza. Hoja kubwa ambayo imechukua nafasi ilikuwa ni watu kuona huruma kwa wafungwa na chakula wanachopatiwa cha Shilingi 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliolichangia hili kwa hisia. Kwa kweli, kilio hiki kimefika kwa Serikali, hatua zitachukuliwa ili tuweze kurudi kwenye msingi wa haki za binadamu za kuwapatia chakula ambacho kingeweza kikawasaidia. Kama walivyosema Wajumbe hapa wakati fulani, sote ni wafungwa watarajiwa.

Tufanye kazi hivi ili wale ambao watanusurika, bado wajisikie wamepata faraja kwamba, wafungwa wanapata chakula cha kuridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba labda Sheria ya *Parole* tuiangalie. Sheria ya *Parole* hivi sasa tunaifanyia kazi, lakini nayo ni lazima niseme kwamba, pamoja na kuwa hatujaifanyia kazi, ni sehemu ya msaada mkubwa katika kupunguza msongamano Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kusema kwamba, tuangalie uwezekano wa posho za Askari. Hili lina-*cut across* Askari wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kuiongeza kutoka Sh. 5,000/= hadi Sh. 7,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi hili tumelipeleka na wachambuzi wanaendelea kulifanyia kazi. Ni tamaa yetu kwamba tunaweza tukawapa motisha Askari wakafanya kazi vizuri kuliko wanavyofanya leo.

Hata hivyo, nawaomba Askari wakati tunasubiri hili lifanyike, basi tuendelee kufanya kazi kwa ari tukijua kwamba jitihada nzuri zinafanywa kutukwamua na mambo ambayo yanatuandama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za makazi; ni kwamba, kweli kwenye Majeshi yetu, hasa Magereza, kuna tatizo kubwa sana la nyumba za makazi, na hatuwezi tukalitatua tatizo hili kwa kutegemea bajeti. Lakini mbali na bajeti tunafanya jitihada kwa maelekezo ndani ya Jeshi, kuna utaratibu wa ubunifu ambao kila Kituo au Gereza, linaanza kwa kujitatulia matatizo yao wenyewe. Wanajenga majengo ambayo yanatumia rasilimali ambazo zinapatikana pale na hatimaye Jeshi, Makao Makuu linamalizia. Lakini pia, tuna mazungumzo na Sekta Binafsi kuweza kupata au mikopo au ubia ambao utasaidia kuweza kujenga nyumba na kuliondoa hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni la msongamano Magerezani. Msongamano Magerezani pamoja na kuwa unapungua, lakini unapungua kwa *speed* ndogo kuliko ambavyo sote tungeridhika. Bado kuna msongamano mkubwa na kuna hatua nyingi tunazichukua. Hatua ya kwanza ni ujenzi wa Magereza mapya, lakini pia kutumia Sheria zilizopo za *Parole,* huduma kwa Jamii na nyingine kupunguza msongamano; lakini pia kuna hatua za usukumaji kesi ili kesi zimalizike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka tatizo ambalo lilikuweko kule Arusha hivi karibuni lilihusika na mwenendo wa kesi. Hili kwa kushirikiana na wenzetu katika Jukwaa la Haki Jinai tunalisimamia na tutahakikisha kwamba, siku zote msongamano unapungua. Pamoja na mambo mengine yatakayofanywa pia kwa kesi ambazo ni ndogo ndogo, basi uwazi wa dhamana utasaidia.

Pamoja na ujenzi na upanuzi wa Magereza ambayo sidhani kama ni suluhisho, sote ambao ni wazazi tuhakikishe kwamba watoto wetu hawapati nafasi; hatuwaruhusu wakawa nao wahalifu. Kwa hiyo, ulezi, ulezi, ulezi, ni moja katika jambo ambalo ni lazima tulisimamie. Vinginevyo, kwa sababu tunaongezeka na tunazaa kila siku, ukubwa na ujenzi wa Magereza hautakuwa suluhisho la kuondoa msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia, kuna mtu aliuliza hili Shirika la Magereza, lina faida gani? *In fact* Shirika hili linasaidia na miradi yake inasaidia sana urekebishaji wa wafungwa. Wafungwa wanarekebishwa kwa kuwemo au viwandani kuzalisha au kilimo kuzalisha au kufanya kazi za ujuzi fulani kama ujenzi na nini. Kwa hiyo, hata tusingepata pesa moja kutoka kwenye Shirika la Magereza, Shirika hili linatusaidia sana katika kazi ya msingi ya kurekebisha wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu kukarabati Magereza na kujenga au kumalizia kwenye maeneo mengine kama Meatu na kwingine. Kwa kweli jitihada zinafanyika, lakini kama mnavyoona, bado tunategemea bajeti ambayo kwa kweli ni ndogo. Nilisema rai nyingine za umaliziaji na kutumia *resources* zilizokuwepo kwenye maeneo zinasaidia lakini Serikali itaendelea kuboresha makazi ili Askari wa Magereza na wengine waishi kama wanavyoishi Watanzania wengine wanaofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na jambo moja la Ndugu Said Mtanda la Kisima kwenye Gereza la Kigulugundwa. Kwa kweli hapa kuna tatizo kwa sababu tumeshachimba kisima kirefu, lakini maji hakuna. Tumejaribu tena na tena hatujapata. Hapa kinachoendelea ni kufanya utafiti na labda tunaweza tukafanikiwa. Tukishindwa, tutawachukua baadhi ya washirikina watusaidie kuliko kuwatafuta wenzetu walemavu wa ngozi wakawashughulikia waende wakatusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenda kwenye Idara ya Uhamiaji. Jambo moja ambalo limejitokeza kwa nguvu sana ni kwamba kuna watu wanahisi kupunguzwa kwa *retention* ya Idara hii ni tatizo kutoka asilimia ambayo walikuwa wanaipata asilimia 61 mpaka asilimia ya sasa 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo bado tunalifanyia kazi na tunashirikiana na wote ambao nia yao ni kutaka iendelee kurudishwa kule ilikotoka ili itusaidie zaidi kuliko sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine kuhusu *visa*. Wabunge wengi walishauri kutumia *visa* za stika ili kudhibiti upotevu wa mapato katika Balozi zetu za nje na tunawashukuru kwa mawazo haya ambayo tunayafanyia kazi na si punde tu tunategemea kwamba vituo vyote vya *visa* vitatumia stika ili tuweze kupata mapato lakini pia kuweza kujenga uaminifu katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu wahamiaji haramu. Ni kweli tuna tatizo kubwa sana la wahamiaji haramu hasa kutoka nchi za pembe za Afrika ambao wanapita kwenye nchi zetu katika kwenda Kusini mwa Afrika. Tatizo ni kwamba wale watu inawezekana wakawa hawaji kwa makazi hapa kwetu, lakini kwa vyovyote, Sheria zetu wanazivunja na tumeendelea kusimamia Sheria hizo, wengine tunawachukua tunawapeleka Mahakamani na kushitakiwa na adhabu mbalimbali zimekuwa zikitolewa. Kulikuwa na tatizo la wengi kubaki Magerezani wakati wameshatumikia vifungo vyao na hili tunalifanyia kazi. Serikali inaendelea kuwarejesha na tumesharejesha wengi na tunaendelea kati ya 445 waliobakia Magerezani tutachukua hatua nao kuwasindikiza ili warudi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Mangungu alikuwa na swali la wahamiaji ambao wanachukua ajira; hili nalo tunalifanyia kazi. Kuna Taasisi mbalimbali zinazoshirikiana

kuona kwamba ajira zinawasaidia zaidi wazawa kuliko watu ambao wanaamua kutoka kwenye maeneo yao wakaja kuchukua ajira ambazo tunazo.

Kuna swali la *electronic visa, electronic immigration;* jitihada, kwa kweli tunaendelea, upembuzi yakinifu tumemaliza kuhusu jambo hilo na kwa kweli tunategemea kuendelea na mradi huu na kuukamilisha ili *visa* zetu ziwe za namna tofauti na zilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na maelezo kwamba Wahamiaji haramu ambao tuliwaondoa hasa kwa *operation* tokomeza wanarudi. Naomba kutoa taarifa kwamba ni kweli lakini huko ambako walikuweko bado Serikali ipo na kuna hatua mbalimbali ambazo tulizifanya ili kuwafanya wakirudi washughulikiwe.

Kuna *task force* tulizozianzisha kwenye Wilaya ambazo ziko *permanent* na zitasaidia kuhakikisha kwamba wanaorudi wanafuatiliwa, wanahojiwa na hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao. Kulikuwa na wahamiaji wa Dar es Salaam, hawa tunashughulikia kwa kupitia doria, tunapitia kwenye maeneo ambayo wapo na pia tunatoa elimu kwa wenyeji ambao wanawahifadhi au wanawaleta. Lengo ni kwamba sote tushirikiane ili kuweza kuona kwamba hawa wahamiaji tumewadhibiti na faida za nchi hii na za maendeleo zinawafikia wazawa na wale ambao wanazistahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga ambaye alizungumzia sana kuhusu wahamiaji wa Ethiopia. Kwa kweli nimuahidi kama nilivyosema kwamba tunachukua hatua za kuongeza doria ili tuweze kuwadhibiti na wengine ambao wameshafika kwenye maeneo ndani ya nchi tuwashughulikie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la vitendea kazi kwa ajili ya misako na doria za uhamiaji; hizi tunazifanyia kazi. Kama nilivyosema, tunaendelea kutafuta fedha ndani na nje ili tuweze kuvinunua na kuwa navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye *NIDA*. Hoja kubwa ya *NIDA* ilikuwa ni kuhusu vitambulisho, uandikishaji na hasa uandikishaji ambao unaonekana haujaenda vizuri kule Pemba. Kama nilivyokwisha kutolea maelezo jambo hili ni kwamba utaratibu wa kuandikisha Watanzania ni wa kawaida na lengo letu *in fact* ni kuhakikisha kwamba siyo Watanzania tu ambao wanapata hivi vitambulisho. Vitambulisho vitatolewa kwa Watanzania, kwa wageni wa Watanzania na wakimbizi.

Kwa hiyo, kitu ambacho labda ningekisema hapa ni kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika zoezi hili haliendi mara moja kwamba likimalizika wanaondooka na waliokosa hawatapata. Dar es Salaam kumefanywa zoezi hili, Dar es Salaam tunajua watu wangapi wanakaa lakini mpaka leo *total* ambayo tumeipata kuandikisha Tanzania nzima ni 3,300,000.

Kwa hiyo, kila tunapokwenda tunawahudumia wale ambao tumewapata lakini bado fursa ya kuwahudumia wengine ipo na Watanzania wasiogope kwa hili. Hata wageni wao wataweza kupata vitambulisho.

Jambo lingine ambalo labda lilikuwa na tatizo ni kuhusu Micheweni. Nimepata taarifa kwamba tatizo ambalo lilikuwa *alarming* pale Wilaya ya Micheweni ni kwamba badala ya kufanya wiki mbili kama walivyofanya kwenye Majimbo mengine, pale waliishiwa na vifaa na wakafanya wiki moja. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Kai na Mheshimiwa Khatib kwamba kazi hii itafanywa haraka baada ya bajeti kwa sababu kuna tetesi kwamba fedha za vifaa hivyo tulivyovitaka imepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu fedha kwa ajili ya kuandikisha Watanzania. Kwanza nawashukuru Wabunge wengi sana, wamelisemea hili kwamba hili zoezi pengine linakwenda taratibu na sisi tunasema kwamba kweli linakwenda taratibu, lakini tatizo ni fedha. Katika bajeti ya mwaka huu ambao tunao tulikuwa tumetengewa Shilingi bilioni 151 na mpaka jana tumepata Shilingi bilioni 35. Bado miezi miwili pengine kumaliza mwaka huu na kwa kweli tufanye jitihada ili Serikali isaidie tuweze kutimiza malengo ya jambo hili.

Jambo kubwa ambalo halifanyiki vizuri ni kwamba katika makisio yetu tulikuwa tuwe na *MEU* au *Mobile Enrollments Units* ziwe kama 5,000 ndiyo tungemaliza kwa wakati, lakini mpaka sasa tuna asilimia kumi tu ya vifaa hivi. Kwa kweli Serikali tunaendelea kuifuatilia na Serikali hii haidanganyi wala haina tatizo inaweza ikatupatia fedha tukamaliza jambo hili kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho ni muhimu, siyo tu kama wengi wanavyofikiria litasaidia kwenye Serikali mbili au tatu, lakini malengo hasa ya Serikali ni jambo hili lisaidie uchumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri a Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu murua. Tunakushukuru sana kwa kazi nzuri uliyoifanya.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mathias Chikawe ili ahitimishe hoja aliyoitoa kuanzia jana. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha jana jioni mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ya kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa uongozi wake mzuri na ushauri ambao amekuwa akitupa mara kwa mara katika kuendesha Wizara yetu.

Naomba nichukue nafasi hii pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lema, anaitwa Waziri Kivuli, ndivyo alivyoteuliwa na Mheshimiwa Mbowe, lakini naomba nimteue kama Waziri mwenza kwa sababu tunasaidiana katika kuendesha Wizara hii ambayo ni nyeti sana kwa manufaa na maslahi yetu wote. Namshukuru kwa mawazo yake mazuri, *style* yake ya kusema ni tofauti lakini yapo mawazo ambayo tumeona ni mazuri na tutayatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote kwa michango mizuri sana na ushauri mzuri waliotutolea kwa maandishi na wengine waliozungumza hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Nami nakusudia kusema kwamba pengine hatutaweza kujibu hoja zote hizi au kuzitolea maelezo hoja zote zilizotolewa mara moja, lakini tunaahidi kwamba tuta-*compile* majibu yetu halafu tutapeleka kwa Wabunge wote wayapate ili waweze kufanya rejea katika vikao vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutolea maelezo hoja za Waheshimiwa Wabunge naomba nitoe tamko la Serikali kuhusu mauaji yalitokea kule Simiyu ya mwanamke

mlemavu wa ngozi. Kwanza niseme kwamba juzi baada ya mauaji hayo kutokea, Kamishna Mkuu wa *Human Right Commission* ya Umoja wa Mataifa alitoa *statement* kulaani mauaji yale na mimi pia kwa niaba ya Serikali nataka kusema na sisi tunalaani sana tena sana mauaji haya na nataka kuahidi hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Polisi wetu hawatalala mpaka tumkamate yule aliyehusika na kumpeleka mbele ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakusudia kujaribu kujibu hoja za Wabunge kwa kuchukua hoja zenyewe mbalimbali kwa ujumla wake, badala ya kuchukua hoja moja moja. Hoja ya kwanza ambayo ni kubwa sana ni hoja inayohusu madeni ya Majeshi yetu. Kama mnavyofahamu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokozi na sasa majeshi yote haya yanatoa huduma kwa wananchi.

Katika kutoa huduma kwa wananchi, kama zilivyo Idara nyingine za Serikali ambazo kutokana na ufinyu wa bajeti zimekuwa zikipewa huduma na kukusudia kuzilipa baadaye; Idara hizi zimelimbikiza madeni makubwa sana. Idara ya Magereza peke yake mpaka leo hii ina madeni ya Shilingi bilioni 65, Idara ya Polisi ina madeni yasiyopungua Shilingi bilioni 123 na haya ni madeni kwa Watumishi, likizo zao na stahili zao mbalimbali; ni madeni kwa wazabuni wale wanaotoa huduma, wanawapatia vitu mbalimbali kama mafuta, vyakula na kadhalika, madeni ya mikopo na riba kwa Mashirika kama vile *NSSF* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo la madeni katika Jeshi letu hili linakuwa kubwa kwa sababu bahati mbaya sana kila tunapoomba bajeti ya kukidhi Idara hizi, nanyi Waheshimiwa Wabunge mmesema imekuwa bahati mbaya hazitoki, na zinapotoka wakati mwingine hazitoki kwa wakati.

Sasa hili limekuwa tatizo na tumekuwa tunalimbikiza madeni. Kwa hiyo, hata tutakapopata pesa mwaka huu, tutakapoanza mwaka ujao wa fedha tutaanza kwa kulipa madeni na kwa hiyo, tutaanza kuchukua madeni mengine tena.

Jambo hili tunashauriana na wenzetu wa Hazina tuone ni kwa namna gani tunaweza tukatoka hapo. Hatuwezi tukawa tunazunguka katika mzunguko huu wa madeni makubwa ambayo yanatufanya tusiweze kuendelea katika makusudio yetu. Tunapanga mipango hii tunashindwa kuifikia kwa sababu kwanza lazima tulipe madeni halafu ndiyo tutoe huduma.

Kutokana na hilo inakuwa vigumu sasa kutekeleza mahitaji yetu na makusudio yetu tuliyojiwekea katika mwaka wa fedha uliotangulia. Hili ni tatizo kubwa siyo kwa Majeshi ya Wizara yangu peke yake, nafikiri kwa Idara zote za Serikali na ni jambo ambalo kama Serikali tunakaa, tunalitafakari tulipatie ufumbuzi wa kudumu ili tuweze kupiga hatua mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuwa linasumbua sana katika Majeshi yaliyoko chini ya Wizara yangu ni suala zima la posho za Askari zinazoitwa *ration allowance*.

Waheshimiwa Wabunge karibu wote mmezungumzia hili na mmesema wazi kabisa kwamba posho hizi hazitoshi na kwamba jambo hili hamkulisema leo tu, mmelisema hata kabla ya mwaka 2013 na kadhalika. Nami nakubaliana na nyinyi na mimi niko na nyinyi kabisa kwamba posho ya Sh. 5,000/= kwa siku haitoshi. Watu hawa wanafanya kazi sana, ninyi mnawaona, mnawaona kwenye *parade*, mnawaona wanavyofanya kazi usiku kufukuzana na majambazi na kadhalika, na mnawaona wanavyodhibiti wafungwa kwenye majela.

Sasa watu hawa tunawaombea, mwaka 2013 bahati mbaya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, rafiki yangu Marehemu Mgimwa alikubali tufike Sh. 7,500/= lakini bahati mbaya haikuwemo kwenye bajeti. Yeye alikubali kimsingi, lakini haikuwemo.

Kwa hiyo, tumeendelea kupata Sh. 5,000/=. Mwaka huu tunaomba na tumeomba ifike Sh. 8,000/=. Mpaka hivi ninavyozungumza, bado tumepewa hizo Sh. 5,000/= lakini tumo katika majadiliano mazito sana na Hazina ili tupate angalau Sh. 8,000/=.

Nami nafikiri watu wa Hazina baada ya kusikia hoja ambazo nyinyi Waheshimiwa Wabunge mmezisema na kwa nguvu ile ile ambayo mmezisemea, wamewaelewa na watakuwa wepesi sana kulielewa jambo hili hasa wakizingatia kazi ambazo zinafanywa na Majeshi haya katika kutoa huduma kwa wananchi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la posho limekuwa ni *issue* na wote nyinyi mmelisemea nami nataka kusema siwapingi, tuko pamoja kwenye hili, ila tu sasa tuone uwezo wa Serikali na bado tunao katika mazungumzo tuone ni kiasi gani wanaweza kutoa katika mwaka huu wa fedha.

Suala lingine ambalo limezungumzwa na kila mmoja aliyesema katika Bunge hili, ni suala la chakula cha wafungwa, ndugu zetu ambao wamefungwa Magerezani. Ndugu zetu ambao wako Magerezani kama mahabusu pengine hawana hatia wakisubiri kesi zao. Kiwango ambacho tunawapa ni Sh. 500/= kwa siku. Sasa katika hali ya sasa hali ya maisha imebadilika bei zimepanga sana. Duniani hapa na Tanzania kwa kweli Sh. 500/= mno.

Mwaka 2013 vilevile katika mazungumzo na Kamati yangu ya kudumu ya Ulinzi na Usalama, ilikubaliana kwamba kiwango hiki kifike Sh. 1,500/= lakini bahati mbaya hali ya bajeti wakati ule haikuweza kukidhi na hatukupata kiwango hicho. Tunaendelea na mazungumzo na Hazina mpaka sasa hivi ninavyosema, tupate angalau Sh. 3,000/=. Tukishindwa hiyo, tupate basi hiyo Sh. 1,500/= ambayo tulikuwa tumekubaliwa mwaka wa fedha uliopita (2013/2014).

Hili nalisema kwa sababu ni kweli siyo binadamu wa kawaida anaweza kuishi kwa Sh. 500/=; ni taabu sana. Hizi zinakuwa siyo zaidi kwa sababu siku nyingine mahabusu wanakuwa wengi, kwa hiyo, lazima itakuwa chini kidogo kwa Sh. 500/=. Sasa mimi nasema kweli bajeti yetu ni ngumu sana! Ni ngumu sana na mimi nakubali, lakini tutaendelea kuomba, tutaendelea kuzungumza na wenzetu wa Hazina ili waone ni jinsi gani wanaweza kututoa hapa kwenye Sh. 500/=. Kwa sasa ni Sh. 500/=.

Tunayo matatizo pia ya sare za wafungwa. Wafungwa hawa wanaweza wakafika mle ndani wakaa miezi sita; anapoondoka ile sare yake anakuja kuvaa mfungwa mwingine anayeingia. Bado hatujapata uwezo wa kutoa sare kwa kila mfungwa anayeingia. Tunayo matatizo pia katika sehemu nyingine ambazo zina hali ya hewa kidogo siyo rafiki, baridi sana; Mbeya kule, Iringa, Lushoto, wafungwa wa pale wanapata matatizo na hatuna nguo zile nzito za kuwapatia wafungwa hao kuvaa.

Sasa tunafanya jitihada na katika bajeti ya mwaka huu ya Idara ya Magereza angalau tumepata pesa ambazo tutanunua hizi nguo, sare kwa ajili ya wafungwa. Pia tutanunua sare kwa ajili ya askari, tumewawekea bajeti kiasi kidogo, tunadhani kitatosha kwa kununua sare kwa ajili ya wafungwa na kwa ajili ya Askari wanaowalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo suala lingine kubwa sana ambalo limezungumziwa pia na Kamati, limezungumziwa pia na Waheshimiwa Wabunge mlipokuwa mkitoa michango yenu, ni suala la *retention*. *Retention* ni utaratibu ambao Serikali ilikubaliana kwamba Idara za Serikali zinaweza zikapewa motisha kwa kuzalisha zaidi, kukusanya maduhuli zaidi kisha

wanapewa kiasi ambacho kitawasaidia kuendesha mambo yao kabla ya hata zile *issue* nyingine za *treasury* zinapotoka.

Sasa Idara zetu zinayo *retention* na tumeona zimeisaidia sana hasa Idara ya Uhamiaji, imeweza kujenga majengo, hata Idara ya *fire* imeweza kujenga majengo kwa kutumia fedha hizi, tunaongea na Hazina ili utaratibu huu uendelee ili Idara hizi ziweze kupata fedha za kujiendeleza katika shughuli zao hasa hasa kujipatia nyenzo pia za kuweza kukusanya maduhuli zaidi kwa ajili ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge, lipo tatizo limezungumzwa la Ofisi na nyumba za Askari hasa Polisi, Magereza na Uhamiaji. hili ni tatizo kubwa na sisi tumeliona na hata mlivyoona katika bajeti ya mwaka uliopita, siyo fedha nyingi sana zilitolewa katika Idara hii.

Sasa sisi tumeona pengine tusikae kuitegemea bajeti hii ya Serikali, pengine sasa tuwe wabunifu zaidi tuone ni namna gani sisi wenyewe tunaweza kufanya ujenzi huu bila kutegemea bajeti ya hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango huo tulianzisha kitu pale Wizarani, kinatiwa *Tanzania Police Public Safety Trust Fund. Public Safety Trust Fund,* nia yake ni kukusanya fedha kwa kushirikiana na wanajamii na wafanyabiashara wakubwa na wadogo na wananchi kwa ujumla ili pesa hizi tukizipata tuweze kujenga Ofisi na nyumba za watumishi na Askari. *(Makofi)*

Sasa mfuko huu tumeshauanzisha, Bodi yake imekwishazinduliwa, tunachotaka kufanya sasa ni kuanza kazi hii ya kufanya *fund raising* kutafuta hizi fedha ili tuweze kupata pa kuanzia kujenga nyumba hizi. Nataka baadaye niongee na Waziri Mwenza, au Waziri Kivuli tuone kama tunaweza tukaanzia zoezi hili mjini Arusha pale ili tukusanye pale pesa nyingi tuanze kujenga nyumba pale Kisongo kwa ajili ya Askari wetu ambao hawa nyumba pale Arusha. *(Makofi)*

Baada ya Arusha tutarudi Dar es Salaam, tutakwenda Mbeya, Mwanza na sehemu nyingine, lakini tunaamini kabisa kwa mpango huu mafanikio yatakuwa ni makubwa zaidi kuliko tukisema tusubiri kila siku tupate pesa kutoka Hazina. Tumeona hatukupata mwaka 2013, tumeona hatukupata mwaka 2012, kwa hiyo, ubunifu wetu ni huo na tutaanza zoezi hili mara tukimaliza tu bajeti hii. Tutaanza kuzunguka katika Mikoa mbalimbali ili tuweze kukusanya pesa kwa wadau ambazo zitatusaidia katika kujenga nyumba za Askari. *(Makofi)*

Tumekubaliana Bodi yetu ile ina watu mahiri, watu wa *private sector,* Mwenyekiti wetu anaitwa Bwana Ali Mafuruki na wamo mle, akina Mzee Bakhresa, Wajumbe wa Bodi ile. Kwa hiyo, tuna hakika kabisa tukikaa vizuri tukijipanga tunaweza tukaondoa tatizo hili la nyumba na Ofisi chakavu na nyumba chakavu ambazo Mheshimiwa Azzan amezizungumzia pale Magomeni ambazo Askari wetu wanaishi.

Kuhusiana na hilo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Azzan kwamba niko tayari kwenda naye Mara tu tukimaliza bajeti hii, twende pale Magomeni napajua, nazijua zile nyumba na mimi bahati nzuri nimekulia katika mji huu, nazifahamu sana zilivyo, sizipendi; tutafanya mipango ili angalau basi kupitia mfuko huu *Tanzania Pulic Safety Trust Fund*, tubadilishe hali ya pale Magomeni iwe nzuri zaidi na nimwombe ndugu yangu aachane na lile wazo lake la kutoa Shilingi katika mfumo huu. Mipango tunayo na hii mipango ni ya uhakika zaidi kuliko mingine ambayo tumewahi kuitoa huko nyuma. *(Makofi)*

Nizungumzie sasa suala la usalama barabarani. Katika kipindi cha mwaka uliopita wa fedha na hivi karibuni, zimetokea ajali nyingi sana ambazo zimewajeruhi ndugu zetu na zimeua ndugu zetu wengi na kuharibu mali nyingi sana za raia wetu. Sasa jambo hili linatutekela, jambo

hili kwetu tunalipa kipaumbele sana, tunaona kwa kweli haiwezekani raia wetu wakawa wanaumizwa sana na ajali hizi na sababu kubwa za ajili hizi ukitazama sana ni mwendo kasi na uzembe wa madereva; wakati mwingine magari yenyewe yanayotumika pia ni mabovu, lakini pia hata alama za barabarani zinazowekwa na *TANROADS* kuna watu wanazitoa. Kwa hiyo, ukosefu wa alama hizi pia unasababisha ajali hizi na vifo na majeruhi, wananchi wetu wanapata matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakusudia kufanya nini ili kuondoa tatizo hili? *Of course* lipo pia tatizo la rushwa. Lilisemwa tatizo la rushwa, nami mwenyewe nimewahi kulishuhudia barabarani. Kwa hiyo, nasi kama Polisi tumeanzisha operesheni ambayo sasa tunawadhibiti wale Polisi wa barabarani wanaojihusisha na rushwa, tumewakamata wengi, tumewafukuza kazi, waliopata bahati sana wamebadilishwa vitengo, lakini wengi tumewafukuza baada ya kuwakamata. Tumetumia Polisi kufanya kazi hii na tutaendelea nayo.

Nichukue nafasi kuwaonya wale Polisi wa Usalama Barabarani waache tabia hiyo, maana sasa tuko nao na tutawakamata na tutawafukuza wale ambao wanajihusisha na rushwa kwa sababu vitendo vyao vya rushwa vimesababisha pia ajali hizi zikatokea. Wameruhusu magari mabovu yakaenda, wameruhusu madereva walevi wakapita kwa sababu wametoa rushwa, mambo haya yamekwenda baadaye yakaleteleza ajali ambazo zimesababisha vifo na majeruhi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala hili Askari Polisi wa Usalama Barabarani wanalijua na mimi nataka kuwahakikishia tuko macho, tutakuwa wakali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie leo ambalo pia Waheshimiwa Wabunge mmelizungumzia ni suala la wananchi kuchukua sheria mikononi. Kuchukua sheria mikononi maana yake ni kutoa adhabu kwa watuhumiwa bila kufuata sheria. Jambo hili ni baya, tumelisemea, tumelikemea, tunawaomba wananchi, tunawaomba sana watakapomkamata mtu au watakapomshuku mtu kwamba amefanya kosa fulani au amevunja sheria, wamchukue mtu Yule, wampeleke kwenye vyombo vya sheria.

Najua wapo wanaosema kwamba tukimpeleka Polisi leo, kesho tunamwona anatoka. Hawezi kutoka kama haijazingatiwa sheria. Anapokamatwa mtu, sheria zetu zinasema mtu huyu hana hatia mpaka pale Mahakama itakapomwona ana hatia. Kwa hiyo, kumwachia huru, Polisi wanapompa *bail* mtuhumiwa. Ni haki yake. Dhamana ni haki ya kila mtuhumiwa anapokamatwa.

Kwa hiyo, anapokamatwa mtu mkampeleka Polisi kisha mkamwona baadaye anatembea Mtaani ni kwamba ametimiza masharti ya dhamana na amepewa, wala siyo rushwa, wala siyo uvunjaji wa sheria. Wananchi tuwe wavumilivu mpaka mtuhumiwa huyo atakapopelekwa Mahakamani na hatua za kisheria zikachuliwa dhidi yake. *(Makofi)*

Naomba niwaase na kuwaomba wananchi tuache kufanya vitendo hivi vya kuvunja sheria kwa kuwahukumu watu Mitaani na huko barabarani. Nimeona mwenyewe kwa macho yangu watu wakifanya vitendo vya kikatili kabisa kwa mtu ambaye ameiba simu, wanampiga mpaka wanamuua wanamchoma moto. Kwa mtu ambaye ameiba mfukoni kwenye daladala, wanampiga mpaka wanamuua. Hivi ni vitendo ambavyo havifai katika jamii yetu, tuzingatia sheria. Tumkamate mtu huyo, tumpeleke Kituo cha Polisi, atachukuliwa hatua za kisheria kama inavyopaswa. *(Makofi)*

Tatizo lingine kubwa ambalo limezungumziwa hapa ni dawa za kulevya, nami nimelizungumza katika hotuba yangu ya jana. Tunalo tatizo kubwa la dawa za kulevya, dawa za viwandani na dawa hizi za mashambani kama bangi na mirungi. Kikosi cha Polisi

kinapambana na tatizo hili sana. Lakini nanyi mtakubali kama ni tatizo kubwa na limekuwa linakuwa kwa sababu lina sura ya Kimataifa.

Bangi zinazolimwa Musoma zinauzwa Kenya. Wakati mwingine inafanywa *contract farming* kabisa. Inatolewa *order* kule, limeni, hela zinatolewa, watu wanalima wanapeleka Kenya. Sasa katika hali hiyo, mapambano yanakuwa ni makubwa; na kwa sababu ni biashara ambayo ina pesa nyingi, suala la rushwa pia halikosekani. Lakini niseme tuna vikosi imara vinapambana sana tena sana katika kuzuia madawa haya ya kulevya. *(Makofi)*

Sasa tatizo la dawa za kulevya Tanzania na duniani linafanana kabisa na tatizo la biashara haramu ya binadamu ambayo inafanyika. Biashara hii inafanyika ndani na nje ya nchi hii.

Waheshimiwa Wabunge, mmechangia hapa, mmeleta kwamba wapo wasichana wadogo wanatolewa Tanzania wanapelekwa China. Wakifika kule Guazhou kazi yao ni kufanya biashara ya miili na hawajifanyii wao wenyewe, wanawafanyia watu. Jeshi la Polisi linafahamu, sasa hivi tumeunasa mtandao huu.

Kama mlivyosikia hata kule China walishawakamata; nasi hapa tunawakamata. Walichofanya, wanakuja hapa wanawarubuni wasichana wanawaambia twende Guang zhou mimi nina *salon* yangu au nina duka langu twende ukauze kule. Sasa msichana kwa kurubuniwa hivyo, anakubali. Akienda kule ananyang'anywa kwanza *passport* na yule mama. Anaitwa mama, huyo mama anamnyang'anya *passport;* anamwambia sasa ukitaka *passport* yako hii, kila siku uniletee; mpaka utakapotimiza kuniletea Dola 8,000 mpaka 10,000 ndipo nitakapokupa *passport* yako.

Sasa wasichana hawa wanalazimishwa kufanya biashara hiyo ya ngono ili kupata hizo pesa wamrejeshee huyu mama awalipe. Wanaposhindwa, wanakutana kule na jamaa wengine wa Nigeria. Wale yame-*specialize* kwenye biashara za dawa za kulevya. Anapewa *passport* bandia ya nchi nyingine anaanza kuzunguka huko akipeleka dawa za kulevya huku na huku na malipo yake vilevile ni ya hati hati.

Wapo ambao wamekufa katika biashara hii, tunafahamu. Ndiyo maana Jeshi la Polisi limechukua jambo hili kwa makini sana na mtandao huu sasa tumeunasa, na tunauvunja.

Niseme tu, juzi kuamkia jana tumemkamata mwingine Dar es Salaam anajaribu kwenda kumpatia *passport* binti ambaye akiulizwa wewe binti unajua unakwenda wapi? Anasema, sijui. Napewa *passport*, halafu nitapewa tiketi, nitasafiri. Basi, ndiyo anachojua.

Sasa mtandao ni huo. Biashara hii ni mbaya na inafanywa na sisi. Sisi wenyewe ndio tunaifanya biashara hii, tunapeleka vijana wetu huko nje na sasa nasikia kuna hata Wakala wanafanya biashara hii kabisa, kwamba tutakutafutia kazi mahali na kumbe siyo hivyo. Polisi inafahamu na iko makini na tunapambana na biashara hii.

Pamoja na biashara hii, ipo pia biashara ya wahamiaji haramu. Hii nayo tumeinasa na hasa kule Moshi. Nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa kule Moshi amboa wao wenyewe wanajitolea kutoa taarifa kusema nani anahusika na biashara ya kupitisha wahamiaji haramu kuingia katika nchi yetu. Wapo hao, lakini wapo pia na wale wa kule Kagera ambao Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema hapa kwamba wameanza kurudi.

Ni kweli lakini na sisi Jeshi letu la Polisi na uhamiaji wako macho kuwadhibiti ili wasirudi ili tukabiliane, tupambane kwa umakini zaidi na biashara hii ya uhamiaji haramu. Nayo ni

biashara. Wananiambia karibu kila kichwa unafika mpaka dola 1,500 kumpitisha Tanzania, kumpeleka Malawi, ama nchi ya jirani. Kwa hiyo, ni biashara ambayo ina pesa. Kwa hiyo, biashara ambazo zina pesa namna hii utakuta watu wengi sana wanaziingilia na wanatuletea matatizo. Lakini sisi kama Jeshi la Polisi ambalo jukumu tu ni kulinda usalama wa raia na mali zao tunaendelea kupambana nao.

Lipo suala vitambulisho vya Taifa, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa Mheshimiwa Silima amelizungumza vizuri sana, vitambulisho hivi vitatolewa kwa kila mtu aliyeko Tanzania. Vitatolewa kwa Watanzania vitatolewa kwa Wageni, vitatolewa kwa wakimbizi na vitatolewa kwa kila mtu. Hii ni kwa sababu ya usalama tu, tutakupa tukujue wewe ni nani. Kwa hiyo, hakuna atakayekosa kitambulisho.

Kwa sasa tumechukua takwimu za watu katika maeneo fulani fulani tu Dar es Salaam, Pemba na Ugunja, lakini hatujakamilisha kuwapa. Wote watapata. Kila tunapopita, tunaacha kituo. Kama hukupata katika mkumbo huu wa jumla, basi utaenda taratibu, utachukua cha kwako. Lakini lazima wote watapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisikia Mheshimiwa Mbunge akilalamika kwamba kuna watu wamekosa, labda wamekosa kwa mkupuo huu, lakini watapata. Sheikh Khatib, watapata! Wale wanaotoka Shimoni pia watapata, lakini wataandikwa, huyu ni Mkenya. Hatutampa akasema mimi ni Mtanzania, hapana. Tutasema tutasema huyu anaishi kwetu, lakini ni Mkenya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutaweka Ofisi kila Wilaya kwa sababu zoezi hili ni endelevu. Ombi langu sasa, kila mtu anayekwenda kuomba kitambulisho awe na vile vielelezo sahihi kwa ajili ya utambuzi, ni muhimu sana. Akikosa vyote hivyo, ndiyo pale tunapomwomba Mwenyekiti wa Mtaa akutambue au Sheha akutambue. Lakini vitambulisho vingi sana vya kujitambulisha kama wewe ni raia ama ni mtu wa mahali popote pale, ama ni mkazi, ama wewe ni mgeni, vipo vitambulisho vingi unaweza ukavitoa pale ili uweze kutambulika wewe ni nani, utaandikishwa *accordingly*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishakamilisha zoezi hili, huu utakuwa ndiyo mfumo mama katika nchi nzima wa utambuzi wa raia wote na utatumiwa na vyombo vingine vyote kwa ajili ya usalama wa nchi yetu, kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu na mipango na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuahidi kama nilivyosema, sitaweza kujibu yote, lakini tutayajibu haya, tutaandika na tutawagawia Wabunge wote. Yote mliyoyasema, tutayajibu, tutawagawia kwa ajili ya kumbukumbu za baadaye.

Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru makamanda wote wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Uhamiaji, Zimamoto, Magereza na Wakurugenzi katika Ofisi yangu, lakini sana sana nichukue nafasi hii kumshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yangu ambao wamenipokea na kunipa miongozo mizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo mwisho kwa umuhimu ni Naibu Waziri wangu. Huyu wala siyo Naibu Waziri wangu, ni Waziri mwenzangu, tunafanya kazi vizuri sana, ni hazina kubwa kwangu, ananielekeza; sina kitu ambacho nimefika pale nikakosa kukipata kutoka kwake. Kwa hiyo, namshukuru sana. Tutaendelea kufanya kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Lema, Waziri mwenza kwamba kituo changu cha kwanza ni Arusha, tufanye kazi tujenge nyumba za Askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI: :** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mathias Chikawe kwa ufafanuzi. Kwa hakika kwa muda tuliokupa usingeweza kufafanua hoja zote zilizotolewa. Kwa hatua hiyo, tunakushukuru sana. Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**MWENYEKITI:** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, natumaini Waheshimiwa sisi sote tuko pamoja, kitabu cha pili. Endelea Katibu!

Kif. 3001 - *Fire and Rescue Services* ......Tshs. 15,716,234,870/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Wizara kasma 220500 - *Military Supplies and Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ndicho ambacho kina kasma vilevile ya *operation* za ukaguzi maalum na ufuatiliaji wa tahadhari dhidi ya majanga na moto. Kumekuwa na kujirudia rudia kidogo kwa matatizo haya ya majanga na moto na Zimamoto kushindwa kuchukua hatua kwa wakati. Sasa kiwango cha rasilimali kinaashiria vilevile nguvu ya kufanya hii kazi ya *operation* ya ukaguzi.

Mwaka 2012/2013, walitengewa Sh. 848,000,000/=, mwaka 2013 walitengewa Sh. 241,000,000/= na mwaka huu, 2014 wametengewa Sh. 200,000,000/=.

Kwa hiyo, maana yake kila mwaka kiwango cha fedha kwa ajili *operation* hizi maalum za ukaguzi kwa tahadhari dhidi ya majanga na moto kinazidi kupungua. Ningependa kupata ufafanuzi ni kwa nini wakati ambapo majanga yanaongezeka, matukio ya moto yanaongezeka, kiwango cha tahadhali kinapungua?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki bado hakijapungua. Kimepungua kwa sababu hapa ni Makao Makuu, lakini tumesambaza Mikoani ambako hakuna fedha kwa ajili hiyo, na hivyo wataendelea kufanyia kazi. Kifungu hiki kimeongezeka *in fact*.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inasimama katika kifungu 220600 ambapo hapa hoja ni ile ile kwamba, kiwango cha pesa hapa kimepungua wakati naona kuna vifaa vya kununua. Mavazi yale yanayohusika katika suala zima la uokoaji; japokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hapa kwamba hapa ni Makao Makuu, lakini nina

imani kwamba endapo vile vifaa vinapatikana Makao Makuu, maana yake vitaweza kuwa *supplied* katika sehemu mbalimbali.

Sasa kwa nini pesa imepungua kiasi kwamba hata ukifanya *comparison;* na miaka mingine tunajua kwamba Makao Makuu pesa zinapatikana na *Centre* za kazi pesa zinapatikana. Sasa kwa nini hii *figure* inaonekana inashuka kwa kasi zaidi na tuangalia majanga yanakuwa ni hali ya hatari katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Pamoja na ukweli kwamba tumefanya ugatuaji, lakini bajeti pia ndiyo inayo-*determine,* nani apate kiasi gani? *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Fire & Rescue Services*
*Training Isnt*. ............................ Tshs. 2,118,330,000/=

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo Katibu, naona kuna Wabunge watatu wamesimama. Kuna Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Rukia na Mheshimiwa Machali.

Natumaini yale maswali ya kusema kwa nini fungu fulani limepungua, majibu yake yamekwishapatika. Kwa sehemu kubwa majibu yake ni yale yale! Natumaini maswali yatakuwa ni mengine, siyo kwa nini kuna tofauti ya upungufu ambao siyo mkubwa kiasi hicho. Mheshimiwa Rukia!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ikubaliani na wewe kwamba ikiwa kifungu kimepungua, ukasema majibu yatakuwa ni yale yale, haiwezekani. Niko kwenye kasma 220800 - *Training Domestic*. Mwaka uliopita kulikuwa na Sh. 747,656,000/= na sasa hivi kuna Sh. 492,800,000/=, upungufu ni mkubwa muno. Ni kwa nini wakati kila siku majanga yanaendelea kutokea? Hebu naomba ufafanuzi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba jibu jipya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jibu jipya, ni bajeti. Tulilazimika tupunguze baadhi ya maeneo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Rukia, mimi naamini katika baadhi ya mambo tuelewane tu. Lakini ukitaka kujifurahisha, mtu asimame ili apate jibu lile lile, nayo inaruhusiwa vile vile. Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza kwenye ile *item* namba 410400 - *Acquisition of specialized equipments.* Naona zimetengwa Sh. 35,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu nafikiri labda pengine kifungu hiki kinaweza kuwa kinahusika na hizo *specialized equipments* labda ni vitu kama magari ya Zimamoto. Nimekuwa nikihoji hapa, hata mwaka 2013 nimehoji. Ukija kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ni kwamba tuna matatizo, tulikuwa tunahitaji pengine kuwa na vifaa kama hivi vya Zimamoto na wananchi wamepata wakati fulani wakachangishwa pesa ikaleta kidogo hali ambayo kama vurugu fulani, hawakufurahishwa na kitu kile. Wakati huduma za Zimamoto hazipo katika Wilaya ya Kasulu.

Sasa nilikuwa naomba pengine kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hizi fedha ambanzo zimetengwa hapa na nimejaribu kwenda kwenye *vote* nyingine ya Kigoma kule mbele, sijaona fedha ambazo pengine zimetengwa kwa ajili uwezekano wa kupata vitu kama magari ili kusudi zinapotokea ajali za moto, wananchi wale waweze kuokoa rasilimali zao. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na kifungu hiki ambacho pengine inaona kina fedha kidogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, kabla hajajibu, katika kufahamiana tu ili kufafanua vizuri, si unaona kichwa cha habari pale juu? Kinahusu *training institute*.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ume-*withdraw*?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri tu kwamba, kwa kuwa kuna ile wiki ya majumuisho kati ya Serikali na Wizara, kuna maeneo ambayo kwa kweli ni nyeti. Hiki ni Chuo cha Zimamoto na Uokoaji na Chuo chenyewe kabisa kimeshauri kwamba, kitendo cha kupunguziwa fedha kwa kiwango kikubwa kitakuwa na athari katika ufanisi na weledi wa masuala ya Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tunaweza tukaliacha, lakini ni vizuri katika ile wiki ya majumuisho, mambo kama haya yakatafakariwa ili Bunge hili lisiwe *rubber stamp* tu ya kupitisha kila kitu, tusaidie Taasisi zetu. Ni hilo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa ushauri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3003 - *Fire Safety* .....................................Tshs. 708,970,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab peke yake.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu naielekeza kwenye kasma namba 410400 - *Acquisition of Specialized Equipment*. Nimeona hapa fedha iliyotengwa kwa ajili ya manunuzi ya hivyo vifaa muhimu ni kiasi cha Sh. 2,500,000/= kwa mwaka wa fedha huu 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kasi ya maendeleo katika nchi yetu inakuwa sana na hasa nazungumzia katika suala la majengo. Tuna majengo mengi, magorofa mengi sana yanajengwa hasa kwenye maeneo ya Miji, kwa mfano pale Dar es Salaam; ikitokea dharura ya moto pale nina uhakika uwezo wa Zimamoto hauwezi kuhimili ile aina ya majengo ambayo yanajengwa hivi sasa, hasa ukilinganisha na hiki kiwango cha hii Sh. 2,500,000/= ya kununua hivyo vifaa vinavyoitwa *Specialized Equipments*. Sasa nilitaka kujua, Serikali ina mpango gani katika kuliangalia hilo, kwamba kuna ukubwa wa haya majengo ambayo kwa sasa nina uhakika *fire* haiwezi kuyahimili na wakati huo huo hapa inaonyesha *specialized equipment* fungu lake ni kiasi kidogo sana. Nitashukuru kama nitapata majibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi; Fungu dogo!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni pesa ambazo pengine zitanunua nyongeza ndogo sana katika vifaa hivi. Vifaa anavyosema Mheshimiwa Mbunge hasa gari la masafa marefu kwenda juu tunalo moja Dar es Salaam ambalo linaweza likafika sehemu ya majengo marefu. Hatupendekezi sana kujenga majengo marefu bila kufikiria kwamba moto utatokea. Pale ambapo linafika ni ghorofa 18. Sasa hivi kuna 36 na kwenda juu. Kule juu tunawaagiza wajenzi pamoja na wamiliki wahakikishe kwamba wanaweka *detectors* zile ambazo ni *automatic (sprinklers)* ambazo kama moto ukitokea hata kama mkonga haukufika zinaweza kusaidia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kabla Katibu hajaendelea, niseme tu kwamba watu wa *Fire* walituletea gari la Zimamoto kabisa hapa katika viwanja vyetu vya Bunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuona aina ya vifaa walivyonavyo. Lilikuwa gari la uhakika. Natumaini wengi mmeliona. Kwa hiyo, leo msiwe na wasiwasi wa moto hapa! Katibu tuendelee!

Kif. 3004 - *Operations* .................................. *Tshs*. 658,920,000/=

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika fungu hili subvote 230400 inazungumzia *routine maintenance and repair of vehicle and transportation equipment*. Hakuna hela yoyote. sasa hivyo vifaa mlivyoweka hapa, mwaka mzima huu hakuna chochote kitakachofanyika, pamoja na gari hili kutuletea? Ehe, haliharibiki hilo? Kwa nini hili fungu halina kitu?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi! Kwa nini hakuna fedha iliyotengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii imetengwa Makao Makuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sasa hapa ndipo swali langu lina-*qualify*; kutokana na nilivyokuwa najaribu kupitia randama ukurasa ule wa 35, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi wa Serikali, inatoa kauli gani juu ya upatikanaji wa magari kwenye maeneo ambayo tayari yamepata kuwa *affected,* watu wameunguliwa na majumba yao na tayari Jeshi la Zimamoto kuna wakati waliingia kule wakawa wanatoza watu fedha hasa wafanyabiashara lakini hakuna huduma za Zimamoto ambazo tunapata katika Mji wetu wa Kasulu.

Nilikuwa naomba kauli ya Serikali, inazungumza nini sasa pengine juu ya kuweza kupatikana kwa gari la Zimamoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, ili kutusaidia, sijui uko kwenye kifungu gani mwenzetu ili Waheshimiwa Wabunge wote waweze kufuatilia.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *sub-vote* 410400 - *acquisition of specialized equipments.* Ukisoma kwenye randama, inazungumzia kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kununulia vifaa mbalimbali vya kuzimia moto.

**MWENYEKITI:** Lakini ni kwa ajili ya *operations*. Kuna *operation* huko Kasulu? Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi wa swali la Mheshimiwa Moses Machali!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba nchi yote inakuwa *covered* na huduma za Zimamoto. Anaposema Mheshimiwa Machali hajapata huduma, nashangaa kwa sababu ukaguzi na elimu ni sehemu ya huduma muhimu kuliko hata kuzima moto. Huduma hiyo ya kwanza akipata, hahitaji gari pengine kwa sababu tayari ana elimu ya kujikinga.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3005 - *Dar es Salaam Regional Office*.. Tshs. 352,945,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3006 - *Arusha Regional Office*............. Tshs. 343,814,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Kivuli.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina *interest* kwa sababu ni Mkoa wa Arusha, kwamba katika kifungu 221200 - *Communication and Information,* mwaka 2012/2013 walitengewa Sh. 21,000,000/= lakini mwaka huu wa fedha wametengewa Sh. 4,000,000/=. Nilikuwa nataka kujua ni kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe! Ilikuwa milioni sita, sasa ni milioni nne!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba vitu hivi tulipata vingine mwaka 2013 na mwaka huu tunaongezea tu. siyo kama tunaanza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3007 - *Dodoma Regional Office* .......... Tshs. 238,904,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3008 *Mwanza Regional Office*...............Tshs. 388,506,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwia.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye *subvote 3008* kifungu kidogo cha *medical supplies* na 220400.

**MWENYEKITI:** Naomba usogeze *microphone* karibu na wewe ili tukusikie.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Kifungu kidogo cha *medical supplies and services* mwaka 2012/2013 walitengewa Shilingi milioni 14, mwaka 2013/2014 hawakutengewa kiasi chochote na mwaka 2014/2015 hakuna kiasi ambacho kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinanunua madawa ya kuzimia moto pamoja na madawa ya kuhudumia wagonjwa hasa wa *AIDS*. Kwa uchumi tumeamua tutumie *economies of scale* tununue Makao Makuu, halafu tuwapelekee.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Hiyo inajibu kwa Mikoa yote mingine yenye *zero zero*. Tuendelee Katibu!

Kif. 3009 - *Mbeya Regional Office* .............Tshs. 306,143,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3010-*Kinondoni Regional Office…Tshs.368, 145, 000/=*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu Zimamoto Mkoa wa Kinondoni, ningependa kupata ufafanuzi kwenye kasma ya 210300, *personal allowances-(Non-Discretionally),* hiki ni kifungu kinachohusu posho muhimu kwa Askari hawa wa Zimamoto. Kumekuwepo na malalamiko sana kuhusiana na viwango wanavyolipwa na vilevile hata malipo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko nimeshangaa kwamba kiwango hiki kimepungua toka shilingi milioni 96 na kushuka mpaka shilingi milioni 80. Natambua kwamba ufinyu wa bajeti haiwezi kuwa sababu kwa sababu posho za muhimu huwa zinakuwa *first charges* katika malipo kwenye utumishi wa umma. Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi, ni kwa nini kiwango hiki kimeshuka, idadi ya watumishi imeshuka au ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi katika maeneo ya Dar es Salaam, wameondolewa waende Mikoa iliyoanzishwa na Mikoa mingine.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3011-*Mara Regional Office……………Tshs. 198,521, 000/=*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili linahusu Mkoa wa Mara, mimi kama mdau, kasma 229900, inayohusu *other operating expenses*, kwa nini ni sifuri, kwa nini hakuna kitu pal? Nilitaka nipate ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaitwa *other* kwa sababu kama unaihitaji. Kwa maana hiyo ni kwamba kasma nyingine zimepewa fedha za kufaa ili hii isitumike.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3012-*Kigoma Regional Office…Tshs. 193,935, 000/=*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3013- *Pwani Regional Office…Tshs. 274,080, 000/=*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 230100, *routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment.* Ukiangalia miaka ya nyuma kulikuwa na fedha nyingi zaidi za *repair*, ina maana vifaa hivi ikiwepo pamoja na magari, sasa hivi kwa Mkoa wa Pwani yamekuwa mazuri zaidi na mapya kiasi ambacho fedha kwa mwaka huu zimepungua sana kutoka kwenye shilingi milioni 60 mwaka jana mpaka kufika shilingi milioni 28? Nataka ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo hali halisi ya kibajeti.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Nilishasema tangu mapema, jamani maswali haya ya kupunguapungua haya, hebu tuyaepuke kidogo na mkitaka kuufikia mshahara wa Waziri, kama mtakavyoona, vipengele ni vingi vitakavyoweza kuchukua muda wetu, tusipovumiliana hatufiki huko. Katibu!

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3014- *Manyara Regional Office…Tshs. 200,335, 000/=*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3015-*Geita Regional Office…Tshs. 167,132,000/=*

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kasma ya 210300, Mkoa huu ni mpya ambapo mwaka jana tulitengewa shilingi milioni 40 lakini mwaka huu zimepungua na ni sehemu ya mishahara. Je, hawa watu kwa nini wanapunguziwa mshahara, ni kwamba watumishi wanapungua au nini kimetokea? Nahitaji maelezo katika hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania haina utamaduni wa kumpunguzia mtu mshahara. Kwa hiyo, hili ni suala la idadi ya wafanyakazi ambao wako pale, ni kwamba wengine wamehamishwa na ndiyo sababu, hakuna lingine.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3016-*Temeke Regional Office…..........Tshs. 382,947,000/=*
Kif. 3017-*Singida Regional Office….............Tshs. 195,549,000/=*
Kif. 3018-*Tabora Regional Office…............Tshs. 248,225,000/=*
Kif. 3019-*Iringa Regional Office…..............Tshs. 216,915,000/=*

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3020-*Rukwa Regional Office…..............Tshs. 184,173,000/=*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, niko kifungu 220100, *office and general supplies and services*. Katika Mkoa wa Rukwa, kifungu hiki kimekuwa kikpungua lakini kuna miji inachipua. Mji wa Namanyere unachipua, mji wa Laila unachipua, mji wa Matai unachipua na watu wa Zimamoto wanakusanya maeneo hayo. Sasa badala waongeze ili wafungue ofisi huko ambako miji inakua, inahitaji huduma hii muhimu lakini kifungu kinazidi kupungua. Naitaka Serikali iongeze kifungu hapa, kuna maelezo gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vifaa ambavyo anazungumzia vya ofisi, tunaweza kuwa tumenunua mwaka jana na mwaka huu tusihitaji chochote. Kwa hiyo, bado tuna fedha za kununulia na ashukuru kwamba tunaendea kuifanyia kazi, tutakapopata fedha zaidi, Namanyere nako tutapeleka.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3021-*Ruvuma Regional Office…...........Tshs. 219,406,000/=*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3022-*Kagera Regional Office….............Tshs. 220,715,000/=*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa nina jambo moja tu, nataka tu ulingalishe na nije niulize. Ukiangalia katika *subvote* 3021, ukaangalia nyingine 3022, ukaangalia ile ndogo ya 220400 ya Ruvuma na ya Kagera, vinafanana, 221000 ya Kagera na ya Ruvuma zinafanana. Sijui walikuwa wanagawa kwa watu kuleta au wanabunia tu wanaweka. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuangalia ukubwa wa Kagera na ukubwa wa Ruvuma, ni vitu viwili tofauti na katika ku-*set* malipo mengi, ili tusipoteze muda, unaona vyote vinafanana kwa kupewa kifungu sawasawa na fedha ni ileile. Ndiyo utaratibu au ni kwa sababu ndio kiasi kilichopo? Ningependa tu kuelewa, Ruvuma na Kagera, vifungu vyote viko sawasawa ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi hapa huwa tunazungumza tugawane sawa, lakini hapa pengine vile vitendea kazi na wafanyakazi ndiyo vinavyofanana lakini siyo ukubwa wa eneo, naomba kuwasilisha. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kile kifungu kidogo cha 230700, *routine maintenance and repair of office equipment and appliances.* Ukiangalia kadri miaka inavyofuatana kiasi hiki cha fedha kimezidi kushuka sana mpaka mwaka huu wamepata tengeo la shilingi laki nane. Hivi tengeo la shilingi laki nane kwa Mkoa mzima wa Kagera, fedha hii wanakusudia ikafanye nini? Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinajieleza kwamba kazi yake ni kutengeneza vifaa vya ofisi pale ambapo vina matatizo. Ni kweli kwamba Kagera imeendelea kupungua, lakini pia ukitazama kwingine utaona kunafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, wakati tunahitaji huduma hizi zaidi, bado bajeti inapungua zaidi na hiki ndiyo Waheshimiwa Wabunge walikisemea wakati wanachangia. Nawakumbusha na hapa wakikumbuke tena.

**MWENYEKITI:** Wamesahau! *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3023-*Mtwara Regional Office…............Tshs.232, 837,000/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa, Mheshimiwa Murji, Mheshimiwa Haroub samahani, kofia mlizovaa leo zimefanana.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niko katika *subvote 220800, Training-Domestic.* Nikiangalia katika kifungu hiki katika *subvotes* zilizotangulia, walikuwa wametengewa fedha kidogo za mafunzo lakini kule kwa Wajomba zangu Mtwara naona tangu mwaka jana hawajatengewa chochote. Nataka ufafanuzi kwamba wao wameshahitimu mafunzo na hawahitaji tena au vipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji ni hilohilo?

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, ni lingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi kwanza, anasema *training* inazidi kupungua, hakuna kabisa safari hii, hafunzwi mtu huko?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kwanza *effect* yake ya mwanzo inaweza ikawa ni bajeti lakini uamuzi au mipango ya kila Mkoa mara hii tutafundisha ndani au nje, wangapi ndiyo kinachoamua ukubwa wa kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Murji.

**MHE. HASNAIN MOHAMED MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mimi niko kweye *subvote* 220300, inahusu mafuta. Mwaka jana fedha zilitengwa Sh.32,800,000 na lakini mwaka huu naona imetengwa Sh.25,000,000, lakini tuna changamoto nyingi Mtwara, lakini pia magari mengi na vitu vingi vya vyombo vinavyotumia mafuta vimeongezeka. Nilitaka kujua kuna sababu gani ya kupunguza fedha hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, inatakiwa sababu mpya.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua haiwezi kutokea. *(Kicheko)*

Tatizo hapa ni bajeti lakini labda niseme kitu kimoja, Mtwara hawana fedha za kutosha mafuta, Manyara hawana fedha za kutosha za mafuta, tatizo hilo likitokea bado Makao Makuu ipo. Wale ambao watatumia fungu lao na wakwame, hawataachwa kwa sababu ni Mkoa, Makao Makuu itaangalia nini kifanyike.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3024-*Lindi Regional Office*……..............*Tshs. 206, 265,000/=*
Kif. 3025-*Njombe Regional Office*…............*Tshs. 179,649,000/=*
Kif. 3026-*Shinyanga Regional Office*….......*Tshs. 269, 475,000/=*
Kif. 3027-*Ilala Regional Office*…..................*Tshs. 405,478,130/=*
Kif. 3028-*Kilimanjaro Regional Office*…......*Tshs. 306, 951,000/=*

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3029 - *Morogoro Regional Office*……..............Tshs.275,554,000

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba unasema tusirudie, mimi niko 230400, kuhusu *maintenance and repair of vehicles and transportation equipment,* Mkoa wa Morogoro. Kama unavyoona Mkoa wa Morogoro ni Mkoa mkubwa nchini Tanzania na miundombinu yake ni mibaya, lakini mwaka jana Sh.60,000,000, mwaka huu mpaka Sh.30,000,000! Huu Mkoa mmeshaupunguza, mmeukata au bado uleule ninaoufahamu mimi? Ingawaje anasema iko Makao Makuu, kwa nini msiwawekee hapa na miundombinu yote Morogoro imeharibika? Kila Wilaya sasa hivi inakua, hawa Mkoani watafika vipi kwenye hayo maeneo? Tafadhali, hiki kifungu hapa, ndiyo maana tumesema hii bajeti tusiipitishe, tuikwamishe ili wakaongeze fedha!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe jibu jipya sasa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba bajeti hii ya Zimamoto imepungua. Mwaka jana walikuwa wana-*retain 70%,* mara hii wana *retain 49*. Hatuwezi tukafanya za mwaka jana zilingane na mwaka huu au ziongezeke, *unless* Bunge hili lifanye uamuzi tuongezewe irudi *70%. (Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3030-*Katavi Regional Office*…..............*Tshs. 223,425,000/=*
Kif. 3031-*Tanga Regional Office*…..............*Tshs. 323,509,000/=*
Kif. 3032-*Simiyu Regional Office*…...............*Tshs. 177,387,000/=*

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Tusonge mbele.

**Fungu 28 - Jeshi la Polisi**

**MWENYEKITI:** Haya, sasa Jeshi la Polisi, kwa Mikoa vilevile. Twende Katibu!

Kif. 1002-*Finance and Accounting*….......*Tshs.* 2,327,966,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2001-*Police Enforcement*…............*Tshs.*131,174,380,106/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 210300, *Personal Allowances-(Non-Discretionally),* ambalo ndilo fungu la posho mbalimbali. Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, alieleza kwamba jambo hili la nyongeza ya posho wamelipeleka kwa Serikali na liko katika hatua ya mwisho na mimi naamini Serikali ni moja. Hili fungu hapa limeongezeka kutoka Sh.77,000,000,000 mpaka Sh.80,000,000,000. Sasa yale maombi ya nyongeza ambayo Wizara hii imeomba, tungependa kupata kauli ya Serikali kwa maana ya Wizara ya Fedha, je, wamekwishayakubali au majadiliano yanaendelea, ili tuelewe tunapopitisha hivi, tujue mambo mengine yamekwamia wapi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU N. L. MADELU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pamoja na Wizara mbalimbali inaendelea na majadiliano lakini tunachojaribu kukifanya na ambacho ningewaomba Wabunge wazingatie, katika bajeti inayofuata tunajitahidi sana kuwa *realistic*, kuliko tu kuahidi kupandisha hiki na hiki, halafu kisije kikatekelezeka. Kwa hiyo, tunajitahidi kuhamasisha mapato na tunajitahidi kuwa *realistic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2002-*Police Marine*…........................Tshs. 1,540,915,600/=

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tunazungumzia *Police Marine* na tumezungumzia sana suala la uhalifu kwenye maziwa yetu, Viktoria, Tanganyika na mengine mpaka Jipe. Sasa nikiangalia ile kasma ya 220300 inayohusu mafuta, naona kiwango

kinaendelea kupungua hata kutoka kile cha mwaka jana. Sasa nilitaka nipate ufafanuzi, kama hata ile boti iliyoko pale Sota, Mkoa wa Mara ambayo inahudumia Wilaya sita ni ya kizamani, inatumia lita 3000 katika mkupuo mmoja, sasa nataka nipate ufafanuzi kama kweli hapa kuna dhamira ya dhati au pengine niambiwe kwamba Mikoa, kwa maana pengine ya Tarime, Rorya, ndiyo wanaopewa fungu lingine la mafuta kwenye kasma yao na siyo hizi ambazo zinatoka moja kwa moja *Police Marine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka nipate ufafanuzi na kama sitapata majibu ya kuridhisha kwa sababu wananchi kule Mwibara, Ziwa Victoria kule Goziba, wanauawa na maharamia, wananyang'anywa nyavu, kwa kweli hapa itabidi nitoe shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kangi Lugola, hiyo shilingi yako naomba uiahirishe, uendelee kuikumbuka tutakapofika kwenye mshahara wa Waziri kule basi utaona namna gani ya kufanya. Kwa sasa tupate ufafanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Jeshi la Polisi linapata mafuta machache sana na jitihada zinazofanywa, pamoja na kuwa tuna boti kubwa ambazo zinahitaji mafuta mengi zile kwa sasa ni mbovu. Tumepata boti 11 ambazo tumepata msaada kutoka Marekani, kwanza zinatumia mafuta machache kuliko zile zetu za asili na zitatusaidia mpaka tuone tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba huko Mikoani nao wana vifungu kwa pale ambapo kuna Kituo cha *Marine*.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ndio utaratibu wetu, *hold on,* kule mbele nitakupa nafasi. Katibu tuendelee.

Kif. 2003 - *Railway Police Division*…….....Tshs. 1,615,211,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2004 *Police Signals Branch*……...........Tshs.1,505,400,300/=

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika *item* 221200, *Communication and Information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa *Polisi Signal Branch*, hili ni eneo muhimu sana la mawasiliano ya simu, *internet*, *fax* na *telex* na jambo kubwa ni suala zima la kukabiliana na uhalifu. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliposema kwamba tatizo ni fedha, lakini tuangalie kwamba katika hali ya kukabiliana na uhalifu na mambo haya ya *police signal* ukaweza kupunguza Sh.350,000,000 za mwaka wa jana, walipata Sh.783,000,000 mara hii Sh.433,000,000. Sasa ile nia ya Serikali kukabiliana na uhalifu inaonekana hapa itakuwa haijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleweshe, atuambie hasa mkakati wa Serikali kutokana na kupunguza fedha kiasi kikubwa katika *Police Signal*,

kipengele cha *communication and information,* mambo ambayo yanachukua nafasi kubwa katika shughuli hizi. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud na Wajumbe wenzako wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, maswali haya si mngeulizana kwenye Kamati leo mtujibu hapa? Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafahamu kama anavyofahamu Mheshimiwa Masoud umuhimu wa *signals*. Hata hivyo, siku zote ulinzi ni kutegemeana; ukiona hiki muhimu, ukikichukua hicho tu hutalinda. Sasa kilichotokea hapa ni kwamba tumelazimika tupunguze pesa ili tukalinde reli, *airport* na kadhalika. Ziko sehemu tatu ambazo imebidi tupunguze kwenye baadhi ya mafungu na mengi tutayakuta huko, kwamba zamani watu wa reli Askari wao walikuwa wanawalipa, Shirika lilikuwa vizuri, Airport vivyohivyo, *TAZARA* vivyo hivyo. Kwa hiyo, baadhi ya vifungu na vitawashughulisha sana Waheshimiwa Wabunge, tumevipunguza ili na hivi vituo vitatu, *airport* lazima tuilinde na tuilinde sana, tukapeleka huko.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2005 - *Police Zanzibar* …….....................Tshs.10,594,418,000/=

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufafanuzi katika *subvote* 210300, *personal allowances (non-discretionary)*. Posho hizi zimeongezeka kwa kiasi kikubwa sana cha kutisha. Pamoja na kwamba tunatetea maslahi ya Askari wetu ili waweze kutulinda vizuri, lakini napata wasiwasi hapa kutoka Sh.150,000,000 mpaka Sh.4,823,000,000. Nataka ufafanuzi kidogo, mbona posho zimekuwa kubwa sana kiasi hiki kuna nini huku Zanzibar?

**MWENYEKITI:** UKAWA siyo! Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna nini Zanzibar, mbona hela nyingi mno. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar hakuna jambo jipya, isipokuwa hili lilifanyika kwa makosa, *item* hasa ni kama ya mwaka wa jana, Hazina wali-*print* vibaya na *infact* waliahidi kwamba wangeweka sawa jambo hili. Hata hivyo, fedha yetu haijaongezeka na asiogope, hakuna jipya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Faida nilikuona.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi niko 213000, *educational material, supplies and services*, sioni kitu chochote hapa na hii 221400, *hospitality supplies and services* sioni kitu na si hilo tu, samahani kidogo, mimi naomba kurudi nyuma. Hapa kwenye *fire and rescue force*, mimi naona sijaona hata Mkoa mmoja wa Zanzibar, Mikoa yote ni ya huku Bara au kule hakuna hizi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida, inabidi sasa uchague katika hayo yote moja lipi unalotaka lijibiwe.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibiwa hayo yote hakuna Zanzibar, sioni, kifungu kimoja hapo, ndicho hicho lakini zote hakuna katika Zanzibar, sioni hata Mkoa mmoja, huku kuna Mikoa yote ya Tanzania Bara lakini Zanzibar sioni hata moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa fafanua vizuri ili Mheshimiwa Waziri akuelewe.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** *Fire and Rescue Force* Zanzibar hakuna? Hata kwenye vifungu ndani Mikoa yote ya huku Bara imo lakini Zanzibar Mikoa yote sioni au hakuna? Mbona tunaiona huduma hii?

**MWENYEKITI:** Basi umeeleweka Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Faida na wenzake kwamba *fire* si jambo la Muungano. Kuna *Fire* ya Tanganyika na *Fire* ya Zanzibar. Serikali ya Muungano na Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida hatusimami mara mbili kwa sababu ni ufafanuzi tu. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Polisi Zanzibar, *item* 230900, *routine maintenance and repair of naval operations including sea.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha za matengenezo ya boti za polisi. Mwaka jana kulikuwa na Sh.10,000,000 na mara hii ni Sh.10,000,000. La kusikitisha hakuna mpango wa kununua boti mpya Zanzibar. Hata hivyo, kwa kuwa majanga na maafa katika bahari zetu yanatokea kwa muda mrefu na boti za Polisi nyingi Zanzibar ni mbovu. Leo naangalia ile nia ya Serikali ya kuweza kukabiliana na maafa wanasema ufinyu wa bajeti, ufinyu wa bajeti mpaka kwenye maisha ya binadamu? Kila siku vifo vinatokea tunapiga kelele…

**MWENYEKITI:** Swali lako?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema kwamba je kwenye Kamati yenu hamkuambiana, tunaambiana lakini Serikali ndiyo hiyo. Sasa atupe ufafanuzi, ni kwa nini fedha za matengenezo ya boti zimekuwa kidogo kupita kiasi wakati kuna machafuko ya bahari na vifo vinatokea. Kwa nini Serikali hili hamkuliangalia kwa makini sana, naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuase Mheshimiwa Masoud asitusemee kwanza, atuulize tu tumjibu halafu kama tumekosea aulize. Zanzibar katika boti tulizopewa na Marekani tumewapa mbili.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kama Mjumbe wa Kamati alipaswa kujua hilo. *(Kicheko)*

Kif. 2006 - *Police Airwing* ………..................Tshs.2,225,423,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2007 - *TAZARA Police*………..................Tshs.1,505,092,300/=

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nipo kwenye kasma 210200, *Basic Salary (Non-pensionable*. Mwaka jana wakati tunapitisha Sheria ya *SSRA* hapa tulielezwa umuhimu wa kila mwajiri kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake wote wanaingia kwenye *Social Security Schemes* kupitia Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii iliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kupata maelezo, ni watu wa namna gani wanaajiriwa na kampuni kubwa kama *TAZARA* halafu hawako kwenye *pension* na Polisi kwa sababu tumepitisha ile *GEPF* ambapo kabla ya hapo ilikuwa Mfuko wa Akiba sasa ni *pensionable*, nataka nijue ni watu gani sasa hawa ambao hawako kwenye *pension* yoyote? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotengwa kwa ajili ya *pension* katika mashirika mbalimbali na waajiriwa wengine ni kwa ajili ya wale ambao walistaafu kabla ya 2004. Baada ya hapo watumishi wengi wako katika mifuko mbalimbali ambayo ndiyo inayowajibika kuwatengea fedha zao. Kwa hiyo, hata juzi kwenye maswali tulipokuwa tunajibu kuhusu nyongeza zilizokuwa zinauliziwa zilikuwa kwa wale ambao wanawajibika Serikalini kwa wale ambao wako kwenye mifuko, mifuko inawajibika.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2008 - *Field Force Unit* ……..................Tshs.1,271,639,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, hela za *Field Force*, endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Samahani nilikuwa nataka nijue tu, maana nilikuwa naangalia hii *subvote* 2008 kasma ndogo ya 210100, *basic salaries (pensionable posts)*. Naona imepungua kutoka Sh.3,130,000,000 mpaka Sh.355,000,000 tu. Kwa uelewa wangu najua kwamba hii ni kwa wale waliojiriwa *permanent,* si ndiyo? Kwa nini imepungua kutoka Sh.3,100,000,000 kufikia Sh.355,000,000, ina maana wote wamestaafu au?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Esther anaulizia habari za *FFU*, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pana mambo mawili. Moja ni kustaafu lakini lingine ambalo nafikiri ni muhimu zaidi ni kwamba tuna-*decongest* Dar es Salaam. Kwa hiyo, vikosi hivi vinapata watu zaidi huko ambako kunafanywa maandamano. *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2009 - *Traffic Police* ……...........................Tshs.783,487,400/=
Kif. 2010 -*Police Airport* …….........................Tshs.1,209,229,000/=
Kif. 2011 - *Police Dog and Horses* …….........Tshs.872,885,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther kama hujaridhika maswali ya *FFU* utapata upendeleo wa Kiti, unaweza ukauliza tena ya ziada, endelea Katibu. *(Kicheko)*

Kif. 2012 - *DSM Special Zone* …...................Tshs.7,084,624,500/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu hiki kinahusu Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam. Napenda kupata ufafanuzi ili kuepusha *possibility* ya makosa ya kimahesabu baadaye ambayo yanaweza kusababisha mishahara hewa. Kiwango cha fedha kilichoandikwa hapa kwenye *Basic Salaries – Pensiobale Posts* na *Basic Salaries Non-Pensionable Posts* kinatofautiana kabisa na kiwango cha fedha kilichoko kwenye randama, sehemu zote

mbili za randama kwenye ukurasa wa 54, kwenye *GFS codes* na hata kwenye zile *items,* viwango vinatofautiana kabisa. Kwa hiyo, ningependa kupata ufafanuzi, viwango halisi vya mishahara kwa upande wa Kanda Maalum Dar es Salaam ni vipi, ni hivi vilivyoko hapa au ni hivi vilivyoko kwenye randama sehemu ya chini ya *item* au ni vile vilivyoko kwenye randama sehemu ya juu ya *GFS codes*. Kipi ni sahihi zaidi ili tujue tunapitisha viwango vipi?

**MWENYEKITI:** Swali lako linahitaji upekuzi kidogo, ngoja pafanyike ulinganifu, kwenye randama iko kwenye ukurasa wa ngapi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye randama ukurasa wa 54, Dar es Salaam *Police Special Zone, subvote* 2012.

**MWENYEKITI:** Ambako inaonesha ni shilingi ngapi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ambapo kwenye *segment four, GFS codes* kwenye *Basic Salaries – Pensionable* inaonesha Sh.3,900,000,000 na *Basic Salaries No-Pensionable* inaonesha Sh.2,200,000,000, hii sehemu ya kwanza lakini sehemu ya pili *basic salaries* kwenye *item* 210100 inaonesha Sh.4,400,000,000 na kwenye *basic salaries non-pensionable* inaonesha Sh.3,600,000,000. Kwa hiyo, maana yake kuna *fugure* tatu tofauti, sehemu tatu tofauti kwa suala lile lile la mishahara.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulinganisha mimi naona ni sawa kati ya randama na *print-out*. Ile ya mwanzo ni Sh.3.937 na hii ya pili ni Sh.2.203, ziko sawa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haziko sawa. Kwenye mkokotoo, yaani unavyokokotoa sasa chini ya lile jedwali unaanza *item* 2100100, *Basic Salaries – Pensionable Posts,* fedha zinazoombwa mwaka 2014/2015 ni Sh.4,400,000,000 lakini huku ni Sh.3,900,000,000. Huku zimeandikwa Sh.3,600,000,000 huku zimeandikwa Sh.2,200,000,000, haiwezekani hizi *fugure* zikawa sawasawa.

**MWENYEKITI:** Namuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU N. L. MADELU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye randama inawezekana ikawa uhamishaji wa *figures*, nakuomba Kiti chako na Bunge wachukue *main print-out*.

**MBUNGE FULANI:** Ya Hazina.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tuchukue hiki ambacho tunakishughulikia hivi sasa.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2013- *Police Ilala* ……………..................Tshs.4,586,368,300/=

**MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kidogo ufafanuzi katika *subvote* hii 220300, *Fuel, Oils and Lubricants* ambayo imetengewa kiasi cha Sh.171,500,000. Hii ni Polisi Ilala na Ilala ndiyo tunajua ndipo ilipo Serikali, Ikulu iko Ilala, Wizara zote za Serikali ziko Ilala na fedha za mafuta zimepunguzwa. Pamoja na kwamba tunaambiwa bajeti lakini huku hatuoni kama ndiko kwenda kumshika simba sharubu, kupunguza mafuta Ilala Polisi wakakosa mafuta? Ni hatari kumshika simba sharubu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, sijui sharubu gani zinaongelewa hapa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba pesa za mafuta Ilala zimepungua lakini moja ni kwamba kuna *stock* halafu ya pili ni kwamba pia tumelazimika tuwape wale wengine ambao walikuwa hawana kabisa, *TAZARA* na *Airport*.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2014- *Police Kinondoni* ……..................Tshs.5,198,033,400/=
Kif. 2015 - *Police Temeke* ……......................Tshs.6,050,151,500/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2016 – *Police Arusha* ……......................Tshs.8,011,204,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Godbless Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea kasma ya 221700, *food supplies and services* ambapo kwenye randama inasema ni chakula cha mahabusu na mimi Arusha mara nyingi nimekuwa mteja wa mahabusu. Miaka yote toka nimechaguliwa kuwa Mbunge, nimekuwa mteja mzuri wa mahabusu na sijawahi kuona chakula mahabusu. Sasa ninauliza pengine kililetwa nikiwa nimelala ama walininyima makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linatakiwa lazima limlishe mahabusu ambaye linamshikilia. Sasa jambo ambalo linatokea ni kwamba wale mahabusu wengine wanapendelea kula chakula walichozoea nyumbani. Kwa hiyo, wanaagiza waletewe na familia. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa!

**TAARIFA**

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nimpe taarifa mzoefu wa mahabusu na mimi pia ni mzoefu sana wa mahabusu lakini mimi nilipokaa mahabusu chakula nilikuwa ninapata. Kwa hiyo, nilitaka kumuambia kwa Mtwara chakula nilikuwa napata. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa yake kwa sababu tunatofautiana vyama. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa. Mheshimiwa Maryam ulichelewa kusimama mwanzo, bahati mbaya sana. Ila nisema tu kwamba kwa Waheshimiwa ambao mngependa

kupata uzoefu kidogo wa mahabusu basi mnaweza mkajiorodhesha hapa ili tupate uhakika Mheshimiwa Waziri anatuambia ni kweli kuna chakula au hakuna kule? *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2017 – *Police Iringa* …...................... Tshs.5,776,169,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Ritta Kabati, ni watatu si ndio? Haya twende hivyo nilivyowaita.

**MHE. LEDIANA M. MMG'ON'GO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 2017 – Polisi Iringa. Ninaulizia *item* 221000 – *Travel in country.* Mwaka jana zilikuwa ni Sh.127,000,000/= lakini mwaka huu zimepungua zimekuwa Sh.71,000,000/=. Napenda kufahamu ni sababu ipi iliyofanya wakapunguziwa fedha kiasi hiki karibia nusu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tumerudi kulekule, kwa nini fedha imepungua?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ikiwa mwaka jana nyingi na safari hii ni chache ni kwamba hizo shughuli zimeshafanyika. Inawezekana watu wa Iringa walikuwa na *need* ya kusafiri mwaka jana zaidi kuliko mwaka huu. Kwa hiyo, zile shughuli za kule nje wamezifanya.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko *item* 210200. Kero kubwa ya Askari wetu ni mafao. Wachangiaji wengi wameongea kwa uchungu jinsi Askari wetu wanavyovunjwa moyo kwa kutokulipwa mafao yao, pesa ya uhamisho na kadhalilka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mwanzoni nilikuwa ninazungumzia juu ya mafao ya wafanyakazi hawa. Tunazo sheria ambazo Wabugne watakumbuka kwamba sisi wenyewe tumezitunga hapa Bungeni kwamba hairuhusiwi mwajiri yeyote kumu-*engage* mfanyakazi bila ya kumwekea mafao ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yaliyotolewa ni kwamba wapo Askari wanaofanya kazi kwa mkataba, kwa muda wa miaka mitatu mitatu vipindi vitatu kwa maana ya miaka 12. Kama mwajiri angemwekea mfanyakazi kwa miaka 12 na mfanyakazi yule baada ya miaka 12 akajitolea kujiongezea miaka mitatu afikishe miaka 15 *already* anakuwa *pensionable* na anaweza akalipwa *pension* maisha yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kuuliza kwa nini Serikali imeendelea kuvunja sheria ambayo tuliiweka wenyewe hapa Bungeni ambayo inamtaka kila mwajiri amuwekee *pension* mfanyakazi wake? Katika Wizara hii ninaona moja kwa moja iko karibu na utekelezaji wa sheria za nchi lakini inavunja sheria kwa kutokuwawekea wafanyakazi wake *pension* kama tulivyoagiza katika Bunge lako Tukufu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya *pension* kwa Polisi yako namna hii. Anapoingia anapewa mkataba wa miaka mitatu. Akifanya vizuri na ni kipindi ambacho Polisi anakuwa anapimwa au anaangaliwa, ataendelea mpaka akifikishe miaka 12 anaingia kwenye *pension* na miaka ile 12 inahesabiwa. Kwa hiyo, siyo kama ataanza baada ya miaka 12 ndio wanahesabu, hapana! Akifikisha ile miaka 12 anaambiwa sasa wewe ni Polisi mzuri *pensionable* na miaka yako ile ya nyuma tunaihesabu. Kwa hiyo, si kweli kusema kwamba hawalipiwi, watalipiwa pale watakapo-*qualify* na *qualification* yao ni miaka 12.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nilikuwa nataka kuhoji kuhusu *subvote* 2017 – *Police Iringa*. Kasma 227500, *Other Supplies and Services,* mwaka juzi zilitengwa Sh.285,107,980/=, mwaka uliofuata hakikutengwa chochote na mwaka huu hakikutengwa chochote lakini kumekuwa na matatizo makubwa sana. Pia ninataka nijue kwamba fungu la kuwalipa wazabuni, limewekewa tengeo namba ngapi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wakati unafunga hoja yako sikusikia ukimpongeza Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kujenga Kituo cha Polisi. Ufafanuzi Mheshimiwa kwa swali aliloliuliza. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Tukiwataja wadau werevu wa Polisi, hawezi akawa namba mbili Iringa kule. Ana Kituo ambacho amejenga, ni kizuri sana na ananihimiza nikakifungue, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kuhusu kifungu hiki cha *Other Supplies,* kama nilivyojibu pale mwanzoni, kinatumika ikiwa vifungu vingine vimeishiwa au kumetokea jambo lingine. Kwa hiyo, hiki ni *other,* pengine siyo muhimu wakati vile vifungu vimepewa kasma ya pesa.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2018 – *Police Kilimanjaro* …...............Tshs. 8,522,284,894/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2019 – *Police Kigoma* …....................Tshs. 6,690,499,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Susan. Tuanze na Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wengine watashangaa kwa nini nimesimama Kigoma lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na tulikwenda kufanya ziara katika Hifadhi ya Mahale kule Kigoma na sasa ninazungumzia kwenye *item* 220300 kuhusu mafuta nay ale mambo ya vilainisho. Mwaka jana walipata Sh.366,500,000/=, mwaka huu wamewekewa Sh. 274,100,000/=. Mimi ningeomba viongozi wa Wizara hii wangekwenda kule Mahale wakaone wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwanza kuna wakimbizi yaani kule ni kama nchi nyingine. Hata wafanyakazi wale wa Maliasili pale *TANAPA* wanaogopa kwenda kijiji kwa sababu waliopo pale karibia wote ni wakimbizi. Hakuna ulinzi, Mkuu wa Wilaya analalamika, Polisi wanalalamika, hawana mafuta ya kwenda kule kuweka ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ule ni mpaka mmeuacha wazi, haya mafuta mmeyapunguza hivi yatatosha nini wakati tumeenda wanalalamika. Jamani tusipitishe hii bajeti hawa jamaa wakaongezewe pesa, kule kuna hatari. Hebu nendeni ninyi mkalale hata siku moja kama mtalala kule, wakimbizi watupu yaani kule ni nchi kama ya Congo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba jitihada kubwa zimefanywa kukifanya kifungu hiki kiwe na fedha kwa kujua Mkoa wa Kigoma una matatizo gani. Naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, anasaidia sana katika eneo hili. Kwa hiyo, tuko salama Kigoma. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina-*declare interest* mimi ninatoka Mkoa wa Kigoma. Ninajielekeza kwenye kasma 210300, *personal allowances (Non-Discretionary).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye randama ni kwamba fedha hizi zinaonekana ni kwa ajili ya kugharamia likizo pamoja na uhamisho wa Askari. Nimekuwa nikilalamikiwa sana na Askari Polisi na hata pengine Magereza lakini kwa sababu kifungu hasa kinawahusu Askari Polisi, nilikuwa naomba kupata kauli ya Serikali iwapo fedha hizi walizozitenga, maana yake madai ambayo mimi ninayafahamu, ya Askari wachache, sasa pesa hizi inaonekana sijui ni madeni au itakuwa ni kwa ajili ya mwaka wa fedha unaoukuja? Kama ni kwa ajili ya mwaka unaokuja, Serikali kupitia Wizara, mnatoa kauli gani kuhusiana na madai ya Askari ambayo yanahusiana na masuala ya likizo na uhamisho, hata pengine na malipo mengine ambayo Askari wanastahili kulipwa kwa sababu kuna malalamiko makubwa sana ya Polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, naona kama unachombeza swali la sera hivi, la mshahara wa Waziri, hapa inatakiwa tujielekeze kwenye hivi vifungu na hizi pesa zilizowekwa pale, tatizo liko wapi kwenye kiasi hiki cha fedha?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye randama inasema kwamba fedha hizi zitatumika kugharamia likizo na uhamisho wa Askari.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Waziri aweze kunisaidia kufahamu, je, fedha hizi zitaweza ku-*include* madai ya Askari ambayo yanahusiana na likizo pamoja na uhamisho?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kwa sababu kuna malalamiko makubwa sana kule ambako ninatokea.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua ukubwa wa matatizo ya madeni wanayodai Askari na ilitoa rai kwamba tuwapeleke hesabu za madeni zihakikiwe na kauli imetoka kwamba kuna madeni ya wafanyakazi yatalipwa yaliyohakikiwa katika kipindi hiki. Hata kama hayakulipwa, hili linaweza kusaidia *both* kwenye madai na mwaka huu.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2020 – *Police Kagera* …......................Tshs. 8,138,997,600/=

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijielekeze kwenye kifungu kidogo cha 220300. Sababu alizozieleza Mheshimiwa Susan hapa wakati akitetea Mkoa wa Kigoma ndizo sababu hizohizo zilizoko katika Mkoa wa Kagera kwa sababu ya ile mipaka na sababu ya jiografia ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana waliweza kutengewa angalau pesa ilikuwa Sh.355,650,000/= lakini kipindi hiki imeteremka na kuwa Sh.269,850,000/= tofauti ya Sh.85,000,000/=. Kule bado kuna matatizo mengi sana ya ujambazi, kuna mazingira magumu,

wakimbizi, wahamiaji haramu wameenda na kurudi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, atueleze kwa nini amepunguza kiasi hiki wakati ulinzi unahitajika kuimarishwa kule katika Mikoa ya pembezoni. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulilazimika kupunguza kama tulivyopunguza vifungu vingine ikiwemo Zanzibar kusaidia Zanzibar *Airport* na *TAZARA*.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2021 – *Police Lindi* …….....................Tshs. 6,132,640,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda umesimama?

**MHE. SAID M. MTANDA:** Ndiyo Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakupa nafasi.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kwa nini kifungu 220400 cha *Medical Supplies and Services,* kwa Mkoa huu wa Lindi mwaka jana walitengewa Sh.1,200,000/= kwa ajili ya matibabu lakini mwaka huu ni sifuri. Naomba kujua Askari Polisi wa Mkoa wa Lindi hawataugua kwa mwaka huu au fedha yao iko Makao Makuu na kama iko Makao Makuu, kwa nini isiwekwe hapa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tamaa kubwa kwamba Lindi nako wataumwa na kule kuna mbu wengi sana. Jitihada hizi za kuweka vifungu hivi imekuwa ngumu, isipokuwa Makao Makuu italichukulia hatua jambo hili na kulirekebisha.

**MWENYEKITI:** Hii inaonesha jinsi gani Mheshimiwa Mathias Chikawe ni Waziri asiyefanya upendeleo wowote vinginevyo angejaza fedha hapa.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2022 – *Police Mwanza* ….....................Tshs.9,812,696,400/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2023 – *Police Mara* …...........................Tshs.6,682,208,500/=

**MWENYEKITI:** Akina Ester wamesimama pamoja na Susan. Tuanze na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimwia Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kupata ufafanuzi kwenye kasma 221100, *Travel Out of Country.* Miaka miwili mfululizo kifungu hiki hakijatengewa fedha. Tunajua mbali na mazingira magumu wanayopata Askari wetu, tunajua wanapopata safari za nje, ni moja ya kujiongezea kipato lakini wanapata *exposure* na mafunzo mbalimbali. Kwenye maeneo mengine tumeona wamepata fursa hiyo na kumekuwa na malalamiko wanaopata fursa ya kusafiri nje ya nchi ni Askari wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ningependa *commitment* ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha.

**NAIBU WAZIRI WA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu watu wa Mikoa huwa tunawashirikisha, wao wanajua nini muhimu na nini labda ni

daraja la pili. Pamoja na hayo yote kusafiri ni muhimu kwenye mahitaji na tutajitahidi katika mwaka wa fedha ujao tulione hili. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba kuhoji *Subvote* 2023, kasma ndogo ya 221200, *Communication and Information.* Mwaka 2013/2014 zilitengwa Sh.61,400,000/= sasa hivi wametenga Sh.31,400,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua *Police Mara*, kwa maana ya jiografia ya Mkoa wetu wa Mara na matukio kama ya Butiama na kwingineko ina maana mahitaji mengi yanakuwepo ya mawasiliano na vitu kama hivyo. Hata hivyo, nimejaribu kuangalia hii kasma ya 221200, kwa Mkoa wa Mwanza mwaka jana walikuwa na Sh.61,440,000/= kama sisi na kwa mwaka huu wana Sh.60,000,000/=. Sasa nilikuwa nataka nijue ni vigezo gani wanavyotumia kuweza ku-*allocate* hizi pesa na kuzipunguza. Kwa sababu nilifikiri kwa Mkoa wa Mara, kwa wengine wanaongezewa, wengine imebaki hivyohivyo na sisi wengine tunapunguziwa nusu licha ya kwamba jiografia ya Mara ni Mkoa mkubwa na matukio kama nilivyoeleza mwanzo. Ninaomba kuja ni kigezo kipi kinachotumika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Esther anasema mnafahamu mambo kule Mara yalivyo mnawekaje fedha kidogo na Mkoa ule kimatukio ni Mkoa mkubwa kuliko yote Tanzania? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mara nyingi tu kwamba upangaji wa hivi vifungu vidogo vidogo vinafanywa kwa ushirikaino na Ma-*RPC*. Wao wanajua zikipungua hapa wanaweza kufanya nini au mwaka jana walitumia vipi. Hata hivyo, hakuna Mkoa ambao utakuwa na tatizo kusiwe na mawasiliano, hilo naomba niwahakikishie. Mara pia kuna Rorya Kanda Maalum, kwa hiyo, kwa vyovyote mahusiano ya Ma-*RPC* pamoja na *headquarters* hayawezi hayawezi yakafanya mahali pawe hapana mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru kwa maelezo yako hayo. Alichokuwa anasema Mheshimiwa Esther Matiko ni kwamba katika nchi yetu ukitembelea Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine, ukifika mpakani utakuta bango limeandikwa karibu Mkoa fulani, karibu Mkoa wa Morogoro, karibu Mkoa wa Ruvuma, karibu Mkoa wa Iringa lakini unapo-*cross* kuingia Mara unatoka Mwanza unakuta bango limeandikwa sasa unaingia Mkoa wa Mara. *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2024-*Police Tarime Rorya*……...............Tshs. 4,853,129,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Polisi Tarime Rorya, kasma ndogo ya 220400, *Medical Supplies Services*, Tarime Rorya hamjawatengea jamani kama ilivyo Lindi. Kwa hiyo, nataka nijue hawa Maaskari wa Tarime Rorya hawataugua wala hawatapata madhila yoyote yale ya kuhitaji *medical services*? Kwa nini mmewatengea sifuri? Pia msituambie kwamba yanatoka Makao Makuu kwa nini Mikoa mingine mme-*allocate* na hapa msi-*allocate*?

**MWENYEKITI:** Inauliziwa Kanda Maalum, Tarime Rorya!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda Maalum nao wataugua na tutahakikisha kwamba hawafi kwa sababu hakuna kasma hii.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2025 Police Mbeya…….........................Tshs. 9,720,696,800/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Aliko Kibona.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi niko kwenye *subvote 2025,* kasma ndogo ya 220800*, Training domestic*. Nilitaka kujua kwa sababu Mbeya ni *outlet* ya nchi nyingi za Kusini mwa Afrika na kwa hiyo ina maana Maaskari wanatakiwa kupata *training* ambayo ni *continuous*. Cha kushangaza mwaka juzi allocation ilikuwa ni zero, mwaka jana ilikuwa ni Sh.3,000,000 na mwaka huu ni zero tena. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie ni kwa nini? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa swali hilo kuhusu Mbeya!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya hawana lakini wataweza kutumiza malengo yao kupitia *training* ambazo zinafanywa kwenye vyuo, kwa sababu zile zipo kwenye vyuo na pesa za mambo hayo zipo palepale.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kifungu kidogo cha 220300. Wakati akichangia Mjumbe mmoja Mheshimiwa Chiku Abwao ameongea kwa hisia na uchungu mkubwa jinsi ambavyo Jeshi la Polisi linaonekana kusahaulika katika kupewa mafungu ya kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye fungu hili, naona Mbeya, *Fuel, Oil and Lubricants* Sh.179,000,000, nilikuwa nafanya hesabu kulingana na idadi ya Wilaya zilizopo nakuta kila Wilaya takribani inapata Sh.2,000,000 kwa maana ya kwamba kila mwezi Wilaya inatumia Sh.160,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo kutoka Serikalini…

**MWENYEKITI:** Hiyo hesabu yako Mheshimiwa Aliko iko sawasawa?

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko sawasawa *subject to corrections*.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, sema *subject to corrections!*

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo kutoka Serikalini, tumekuwa tukipata shida na tumeona Askari wetu, Wakuu wa Vituo na Makamanda wa Wilaya wamekuwa wakihangaika kuombaomba kwa wafanyabiashara mafuta pindi matukio yanapotokea. Kwa nini mpaka sasa hivi Serikali haijaona umuhimu wa kuwasaidia hawa Ma-*OCD* na Wakuu wa vituo vidogo katika Wilaya zetu ili wafanye kazi zao kwa utulivu bila kuhangaika kuliko kuwapangia kiasi hiki kidogo cha pesa takribani Sh.200,000/= kwa mwezi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niungane na Mheshimiwa Mbunge kusema kwamba bado Serikali haijaweza kuchangia kitu ambacho kinatakiwa lakini kile kidogo tulichonacho tukitumie kwa busara. Hapa busara kubwa ambayo imetumika ni kwamba zile ambazo zilipewa Mbeya mwaka juzi tulilazimika tupunguze kidogo kupeleka sehemu nyingine ambazo *otherwise* itakuwa *disaster*. Tuendelee kuvumiliana na tuendelee kugonga mlango mpaka tuweze kupata pesa zaidi.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2026 -*Police Mtwara*……........................Tshs.6,727,990,400/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji!

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 220400, niko katika *Medical Supplies and Services*. Hizi fedha mwaka jana ilikuwa ni karibu Sh.27,000,000 lakini mwaka huu ni Sh.1,200,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba hizi Zahanati za Polisi pia zinatibu raia na ni msaada mkubwa sana kwa raia. Wale raia wanaoishi jirani na zahanati, wananufaika sana na zahanati hizi. Sasa hivi fedha ni Sh.1,200,000/= haziwezi kutusaidia kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mtwara tuna zahanati ambayo ina Mganga mzuri lakini fedha hakuna. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari tumhamishie Unguja yule Daktari wetu wa kutoka Mtwara kwa sababu fedha hakuna kwa maana hiyo hakuna kazi atakayofanya pale.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi kwa nini kachagua kumpeleka Unguja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimekuwa nasema sana mambo haya, ni kwamba ukishapewa bajeti lazima kuwe na sehemu ina fedha kidogo. Mtwara hapa wamepata Sh.1.2 lakini Lindi na Mbeya hawakupata. Aone kwamba Mtwara kuna gesi tunaanza kuwasaidia. *(Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba bado tupo mbali, kufuatana na malengo yetu ya leo na kwa hiyo mnikubalie kwa mamlaka mliyonipa kwenye Kanuni niongeze muda wa nusu saa. *(Makofi)*

Katibu tuendelee!

Kif.2027-*Police Morogoro*…......................Tshs. 10,309,191,500/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawaje Waziri majibu yake ni yaleyale lakini ni bora nikasema, kifungu kidogo 220300 kuhusu *Fuel, Oils and Lubricants*. Wanasema mwaka jana walitoa Sh.349,650,000 na mwaka huu Sh.277,750,000 lakini akumbuke kwamba Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wenye matatizo makubwa, mapigano ya wakulima na wafugaji, sasa hivi kuna mafuriko mengi sana, barabara hazifanyi kazi, sasa mnapunguza hicho kiasi mnataka wale watu wahudumiwe vipi na Polisi Mkoa? Mkoa wa Morogoro muuangalie kwa jicho lingine siyo sawa na Mikoa mingine, hakuna barabara tumenyimwa miaka mingi na mafuriko kibao, daraja pale hakuna kitu! *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi hatufanyi ubaguzi wa Mikoa na *in fact* ukitutazama vizuri Morogoro tunaipenda. Sasa hapa fedha hii imepungua ili kwenda *airport* na *TAZARA,* Sh.71,000,000 imepunguzwa.

**MWENYEKITI:** *TAZARA* ambayo inapita hukohuko!

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2028 - *Police Manyara*…......................Tshs.6,286,321,000/=
Kif.2029- *Police Singida*…….......................Tshs.6,249,377,400/=
Kif. 2030-*Police Pwani*……….......................Tshs.8,645,174,900/=
Kif.2031-*Police Ruvuma*…..........................Tshs. 4,317,384,400/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2032-*Police Rukwa*……........................Tshs.5,043,032,500/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 230900, *Routine Maintance and Repair of Naval Operations including Sea*. Mkoa wa Rukwa una eneo kubwa sana la maji, Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika na Ziwa Tanganyika lina-*cover* Wilaya mbili za Kalambo na Nkasi. Kifungu hiki kimepunguziwa sana pesa, mwaka jana tulikuwa na Sh.20,000,000 na mwaka huu ni Sh.8,000,000 tu. Kwa kweli kazi haiwezi kufanyika hapa, tunatakiwa tuongeze pesa kama mwaka jana ilivyokuwa. Naomba maelezo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukizidi kutafuta majibu mapya sina hakika sana kama tutayapata. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni tatizo la bajeti kama nilivyosema lakini pia kulikuwa na boti ambayo ina matatizo. Kwa hiyo, tunategemea tuitengeneze halafu ikiwa sawa mafuta yatapelekwa.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Namwomba Mbunge yeyote yule atakayesimama awe na swali jipya tusirudie maswali yaleyale na majibu yaleyale.

Kif.2033-*Police Shinyanga*….......................Tshs.5,655,789,800/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lembeli!

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu mimi ni jipya. Mwaka jana wakati nikichangia bajeti hii nilizungumzia matatizo yaliyopo Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wenye migodi mingi lakini pia kuna matatizo ya mauaji ya vikongwe…

**MWENYEKITI:** Uko kwenye kifungu gani Mheshimiwa Lembeli?

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** *Subvote* 2033, kasma ndogo 220300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fungu hili, ukazingatia na matatizo ya Mkoa huu unajiuliza, ni kigezo gani kimetumika Mkoa wa Shinyanga na matatizo yake umetengewa Sh.182,000,000, Mikoa mingine kama Kusini Pemba Sh.204,000,000. Mazingira ya Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Shinyanga ni tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisema na ndiyo swali langu, nilisema Wilaya ya Kahama ambayo ina watu karibu milioni moja ina matatizo makubwa, matokeo yake kwa bajeti ya mwaka jana Wilaya ya Kahama *OCD* amekuwa akipewa mafuta na wafanyabiashara. Je, Serikali imebinafsisha Jeshi la Polisi kwa wafanyabiashara? Nataka ufafanuzi tu.

**MWENYEKITI:** Swali hilo ni la kisera zaidi lakini Naibu Waziri ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubali kuchukua mafuta kwa utaratibu mzuri kisheria kwa sababu *private sector* ni wadau wetu na Mheshimiwa Lembeli ni mdau wetu, kile kitu ambacho kitatolewa hadharani na sote tukajua basi ni haki kukitoa kwa sababu sote tunahitaji kulinda.

Mheshimiwa Ritta pale alijenga Kituo cha Polisi, gharama yake pengine ni kubwa kuliko mafuta lakini alijitoa akasema anataka kufanya hivi na akafanya *openly*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyokuwa tunajibu pia tulisema kwamba tuna mfuko, *Trust Funds* ili tujilinde kupitia mfuko ule. Kwa hiyo, tunaweza pia badala ya kumpa *RPC* au *OCD* moja kwa moja tukaingiza kwenye mafuta na maelezo basi zinaweza zikafika vizuri na wengine wanatoa magari na wengine wanatoa pikipiki. Nitumie fursa hii pia kuwashukuru wale wadau werevu na nikemee wale ambao wanataka kusaidia kwa nia mbaya lakini kusaidia kwa nia safi na sote tukajua kumesaidiwa haina tatizo. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2034-*Police Tabora*…….........................Tshs.6,280,660,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mfutakamba, tafadhali!

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru! Nilikuwa ninaangalia kwenye kifungu 220400, *Medical Supplies and Services,* nimeona kiasi kilichowekwa ni kidogo sijui mahitaji ni madogo kiasi hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru!

**MWENYEKITI:** Hili darasa gumu kweli, Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumpata naomba arudie.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mfutakamba rudia, ongea Kiswahili acha kuongea Kinyamwezi, rudia tafadhali! *(Kicheko)*

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna taabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 220400, *Medical Supplies and Services,* ukiangalia huko nyuma ilikuwa inawekwa kiasi kikubwa lakini sasa kiasi kimekuwa ni Sh.1,200,000/=. Hayo mahitaji kuhusu *Medical Supplies and Services* yamepungua kwa Askari wetu wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Nimeruhusu tu lijibiwe lakini swali hili limejirudia kwa Mikoa mingi, ndiyo yale nilikuwa nasema kwamba sitarajii huko mbele kupata maswali ya aina ileile. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nzuri nimeipata hapa kwamba hawa Maaskari kumbe wengi wameingizwa kwenye *insurance*. Kwa hiyo, hawatarudi hata Makao Makuu, wana *Medical Insurance* wanatibiwa huko.

**MWENYEKITI:** Bima ya Afya kaka!

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2035-*Police Tanga*…...........................Tshs.8,688,087,300/=
Kif.2036-*Police Mjini Magharibi*…............Tshs. 9,454,245,000/=
Kif.2037-*Police Kusini Unguja*…................Tshs. 4,156,116,300/=
Kif. 2038- *Police Kaskazini Unguja*…..........Tshs. 3,174,094,900/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2039 *Police Kusini Pemba*……..............Tshs. 3,050,309,900/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *fuel and lubricant* Kusini Pemba, Mheshimiwa Lembeli amelinganisha na Shinyanga, hapa imekuwa ni Sh.204,500,000/=. Shinyanga ni kubwa mara sita au mara nane, ni vigezo gani vimetumika Pemba iende pesa ya mafuta namna hiyo wakati Pemba hata kilomita za barabara ni chache kuliko Shinyanga au Rukwa? Swali la Mheshimiwa Lembeli halijajibiwa inavyotakiwa! Huu mgawanyo tugawane sote, siyo wananchi wajitolee mafuta, *Lake Tanganyika* watu wanauawa hakuna mafuta, Kusini Pemba zimekwenda bilioni za fedha, hatukubali kitu cha namna hii, tupate jibu sahihi hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya Pemba ni tofauti na Shinyanga na huko kwa ndugu yangu Keissy. Tumezungumza kuhusu boti na ni kiasi gani inatumia mafuta ukilinganisha na gari. Kilomita ya boti inahitaji mafuta mengi kuliko kilomita ya gari.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kwa hiyo, visiwa ambavyo tunataka tutumie boti kuvilinda vitatumia gharama zaidi kuliko Mkoa mkubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuna watu huku kushoto Mheshimiwa Waziri wananiambia kuna UKAWA.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hapana, Ziwa Tanganyika tuna visiwa.

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Hapana!

**MBUNGE FULANI:** Kule Ukerewe kuna visiwa.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Taarifa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Tusikimbie hoja hii, nimpe taarifa Naibu Waziri. Ziwa Victoria tuna visiwa vya Ukerewe, Ukara, Nafuba, Rwiga lakini tuna mafuta kidogo sana, lazima tujue hii fedha Pemba kule vipi? Nampa taarifa kwamba, tuna visiwa vingi mno lakini tuna mafuta kidogo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Lake Tanganyika kuna visiwa vingi sana na majambazi kutoka Kongo DRC.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa na mimi nataka kutoa taarifa.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Tusikurupuke, naomba tukae, wala tusikasirishwe wala nini. Ni vizuri tukawa na usikivu, tukaelewana, tumeanza vizuri, tumalize vizuri. Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu, tukumbuke kwamba hapa tunaongelea Mkoa na mifano mnayoitoa siyo Mikoa, ya vile visiwa mnavyovitoa. Naomba tuyachukue majibu ya Serikali kama ndiyo majibu rasmi.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

*Kif. 2040-Police Kaskazini Pemba…..........Tshs.3,185,978,300/=*
*Kif. 2041 - Police Dodoma …....................Tshs.9,638,103,600/=*
*Kif. 2042-Police Geita …...........................Tshs.5,140,085,600/=*
*Kif. 2043-Police Katavi……......................Tshs.3,286,148,700/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2044 -Police Njombe……....................Tshs. 4,442,500,200/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga, nilikuona na Mheshimiwa Mng'ong'o.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pamoja na kwamba umesema tusijirudierudie lakini niombe kwamba kwa sababu Mkoa huu ni mpya, imenilazimu nisimame niseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 230900, Routine Maintenance of and Repair of Naval Operations Including Sea,* mwaka jana palikuwa na Sh.20,000,000 na sasa hakuna na Mkoa huu ni mpya, naomba majibu tatizo ni nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumefanya mwaka jana kwa Sh.20,000,000 mwaka huu tunaweza tukapitisha tukafanya mwaka ujao. Kwa hiyo, ni kwamba *maintenance* imefanywa mwaka jana tu, hatuhitaji kila mwaka kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mng'ong'o!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu *411000, Rehabilitation and Civil Works.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Deo Sanga, huu Mkoa ni mpya na Polisi makazi yao ni duni na pia linahitajika jengo la Mkoa. Sasa nauliza hizi fedha ni za ukarabati au ni za kuanza ujenzi wa nyumba za Polisi ambazo zinalingana na hadhi ya Mkoa?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya ukarabati.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 2045 - Police Simiyu……….................Tshs. 3,745,525,900/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Opulukwa.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko kwenye kile kifungu kidogo 220300, *Fuel, Oils, Lubricants* ambapo inaonekana kuna pendekezo la Sh.149.5 kama fedha ya mafuta, oil pamoja na vilainishio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda tu kujua vigezo ambavyo huwa vinatumika kwa ajili ya kugawa fedha hizi kwenda kwenye Wilaya, kwa sababu hizi fedha zinakwenda Mikoani, kwenye Wilaya ni kigezo gani kinatumika kwa ajili ya kupeleka mafuta kwa mfano dizeli kwenye Wilaya kwa ajili ya yale magari ya operesheni kuweza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya fedha kupelekwa Mkoani, kwenda Wilayani itategemea jiografia ya Wilaya ile lakini kingine ni wingi wa magari, jenereta au pikipiki ambayo *OCD* anayo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 3001-Police College Moshi...............Tshs. 11,075,499,300/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulisimama pale? Tumeshapita, Katibu tuendelee.

*Kif. 3002- Police College….......................Tshs. 2,514,462,400/=*
*Kif. 4001- Police Vehicle Maintenance*
*Unit …….…...............................Tshs. 2,768,320,800/=*
*Kif. 5001-Police Medical Unit …...............Tshs. 2,052,287,900/=*

*Kif. 6001-Police Building Brigade…..........Tshs. 5,589,872,800/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 7001-Criminal Investigation Division…....................................Tshs. 6,932,961,700/=*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Kange Lugola, Mheshimiwa Betty Machangu. Anza Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kuuliza kwa ufahamu. Kifungu hiki najua siku hizi kumeanza mtindo wa wauza *drugs* kupitisha baharini, sasa sioni *fuel* na *lubricants* hapa, hivyo nikataka nifahamu *fuels* na *lubricants* zimewekwa kwingine au vimesahaulika?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *the fact* haipo ni kwamba iko sehemu nyingine. Ingeweza ikawepo ikawa sifuri, lakini ikakumbukwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya nyongeza, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala *specific* la Mheshimiwa Machangu linalohusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kazi hii kubwa huwa inafanywa pia na *Task Force* ambayo fedha zake mmeziona pia kwa Waziri Mkuu kwenye kifungu cha dawa za kulevya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu ya nyongeza, Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma *229900, Other Operating Expenses.* Kifungu hiki kati ya mambo mengine ni kasma kwa ajili ya Jeshi la Polisi kununua taarifa za uhalifu kwa lengo la kuwakamata wahalifu. Sasa mwaka uliopita 2013/2014 kilitengewa shilingi bilioni 2.8 (shilingi milioni 2,800) mwaka jana shilingi bilioni 2.6 (shilingi milioni 2,600) na mwaka huu shilingi bilioni 1.2 (shilingi milioni 1,200), kwa hiyo, kiwango kinakwenda kikipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua tu ni kwamba hii dhana ya kununua taarifa za uhalifu kwa ajili ya kukakamata wahalifu, Jeshi la Polisi linaanza kuiona haina umuhimu tena? Ningependa kupata majibu ikiunganishwa na taarifa ambazo Mheshimiwa Waziri amezizungumza kwenye vyombo vya habari leo asubuhi juu ya kutoa *offer* kwa wananchi wanaotoa taarifa za uhalifu. Zile shilingi bilioni 3 ni sehemu ya hizi ama zenyewe ziko sehemu nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa nini umefanyika uamuzi wa kuhamisha kikosi maalum kutoka kwenye Jeshi la Polisi na kukipeleka Mambo ya Ndani moja kwa moja, kile kikosi Maalum cha kupambana na uhalifu mkubwa wa ujangili, utoroshaji wa fedha haramu na kadhalika. Ningeomba kupata ufafanuzi kuhusu mambo haya.

**MWENYEKITI:** Umechomekea bwana mzee, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mnyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko ule ambao tuliutangaza *CIF* (*Criminal Investigation Fund*), hizi za hapa ni za kwenye *CIF* lakini ule Mfuko niliotangaza zile zinatokana na shughuli tunazofanya kwenye kulinda benki na kadhalika, huwa tunalipwa, sasa zile tunazolipwa ndiyo tunazitumia hasa katika kununua *information* na kutoa zawadi kwa Polisi wanaofanya vizuri au kwa wananchi wanaofanya vizuri katika kutuletea taarifa na sisi tukafanikiwa katika kupambana na ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile Kikosi Maalum kweli kimehamishiwa kwenye Idara yetu ya Mipango kwa sababu tu kilipokuwa kule Polisi ikawa bajeti ya Polisi ikawa ina-*burst* sana, sasa wakikata na kile kikawa kinapungua. Mwaka jana utakumbuka kilikatwa kikapata shilingi bilioni 2. Sasa tukasema ili kikosi hiki kiweze kuendelea, tumekubaliana na Hazina kikahamishiwa kwenye Idara hii ya Mipango, sasa mwaka huu wanapata shilingi bilioni 4 ambazo zitawasaidia kufanya kazi. Mwaka jana walipata shilingi bilioni 2 na kama wangeendelea kubaki Polisi, kila siku bajeti ya Polisi ikipanda wakipunguziwa na wao inapunguzwa wakati wao bado shughuli zao zinaendelea kupanda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kange Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, sasa na mimi nikawa sioni hapa kasma inayohusu mafunzo (*training*). Pamoja na kwamba mwenzangu aliuliza kasma ya mafuta haioni na majibu tunapewa yako sehemu nyingine, sasa hiyo sehemu nyingine sijui ndiyo ipi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na mimi nataka nijue hapa, hawa makachero ambao tunawategemea sana na humuhumu ndimo kuna intelejensia wa kutafuta habari ambao wanahitaji mafunzo ya kisasa. Sasa nilitaka nijue kasma hiyo ya mafunzo kwenye Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, iko sehemu gani na kama majibu ndiyo hayohayo kwamba iko sehemu nyingine, lazima pia nipeleke huko. Lazima tuzifuatilie hizo fedha tuone kweli hawa watu wanapewa fedha za mafunzo? Vinginevyo uhalifu hatuwezi kuudhibiti kama majibu yenyewe ndiyo haya ya kwamba ziko sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niliweke sawa hili ninalosema ziko sehemu nyingine, maana yake ni kwamba ziko Makao Makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nijibu hili swali la mafunzo kwa hawa makachero. Fedha zimetengwa vyuoni ambako watakwenda hasa Moshi na pia kuna kasma Makao Makuu ambayo inashughulikia suala hili.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri. Makao Makuu anayosema hata hii tunayozungumzia ni *CID Headquarters* yaani ndiyo Makao Makuu haya, sasa sijui ni wapi huko sehemu nyingine? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Kabla hujajibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri Kivuli kuna nini?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ya 221200, *Communication and Information,* unaona mwaka 2012/2013 walitengewa shilingi milioni takribani 26 na mwaka 2013/2014 shilingi milioni 145, lakini mwaka 2014/2015 wametengewa shilingi 17,200,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyosema hii ni *Criminal Investigation Division* na *information* na *communication* ni *very crucial* lakini fedha imepungua kwa kadri tunavyozidi kwenda mbele, nilikuwa nataka kujua ni kwa sababu gani?

**MWENYEKITI:** Basi yaunganishe yote ya Waheshimiwa wote wawili, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la Makao Makuu, hizi fedha zimetengwa kwenye *main force* tunaita, Polisi Kuu, ndiko ambako ziko zile fedha ambazo nilisema ziko Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la kupungua fedha kwenye *communication* ni kwamba, kwenye Polisi tuna mahali ambapo kuna fedha nyingi kwenye mradi kwa ajili ya mawasiliano. Kwa hiyo, tunategemea kwamba tunakwenda *digital,* jambo hilo litatusaidia kuweza ku-*meet demands* za makachero.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*Kif. 7002 - Stock Theft Prevention Unit …...Tshs. 532,867,500/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tulionao kwa utaratibu tuliojiwekea, Mshahara wa Waziri unatakiwa tuujadili kwa muda wa dakika zisizopungua 25, dakika zilizobaki ni kidogo sana, hazitoshi tufanye chochote kile na tuna mafungu mengine mengi tu ambayo yamebaki huku mbele, tunaenda kwenye *guillotine*. Kwa hiyo, Katibu naomba utupitishe kwenye mafungu.

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

*Kif. 1001- Prisons Headquarters…...........Tshs.10,233,232,000/=*
*Kif. 1002-Finance and Accounts…..............Tshs.275,203,000/=*
*Kif. 2001 - Parole Department……............Tshs.737,189,000/=*
*Kif. 2002 -Prisons Welfare and Rehabilitation …....................Tshs.119,681,771,000/=*
*Kif. 2003 - Resettlement of Offenders…....Tshs.1,734,425,000/=*
*Kif. 2004-Prisons Arusha…..........................Tshs.237,824,000/=*
*Kif. 2005-Prisons Dar es Salaam ….………..Tshs.681,346,000/=*
*Kif. 2006 - Prisons Dodoma…......................Tshs.353,152,000/=*
*Kif. 2007 - Prisons Kigoma……..................Tshs.230,377,000/=*
*Kif. 2008 - Prisons Tanga …………..…........Tshs.277,457,000/=*
*Kif. 2009- Prisons Kagera…….. ….……........Tshs.226,536,000/=*
*Kif. 2010 - Prisons Mwanza……...…….........Tshs.314,724,000/=*

*Kif. 2011 - Prisons Tabora …….…..…...........Tshs. 243,157,000/=*
*Kif. 2012 - Prisons Mbeya……. …..……..........Tshs.296,945,000/=*
*Kif. 2013 - Prisons Singida……….…..……..........Tshs.199,934,000/=*
*Kif. 2014 -Prisons Coast …….…...……….........Tshs.212,529,000/=*
*Kif. 2015 - Prisons Lindi……………………........Tshs.236,455,000/=*
*Kif. 2016 - Prisons Manyara ……..………........Tshs.183,432,000/=*
*Kif. 2017 - Prisons Mtwara…………………........Tshs.187,502,000/=*
*Kif. 2018 - Prisons Ruvuma……...……...........Tshs.228,394,000/=*
*Kif. 2019 - Prisons Rukwa………..…...............Tshs. 214,040,000/=*
*Kif. 2020 - Prisons Mara………...……..............Tshs.224,565,000/=*
*Kif. 2021 - Prisons Iringa……. …..……............Tshs.218,206,000/=*
*Kif. 2022 - Prisons Kilimanjaro….………........Tshs.244,644,000/=*
*Kif. 2023 - Prisons Morogoro…..……………......Tshs.298,987,000/=*
*Kif. 2028 -Prisons Shinyanga…..……………...Tshs. 230,000,000/=*
*Kif. 3001 - Prisons Staff College ………… Tshs. 3,409,078,000/=*
*Kif. 3002 - Prisons Driving School.……………Tshs.502,786,000/=*
*Kif. 3003 - Prisons Trade School….…………...Tshs.960,528,000/=*
*Kif. 3004 - Prisons College Kiwira.………... Tshs.1,911,497,000/=*
*Kif. 4001 -Prisons Building Brigade………...Tshs.2,043,553,000/=*
*Kif. 4002 - Prisons Industries …………………..Tshs.902,055,000/=*
*Kif. 4003 - Prisons Farms………..……....Tshs.1,620,273,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

*Kif. 1001 - Administration and HR*
*Management …..……............Tshs. 2,273,567,000/=*
*Kif. 1002 - Finance and Accounts ………….Tshs.419,229,000/=*
*Kif. 1003 - Policy and Planning …………Tshs. 4,731,642,000/=*
*Kif. 1004 - Probation and Community*
*Services Division…..…............Tshs.1,771,262,000/=*
*Kif. 1005 - Government Communication*
*Unit ……..………………...................Tshs.301,825,000/=*
*Kif. 1006 - Management Information*
*Unit ………….….............................Tshs.267,058,000/=*
*Kif. 1007 - Internal Audit Unit ………………Tshs.410,104,000/=*
*Kif. 1008 - Procurement Management*
*Unit ..…….....................................Tshs. 345,224,000/=*
*Kif. 1009 - Complaints Division ……………...Tshs. 299,510,000/=*
*Kif. 1010 - Legal Services Division …………..Tshs.559,008,000/=*
*Kif. 4001 - Refugees Unit ……………………..Tshs.742,510,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji na NIDA**

*Kif. 2001 - Immigration Zanzibar ………….Tshs.5,428,078,000/=*
*Kif. 2002 - Immigration Mainland ……….Tshs.52,978,336,000/=*
*Kif. 2003 - Regional Immigration*
*Offices ……..........................Tshs.14,078,882,000/=*
*Kif. 2004 - TZ Regional Immigration*

*Training Academy ……...............Tshs.1,603,940,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

*Kif. 2001- Police Main force ….…………..Tshs. 4,407,500,000/=*
*Kif. 2005 - Police Zanzibar ……………....…Tshs.300,000,000/=*
*Kif. 2017 - Police Iringa….…………...……………........Tshs. 0/=*
*Kif. 2020 - Police Kagera…………...……..Tshs. 450,000,000/=*
*Kif. 2022 - Police Mwanza.……………..……..Tshs. 565,000,000/=*
*Kif. 2020 - Police Mara ………………….…..Tshs.535,000,000/=*
*Kif. 2026 - Police Mtwara.…………..……….Tshs.12,500,000/=*
*Kif. 2041 - Police Dodoma ….…………………..........Tshs. 0/=*
*Kif. 2044 - Police Njombe………………......Tshs. 530,000,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

*Kif. 1001 - Prisons Headquarters ……………………..Tshs. 0/=*
*Kif. 2002 - Prisons Welfare and*
*Rehabilitation .............................Tshs.12,748,000/=*
*Kif. 4001 - Prisons Building Brigade……..…Tshs.1,547,500,000/=*
*Kif. 4002 - Prisons Industries ……………………………….Tshs.0/=*
*Kif. 4003 - Prisons Farms…………...…….……Tshs.52,500,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51- Wizara ya Mambo Ya Ndani**

*Kif. 1003 - Policy and Planning ……………Tshs.1,500,000,000/=*
*Kif. 4001 - Refugees Unit ……………………Tshs.725,075,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji na NIDA**

*Kif. 2002 - Immigration Mainland ……Tshs. 206,008,980,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Mambo

ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya hapa. Vilevile, tumshukuru Katibu Mkuu na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama ndani ya Wizara hii na Wasaidizi wao kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwa mwaka ambao unaisha sasa. Tunawatakia kila la kheri katika bajeti hii ambayo tumewapa, tunajua fika kabisa kwamba bajeti hii ni ndogo kuliko mahitaji yetu, sote tungependa mpate fedha nyingi zaidi ili muweze kufanya kazi nzuri zaidi kwa vile ulinzi wetu unawategemeeni sana. Kwa hiyo, tunawatakieni kila la kheri katika utendaji wenu wa kazi. Ni matumaini ya Watanzania kwamba hali ya amani itazidi kuimarika. Mimi binafsi na wapiga kura wangu tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Kule ninakokupigia kelele sana mwananchi mwingine tena ameuawa leo. Hili jambo ninapolisema baadhi ya watu huwa hawanielewi, lakini hatuwezi kunyamaza tunapoona mauaji yakiendelea. *(Makofi)*

Tatizo la kule siyo kubwa hivyo, ni dogo sana, ni tatizo la *leadership* tu. Safari hii aliyeuawa anatoka katika kijiji cha Soya, kule kwenye Jimbo la Chemba la Mheshimiwa Nkamia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nkamia na wewe jiandae kesho kwenda kuzika.

Baada ya maelezo hayo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 8.25 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi, Tarehe17 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*